

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 29 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN - K.n.y. MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Na. 158

Serikali Kukamilisha Ujenzi wa Zahanati – Busega

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Imalamate Wilayani Busega wamejenga zahanati na kumaliza maboma manne kwa maana ya zahanati moja kila kijiji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao kuezeka maboma hayo ili waweze kupata huduma za afya kwenye zahanati hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya huduma za afya katika Wilaya ya Busega, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Busega shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Nasa na kukiwezesha kuanza kutoa huduma za dharura za upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Serikali iliipatia halmashauri hiyo shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Vilevile, mwezi Februari, mwaka 2021 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Busega shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tati katika Hospitali ya Halmashauri na imetenga shilingi milioni 500 katika bajeti ya mwaka 2020/2021 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, 2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Busega shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati za Ng'wang'wenge, Sanga na Mkula. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati ya Imalamate, Ijutu na Busami katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya huduma za afya katika Jimbo la Busega na nchini kote ili kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swalii la nyongeza.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Niishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo Naibu Waziri amewasilisha, lakini nina maswali mawili ya

nyongeza. Swalii la kwanza; wananchi wa Kata hii ya Imlamate yenye vijiji vitatu, kwa maana ya Mahwenge, Imlamate pamoja na Jisesa, wamejitleea sana kwa kujenga maboma ya kisasa ya zahanati. Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuifanya kata hii kuwa moja ya kata za mfano ambazo wananchi wamejitleea kwa kujenga maboma haya ili waipatie kipaumbele cha kukamilisha maboma haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; je, Naibu Waziri yuko tayari sasa baada ya Bunge baada ya Bunge hili la Bajeti kuambatana pamoja nami ili kwenda kuwatemeblea wananchi wa Kata ya Imlamate kuona kazi kubwa ambayo wameifanya ambayo itakuwa ya kuigwa katika nchi yetu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuhakikisha anawasemea wananchi wake na kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya huduma za afya. Pia niwapongeza sana wananchi wa Kata hii ya Imlamate na wananchi wa Busega kwa ujumla kwa kuendelea kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa miundombinu ya kutoa huduma za afya kwa maana ya zahanati na vtuo vyaa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua na inathamini kwamba wananchi hawa wameendelea kutoa nguvu zao. Na ni kweli, ni moja ya kata ambazo zimefanya vizuri katika ujenzi wa vituo vyaa afya na hivyo katika mwaka ujao wa fedha,

tumetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya maboma matatu katika Jimbo la Busega. Kwa hiyo bila shaka fedha hizi zitakwenda kukamilisha majengo haya katika Kata ya Imalamate.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kushirikiana naye kuwashudumia wananchi wa Busega, lakini pia kutambua michango yao. Hivyo baada ya kikao hiki, tutapanga na Mheshimiwa Simon Songe tuweze kuona lini muda muafaka tutaambatana kwenda Jimboni kwake Busega.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali la nyongeza.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wananchi wa Jimbo la Meatu wapo wanaotembea hadi kilometra 40 kwenda tu kufuata huduma za afya katika zahanati. Je, ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Meatu italetewa fedha za kukamilisha maboma katika ule utaratibu wa kukamilisha maboma matatu kwa mwaka 2020/2021?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Leah Komanya kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwasemea wananchi wa Meatu, lakini pia kuhakikisha miradi ya huduma za afya inakamilishwa na kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Jimbo la Meatu ni jimbo kubwa na wananchi wanafuata huduma za

afya mbali kutoka kwenye makazi yao. Ndiyo maana Serikali imeweka mpango wa maendeleo ya afya msingi kuhakikisha tunajenga zahanati katika kila kijiji, vituo vya afya katika kata ili kusogea huduma hizi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, Serikali ilitenga shilingi bilioni 27.75 na tayari imekwishatoa shilingi bilioni 23 katika majimbo na wilaya zipatazo 133 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma matatu kwa kila halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimhakikishie kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha, Juni 30, Jimbo la Meatu pia litakuwa limepata fedha zile shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo. Hili ni sambamba na majimbo na halmashauri zote ambazo bado hazijapata milioni 150, shughuli hiyo inaendelea kutekelezwa na kabla ya Juni 30, fedha hizo zitakuwa zimefikishwa katika majimbo hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza, amepotea.

Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo lilioko Busega linafanana kabisa na tatizo lilioko katika Jimbo la Magu. Jimbo la Magu lina vijiji 82, vijiji 40 vina zahanati, vijiji 42 havina zahanati. Tunavyo vijiji 21 ambavyo vimekamilisha maboma ya zahanati. Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia maboma hayo 21 ambayo yanahitaji bilioni moja na milioni 50 ili wananchi waweweze kupata huduma kama inavyosema llani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba kila kijiji kiwe na zahanati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza

la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inaendelea kujenga vituo vya afya na zahanati katika vijiji na kazi kubwa imekwishafanyika nchini kote ikiwepo katika Jimbo la Magu. Hata hivyo, ni kweli kwamba bado kazi ni kubwa, bado kuna vijiji vingi na kata nyngi ambazo bado zinahitaji kujenga vituo vya afya na zahanati. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kiswaga kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa fedha kuhakikisha tunaendelea kujenga vituo vya afya na zahanati nchini kote, lakini pia katika Jimbo hili la Magu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue kwamba katika mwaka huu wa fedha, tayari Jimbo la Magu limeshapelekewa millioni 150 kwa ajili ya kuchangia nguvu za wananchi kujenga na kukamilisha maboma matatu na katika mwaka ujao wa fedha pia imekwishatengewa shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya zahanati. Kwa hiyo maboma haya yote yaliyobakia pamoja na nguvu za mapato ya ndani ya halmashauri, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha maboma haya yanakamilika na kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kasalali, swali la nyongeza.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa hali ilivyo katika Jimbo la Busega inafanana kabisa na hali ilivyo katika Jimbo la Sumve. Katika Kata ya Mwabomba wananchi wamejenga maboma katika Viji ya Mwambomba, Mulula na Ngogo na mpaka sasa maboma haya hayajamaliziwa, ni maboma ya zahanati. Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa Serikali itamalizia maboma haya ili wananchi wa Kata ya Mwabomba na wenyewe wapate huduma ya afya kama yalivyo maeneo mengine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Kasalali, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata hii ya Mwabomba katika Jimbo hili la Sumve, ni kweli kwamba wananchi wameendelea kuchanga nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa maboma ya zahanati na katika vijiji hivi vitatu, kwanza niwapongeze sana kwa kutoa nguvu zao na kujenga maboma haya kuonesha kwamba kimsingi wana uhitaji mkubwa wa huduma za afya. Ndiyo maana Serikali imeendelea kutambua na kuthamini sana nguvu za wananchi kwa kutenga fedha kwa ajili ya kila jimbo kupelekewa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya ya zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika Jimbo la Sumve pia, nimhakikishie Mheshimiwa Kasalali kwamba fedha zimetengwa kwa mwaka ujao wa fedha, maboma matatu, ambayo yanahitaji kwenda kukamilishwa yatakwenda kukamilishwa. Nimweleze Mbunge, kwa kuwa vipaumbele ni haya maboma matatu na tayari millioni 150 zimetengwa kwa ajili ya maboma hayo, kwa hiyo tatizo hilo limeshapatiwa majawabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni endelevu. Katika kila mwaka wa fedha tutaendelea kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma yote yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuendelea kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swalii nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii nyongeza. Changamoto zilizopo kule Busega zinafanana sana na changamoto ambazo tunazo Arumeru Mashariki.

Wananchi Kata za Kikatiti, King'ori, Majengo, Gabobo na Kikwe, wanahanganya kila leo kujenga zahanati wenyewe lakini hatujaona Serikali ikija kutusaidia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuja kutupa msaada na sisi tuweze kupata huduma za afya kikamilifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Arumeru Mashariki wameendelea kuchangia nguvu zao kujenga maboma ya zahanati na vituo vya afya. Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wale wanaungwa mkono kwa juhudini zao ambazo wanazonesha katika kuwekeza katika miundombinu hii ya huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pamoja na maboma hayo mengine ambayo Mheshimiwa Dkt. Pallangyo ameyasema, nimhakikishie kwamba, kwanza katika mwaka huu wa fedha ambao tunaendelea, 2020/2021, shilingi milioni 150 kwa ajili ya maboma matatu, kuhakikisha kwamba yanakamilishwa, zimetengwa na zitafikishwa kabala ya tarehe 30, Juni, mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha, 2021/21, Serikali pia imetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya maboma matatu katika Jimbo hili la Arumeru Mashariki. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Pallangyo kwamba tutahakikisha tunaendelea kutenga fedha za kuchangia nguvu za wananchi kukamilisha maboma ya zahanati na vituo vya afya ili tuendelee kusogea huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, amekuwa mfuatiliaji wa karibu sana kwa ajili ya wananchi wa Arumeru Mashariki, amehakikisha anasimamia miradi mbalimbali ikiwemo miradi hii ya huduma za afya. Na sisi tumhakikishie kwamba tutaendelea kushirikiana kwa karibu sana na wananchi wa Jimbo la Arumeru Mashariki, lakini pia na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo kuhakikisha kwamba tunahudumia wananchi wetu kwa karibu zaidi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Na. 159

Ujenzi wa Mto Msimbazi - Dar es Salaam

MHE. TARIMBA G. ABBAS aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mto Msimbazi ambaao umeainishwa katika llani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 – 2025?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA** aliujibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas Mbunge Jimbo la Kinondoni naomba kutoa maelezo yafuatayo kuhusu Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatekeleza mradi wa kuendeleza

Jiji la Dar es Salaam (Dar es Salaam *Metropolitan Development Project*) kwa mkopo nafuu wa Dola za Marekani milioni 300 kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza *DFID*, inatekeleza programu ya *Tanzania Urban Resilience Programme* ambayo imelenga kuzisaidia halmashauri na Serikali Kuu katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kuanzia, programu itanza kutatua changamoto zinazolikibili Bonde la Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari *DFID* imeshatenga kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 20 kwa ajili ya Bonde la Mto Msimbazi. Pia Benki ya Dunia, kupitia mradi wa *DMDP*, imekubali mkopo wa nyongeza wa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 100 kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za Bonde la Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Tarimba Gulam Mbunge wa Kinondoni:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kubadili eneo la bonde la Mto Msimbazi kuwa eneo la uwekezaji na fursa mbalimbali. Ili kufikia azma hiyo, usanifu wa mradi huo umekamilika. Utekelezaji wa mradi utaanza baada ya kupata idhini ya Serikali kuhusu matumizi ya fedha hizo za mkopo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ili kupunguza athari za mafuriko kwa sasa, kipande cha Mto Msimbazi cha daraja la Jangwani kinafanyiwa usafi wa mara kwa mara na wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Abbas, swali la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa juhudini wanazozifanya katika kutafuta majawabu ya eneo hili. Lakini vilevile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Msimbazi sasa hivi umepoteza kina kutokana na kujaa michanga mingi sana kiasi kwamba tupo katika kipindi cha mvua, kipindi ambacho maji hutapakaa na wananchi wa maeneo ya Kigogo Jaba, Kigogo Kati, Kata ya Mzimuni, Daraja la Magomeni na hata Kata ya Magomeni yenyewe, pale wanapata athari kubwa sana ya mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *commitment* ya Serikali kwamba wasaidie juhudini za wananchi katika maeneo hayo, juhudini ambazo zinaongozwa na Madiwani wangu Mheshimiwa Richard Mgana, Mheshimiwa Loto na Mheshimiwa Nurdin katika kuondoa mchanga katika maeneo yale ili mvua hizi zisiletu athari tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, changamoto hii pia...

NAIBU SPIKA: Hilo swali la pili nenda moja kwa moja kwenye swali.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningemuomba Mheshimiwa Waziri aambatane nami kutembelea Kata za Tandale, Magomeni, Ndugumbi, Makumbusho, Kijitonyama, Mwananyamala na Hananasif ili kwenda kuona athari za mto Ng'ombe kutokana na mafuriko vilevile ili aweze kusaidia juhudini za Serikali ambazo zimeshaanza kuujenga mto huo. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

naomba kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Abbas Tarimba Gulam kwa juhudini yake ambayo analifanya katika jimbo lake la Kinondoni. Lakini pili kuwa ni Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* kwa awamu ya pili nadhani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimba. Swalii la kwanza, kwa kuwa juhudini imeshafanyika kwa wananchi wa Jimbo la Kinondoni katika kuhami, kuokoa mafuriko ambayo yanatokea katika Mto Msimbazi, basi Serikali ipo tayari kushirikiana nao kwa ajili ya kuondoa mchanga huo kuongeza kina cha maji, kuongeza kina cha mto ili maji yaweze kupita kwa usalama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lake la pili, niko tayari Mheshimiwa Abbas kufuatana na wewe kwenda katika sehemu inayohusika. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zaytun Swai swalii la nyongeza.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, Mkoa wa Arusha una mito mingi ambayo ni vyanzo vizuri vya maji na vilevile ni vivutio vya utalii. Kama vile Mto Temi, Mto Nduruma na n.k. Lakini mito hii mingi imetekelizwa na kupelekeea kukauka maji kutokana na shughuli nyingi za kibanadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu kwa Serikali, Je, Serikali inampango gani wa kuirudisha mito hii katika hali yake ya asili? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo katika harakati ya upandaji wa miti kuimarisha mazingira

ili kuhami mito hiyo iweze kuwa salama na kurudi katika hali ya kawaida.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuuliza swali ambalo linafanana na ambalo muuliza swali wa kwanza alivyouliza.

Swali langu ni kwamba katika Mji wetu wa Tarime Mjini lipo korongo maarufu kama korongo la starehe, na korongo hili limekuwa hasa wakati wa mvua linaleta madhara makubwa maana linapitisha maji mengi na hatimaye linahatarisha nyumba za wakazi ambao wanaishi kandokando ya korongo hili.

Je, Serikali ni lini litajenga Korongo hili ili *at least* wakazi ambao wapo katika mtaa huu waweze kuwa na uhakika wa makazi yao? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tutatuma wataalam wetu kwenda kuangalia na kufanya tathmini katika Korongo hilo ili kusudi wataalam hao walete tathmini ambayo ni sahihi kwa ajili ya kufanyia kazi ndani ya mwaka wa fedha ujao. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtevu swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa changamoto zilizopo ndani ya Jimbo la Kinondoni kuhusiana na Mto Msimbazi ni sawa kabisa na changamoto zilizopo katika Mto Mbezi na Mto Mpiji ndani ya Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ni lini sasa itaanza kutengeneza kingo za mto Mbezi ili kuokoa taasisi za Serikali mashule lakini vile vile na nyumba za wananchi, kuondolewa na maji? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa juhudhi yake ya kupitia na kufanya mambo yaliyomengi ndani ya Jimbo la Kibamba. Kwa hakika Serikali ipo tayari kufanya tathimini ama inafanya tathmini juu ya jambo hilo mara tu mwaka wa fedha tutakapopata idhini ya fedha za kutosha basi tutapita ndani ya Jimbo hilo na kutatua changamoto ambazo zinazikabili Jimbo la Kibamba.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Ofisi ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo sasa aulize swali lake.

Na. 160

Hitaji la Maji – Jimbo la Namtumbo

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Jimbo la Namtumbo lina tatizo la maji karibu maeneo yote ya Vijijini pamoja na Makao Makuu ya Wilaya: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili katika bajeti ya mwaka 2020/2021?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Winfred Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya Maji vijijini Wilayani Namtumbo ni asilimia 69. Katika kutatua tatizo la maji Jimbo la Namtumbo, Serikali Katika mwaka wa fedha 2020/2021 kuititia *RUWASA* imekamilisha miradi miwili, ambayo ni mradi wa maji Mkongogulioni - Nahimba na mradi wa maji Mtakuja. Miradi hiyo itahudumia jumla ya wananchi 9,683 katika vijiji vya Mkongogulioni, Nahimba na Mtakuja. Utekelezaji wa miradi ya maji ya Likuyusekamaganga, Njoomlole, Ligunga, Lusewa na Kanjele unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2021 na miradi ya Litola – Kumbura, Luhimbalilo – Naikesi, inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mji wa Namtumbo Serikali inaendelea na mipango ya muda mfupi na muda mrefu. Kwa muda mfupi utekelezaji wa mradi wa uboreshaji, ambapo bomba kuu na mabomba kwa ajili ya usambazaji yamelazwa umbali wa kilometra 31.92 na umegharimu Shilingi milioni 653.2. Pia, kazi ya kuunga wateja 1500 katika urefu wa bomba kilometra 24 inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia mpango wa muda mrefu, Serikali imepanga kutekeleza mradi mkubwa kwa ajili ya maji kutoka vyanzo vya maji vya Likiwigi na Libula vyenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya Lita Milioni Nne kwa siku. Usanifu wa mradi umekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa swalii la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza naomba niishukuru Serikali kwa kuwa mradi huu wa Likuyusekamaganga ambao ultumia muda

mrefu umeanza kuonyesha dalili na sasa vituo vitano vinatoa maji kati ya vituo hamsini na tatu vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili (a) na (b);

(a) Kwa kuwa mradi wa Njoomlole, Ligunga, Lusewa na Kanjele mabomba yametandazwa ila tunapewa sababu ya kutokuwa na viunganishi katika mradi huo. Je, Serikali viunganishi hivi vinatoka wapi kwa nini wasituletee mara moja ili watu wapate maji? (*Makofii*)

(b) Swali la pili, kwa upande wa Mji wa Namtumbo, vitongoji vyake na maeneo la Rwinga, Minazini, Lusenti, Libango, Suluti na Luegu wanapata maji mara moja kwa wiki mgao wake ni mkubwa sana na watu wanalamika sana.

Je, Serikali inaweza ikafanya uboreshaji wa huu wa haraka ili wananchi wapate maji inavyotakiwa? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, mabomba ni kweli yametandazwa na hivi viunganishi tayari na vyenyewe vimeshafika hapa nchini. Nipende kumuagiza Meneja wa Mkoa wa RUASA – Ruvuma kuhakikisha mradi huu anakwenda kuukamilisha mara moja na maji sasa yaweze kuwafikia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lako la pili, umeongelea kuhusiana na ule mgao mkali wa mara moja kwa wiki, tayari sisi kama wizara tumeendelea kujipanga kuhakikisha mgao wa maji maeneo yote yanakwenda kushughulikiwa na tunapunguza hayo maumivu ya mgao wa maji. Na hili pia ninamuagiza RM – Ruvuma kuhakikisha anaendelea kuona namna bora ya kufanya kuititia vyanzo tulivyonavyo kuhakikisha mgao huu unapungua kutoka mara moja kwa wiki angalau mara nne kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini vile vile nipende kuagiza mameneja wa Mikoa wote hata pale Mwanza kwenye Jimbo la Illemela maeneo ya Ilalila, Kahama, Nyamadoka, nahitaji kuona kwamba kila mmoja anawajibika vema. Kwa hiyo, mameneja wote wa Mikoa waweze kuhakikisha wanawajibika na maji yanaweza kuwafikia wananchi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza kwa kifupi.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, kwa kuwa tatizo la maji lilitopo katika Jimbo la Namtumbo linafanana kabisa na tatizo lilitopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati katika Kata ya Riroda, Duru, Hoshan, Gidas, Hewasi.

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya maji yaliyopo katika maeneo hayo ili kumtua mama ndoo kichwani? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Maryprisca Winfred Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lengo jema kutoka Wizara ya Maji ni kuona kwamba miradi yote ambayo inatekelezwa inakamilika kwa wakati. Kwa hiyo, hii miradi ambayo ipo Babati inaendelea na utekelezaji itakamilika kulingana na muda wake wa utekelezaji namna ambavyo usanifu ulionyesha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye hili suala la maji, ninashukuru sana kwamba matatizo haya yanayotokea kwenye Jimbo la Namtumbo yanafanana sawa kabisa na matatizo yaliyopo Jimbo la Ndanda hasa kwenye Kata za Mlingula, Msikisi, Namajani pamoja na vijiji

vyake. Ninataka kufahamu sasa mpango mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kabla ya kiangazi kikuu tunapata maji ya kutosha na uhakikisha kwenye maeneo haya. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tatizo la maji linapungua. Na ndio maana Wizara ya Maji iliweza kuunda chombo hiki cha kushughulikia maji vijijini pamoja na usafi wa mazingira kwa maana ya RUASA. Hivyo maeneo yote ambayo kwa sasa hivi yamekuwa yakipitia changamoto ya maji tunaendelea kuyashughulikia kwa karibu kabisa kwa nia ya dhati kuona kwamba tatizo la maji tunakwenda kulipunguza kama si kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi na maeneo ya Ndanda kama tulivyoongea Mheshimiwa Mbunge nimekuahidi kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha tutakuja angalau tuanze na kisima kimoja, viwili. Lakini mpango wa muda mrefu ni utaanza mwaka ujao wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa swalilala nyongeza.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulizwe swalilala nyongeza kwenye Wizara hii ya Maji.

Kwa kuwa Wilaya ya Longido ni moja ya wilaya kame sana nchini na kwa kuwa tuna baadhi ya milima ambayo inavyanzo vya chemchem kwenye misitu ya Serikali kama mlima Gilay, Mlima Kitumbeine, Mlima Longido na chemchem iliyopo matali A na chemchem zinazotoka upande wa West Kilimanjaro Kata za Ormololi na Kamwanga na kuna mabonde ambayo yangeweza kuchimba mabwawa pamoja na visima kirefu... (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Swali Mheshimiwa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali ina mpango kusaidia kumaliza kero ya maji kwa wananchi wa Jimbo la Longido.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Engineer Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuona kwamba maeneo yote ambayo yana matatizo ya maji tunakwenda kuyashughulikia. Mheshimiwa Dkt. Steven tumekuwa tukiwasiliana kwa karibu na nampongeza sana kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa suala hili. Nachoweza kumhakikishia kama tulivyozungumza, Kijiji cha Opkeli, Kata ya Mundarata; Kijiji cha Ogira, Kitongoji cha Ingokin, maeneo haya yote tunakwenda kuyashughulikia. Lengo ni kuona maeneo yale yote maji yanakwenda kutoka bombani iwe kwa chanzo cha maji cha kisima ama chanzo kingine cha maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mloo wenyewe wakazi zaidi ya 70,000 unakabiliwa na changamoto kubwa sana ya maji. Naomba kufahamu nini mpango wa Serikali katika kuwatua ndoo wanawake wa Mji Mdogo wa Mloo? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Engineer Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeendelea kutoa maelekezo na kutekeleza miradi maeneo ya Mloo mpaka Tunduma. Kote huko tunaendelea kuhakikisha maji yanakwenda kupatikana. Katika maeneo ambayo nimefanya ziara yangu ya awali kabisa ni Mloo pamoja na Tunduma. Tayari tumemsimamisha yule mtumishi ambaye hakuwa tayari kuendana na kasi ya sasa na tukamweka pale Meneja wa Mkoa wa RUWASA kwa sababu ni mtendaji mzuri. Pia tayari mkeka tumeshauandaa tunaenda kuongeza timu maeneo yale ya Mloo na Tunduma ili kuhakikisha maji yanakwenda kutoka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jeremiah Mrimi, swalii la nyongeza.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwa kuwa, tatizo la maji katika Jimbo la Serengeti ni sawa kabisa na tatizo la maji kule Namtumbo. Naipongeza sana Wizara, rafiki yangu Mheshimiwa Jumaa amejitahidi sana kuhakikisha mradi wetu wa maji hasa ule wa chujio unakamilika hata hivyo mpaka sasa hivi mradi ule bado haujakamilika, lakini pia kupeleka maji katika vijiji vya Jirani. Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi yote hii miwili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa namna bora na nzuri ya kujibu maswali. Kweli nimeamini mtoto wa samaki hafundishwi kuogelea, hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa ambalo nataka niliseme ni kwamba Wizara ya Maji tumepokea miradi 177 ambayo ni kichefuchefu na ilikuwa ikichafua Wizara. Mkakati wa Wizara baada ya kuanzisha Wakala wa Maji Vijiji (*RUWASA*), tukasema miradi hii yote kichefuchefu ikiwemo mradi wa Mugumu ambao ulikuwa ukichafua, sasa hivi tunaukwamua. Katika wiki hii tunatoa

fedha zaidi ya milioni 300 kuhakikisha tunakamilisha mradi ule na wananchi wa Mugumu waweze kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tunaenda Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake.

Na. 161

**Ujenzi wa Mabwawa Makubwa na Skimu za Umwagiliaji
Choma Chankola, Ziba na Simbo**

MHE. SEIF K. S. GULAMALI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mabwawa makubwa na Skimu za Umwagiliaji za Choma Chankola, Ziba na Simbo ambazo zimefanyiwa upembuzi yakinifu kwa zaidi ya miaka sita sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Choma Chankola lipo katika Kijiji cha Choma Chankola, Kata ya Choma, Wilaya ya Igunga. Usanifu wa bwawa hili umeonyesha kuwa lina uwezo wa kutunza maji mita za ujazo 6,825,757 na maji haya yaliyovunwa yanaweza kumwagilia hekta 400 za mpunga. Hata hivyo, bwawa la Choma pamoja na mabonde yote ya Ziba yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, yameingizwa kwenye Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa mwaka 2018 kwa ajili ya utekelezaji wake. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Bwawa la Simbo lililopo katika Kata ya Simbo, Wilaya ya Igunga usanifu wake umekamilika. Bwawa hili lina uwezo wa kutunza maji lila 15,228,000 na maji yaliyovunwa yanaweza kumwagilia hekta 1,000 za mpunga. Bwawa hili pia lipo katika Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa Mwaka 2018 kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, andiko la Programu ya Ujenzi wa Mabwawa katika Mikoa Kame ya Tanzania (*Participatory Dams Development Programme in Semi-Arid Areas of Tanzania*) limekamilika ambapo mabwawa haya ni mionganini mwa mabwawa 88 yaliyopangwa kujengwa katika programu hiyo. Andiko limeshawasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kutafutiwa fedha na utekelezaji wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Seif Gulamali, swalii la nyongeza.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza mawili. Katika Skimu ya Umwagiliaji ya Igunga, kumekuwa na wakulima wakichukua mikopo mikubwa kwa riba ya asilimia 18, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji pale Mwanzugi.

Je, nini mkakati wa Wizara kuwasaidia wakulima hao waweze kupata nafuu katika kilimo hicho? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, wakulima wa Mkoa wa Tabora, wamekuwa wakipata mikopo kwa ghamama kubwa (kwa dola) katika zao la tumbaku.

Je, nini mkakati wa Serikali kuwasaidia wakulima wa zao la tumbaku kupata pembejeo kama mlivyowasaidia wakulima wa zao la pamba? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Seif Gulamali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba wakulima katika skimu nyingi za umwagiliaji ikiwemo zilizopo katika Jimbo la Igunga Mjini, lakini maeneo ya Mkoa wa Morogoro, maeneo ya Mbarali, kwa maana ya Mkoa wa Mbeya na maeneo mengine, wamekuwa wakipata *financing* kutoka katika sekta ya fedha kwa riba zaidi ya asilimia 16 mpaka 20 na zaidi ya hapo na wengine wamekuwa wakipata mikopo kwa gharama ya wastani wa riba ya asilimia 3.5 kwa mwezi, ni gharama kubwa. Tumeshaanza mawasiliano na wenzetu wa Benki Kuu ya Tanzania na hivi karibuni tumekutana *MDs* wote wa *Commercial Banks*ili kutengeneza Skimu za *financing* kwenye sekta ya kilimo ambazo zitakuwa na gharama nafuu na zinaendana na uzalishaji wa sekta ya kilimo. Riba hizi za zaidi ya asilimia 20 kwa mazao ya kilimo, wakulima hawawezi kupata faida kutohana na *inputs* zao. Kwa hiyo, hili tunalfanyia kazi na hivi karibuni mtasikia taarifa ya Kamati ya Kitifa ilioundwa na Waziri wa Kilimo kwa ajili ya kuja na *financing models* za sekta ya kilimo zinazoendana na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakulima wa tumbaku, Wizara ya Kilimo tumechukua hatua na mwaka huu wakulima wa tumbaku hawatoenda kukopa *hard cash bank* kwa sababu sasa hivi wamekuwa wakikopa fedha kwa dola na wamekuwa wakilipa riba za asilimia 7 mpaka 8 na hizi zimekuwa zikiwasababishia matatizo na wengi kukata tamaa kuendelea na uzalishaji wa tumbaku. Kwa hiyo, tunatengeneza programu na utaratibu ambapo wakulima watapatiwa pembejeo na *supplier* atapata *LC* na hao wakulima kupitia *AMCOS*zao hawatoenda benki kuchukua *hard cash* kulipia pembejeo, watapata pembejeo na watalipa mwisho wa msimu watakapouza mazao. Hapa *transaction* itakayokuwepo ni *guarantee* kati ya Wizara ya Kilimo na taasisi za fedha kuwapa *guarantee* wakulima wasiweze kwenda kuchukua mikopo ya fedha *cash* kwa

sababu, imekuwa ni mzigzo mkubwa. Utaratibu huu tumeufanya kwenye pamba, wakulima wamepata pembejeo bila kwenda kukopa fedha benki na watalipa katika mjengeko wa bei. Hivyo hivyo, tutafanya kwenye korosho na tumbaku.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitakaowapa fursa ya kuuliza maswali, nenda moja kwa moja kwenye swali usianze na kuchangia wala kulinganisha na swali la msingi. Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekwishafanya upembuzi yakinifu katika Skimu za Tawi na Dirimu zilizoko Wilayani Mbulu. Je, ni lini sasa Serikali itajenga mabwawa ya umwagiliaji katika skimu hizo? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba skimu hizi zote zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu na tumeshajua gharama zake. Tunachokifanya kama Wizara sasa hivi tutakapopitishiwa bajeti mwaka huu tutakuwa tuna Mfuko wetu wa Umwagiliaji na tutatumia *force account* kwa ajili ya kuweza kuzi-develop skimu hizi na tunatarajia mwaka huu tutakuwa na vifaa vya kutosha. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Mpango wetu wa miaka mitano mionganoni mwa skimu ambazo ziko katika programu mojawapo ni hizo zilizoko katika Mkoa wa Manyara.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, swali la nyongeza.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Sengerema,

naomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mradi katika Bwawa la Nyamterera Katunguru, Sengerema na Mradi wa Bwawa la Isole Kishinda katika Halmashauri ya Wilaya Sengerema. Bwana la Kishinda ilipata shilingi milioni 700 na Bwawa la Nyamterera lilipata shilingi bilioni 1.2 lakini pesa hizi hazijulikani ziliko na haya mabwawa hayajachimbwa. Je, Waziri, anaweza akatueleza namna gani wananchi wa Sengerema tutapataje nafuu kuhusiana na uchimbaji wa mabwawa hayo?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa amesema kwamba mabwawa haya mawili yalipata fedha na hizo fedha hazijulikani zilipo, namwomba tu baada ya kipindi cha maswali na majibu tukutane, tuweze kuongea mimi na yeye aweze kutusaidia hizo *information* alizonazo na tuweze kuchukua hatua ili kufahamu kama fedha zimepotea ama kumetokea tatizo gani? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shaban Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina mvua inayonyesha kwa mwaka mzima na kuharibu miundombinu ya barabara zetu, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa hasa maeneo ya Makanya, Mbwei, Garibo Eloi, Kwayi, maeneo ya Kata ya Ubiri ili wananchi wale waweze kulima kilimo cha umwagiliaji? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga na tukizungumzia kuanzia Wilaya ya Lushoto, Wilaya ya Handeni kuelekea mpaka Muheza ni wilaya ambazo kwetu ni *priority* kama Wizara ya Kilimo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka ujao *priority* yetu ni kutumia *resources* zetu wenyewe kwa maana ya kujenga mabwawa. Sasa hivi tunafanya *comprehensive study* ya kuangalia maeneo ambayo tunaweza kujenga mabwawa kwa gharama nafuu. Kwa hiyo, maeneo yake ni mionganoni mwa maeneo ambayo tunayapa kipaumbele, avute subira tutayafanya kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Serikali inisaidie kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na ikasababisha mafuriko makubwa ndani ya Jimbo la Hai na kuharibu skimu nyingi sana zilizoko ndani ya Jimbo la Hai, ikiongozwa na skimu kubwa iliyojengwa na fedha nyingi za Serikali inaitwa Skimu ya Kikafu Chini pamoja na Skimu ya Johari, Mwasha na skimu nyingine ndani ya kata tisa zote zimeharibika pamoja na mifereji. Je, ni lini sasa Serikali itafanya ukarabati wa skimu hizi ikizingatiwa ni kipindi cha kilimo? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Saashisha *is very committed* na kazi kubwa

anayofanya kwa ajili ya wananchi wake inaonekana. Jana tumekuwa naye pamoja na Mbunge wa Moshi Vijijini kwa ajili ya kuongelea madhara waliyoyapata wananchi na wakiomba msaada wa chakula na niji-*commit* kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo tunaifanya kazi *issue* ya chakula na maafa waliyopata wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu skimu hizi, hivi tunavyoongea sasa hivi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Prof. Tumbo, yuko Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Hai na maeneo yote yaliyoathirika pamoja na Moshi Vijijini, wakifanya tathmini ya athari ya mafuriko hayo ili tuwe na *comprehensive plan*. Hatuwezi kusema lini kabla ya *technical team* yetu kurudi na taarifa ya kuweza kuifanya kazi lakini tuwaahidi tunaifanya kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa PhillipoMulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, nipongeze sana Serikali kupitia kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Bashe kwa namna alivyoshirikiana na mimi katika sakata la ufuta Wilayani Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Songwe kuna Kata ya Mbangala bwawa kubwa lilihajengwa toka mwaka 2017 lakini mpaka leo halijamalizika na hatujapewa fedha kwa ajili ya kulimalizia. Ni lini Serikali itatoa fedha kumalizia ujenzi wa Bwawa la Mbangala? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mulugo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maeneo ambayo yatapewa kipaumbele katika mwaka wa fedha ujao, pamoja

na kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu kwa umwagiliaji ni kukamilisha miradi yote ambayo imefanyika *either* nusu ama inahitaji *repair*. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, hatutofanya mradi mpya kabla ya kukamilisha miradi ya zamani na skimu ambazo zina upungufu ili ziweze kuzalisha katika *optimal level*. Huo ndiyo mwelekeo na ndiyo *commitment* yetu kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niulize swali lifuatalo; mafuriko yaliyoikumba Hai na Moshi Vijjjini yamelikumba pia Jimbo la Vunjo hususani Skimu za Kahe. Je, Serikali ina mpango gani pia kuhakikisha kwamba Skimu za Kahe nazo zinafanyiwa marekebisho? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena, Mkoa wa Kilimanjaro, timu yetu ya wataalam hivi tunavyoongea ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo ipo huko. Tunatoa uzito sana athari zilizotokea katika Mkoa wa Kilimanjaro, kwa maana ya Wilaya zote zilizoathirika ikiwemo Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Kimei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba baada ya ripoti ya tathmini kurudi, skimu zote zitakuwa ni sehemu ya *priority*. Vilevile athari ambazo wakulima wamezipata ambao tuna uhakika kwamba hawatapata mavuno au chakula mwaka huu, tutatoa kipaumbele kinachostahili na kuweza kutatua hizo changamoto. Kwa hiyo, niwaombe Wabunge wa Mkao wa Kilimanjaro na hasa wilaya zote zilizoathirika, watuvumilie

wakati watu wetu wanaendelea kufanya kazi hii katika maeneo yao. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali la mwisho la Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 162

Kukamilika kwa Usambazaji Umeme Vijijini

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO - K.n.y. MHE. MWANTUMU M. ZODO aliuliza:-

Usambazaji wa umeme vijijini unapaswa kukamilika ifikapo Mwaka 2021/2022:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa usambazaji wa umeme vijijini unakamilika kama ilivyopangwa?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na Shirika la Umeme (*TANESCO*) inaendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2022. Mradi huu unalenga kufikisha umeme katika vijiji 1,974 ambavyo havijafikiwa na miundo mbinu ya umeme. Aidha, mradi huu pia, utafikisha umeme katika vitongoji 1,474.

Mradi huu utakapokamilika utafanya vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara kufikiwa na miundo mbinu ya umeme na gharama ya mradi huu ni takribani shilingi 1,040,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika kwa wakati, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza usimamizi, kupunguza wigo wa kazi za wakandarasi ili kurahisisha usimamizi, wakandarasi kulipwa kwa wakati na kuhakikisha vifaa vyote vinavyohusika vinapatikana nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Husna Sekiboko swal la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ni ahadi ya Chama Tawala na vilevile ahadi ambayo ipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi kwamba mapema mwaka huu wa fedha vijiji hivyo vitakuwa vimekamilishiwa kupata umeme.

Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha kupeleka umeme kwenye vijiji vilivyobaki vya Mkoa wa Tanga hasa Vijihi vya Lushoto na Kilindi ambako kuna hali ngumu zaidi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kumekuwa na tatizo kubwa la kukatika kwa umeme kwenye Vijihi vya Handeni, Kilindi na Lushoto linalosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha. Je, ni lini Serikali sasa itamaliza tatizo hilo kwa kubadilisha miundombinu ya umeme hasa katika maeneo ya njia ya umeme kutoka Mombo kwenda Lushoto? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba vijiji vyote 1,974 ambavyo mpaka sasa havijapata miundombinu ya umeme, vitapata kufikia Desemba, 2022. Hii awamu ya tatu mzunguko wa pili wa REA utahakikisha kwamba unamaliza maeneo yote ambayo yalikuwa hayajapata umeme na hivyo kufikisha umeme katika vijiji vyote 12,268 ambavyo vilikuwa bado havijapata umeme. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, yeye na Waheshimiwa wengine wote kwamba ifikapo Desemba mwakani tutakuwa tumefikisha umeme katika vijiji vyote ambavyo havikuwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swal la pili, kwanza napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga kwa ufuutiliaji mzuri kabisa wa miundombinu ya umeme katika mkoa wao. Mojawapo ya maeneo ambayo yalikuwa yana matatizo makubwa ya umeme ni Tanga. Serikali kupitia Wizara ya Nishati na TANESCO tumehakikisha tunamaliza tatizo la umeme katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu niseme tu kidogo kwamba Tanga ina matumizi ya umeme takribani *Megawatts* 110 na wanapata umeme katika vyanzo viwili pale Hale *Megawatts* nne na *New Pangani Megawatts* 68 na umeme mwingine pia unatoka kwenye kituo chetu cha Chalinze kwenda Tanga. Sasa hizo njia zinakuwa ni ndefu kidogo na hivyo umeme mwingine unapotea njani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kutoka Chalinze kwenda Tanga, ile njia iliyojengwa pale inashindwa kubebe umeme mkubwa, kwa hiyo, tumeamua kuweka mkakati wa muda mrefu wa kujenga njia ambayo itakuwa ni ya *Kilovolt* 220 itakayowenza kubebe umeme mkubwa kwa ajili ya kufikisha Tanga bila kukatika. Kwa hiyo, tunajiandaa, tumeshafanya *feasibility study*, tumeshapata maeneo ya kujenga *sub-station* ikiwepo eneo la Segera, tutamaliza tatizo hilo. Kwa sasa, Timu yetu ya TANESCO kupitia Shirika lake la ETDCO iko kazini inaendelea kurekebisha miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata takribani shilingi bilioni 4,500 kurekebisha miundombinu ya umeme ya Tanga ikiwemo kurekebisha nguzo, waya na vikombe kwa kilometra zaidi 2,000 na maelekezo ya Wizara ni kwamba ifikapo Mei, 2021 iwe imekamilika. Hivyo timu yao *TANESCO* kupitia *ETDCO* ni kubwa na inaendelea kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, tunawahakikishia wananchi wa Tanga kupitia Wabunge wao kwamba kilio chao tunakifanyika kazi. Vile vile maeneo mengine tutaendelea kuhakikisha tunarekebisha miundombinu ili kuondoa matatizo yaliyopo. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swalî la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swalî la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Lwale ina vijiji 76, vijiji 34 bado havijapatiwa umeme. Naona uzalishaji wa vijiji vifuatavyo mahitaji ya umeme ni makubwa sana; Kijiji cha Mlembwe, Lilombe, Kikulyungu, Mkutano, Mpigamiti, Ngorongopa, Ngongowele, Kimambi, Nahoro na Ndapata, vijiji hivi kwa sababu ya uzalishaji wake mahitaji ya umeme ni makubwa sana. Je, Serikali ni lini mtatupelekea umeme kwenye vijiji hivi ili kuwatia wananchi hamasa zaidi waweze kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalî la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Kuchauka kwa sababu yeye ni mmojawapo wa Wabunge wanaofuatilia pia maendeleo ya majimbo yao katika maeneo mbalimbali katika likiwepo eneo la umeme. Kama nilivyosema hapo mwanzo ni kwamba vijiji vyote ambavyo havijapata umeme, kufikia Desemba, 2022 vitakuwa vimepatiwa umeme vikiwepo vijiji vyote alivyovitaja

vya Jimbo la Liwale. Tunaomba aendelee kutusaidia na kusimamia utekelezaji ambao utafanyika katika maeneo yake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona nami niulize swali dogo la nyongeza. Napenda kuipongeza Serikali kwani ndani ya Kata zangu zote 11 kwenye Jimbo la Korogwe Mjini umeme umefika, lakini changamoto ni kwamba ndani ya Kata hizo ipo Mitaa mingi ambayo umeme haujafika kabisa. Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Korogwe katika kutatua changamoto hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kimea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* inapeleka umeme katika maeneo mbalimbali kwa *program* za kila siku za kawaida, kwenye Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Pia zipo *program* nyingine ambazo zinapeleka umeme kwenye Mitaa na Vijiji vyetu ikiwemo *REA* yenye, *densification* na *peri-urban*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mheshimiwa Dkt. Alfred ambapo tayari Kata zake zote na vijiji vyake vyote vina umeme, yale maeneo machache ambayo hayana umeme, mradi wetu wa *densification* utapelekea umeme katika maeneo hayo kuanzia mwezi Saba. Pia tunavyo Vitongoji na Mitaa takribani kama 3,000 ambavyo vitapelekewa umeme, kwa hiyo, Vitongoji vyake na Mitaa yake Mheshimiwa Mbunge pia ni sehemu ya maeneo hayo yatakayopelekewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pale ambao *densification* tu itaanza mwezi wa Saba, Mheshimiwa

ataweza kupata umeme katika eneo lake kwa sababu amekuwa akifuatilia sana ofisini kwetu na ni mfuataliaji mzuri wa maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, nawapongeza wananchi kwa kupata Mbunge mfuataliaji kama wa aina yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Kitongoji cha Banawanu katika Kata ya Mseke kiko karibu sana na Mji wa Iringa Mjini na kipo katikati ya Tosamaganga pamoja na Uwachani; na hii ilikuwa ni ahadi ya Mbunge ambaye ndiye mimi kwamba tutawapelekea umeme. Je, ni lini sasa *TANESCO* itapeleka umeme ili hata kunifichia aibu Mbunge mwenzake?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Kiswaga kwa kutoa ahadi za ukweli kwa wananchi wake kuwaahidi kuwapelekea umeme. Nawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote walioahidi kupeleka umeme kwa wananchi wao kwamba ahadi hizo zilikuwa ni za ukweli na Serikali sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan itatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitongoji alichokisema kama nilivyosema, mradi wetu wa *densification* ambao sasa tupo IIB utapeleka katika Vitongoji ambavyo

vilikuwa havijapata umeme, lakini maeneo mengine ambayo hayajapata umeme kwa sasa kwa maana ya vijiji, vitongoji vilivyomo, tulivyovitaja 1,474 vitapata umeme pia katika awamu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa wananchi kwamba umeme utapelekwa na ahadi ya Mheshimiwa Jackson Kiswaga itakuwa ni ya ukweli kuanzia mwezi Julai.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali kutoka kwa Wabunge na Majibu kutoka upande wa Serikali. Kabla sijaleta matangazo tuliyonayo hapa, nitoe ufanuzi kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, wapo Wabunge humu ndani huwa wanalamika sana wasipopata maswali ya nyongeza. Nakumbuka nilishasema hapa mbele, kama una swali la jimbo lako, peleka maswali mengi ya msingi. Peleka kule kama unayo hoja. Haya ya nyongeza, Kanuni hazilazimishi Kiti kutoa maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, hutegemea muda; kuna siku nydingine huwa hakuna kabisa swali la nyongeza. Sasa wewe ukianza wananchi wako wanapata taabu, andika swali la msingi.

Sasa hapa mbele pia hua tunazo taarifa za Wabunge waliouliza maswali ya nyongeza. Wapo wengine ni mahodari na wapo wengine ni mahodari lakini kwa sababu hawafahamu humu ndani Kanuni zinasemaje kuhusu kusimama na kupata nafasi, basi hawapati nafasi. Nami kama kiongozi ni kazi yangu kuwalinda Wabunge wote wapate haki sawa. Kuna Wabunge wapya hajauliza hata swali moja; kuna Wabunge wa zamani hajauliza swali hata moja; huyo atapewa kipaumbele, kwa sababu naye ni Mbunge, anawakilisha watu humu ndani. (*Makofii*)

Sasa leo nitatoa mfano mmoja. Wapo Wabunge humu wana maswali matano ya nyongeza, siyo ya msingi; wapo Wabunge wanayo manne ya nyongeza, siyo ya msingi;

na kuna mwingine hana hata moja. Huyo anayelalamika ni yule ambaye anayo maswali ya nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukiamini Kiti hiki kinatoa sawa mamlaka makubwa lakini na sisi tunawahesabu ninyi kama ni Wabunge wenzetu na tunataka kutoa fursa sawa sawa. Kwa hiyo, anapoitwa mwenzako hukuitwa wewe, ukiona unalo swali la msingi, peleka swali la msingi.

Sasa hapa niiliwa nasema mfano, kwamba tunazo taarifa hadi za tarehe ya maswali yaliyoulizwa. Kwa nia njema tu, tutatoa mfano wa Mheshimiwa Esther Matiko. Yeye ameuliza swali la nyongeza tarehe 30 Machi; tarehe 8 Aprili; tarehe 12 Aprili; na tarehe 14 Aprili. Sasa ukiambiwa umeuliza maswali manne ni kwamba taarifa tunazo. Kwa hiyo, usilalamike hujapewa swali wakati sisi huku tunatafuta yule ambaye hana swali hata moja. Sawa sawa! Taarifa tunazo hapa mbele. (*Makof*)

Kama kuna mtu ambaye hana swali kabisa, tunampa utaratibu kama amesimama mara nyingi tunajitahidi, lakini tusionekane kwa namna oyote ile kwamba kuna wengine wanapewa maswali na wengine hawapewi. Ama usipopewa wewe unaanza kumhesabia mwingine, yule mbona ana matano! Labda swali hilo hakuna aliyekuwa amesimama, kwa hiyo, akapewa ye ye nafasi. Kwa hiyo, hakuna mtu atanyimwa haki ya kuuliza swali la nyongeza kama kuna nafasi hiyo. Ila kama wakiomba wengi, atapewa fursa ambaye hajaauliza maswali mengi. Nadhani hilo limeeleweka vizuri. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pia lingine kuhusu maswali, ili tuwe tunapata muda mwingi na tuisilalamike, tuache ile ya kupenda kulinganisha na swali la msingi. Wewe nenda tu kwenye swali, Serikali inafahamu eneo lako ili tutunze ule muda.

Pia niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri, huwa mnakumbuka kuwasifia Wabunge wengine na wengine mnawasahau. Kwa hiyo, una uchaguzi, aidha usifie Wabunge

wote wanaouliza swal la nyongeza ama usisifie kabisa. Kwa sababu unawawekea Wabunge mazingira magumu; mwingine amesifiwa, mwingine hakusifiwa. Sasa yule ambaye hakusifiwa wakisia kule kwake inaoneka kama yeze haji haji huko Serikalini kufuatilia jambo lake; au yeze huwa haulizi sana humu ndani. Nadhani hilo nalo limeeleweka. Ukiamua kusifia, sifia Wabunge wote waliopata fursa ya kukuuliza au usiwasifie wote ili wote tuwe sawa sawa, kwa sababu wote ni Wabunge ambao tunawakilisha wananchi humu ndani. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo ya wageni waliotufikia siku ya leo humu ndani. Tunao wageni ambao wamekaa jukwaa la Spika; na hawa ni wageni wanen wa Mheshimiwa Spika ambao ni Watendaji Wakuu kutoka Benki ya *CRDB* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndugu Abdulmajid Nsekela. Naona ndiyo wanaingia, sasa wacha waingie wakae halafu nitasema vizuri. (*Makof*)

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Doto Biteko ambaye ni Waziri wa Madini kutoka Wizarani na Jimboni wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi Profesa Jusinian Ikingura. Huyu nadhani ni Justinian naona wameandika Jusinian hapa. Sasa sijajua wa Jimboni ni wapi? Tangazo halijaandikwa vizuri hapo. Wanaotoka Bukombe wapo humu ndani pia? Haya, naona wapo kutoka Wizarani.

Pia wapo wageni wengine 15 na hawa ni Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Simon Msanjila. Karibuni sana. (*Makof*)

Sasa niwatangaze wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Watendaji Wakuu kutoka Benki ya *CRDB* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndugu Abdulmajid Nsekela, yeze ameongozana na Ndugu Chabu Mishwaro ambaye ni Meneja Kanda ya Kati, pia ameongozana na Ndugu Kenneth Kasigila ambaye ni Mwandamizi Idara ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi; yupo pia Ndugu Grace Adam, Meneja wa Tawi la Bunge. Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Makofi hayo safari iliyopita yalivyopigwa kwa nguvu namna hii yalisababisha kupanda cheo. Sasa leo naona Mtendaji Mkuu yuko naye hapo nadhani haya makofi yanaashiria kile cheo ulichompa anafanya kazi vizuri. Wakati ule alisema Mheshimiwa Spika, hata sasa hivi unaweza ukampa cheo lakini inabidi abaki hapa hapa. (*Makofi*)

Tuendelee na wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliopo humu ndani siku ya leo. Tunao wageni wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Waziri Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, huyu ni Afisa Misitu wa *SAO Hill* kutoka Mafinga Mkoani Iringa na huyu ni Ndugu Abel Busalli. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, ambaye ni Waziri wa Maji ambaeo ni Watendaji Wakuu wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, *Engineer Anton Sanga* na Mgeni mwingine anatoka Wizara ya Nishati na Madini Zanzibar, Dkt. Mngereza Mzee Miraji. Sijajua wamekaa upande gani. Ehee, karibuni sana wageni wetu kutoka Zanzibar. *Engineer Anton Sanga*, yuko wapi? Jamani yale maji, nadhani umesikiliza maswali ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge, nami hapo sikuongeza swali. Dkt. Mngereza Mzee Miraji anayeongoza timu kutoka Zanzibar, karibu sana. (*Majibu*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambaeo ni wafanyabiashara katika Sekta ya Madini Mkoani Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Rehema Paul Mtatifikolo. Karibuni sana. Jamani, akina mama tunafanya vizuri, mmewaona hao akina mama wa kwenye madini! Kwa hiyo, tuko vizuri. (*Makofi/Vigelegele*)

Haya tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ambaeo ni vijana wa Tanzania kutoka Jijini Mwanza na hawa ni Ndugu Edna Lameck na Kamala Dickson. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ambaye ni Mbunge Mstaafu kutoka Zanzibar, huyu ni

Ndugu Parmukh Singh Hoogan. Karibu sana, karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma ambaye ni mke wake Ndugu Fatma Karume Said pamoja na ndugu yake Ndugu Hamida Mohamed kutoka Zanzibar. Haya, naona wote wamesimama ni wadada. Hebu Ndugu Fatma Karume Said asimame! Haya jamani, nadhani tumemwona wifi yetu na shemeji yetu. (*Makofii*)

Haya Mgeni wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete ambaye ni mpiga kura wake kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndugu Stephano Gwalugano. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Charles Mwijage pamoja na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ambaao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali kutoka Jimboni Muleba wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Muleba Mhandisi Richard Ruyangu.

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava ambaye ni rafiki yake kutoka Meatu, Mkoani Simiyu na huyu ni Agness Marwa. Hee! Humu ndani kuna Mheshimiwa Agness Marwa, naona sasa haya majina yamefanana sana. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Wakili Stephen Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati. Hawa ni viongozi wa CCM na wapiga kura wake kutoka Jimbo la Bukoba Mjini, Mkoani Kagera wakiongozwa na Katibu wa CCM, ndugu Michael Chonya. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaao ni wapiga kura wake kutoka Mbozi, Mkoani Songwe, hawa majina yao hajawawekwa. Karibu sana. Tunao pia wageni 19 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Dunstan Kitandula kutoka taasisi ya HakiArdhi ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo ndugu Rachel Chagonja. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Edwin Sware ambaye ni rafiki yake kutoka Mkoani Njombe na huyu ni Shauku Kihombo. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Nusrat Shaban Hanje ambaa ni babu na bibi yake kutoka Sekuka, Mkoani Singida. Hawa ni ndugu Hamis Msukuya na ndugu Tatu Mbularina. Hao wameshasimama. Haya jamani, karibuni sana babu na bibi yetu. (*Makofii*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ndayisaba George Ruhoro ambaa ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Ngara, Mkoani Kagera, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ndugu George Rubagora. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Mohamed Suleiman ambaa ni mke wake ndugu Fatma Salum na wapiga kura wake kutoka Malindi, Zanzibar. Karibuni sana. Haya jamani. Tumemwona hapo shemeji yetu na wifi yetu. (*Makofii*)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaa ni wapiga kura wake kutoka Manonga, Mkoani Tabora. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Arusha na huyu ni ndugu Belinda Michael. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Askofu Dkt. Josephat Gwajima ambaa ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Pharis Burhani. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa ambaa ni Viongozi wa Halmashauri na Chama Cha Mapinduzi kutoka Longido, Mkoani Arusha wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Longido ndugu Joseph Sadira. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa John Pallangyo ambao ni wajumbe wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Maji ya Chai wakiongozwa na Mkuu wa Shule na Katibu wa Bodi ndugu Titus Kasanda. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoani Rukwa na huyu anaitwa Ndugu Nicholas Mwasumbi. Sijajua amekaa wapi, karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Amrabi Mrimi ambao ni viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Serengeti wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Jacob Bega. Karibuni sana. (*Makofii*)

Naambiwa hapa wapo wageni ambao ni Mheshimiwa Waziri wa Madini ambao ni wawakilishi. Kuna mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa *NMB*, karibu sana. Tuwie radhi hawajaweka jina lako hapa lakini karibu sana mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu. (*Makofii*)

Pia tunaye mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa *NBC*, karibu sana. Karibuni sana tukiyapata majina pamoja, basi tutawataja kwa majina lakini tunatambua uwepo wenu kuwawakilisha hao viongozi ambao wamewapa fursa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo pia kutoka kwa Mwenyekiti wa Wabunge Waislamu, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Wabunge Waislamu kwamba kutakuwa na kikao kitakachofanyika leo tarehe 29 Aprili, 2021, saa saba mchana katika Ukumbi Namba 227, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Mnakaribishwa kwenye kikao hicho na Mwenyekiti wenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA MADINI**

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dotto Biteko aje atoe hoja yake. (*Makofi*)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa mwaka 2021/2022. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu yenye kurasa 152 naomba yote iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama nitakavyoiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na nchi kwa jinsi alivyonijalia afya njema na hata kuniwezesha leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara nyingine tena.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wote wa Tanzania kwa ujumla kwa msiba mzito uliolipata Taifa letu kwa kuondokewa na jemedari, mchapa kazi, mpenda maendeleo, shujaa wa Afrika Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuondokewa na viongozi wengine wa nchi akiwemo Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi za Zanzibar. Balozi John William Kijazi aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Aidha, niwape pole wananchi wa Jimbo la Muhamwe Kigoma kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye na kwa wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM, Mheshimiwa Martha Jachi Umbula. Naomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue wasaa huu kumpongeza kwa dhati, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa kwa kuapishwa kushika nafasi yake ya juu kabisa ya uongozi kwenye Taifa letu. Nampongeza kwa ujasiri mkubwa aliuunesha katika kupokea...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge tunapiga kelele sana na hili litatufanya saa ya kuchangia hata tusjue Waziri kasemaje kwa sababu kusoma tutakuwa hatujasoma na kusikia hatujasikia! Tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue wasaa huu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kushika nafasi hii ya juu kabisa katika uongozi wa Taifa letu. Nampongeza kwa ujasiri mkubwa aliuunesha katika kupokea majukumu haya mazito wakati ambapo Taifa lilikuwa limegubikwa na wimbi kubwa la simanzi na majonzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa limeshuhudia utendaji kazi wake uliotukuka kutokana na umahiri, ujasiri, juhudhi, maarifa, ubunifu na uwajibikaji aliounesha wakati akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miongoni mwa kazi alizozifanya ni pamoja na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini hapa nchini, msisitizo wake juu ya umuhimu wa kutunza mazingira katika uchimbaji madini, afya na usalama migodini na kuhamasisha na kuhamasisha kufanyika kwa mikutano na makongamano mbalimbali ya kimataifa kwa ajili ya kuhamasisha shughuli za uchimbaji madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuaminiwa, kuteuliwa na kuthibitishwa kwa kura zote na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze vile vile Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na wananchi wa Jimbo la Ruangwa na kupitishwa bila kipingwa na kuaminiwa tena na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kwa kishindo na wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini na kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuendelea na wadhifa wako wa kuwa Naibu Spika kwa kipindi kingine cha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Pia, niwapongeze wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuteuliwa kuwa Wajumbe

wa Kamati hiyo. Naahidi kuwapa ushirikiano wangu pamoja na wenzangu wote Wizarani kama ambavyo itahitajika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa kuwa sehemu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niombe ushirikiano wao katika kusimamia Sekta hii ya Madini. Mimi pamoja na wenzangu Wizarani tutawapa ushirikiano wote utakaohitajika wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali ambazo wameteuliwa. Niwapongeze viongozi wote waandamizi wa Serikali walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa mbalimbali. Niwatakie utendaji mwema katika kutekeleza majukumu yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru watu wema wa Bukombe kwa kuendelea kuniamini na kunicagua tena kuwa Mbunge wao. Naomba niwaahidi mbele yako kuwa nitaendelea kufanya kazi yao ya kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya pamoja na Katibu Mkuu Profesa Simon Samwel Msanjila kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi zao. Niwashukuru viongozi wote Wizarani kwa ushirikiano walionipa. Nawashukuru sana sana kwa kusimamia Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, naomba nimshukuru mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo kwa upendo wake na utayari wa kubeba baadhi ya majukumu ya familia yetu.

Nawashukuru wanangu wapendwa pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa upendo na ushirikiano wao. Uvumilivu na maombi yao yameniwezesha kutekeleza majukumu haya bila kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nijielekeze katika maeneo mahsus ya hotuba hii ambayo ni: Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa; Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti wa Mwaka 2020 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko na kasi ya ukuaji wa sekta ya madini. Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 3.8 mwaka 2014 na kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019. Pia, wastani wa mchango wa Sekta ya Madini kwa kipindi cha robo tatu za mwaka 2020 ulikuwa kwa asilimia 6.4. Mwenendo huu wa mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato unatupa tumaini na imani kwamba lengo tulilowekea la kuchangia asilimia 10 kwenye pato la Taifa ifikapo mwaka 2020 litawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 547.73. Kati ya fedha hizo, shilingi 526.72 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi 21.01 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya shilingi bilioni 445.17 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 112.69 ya lengo la makusanyo la shilingi bilioni 395 katika kipindi husika. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 80.52 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 62.78. Bajeti hii ilijumuisha jumla ya shilingi milioni 54.28 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambazo ni fedha za ndani. Katika bajeti ya fedha ya matumizi ya kawaida shilingi bilioni 33.23 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na

shilingi bilioni 21.04 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida ya fedha zilizopokelewa katika kipindi cha miezi tisa ni shilingi bilioni 50.52. Kati ya fedha hizo bilioni 13.09 nikwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 37.43 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara iliweka vipaumbele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini. Katika kutekeleza na kuimarisha kipaumbele hiki, Wizara ilitekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kufuatilia wadaiwa mbalimbali ambao katika kufikia Machi 21, jumla dola za Kimarekani 277,049.33 zimekusanywa kutoka kwa wateja walipewa hati za makosa. Wizara vile vile imetambua na kurasimisha maeneo yote ya uchimbaji katika maeneo ya kimadini, imesajili mialo 6,821 na kuweka kumbukumbu za uzalishaji. Aidha, Wizzara imetoa vibali 2,920 vya kusafirisha madini kwenda nje ya nchi. Kuanzisha na kuendelea kusimamia masoko ya madini na vito, ununuzi wa madini kuititia uwepo wa masoko na vituo vya madini vyenye thamani ya shilingi trilioni 3.19 yameuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi bilioni 222.07 ambayo haya yamefanyiwa biashara katika masoko yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kipaumbele cha kuendeleza uwekezaji, uwezeshaji wachimbaji wadogo, Wizara imetekeliza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuongeza kasi ya urasimishaji na uwezeshaji wachimbaji wadogo ambapo katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, jumla ya leseni 3,540 za uchimbaji mdogo, leseni 1,961 za *brokers* na leseni

41 za utafiti zimetolewa. Kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu faida na matumizi ya masoko ya madini na huduma za uchenjuaji wa madini kupitia Vituo vya Rwamgasa, Katente, Itumbi hadi sasa jumla ya wachimbaji wadogo 864 wamepatiwa mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kipaumbele cha kuendelea kusimamia mafunzo na ukaguzi wa migodi hapa nchini, Wizara imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza imefanya ukaguzi wa fedha za kodi, makampuni 13 yamebainika kuwa jumla ya shilingi bilioni 6.2 inatakiwa kulipwa na kampuni hiyo kama stahiki ya Serikali. Pili, imesimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi, ukusanyaji wa takwimu za madini, kufuatilia maduhuli na kuweka Maafisa Migodi Wakazi katika kila mgodi, mikubwa na kati. Pia, imesimamia taarifa za ununuzi na uuzaji wa masoko katika vituo vya ununuzi wa madini hapa nchini. Tatu, imekagua migodi 1,729 ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya shughuli za uchimbaji madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele kingine ni kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko hapa nchini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo. Wizara imeanzishwa kupitia Tume ya Madini, soko jipya moja na vituo tisa vya ununuzi wa madini na kuyawekea vifaa maalum kwa ajili ya utambuzi na kupima viwango vya madini, uzito na ubora wake. Wizara imehakikisha pia upatikanaji wa huduma wezeshi ikiwemo huduma za kibenki na uwepo wa wataalam wanaohitajika katika kuapatia huduma wateja hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa masoko umekuwa na manufaa makubwa toka kuanzishwa kwake Machi, 2019 hadi Machi, 2021. Jumla ya tani za dhahabu 28.34 zimeuzwa; tani za madini ya vito 2,803.97; *carat* 30,367 za madini ya almasi; tani 259.71 za madini ghafi ya *Tanzanite*; *carat* 222,000.70.4 za *Tanzanite* zilizokatwa na kusafirishwa; tani 91 za madini ya bat; *carat* 39540.4 za madini mengineyo

ya vito yenye thamani ya trilioni 3.19 yaliuzwa kuititia masoko yetu hapa nchini na kuipatia Serikali jumla ya shilingi bilioni 22.7 kama malipo ya mrabaha na ukaguzi wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoroshaji wa madini umedhibitiwa. Katika kipaumbele hiki, Wizara imefanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, imeendelea kushirikiana na vyombo vyta ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa ukaguzi wa kimkakati katika mikoa mbalimbali unafanyika.

Pili, kuendelea kuimarisha udhibiti na usafirishaji wa madini katika vituo vyta mipakani, viwanja vyta ndege na bandari. Tatu, kufanya kaguzi za mara kwa mara katika mialo ya kuchenjulia madini kwa wafanyakishara wa madini hapa nchini. Nne, kuondoa urasimu katika utoaji wa vibali vyta kusafirisha madini ambapo kwa sasa kibali hutolewa ndani ya kipindi kisichozidi saa moja baada ya nyaraka zote za maombi kuwasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha soko la *Tanzanite*. Katika kufanya jambo hili, Wizara imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, imeendelea kuimarisha miundombinu ya vifaa vyta ulinzi katika eneo tengefu ya Mirerani pamoja na ujenzi wa barabara ndani ya ukuta. Pili, kusimamia shughuli zote za uchimbaji na biashara ya madini *Tanzanite*, kuhakikisha kuwa biashara hiyo inafanyika ndani ya ukuta kuititia Kituo cha *Tanzanite* cha Magufuli. Aidha, madini yote yanayopelekwa sokoni Arusha na menngineyo yanaratibiwa kwa kibali maalum cha kuyatembeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara vile vile imeongeza wataalam wa uthaminishaji madini ambapo Wizara ilipeleka masomoni watumishi 10 waliohitimu nchini India kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani Wizara katika kutekeleza kipaumbele hiki imewezesha ujenzi wa viwanda vitatu vya kusafisha madini (*refinery*) Mkoani Mwanza, Dodoma pamoja na Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya ujenzi wa viwanda vya uyeyushaji madini na usafishaji itawezesha kuongeza thamani ya madini yetu na kuongeza fursa ya ajira. Aidha usafishaji wa dhahabu utasaidia kupata madini ambayo yalikuwa kwenye mbale husika kama vile madini ya fedha, shaba, *radium*, ambayo hutumika kama madini ghafi ya viwanda vingine ikiwemo usonara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kipaumbele cha kuimarisha taasisi zilizo chini ya Wizara, Wizara imenunua mashine tano za *XRF Machine* kwa ajili ya masoko ya madini na vito kwa ajili ya masoko yetu hapa nchini. Wizara imezipatia taasisi zake jumla ya watumishi 41 ambapo watumishi 27 wamepelekwa Tume ya Madini, watumishi 13 wamepelekwa *STAMICO*, watumishi 7 wamepelekwa *GST* na 4 wamepelekwa *TGC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa magari sita kwa ajili ya shughuli za utafiti na taasisi za *GST*. Wizara vilevile imeendelea kuijengea uwezo kwa kuiwezesha kupata fedha zaidi za kununulia magari mengine manne kwa ajili ya kuimarisha zaidi shughuli za kiutafiti Taasisi yetu ya *GST*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kipaumbele cha kuendeleza raslimali watu Wizara imeendelea kuongeza weledi na ufanisi katika utendaji ambapo watumishi 13 huhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na kununua vitendea kazi mbalimbali kwa ajili ya watumishi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maeneo Mengine. La kwanza, Ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mipaka, Manyovu. Wizara imeendelea kutoa ushirikiano

katika ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mpaka wa Manyovu Mkoani Kigoma. Lengo la ujenzi huu wa kituo hicho ni kurahisisha shughuli za kuvuka mipakani, ili kuvutia biashara kati ya nchi ya Tanzania na nchi jirani. Wizara itashirikiana katika kudhibiti utoroshaji wa madini, kuweka miundombinu ya ukaguzi wa madini. Miundombinu hiyo ni pamoja na ofisi mbalimbali, maabara, ghala la kuhifadhi madini kwa ajili ya wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sekta ndogo ya baruti. Kwa kutambua umuhimu wa baruti katika shughuli za uchimbaji madini Wizara iliendelea kutoa vibali na leseni mbalimbali kwa kuzalisha na uagizaji usafirishaji na uhifadhi wa baruti nchini. Vibali vilivyotolewa vimeiwezesha Wizara kukusanya jumla ya dola za kimarekani 148,700 na shilingi milioni nane. Aidha, ili kuhakikisha usalama wa matumizi na uhifadhi wa baruti Wizara ilifanya ukaguzi wa maghala na store za kuhifadhiya baruti na kufuatilia shughuli za matumizi ya baruti, ili kudhibiti matumizi haramu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini ni kipaumbele kingine. Katika kipindi cha Julai, 2021 na Machi 21 Wizara kupitia Tume ya Madini imepokea na kuchambua mipango 113 ya ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini kwa wamiliki wa leseni za madini na watoa huduma migodini. Ambapo mipango 110 kati ya hiyo ilikidhi vigezo na kuidhinishwa. Aidha, mipango mitatu haikukidhi vigezo na wahusika walielekezwa kuifanyia maboresho ili iweze kuendana na sheria ya madini na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Wizara ilipangiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara imepokea shilingi bilioni 1.76 sawa na asilimia 27.68 ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi cha miezi tisa. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuzunguka ukuta wa mererani katika eneo tengefu, ununuzi wa vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na ununuzi wa magari manne kwa ajili ya

shughuli za utafiti wa madini na kuendelea na ujenzi wa vituo vitatu vyta umahiri vyta Songea, chunya pamoja na Mpanda. Kazi nyingine Wizara imesimamia taasisi tano ambazo ni Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia Tanzania (*GST*), Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini Mafuta na Gesi Asilia (*TEITI*) na Kituo cha Jiolojia Tanzania (*TGC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Madini. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 jumla ya kilogramu 42,084.76 za dhahabu zenyet thamani ya shilingi trillioni 5.33 zilizalishwa na migodi mikubwa, migodi ya katni na migodi midogo. Aidha kilogramu 12,650.24 za dhahabu zenyet thamani ya shilingi trillioni 1.58 sawa na asilimia 30 zilizalishwa na wachimbaji wadogo pekee. Jumla ya kilogramu 38,561.21 za madini zenyet thamani ya shilingi bilioni 28.19 na tani 7,612.06 za makinikia ya shaba zenyet thamani ya shilingi bilioni 149 zilizalishwa na kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi rejea wachimbaji wadogo wa madini ya *Tanzanite* walizalisha na kuza kilogramu 5,964.82 za *Tanzanite* ghafi na *karat* 111,054.33 za *tanzanite* iliyokatwa na kusanifiwa na kilogramu 52,657.06 za *Tanzanite* zenyet ubora wa chini yaani magonga.

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya *karat* 45,022.85 ya madini ya almasi zilizalishwa na kuuzwa ambapo kiasi cha *karat* 30,448.97 zilizalishwa na mgodi wa Mwadui *WDL* na *karat* 14,573.88 sawa na asilimia 32.37 zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa almasi. Pia madini mengine ya vito ya kiasi cha tani 15,587.53 zilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa madini ya makaa ya mawe jumla ya tani 563,887.95 zilizalishwa katika migodi mbalimbali ya madini hayo nchini na kuuzwa. Halikadhalika katika kipindi tajwa jumla ya tani 17,971,504 za madini ya ujenzi na tani milioni 8,279,564 za madini mengine ya viwandani yalizalishwa ambapo thamani ya madini hayo ni jumla ya shilingi bilioni 610.96.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi rejewa Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) limefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 11.23 sawa na asilimia 77 ya lengo lillokusudiwa ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.8 kwa kipindi kama hiki mwaka uliopita. Aidha, utegemezi wa fedha kutoka Serikalini kwa Shirika la Madini la Taifa umepungua kutoka asilimia 89 ya mwaka 2018/2019 hadi asilimia 16.6 kwa mwaka 2021/2022. Pia, shirika liliweza kutoa mchangwo wake kwa Serikali wa billioni 1.1 August, 2020 vilevile mwaka 2019/2020 shirika lilitoa mchangwo namna hiyo wa shilingi bilioni moja kwa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Madini wa *BACLIF*. Katika kuendeleza mradi huu *STAMICO* na mbia mwenza *TANZAM 2000* wamesimika mtambo wa majaribio wa uzalishaji ambapo wameendeleza tani tano za mbale zenyé jumla yaw akia 885,523.2 zimechenjuliwa zikiwa na thamani ya bilioni 3.99 hivyo, kuliwezesha shirika kupata mapato ya shilingi milioni 29 kutohana na mrabaha na tozo na ada za ukaguzi. Kufuatia mafanikio ya majaribio hayo shirika linatarajjiwa kujenga mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuchenjua tani 40. Kwa sasa tayari maandalizi ya kununua mtambo huo yameanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya mfano Rwamgasa, Katente, Itumbi, jumla ya wachimbaji 864 wameweza kupata mafunzo kwenye Nyanja ya uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini katika vituo hivyo. Jumla ya tani 421.6 za mbale ya dhahabu ziliweza kuchenjuliwa katika vituo hivyo na kuzalisha takribani kilogramu 11.6 za dhahabu ambapo Serikali ilikusanya maduhuru ya shilingi milioni 104.03. Shirika la Madini la Taifa limeweza kupata leseni tatu za uchimbaji madini katika maeneo yaliyoko Wilayani Bukombe, Mkoa wa Geita, leseni ya madini ya shaba ili yoko Wilayani Mwanga, Mkoani Kilimanjaro, leseni ya makaa ya mawe ili yoko Ilima, Wilaya ya Rungwe, Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Jiolojia Nchini. Ili kukamilisha ugani na uutafiti wa jiolojia katika *QDS 279*

inayojumuisha maeneo ya Mpigamiti, Ndapata, Hifadhi ya Wanyamapor ya Selou na Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere Wilayani Liwale, *QDS* 264 Wilayani Malinyi na *QDS* 316 Wilayani Nanyumbu na kufanya ugani na utafiti katika *field checks* katika *QDS* 75 Wiaya ya Kasulu. Taasisi ya Jiolojia Tanzania imefanya kazi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha na kuendelea kutoa huduma za maabara kwa wadu wa sekta Tasisi ya Jiolojia Tanzania imefanya uchunguzi na uchambuzi wa sampuli tatu za malinganisho kutoka makampuni ya *Geostat* ya Australia. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa *GST* ipo kwenye viwango vinavyoaminika vya utoaji majibu ya uchunguzi unaofanywa na maabara mbalimbali zenyetibati duniani. Aidha, ukaguzi huo utendaji kwa mujibu wa taratibu za kimataifa (*ISO Standards*) ulifanywa na Taasisi ya *SADC* inayosimamia ubora wa huduma za maabara katika Ukanda wa *SADC*. *GST*imeendelea kukidhi vigezo vya kubaki na ithibati katika uchunguzi wa madini ya dhahabu kwa njia ya tanuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GST* pia ilikamilisha utafiti wa *geoscience* katika Kijiji cha Lohada Wilayani Chemba, Mkoani Dodoma iliyotokea Septemba 2020, Kunduchi Wilayani Kinondoni katika Mkoa wa Dar-es-Salaam iliyotkea Novemba 2020 kwa lengo la kubaini kilichoripotiwa kuwa ni mlipuko wa *volcano*. Uchunguzi ulibaini kwamba, kulikuwa na tabaka la tope lilidochanganyika na maji ambalo lilibubujika na kusukumwa juu ya uso wa ardhi. Tukio hilo kitaalamu linaitwa *liquefaction* na sio *volcano* kama ilivokuwa imetolewa taarifa ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia. *TEITI* imeendelea kukamilisha ripoti ya ulinganisho kwa kipindi cha mwaka 2018/2019, Malipo ya kodi katika kampuni za madini mafuta na gesi asilia. Ripoti inatarajiwa kukamilika na kuwekwa wazi kwa umma ifikapo Juni 2021. Kwa kushirikiana na wadu mbalimbali *TEITI* iliandaa mpango wa uwekaji wazi

mikataba ya madini, mafuta, gesi asilia. Aidha, *TEITI* ilainisha mikataba na leseni mbalimbali za mafuta na gesi asilia iliyo Hai ambapo ipo wazi na isiyo wazi na kutoa mapendekezo ya namna bora ya uwekaji wazi mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Jimolojia Tanzania. Katika kipindi rejewa kituo kimedahili wanafunzi 78 kwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya cheti katika fani ya teknolojia, madini ya usonara. Aidha, wanafunzi 21 walidahiliwa kujiunga na mafunzo nya muda mfupi katika fani ya utambuzi wa madini ya vito, ukataji, ung'arishaji wa madini ya vito na kufanya jumla ya wahitimu 188 katika kituo hicho toka kimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha mwaka 2021/2022. Maandalizi ya mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 yamezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo muongozo wa Taifa wa maandalizi ya bajeti na bajeti ya mwaka 2021/2022, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa 2021/2022 mpaka 2026, Sera ya Madini ya mwaka 2009, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Hotuba za viongozi aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Awamu ya Tano pamoja na Rais wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyoitoa katika Bunge lako tukufu Aprili, 2022 na maelekezo ya viongozi mbalimbali pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa nyakati tofautitofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini kwa Mwaka 2021 imepanga kutekeleza maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani, kuimarisha biashara na uwekezaji katika sekta ya madini, kusimamia ukaguzi wa shughuli za migodi, kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi,

kuendeleza raslimali watu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi pamoja na kuvutia na kuhamasisha ufanyaji biashara wa madini katika nchi hususan zilizoko kanda ya SADC, Afrika Mashariki na Maziwa Makuu, ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara katika ukanda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nitoe shukrani. Naomba nikiri kuwa juhudhi kubwa zilizofanywa na Serikali zimeifanya nchi yetu kufikia uchumi wa kat i mwaka 2020 ikiwa ni miaka mitano kabla ya muda uliokusudiwa wa mwaka 2025. Ni imani yangu kuwa kwa kasi aliyoanzanayo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu itawenza kufikia katika uchumi wa kat i wa juu muda si mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema amjalle afya njema Rais wetu mpendwa katika kusimamia mpango wa tatu wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano wenye dhima kuu ya nchi ya uchumi wa kat i na maendeleo ya watu na ahadi za ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo wanayotupatia katika kutekeleza majukumu yetu wizarani. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya Naibu Waziri wa Madini kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia sekta ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Prof. Simon Samwel Msanjila Katibu Mkuu Wizara ya Madini kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Mhandisi Davis Robinson Mlagwa Kamishna wa Madini, Profesa Idris Suleiman Kikula Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Justin Rwezahura Ikingula Mwenyekiti wa Bodi ya GST. Meja Jenerali Michael Wambura

Isamu Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Bwana Ludovic Utoh Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITI*, Dkt. John Moforo Mwenyekiti wa Bodi ya Jimolojia Tanzania na Makamishna nwa Tume ya Madini na Wajumbe wa Bod izote kwa kusimamia kwa umakini uendeshaji wa sekta ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru wakuu wa taasisi, wakurugenzi, wakuu wa vitengo, wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wizara yanatimizwa ipasavyo na hivyo kuifanya sekta ya madini kuzidi kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia, kuishukuru Benki ya Dunia, wadau wa sekta ya madini, taasisi za fedha na hapa nleleze kwa muda mrefu utoaji au upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya madini umekuwa ukifanywa na benki za nje. Naomba kwa moyo wa dhati niwashukuru kabisa benki ambazo zimeamua zenyewe *ku-finance* miradi mikubwa ambayo iko hapa nchini; Benki ya *CRDB*, Benki ya *NMB*, Benki ya Azania pamoja na Benki ya *NBC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru vyombo vyanya ulinzi na usalama pamoja na vyombo vyote vyanya habari kwa ushirikiano waliotupatia katika kuendeleza sekta ya madini. Shukrani zangu za pekee na za dhati nizitoe tena kwa wananchi wa Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunituma kuwashukuru sana familia yangu, mke wangu pamoja na watoto wangu kwa kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu, ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa ya kujenga na kutetea maslahi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako tukufu sasa liridhie na kuitisha makadirio ya jumla ya shilingi 64,816,467,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake

kwa mwaka 2020/2022 kama ifuatavyo; bajeti ya maendeleo shilingi 115,000,000,000 ambapo zote ni fedha za ndani. Bajeti ya matumizi ya kawaida ni shilingi 51,816,467,000 ambapo shilingi 18,480,807,000 ni kwa ajili ya mishahara na 33,335,660,000 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyiningine nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa utulivu. Vilevile hotuba hii imeambatana na majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufanuzi na masuala ya takwimu muhimu kwa sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja.
(*Makof*)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO(MB.),
WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochangua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2020/2021 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka 2021/2022. Hotuba yangu yenyewe kurasa 152 naomba iingizwe yote kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard) kama ilivyowasilishwa kwenye Ofisi za Bunge.

2. *Mheshimiwa Spika*, kwa unyenyekevu mkubwa namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara nyiningine tena nikiwa Waziri wa Madini kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2021/2022 wa Wizara ya Madini.

3. Mheshimiwa Spika, kipekee nichukue fursa hii adhimu kutoa pole kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa msiba mzito uliolipata Taifa letu kwa kuondokewa na Jemedari, mchapa kazi, mpenda maendeleo na shujaa wa Afrika Hayati **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Tunatambua jitihada na kujituma kwake katika kutekeleza majukumu yaliyolenga kuliendeleza Taifa kwani alikuwa ni mshauri wake wa kwanza. Msiba huu kwake ni pengo kubwa ambalo ni gumi kusahaulika kwa kuwa maelekezo na maagizo ya Hayati Magufuli yalikuwa ni sehemu ya maisha yake na yetu ya kila siku. Mwenyezi Mungu amtie nguvu na ustahimilivu.


4. Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumpa pole Mama yetu mpendwa Mhe. Janeth Magufuli ambaye ni Mjane wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, watoto, mama mzazi, ndugu na jamaa kwa kumpoteza kipenzi chao. Naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa faraja na ustahimilivu.

5. Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri, Viongozi wa Chama na Serikali kwa kumpoteza kiongozi shupavu mwenye maono, uthubutu na mpenda maendeleo.

6. Mheshimiwa Spika, vilevile, nitoe pole kwako wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika, pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba huu mzito. Nafahamu ushauri wenu kwa Rais katika masuala ya uendeshaji wa Serikali ulikuwa na lengo la kuleta maendeleo mkiendana na kasi na maono aliyokuwa nayo Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ni imani yangu kuwa mtaendelea kutoa ushauri ambao utakuwa chachu katika kuwaletaa watanzania maendeleo.

7. Mheshimiwa Spika, msiba huu si tu pigo kwa watanzania, bali umeigusa Afrika na Ulimwengu kwa ujumla hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Jumuiya za Kimataifa. Haya yamedhihirisha na hotuba mbalimbali zilizotolewa na Wakuu wa Nchi na Serikali waliohudhuria katika msiba huo. Hii ni kwa sababu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa kiongozi aliyejipambanua kushirikiana kwa dhati katika kuhakikisha ustawi na Maendeleo ya Kikanda na Kimataifa.

8. Mheshimiwa Spika, niwape pole watanzania wote kwani msiba huu umekuwa pigo na simanzi kubwa kwetu kwa kumpoteza kiongozi wetu shupavu, mtetezi na rafiki wa wanyonge, mpenda maendeleo wa dhati, Mcha Mungu na Mzalendo wa kweli. Tunu hii ya pekee ingeliweza kuwa katika nchi yoyote duniani lakini Tanzania ilipendelewa zaidi. Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika Nchi ya Tanzania. Kazi alioitiwa hapa duniani ya kutuonesha Dira, kufanya maamuzi magumu kwa maslahi ya Taifa, kukataa utegemezi, kuchukia na kupiga vita rushwa kwa vitendo ameifanya kwa moyo wa ujasiri. Hakika amevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo ameumaliza na imani ameilinda. Apumzike kwa Amani.



Picha Na.1: *Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

9. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu wa Nchi wakiwemo Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Balozi Mhandisi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, niwape pole wananchi wa Jimbo la Muhambye (Kigoma), kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mhe. Atashasta Justus Nditiye na kwa wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mhe. Martha Jachi Umbulla. Vilevile, nitoe pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla waliopoteza ndugu na mali zao kutokana na maradhi mbalimbali, ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Ninaomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

10. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue wasaa huu kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuapishwa kushika nafasi hii ya juu kabisa ya uongozi katika Taifa letu. Nampongeza kwa ujasiri mkubwa aliouonesha katika kupokea majukumu haya mazito wakati ambapo Taifa limegubikwa na wimbi kubwa la simanzi na majonzi. Hakika ametupa heshima kubwa kama Taifa kwa kuwa mwanamke wa kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki kushika nafasi ya urais.

11. Mheshimiwa Spika, Taifa limeshuhudia utendaji kazi wake uliotukuka kutokana na umahiri, ujasiri, juhudhi, maarifa, ubunifu na uwajibikaji aliouonesha wakati akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miongoni mwa kazi muhimu alizofanya ni pamoja na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini, msisitizo wake juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira, afya na usalama migodini na kuhamasisha na kuhakikisha kufanyika kwa mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa ya madini. Ni dhahiri kuwa kazi nyingi nzuri alizofanya Mheshimiwa Rais kwa kushirikiana na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli zimechangia katika kuiwezesha nchi yetu kufikia Uchumi wa Kati wa chini kabla ya muda

uliotarajiwa wa mwaka 2025. Nina imani kasi hii itaendelea zaidi na kuiwezesha nchi kufikia Uchumi wa Kati wa Juu katika siku za usoni. Kupitia Bunge lako Tukufu, naahidi kumpa ushirikiano wa dhati na niko tayari kupokea maelekezo na miongozo yake katika kuhakikisha kuwa rasilimali madini zinaendelezwa na kuwanufaisha ipasavyo Watanzania wote.

12. Mheshimiwa Spika, kupitia juhudzi zao, mageuzi makubwa yamefanyika katika Sekta ya Madini na kuiwezesha Nchi kuongeza umiliki na ushiriki wa Nchi na wananchi katika uwekezaji mkubwa na wa kati na hivyo kushuhudia mafanikio makubwa katika sekta hii ikiwa ni pamoja na:

- a) ongezeko la makusanyo ya Maduhuli ya Serikali kutoka **shilingi bilioni 168** mwaka 2014/2015 hadi **shilingi bilioni 528.24** mwaka 2019/2020;
- b) kuimarika kwa ulinzi wa Eneo Tengefu la Mirerani kwa kufunga kamera za ulinzi na taa kuzunguka eneo la ukuta. Kufuatia ujenzi wa miundombinu hiyo, mapato ya Serikali yameongezeka kutoka **shilingi milioni 165** kwa mwaka 2016 kabla ya ujenzi wa miundombinu hiyo hadi **shilingi bilioni 2.17** kwa mwaka 2020 baada ya ujenzi.
- c) mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 3.8 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2020, wastani wa mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa ulifikia asilimia 6.4;.
- d) kasi ya ukuaji wa Sekta ya Madini imeongezeka na kufikia asilimia **17.7** Mwaka 2019;
- e) kuanzishwa kwa masoko 39 ya madini na vituo vya ununuzi wa madini 50 umeondoa changamoto ya ukosefu wa mahali pa kufanya biashara ya madini hususan kwa wachimbaji wadogo, kuwahakikisha bei stahiki na mazingira salama ya ufanyaji biashara.

f) kuanzishwa kwa Kampuni za ubia za Twiga Minerals Corporation Limited na Tembo Nickel Corporation Limited ambazo zimeongeza ushiriki wa Serikali katika shughuli za uwekezaji kwenye Sekta ya Madini kwa kumiliki hisa kwa kuanzia asilimia 16 kwenye kila kampuni;



Picha Na. 2: Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa akitoa hotuba baada ya kusaini kwa Hati ya Makubaliano ya kuanzishwa kampuni ya Twiga Minerals.

g) kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha usafishaji dhahabu cha Mwanza Precious Metal Refinery ambacho kitawezesha kusafisha dhahabu kiasi cha kilo 480 kwa siku kwa kiwango cha asilimia 99.99



Picha Na. 3. Baadhi ya mitambo ya kusafisha dhahabu katika kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza Precious Metals Refinery

13. Mheshimiwa Spika, napenda kunukuu maneno ya Mwanamajumui wa Afrika Prof. PLO Lumumba kutoka Kenya aliyoyasema katika Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2021 uliofanyika jijini Dar es Salaam Februari, 2021 ya kwamba "*ili rasilimali madini za nchi ziweze kuwanufaisha wananchi wa nchi husika, nchi husika inahitaji kuwa na kiongozi mwenye sifa kuu nne ambazo ni uzalendo, maono mazuri, ujasiri, na uthubutu*". Niseme kuwa **Mhe. Samia Suluhu Hassan** anazo sifa hizo zote. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumpa nguvu, afya na hekima ili azidi kutekeleza majukumu yake kwa uzalendo, ufanisi, umahiri na ushujaa katika kusimamia Sekta ya Madini na Sekta nyiningine.

14. Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kuaminiwa, kuteuliwa na kuthibitishwa kwa kura zote na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

15. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hili ni Bunge la Kwanza la Bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu, naomba nimpongeze **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)** kwa kuendelea kuaminiwa na wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kupita bila kupingwa na kuaminiwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na pia **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuteuliwa kuendelea kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

16. Mheshimiwa Spika, naombanikupongeze wewe binafsi kwa kuendelea kuaminiwa na wananchi wa Jimbo la Kongwa kwa kupita bila kupingwa na pia kuchaguliwa na waheshimiwa wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano. Nitumie fursa hii pia kumpongeza **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)** kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Owananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini na kuchaguliwa na waheshimiwa wabunge kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

17. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza **Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb.)** kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Aidha, nimpongeze **Mhe. Seif Khamis Gulamali (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Pia, niwapongeze wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kwa kuteuliwa kuwa wajumbe wa kamati hiyo. Naahidi kuwapa ushirikiano wa dhati ili kuifanya Sekta ya Madini iendelee kuwanufaisha Watanzania ipasavyo.

18. Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la 12 kwa kuwa sehemu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niombe ushirikiano wao katika kuiendeleta Sekta hii muhimu katika kujenga Uchumi Imara na Maendeleo Endelevu ya Taifa letu.

19. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kwao kuongoza Wizara mbalimbali. Pia niwapongeze Viongozi wote Waandamizi wa Serikali walioaminiwa na kuteuliwa na **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania 11kushika nyadhifa mbalimbali, niwatakie utendaji mwema katika kutekeleza majukumu yao.

20. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru wananchi wema wa kusema na kutenda wa Jimbo la Bokombe kwa kuendelea kuniamini na kunichagua tena kuwa Mbunge wao. Nawaahidi ushirikiano wa pamoja katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya Jimbo letu kwa ufanisi mkubwa.

21. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kuwapongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya (Mb.) na Katibu Mkuu Prof. Simon Samwel Msanjila kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi zao na Prof Idris S. Kikula kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Madini Vilevile, ninawashukuru sana

viongozi hawa wenzangu Wizarani kwa kunipa kila ushirikiano ninaouomba na kuhitaji kutoka kwao. Niwashukuru pia Mhandisi David Mulabwa - Kamishna wa Madini, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini na wafanyakazi wote kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Kwa pamoja tunakiri na kuamini katika kaulimbiu yetu kuwa '*Sekta ya Madini kwa Uchumi Imara na Maendeleo Endelevu*' inawezekana.

22. *Mheshimiwa Spika*, mwisho lakini sio kwa umuhimu, ninamshukuru mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo kwa upendo wake na utayari wa kubeba baadhi ya majukumu yangu ya kifamilia. Ninawashukuru wanangu wapendwa pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa upendo na ushirikiano wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Wamekuwa nguzo muhimu kwangu wakati wote kwa kunihakikishia utulivu wa akili unaoniwezesha kufanya kazi zangu kwa umakini.

23. *Mheshimiwa Spika*, napenda sasa nijielekeze katika maeneo mahsusи ya hotuba hii ambayo ni: Ukuaji na Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

B. MCHANGO WA SEKTA YA MADINI KATIKA PATO LA TAIFA

24. *Mheshimiwa Spika*, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa (GDP) umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la kasi ya ukuaji wa sekta ikishindanishwa na sekta nyingine za kiuchumi. Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka **asilimia 3.8** mwaka 2014 na kufikia **asilimia 5.2** mwaka 2019. Pia, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa kwa kipindi cha robo tatu za mwaka 2020 (Januari hadi Septemba) ulikuwa **asilimia 6.4**. Mwenendo huu wa mchango wa sekta kwenye Pato la Taifa unatupa imani ya kufikia lengo la Wizara la kuchangia **asilimia 10** katika Pato

I. Mapato

25. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2020/2021, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 547,735,863,597.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 526,722,547,000.00** zilipangwa kukusanya na kuwasilishwa Hazina na **shilingi 21,013,316,597** zilipangwa kukusanya na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya **shilingi 445,176,864,174.16** zilikusanya ambazo ni sawa na **asilimia 112.69** ya lengo la makusanyo la **shilingi 395,041,910,250.00** katika kipindi husika. Aidha, katika kipindi rejea, taasisi zilikusanya **shilingi 11,817,355,188.26** ambazo ni sawa na **asilimia 75** ya lengo la **shilingi 15,759,987,447.75**.

II. Matumizi

26. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Mwaka 2020/2021, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya **shilingi 62,781,586,000.00**. Bajeti hii inajumuisha **shilingi 54,281,586,000.00** sawa na **asilimia 86.46** ya bajeti yote kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 8,500,000,000.00** sawa na **asilimia 13.54** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambazo ni fedha za ndani. Katika bajeti ya Fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 33,235,659,000.00** zilitengwa **kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 21,045,927,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

27. *Mheshimiwa Spika*, fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa katika kipindi cha miezi tisa (9) ni **Shilingi 50,528,599,778.51**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 13,091,015,553.81** nikwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 37,437,584,224.70** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hata hivyo, kiasi cha **Shilingi 12,590,689,975** kutokana na matumizi mengineyo kilipokelewa na kutumika katika ununuzi wa madini ya tanzanite kutoka kwa Bw. Saniniu Kuriana Laizer.

III. Vipaumbele VilivyotekelzwakwaMwaka2020/2021

28. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na Rasilimali Madini; kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji Mkubwa na wa Kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija; kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini; kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo; kudhibiti utoroshwaji na biashara haramu ya madini nchini; kuendelea kuweka mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na madini mengine ya vito; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara; kuimarisha shughuli za kitafiti za jiosayansi; kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali Yatokanayo na Rasilimali Madini

29. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, Wizara ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imeweka Maafisa Migodi Wakazi katika migodi mikubwa, ya kati na maeneo mengine yenye uzalishaji mkubwa wa madini. Vilevile, Wizara imeweka Wakaguzi Wasaidizi wa Madini Ujenzi kwenye maeneo yenye madini ujenzi na viwandani. Hadi sasa, kuna Maafisa Migodi 13 na Wakaguzi Wasaidizi wa Madini Ujenzi 182. Aidha, mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za madini umeboreshwa kwa kuanzisha mfumo mpya wa usimamizi wa madini ujenzi na madini ya viwandani ujulikanao kama *Minerals information Management Systems (MiMS)*. Mfumo huo mpyakwa sasa unafanyiwa majaribio



Picha Na. 4. Madini ya ujenzi (maarufu kama Tanga stone) yakiwa tayari kwa matumizi katika eneo la Mkinga mkoani Tanga

(ii) imetoa hati za makosa 943 kwa leseni za Uchimbaji Mdogo, 64 kwa Leseni za Utafutaji wa Madini na sita (6) kwa Leseni za Uchimbaji wa Kati. Aidha, Leseni 587 za Uchimbaji Mdogo wa Madini, Leseni 16 za Utafutaji wa Madini na Leseni nne (4) za Uchimbaji wa Kati zimefutwa kutokana na kushindwa kurekebisha makosa mbalimbali;

(iii) Wizara imeendelea kufuatilia wadaiwa mbalimbali ambapo hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya **Dola za Marekani 277,049.33** zimekusanywa kutoka kwa wateja waliopewa Hati za Makosa. Ufuatiliaji wa madai kwa wale walioshindwa kulipa madeni kwa wakati unaendelea kabla ya kufuta leseni husika kwa mujibu wa sheria;

(iv) imetambua na kurasimisha maeneo yote ya uchimbaji katika mikoa ya Kimadini; kusajili mialo na kuweka kumbukumbu za uzalishaji ambapo hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya mialo 6,821 ya kuchenjua madini ya dhahabu imesajiliwa ili kuitambua na kudhibiti uzalishaji na uchenjuaji haramu pamoja na utoroshwaji wa madini hayo; Aidha, Wizara kupitia Tume ya Madini ilitoa vibali 2,920 vya kusafirisha madini kwenda nje ya nchi;



Picha Na.5: Mchimbaji mdogo akiendelea na shughuli za uchenjuaji katika Mgodi wa Dhahabu wa Mwime Mkoani Geita

(v) kuanzisha na kuendelea kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini ambapo hadi Machi, 2021 kuna jumla ya masoko 39 na vituo vya ununuzi 50 katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kupitia uwepo wa masoko na vituo hivyo, madini yenye thamani ya shilingi **trilioni 3.19** yameuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 222.07** kama mrabaha na ada ya ukaguzi tangu kuanzishwa kwake hadi kufikia Machi, 2021;

(vi) kuendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kudhibiti biashara haramu ya madini ili kuwezesha Serikali kupata mapato stahiki. Hadi kufikia Machi, 2021 madini yenye thamani ya **Dola za Marekani 161.01** na **shilingi bilioni 5.06** yalikamatwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mirerani, Chunya, Morogoro, Kyerwa, Kilimanjaro, Tabora, Mwanza, Iringa, Dodoma, Shinyanga na Katavi;

(vii) kusimamia na kutumia mifumo ya kielektroniki ikiwemo ya usimamizi na utoaji wa leseni. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea na ujenzi wamfumo mpya wa utoaji na usimamizi wa leseni ambapo tayari uchambuzi wa mahitaji na usanifu wa mfumo

huo umefanyika. Aidha, Tume ya Madini imeboresha miundombinu yamtandaokatika ofisi za Afisa Madini Wakazi za Rukwa, Songwe, Mirerani na ofisi ya Tume ya Madini Makao Makuu - Dodoma kwa lengo la kuwa na mfumo madhubuti wa Usimamizi na Utoaji wa Leseni za Madini pamoja na mifumo ya ukusanyaji wa tozo na maduhuli ya Serikali.

30. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na hatua hizo madhubuti zilizochukuliwa, hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya **shilingi 445,176,864,174.16** zimekusanya na kuwasilishwa Hazina ambazo ni sawa na **asilimia 112.69** ya lengo la makusanyo la **shilingi 395,041,910,250.00** katika kipindi husika. Aidha, kiasi cha **shilingi 11,817,355,188.26** sawa na asilimia 75 ya lengo la makusanyo ya ndani la **shilingi 15,759,987,447.75** kwa kipindi husika zilikusanya na kutumiwa na Taasisi.

(b) Kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Uchimbaji Mkubwa na wa Kati wa Madini na Kuweka Mazingira Bora Yatakayohamasisha Uwekezaji Katika Sekta ya Madini

31. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara imefanya kazi zifuatazo:

(i) katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wizara kupitia Tume ya Madini ilifanya yafuatayo: kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na utunzaji wa mazingira katika migodi mikubwa sita (6) ya Bulyanhulu, Buzwagi, WDL, Stamigold, Mantra na North Mara; Migodi ya Kati 12 ikiwemo: Tancoal Energy, Shanta-Songwe, Cata Mining Co. Ltd, Ruvuma Coal, MMG, Mara Mine Development Ltd, ZEM (T) Co. Ltd, Busolwa Mine – Nyarugusu, Busolwa Mine - Ishokela na ZEM Development Ltd. Aidha, mitambo 31 ya uchenjuaji wa dhahabu na stoo na maghala 46 ya kuhifadhi baruti yalikaguliwa;



Picha Na. 6: Wataalamu wakiwa katika ukaguzi wa machimbo ya almasi yaliyopo Wilaya ya Kishapu Mkao wa Shinyanga

Katika ukaguzi huo baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni pamoja na kujaa kwa mabwawa ya kuhifadhia topesumu, kutokuwepo kwa mipango illyohuishwa ya uendelezaji migodi na ufungaji migodi, uhifadhi usio salama kwa kuchanganya baruti na vilipuzi kwenye ghala moja, kutokuwa na vibali nya matumizi ya baruti na kutokuzingatiwa kwa uchimbaji salama na utunzaji wa mazingira kwenye shughuli za uchimbaji mdogo. Wamiliki wa leseni zilizokaguliwa na kubainika kuwa na mapungufu walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo ambapo baadhi ya wamiliki wa leseni wamerekebisha mapungufu hayo na wengine wapo katika hatua mbalimbali za kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa;

(ii) Wizara kuititia Tume ya Madini imefanya kaguzi za kiufundi kuhusu usanifu wa ujenzi na matumizi ya mabwawa ya kuhifadhia topesumu kwenye migodi nane (8) ya Bulyanhulu, MMG, RZ Union mining, Shanta - Songwe, Canaco Mining, El Hilal Minerals, Busolwa Mine - Nyarugusu na Busolwa Mine – Ishokela. Tume ya Madini ilitoa maelekezo ya kuboreshwa kwa taarifa za usanifu ujenzi wa mabwawa hayo. Aidha, vibali sita (6) vilivyoombwa kwa ajili ya ujenzi na matumizi ya mabwawa hayo vilitolewa isipokuwa kwa migodi ya Shanta – Songwe na RZ Union Mining ambapo wamiliki walielekezwa kuboresha taarifa za mabwawa hayo kwa kuzingatia tafiti za kisayansi ili kubaini njia bora na salama za ujenzi wa mabwawa hayo;

- (iii) Wizara kuititia Tume ya Madini imepitia na kuchambua mipango sita (6) ya ufungaji mgodi kwa Migodi Mikubwa na ya Kati ya GGM, North Mara, Buzwagi, Tanga Cement, Shanta – Songwe na WDL. Kati ya hiyo, mipango ya migodi ya GGM na Shanta - Songwe iliyodhinishwa baada ya kukidhi vigezo. Aidha, majadiliano ya kuweka Hati Fungani kwa kuzingatia mipango iliyodhinishwa yanaendelea. Migodi minne (4) ambayo Mipango haikuidhinishwa ilielekezwa kufanya maboresho katika maeneo ambayo yalioneckana kuwa na mapungufu;
- (iv) maboresho ya kuimarisha ulinganisho wa mrabaha kwa madini yanayosafirishwa nje ya nchi yamefanyika kwa kuanzisha dawati maalum. Dawati hilo linafanya uchambuzi wa taarifa kwa kuhakiki nyaraka zote za malipo ambapo majibu ya Maabara ya Tume ya Madini yanatumika sambamba na majibu ya migodi na yamitambo ya kusafisha madini. Hii imewezekana baada ya kumpata mkandarasi ambaye analeta na kurudisha sampuli za mikuo ya dhahabu kwa kila mzigo unaosafirishwa nje ya nchi kwa migodi husika.
- (v) kuhakikisha Serikali inapata gawio stahiki linalotokana na hisa za Serikali katika Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited ambapo kiasi cha takriban **shilingi bilioni 100** kilitolewakwa mwaka wa fedha 2020/21.



Picha Na. 7: Hayati Dkt. John Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipokea gawio la takriban shilingi bilioni 100 kutoka Kampuni ya madini ya Twiga.

(vi) kuboresha mikataba iliyokuwepo na inayotarajia kuanza utekelezaji kwa lengo la kuongeza ushiriki wa Serikali na uwazi katika Sekta ya Madini kwa kuendelea kufanya majadiliano na wadau na Kampuni mbalimbali za uchimbaji Mkubwa na wa Kati ili kuongeza ushiriki wa Serikali katika Sekta ya Madini. Kufuatia jitihada hizi, Serikali pia imefanikiwa kusaini Mikataba ya Ubia na Kampuni ya LZ Nickel ya nchini Uingereza ya kuanzisha Kampuni ya Tembo Nickel Corporation Limited yenye Kampuni tanzu mbili ambazo ni Kampuni ya uchimbaji wa madini ya *Tembo Nickel Mining Company Ltd* na Kampuni ya Usafishaji wa Madini ya *Tembo Nickel Refinery Company Ltd* ambapo Serikali ina umiliki wa asilimia 16 za hisa katika kampuni hizo.



Picha Na. 8: Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliposhiriki katika hafla ya utiaji saini katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya LZ Nickel Limited iliyofanyika Mjini Bukoba Tanzania.

(vii) kutoa elimu ya fursa zilizopo katika Sekta ya Madini kwa Taasisi za Fedha kwa lengo la kuzishawishi ziweze kuwakopesha wachimbaji wa madini na hivyo kuboresha mazingira ya uchimbaji na biashara ya madini ambapo baadhi ya taasisi za fedha tayari zimeanza kutoa mikopo katika Sekta ya Madini na nytingine zinaendelea na taratibu za kuanza kuwakopesha;

(viii) kuandaa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2021 uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam

kuanzia tarehe 21 hadi 23 Februari, 2021. Kaulimbiu ya Mkutano huo ilikuwa ni '**Sekta ya Madini kwa Uchumi Imara na Maendeleo Endelevu**'. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huu uliwakutanisha wadau wa Sekta ya madini ambapo walijadili fursa za uwekezaji zilizopo, kubainisha changamoto mbalimbali zinazoikibili Sekta ya Madini na kuweka mikakati ya namna ya kuzitatua. Maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo yamewekewa mpango kazi wa utekelezaji na mengine yameshaanza kufanyiwa kazi. Aidha, mkutano huo uliambatana na maonesho ya madini, bidhaa za madini na elimu kuhusu teknolojia mbalimbali zinazotumika katika Sekta ya Madini. Matarajio ya matokeo ya Mkutano huo ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika Sekta ya Madini, kupata malighafi madini kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kusafishwa katika mitambo yetu ikiwemo wa STAMICO Mwanza, kuongezeka kwa mauzo ya madini kutoka nje ya nchi yatakayouzwa katika masoko yetu ya madini na kuongeza nafasi za ajira kwa watanzania kuitia uwekezaji.



Picha Na. 9: Watoa mada na washiriki wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliofanyika kuanzia tarehe 21 hadi 23 Februari, 2021 Jijini Dar es Salaam.

(c) Kuendelea Kuwawezesha Wachimbaji Wadogo ili Waweze Kufanya Shughuli zao kwa Tija

32. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Uchimbaji Mdogo katika kuongeza fursa za ajira na uwekezaji kwa watanzania na wageni ili kukuza Pato la Taifa

na kufungamanisha uchumi wa madini na sekta zingine za kiuchumi. Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) Wizara iliongeza kasi ya urasimishaji na uwezeshaji wachimbaji wadogo, ambapo katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, jumla ya leseni 3,540 za uchimbaji mdogo wa madini sawa na asilimia 56 ya leseni zote zilitolewa. Wizara pia ilitoa jumla ya Leseni 1,965 za biashara ndogo za madini; na Leseni 41 za Uchenjuaji wa Madini. Aidha, jumla ya maeneo nane (8) ya uchimbaji wa madini ya vito yaliyopo Mkoani Tanga yalisanyiwa ukaguzi na kutengwa kwa ajili ya kutolewa leseni kwa njia ya zabuni. Vilevile, maeneo mawili (2) katika Mkoa huo yamependekezwa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini ya vito.

(ii) kutoa elimu ya fursa zilizopo katika Sekta ya Madini kwa Taasisi za fedha (NMB, CRDB, TIB na NBC) kwa lengo la kuwashawishi waweze kuwakopesha wachimbaji wadogo na hivyo kuboresha mazingira ya uchimbaji na biashara ya madini ambapo Benki za NMB, CRDB, TIB na benki ya Azania tayari zimeanza kutoa mikopo katika Sekta ya Madini. Aidha, maeneo ambayo ni muhimu kwa uchimbaji na Biashara ya madini yametembelewa kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili. Vilevile, vikao na FEMATA na TAMIDA vimefanyika kwa lengo la kutatua changamoto za biashara ya madini kwa wachimbaji wadogo;

(iii) kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu faida za matumizi ya masoko ya madini yaliyoanzishwa kuititia maonesho mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba ya mwaka 2020 yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jjini Dar es Salaam kuanzia tarehe 01 hadi 13 Julai, 2020 na Maonesho ya Tatu ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika katika Viwanja vya Bombambili mjini Geita kuanzia tarehe 17 hadi 27 Septemba, 2020 pamoja na vyombo vya habari kama vile runinga, magazeti, tovuti, mabango na viperushi na mitandao ya kijamii;

(iv) kutoa mafunzo kwa vitendo na huduma za uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo kuititia vituo vya mfano vya

Lwamgasa, Katente na Itumbi ambapo jumla ya **wachimbaji wadogo864** wamepata mafunzo ya uchimbaji na uchenjuaji salama na biashara ya madini. Aidha, jumla ya **tani 421.6** za mbale zilichenjuliwa na kuzalisha takriban **kilogramu 11.6** za dhahabu katika vituo hivyo. Uzalishaji huo umeiwezesha Serikali kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 104,038,097.73**. Pia, mafunzo ya uchimbaji na uchenjuaji salama wa madini yalitolewa kwa wachimbaji wadogo viziwi waliopo Geita.



Picha Na. 10: Wataalamu kutoka Taasisi ya GST wakitoa elimu juu ya namna bora ya uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogo – Nyamongo – Tarime.

(d) Kuendelea Kusimamia Mfumo wa Ukaguzi wa Shughuli za Migodi na Kukusanya Takwimu za Madini

33. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini Wizara ilitekeleza yafuatayo:

(i) kufanya kaguzi za fedha na kodi kwa Kampuni 13 ambapo imebainika kuwa jumla ya kiasi cha **shilingi 6,202,648,657** kinatakiwa kulipwa na Kampuni hizo kama stahiki za Serikali. Kampuni nane (8) zimekubali kulipa kiasi cha **shilingi 3,589,321,328** ikijumuisha ada ya pango, Mrabaha na Ushuru wa huduma. Majadiliano ya hoja hizo na Kampuni nyingine tano (5) yanaendelea ili kuhakikisha Serikali inapata tozo zake stahiki kwa mujibu wa Sheria;

- (ii) kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi, kukusanya takwimu za madini na kufuatilia maduhuli kwa kuweka Afisa Mgodi Mkazi katika Migodi Mikubwa na ya Kat ikiwemo mgodi wa Geita, North Mara, Bulyanhulu, Buzwagi na Shanta na maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa madini kama Lugoba, Nyarugusu, Mbinga, Handeni na Mahenge. Lengo ni kuhakikisha taarifa sahihi za uzalishaji madini zinapatikana ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato stahiki ya Serikali;
- (iii) kusimamia taarifa za ununuzi na uuzaji kwa kuweka Maafisa ambao wanaratibu biashara ya madini katika Vituo vyote vya Ununuzi na Masoko yote ya madini kwa ajili ya kuwezesha upatikaji wa taarifa sahihi za biashara kwa siku, wiki na mwezi. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni 10(5) ya *the Mining (Minerals and Mineral Concentrates Trading) Regulations 2018* kwa wafanyabiashara wanaopeleka marejesho yao kwa Afisa Madini Wakazi; na
- (iv) kukagua migodi ya wachimbaji wadogo 1,729 katika maeneo yenye shughuli za uchimbaji wa madini nichini katika mikoa ya Geita; Shinyanga; Singida; Ruvuma; Mbeya; Tanga; Morogoro; Pwani; Songwe; na Dodoma. Mapungufu yaliyobainishwa katika ukaguzi huo ni pamoja na kutokuzingatiwa kwa uchimbaji salama na utunzaji wa mazingira; kutokuwepo na wasimamizi migodi wenye uelewa kuhusu uchimbaji madini, uhifadhi wa baruti na uzinamizi wa mazingira na baadhi ya mitambo ya uchenjuaji kutokuwa na vibali stahiki. Baada ya kubaini hayo, wamiliki wa leseni hiso walielekezwa kurekebisha mapungufu yote yaliyobainika.

(e) Kuimarisha na Kuhimiza Uanzishwaji wa Masoko ya Madini na Kuhakikisha Upatikanaji wa Huduma Wezeshi katika Masoko

34. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo, Wizara imefanya kazi zifuatazo:

(i) Kuanzisha soko moja (1) jipya lilitopo Kiteto mkoani Manyara na vituo tisa (9) vya ununuzi wa madini katika maeneo ya Nyang'wale mkoa wa Geita, Segese Wilaya ya Kahama, Ifwenkenya na Mwembeni Mkoa wa Songwe,Masasi Mkoa wa Mtwara, na vituo vya Mbugani, Kiwanja, Mwaoga na Mkola vilivyopo Wilaya ya Chunya. Hii inafanya jumla ya masoko hadi Machi, 2021 kuwa 39 na vituo vya ununuzi 50. Aidha, vifaa maalum vinavyotumika kwa ajili ya utambuzi wa madini, kupima viwango vya madini na kupima uzito vimenunuliwa katika masoko hayo na yale yaliyokuwepo ili kuweka mazingira mazuri ya kibiaшара. Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na: mashine 24 za XRF, seti 15 za vifaa vya utambuzi wa madini ya vito (gemology mobile Kits), mizani 30 na mashine moja (1) ya kupima ubora wa almasi ghafi;



Picha Na. 11: Baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya Masoko ya Madini nchini.

(ii)kuimarisha masoko yote ya madini kwa kuhakikisha upatikaji wa huduma wezeshi ikiwemo benki ili kutoa huduma kwa wafanyabiashara na wachimbaji wa madini kwa uratibu wa Afisa Tawala wa Mkoa; na

(iii) Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa masoko ya madini kwa kuhakikisha uwepo wa wataalamu wanaohitajika katika Masoko. Kwa sasa wataalamu wa madini ya metali wapo katika masoko yote nchini. Aidha, wataalamu wa Vito wapo katika baadhi ya masoko yenye uzalishaji mkubwa wa madini ya vito.

35. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli hizi umeimarisha biashara ya madini nchini na kunufaisha Wachimbaji Wadogo wa madini. Kuanzia kipindi cha **Julai 2020 hadi Machi 2021**, Utendaji kazi wa masoko hayo umeendelea kuimarika ambapo kumekuwa na ongezeko la Maduhuli ya Serikali ambapo kiasi cha Shilingi **93,455,156,963.7901** kilikusanya kama mrabaha na Shilingi **15,762,902,104.1082** kilikusanya kama Ada ya Ukaguzi kutokana na mauzo ya madini kwenye masoko hayo.

36. Mheshimiwa Spika, aidha, uanzishwaji wa masoko ya madini umekuwa na manufaa makubwa ambapo toka kuanzishwa Machi, 2019 hadi Machi, 2021 jumla ya **tani 28.34** za dhahabu; **tani 2,803.97** za madini ya vito; **karati 30,367.44** za madini ya almasi; **tani 259.71** za madini ghafi ya tanzanite, **karati 222,070.40** za tanzanite iliyokatwa na kusanifiwa; **tani 91.20** za madini ya batu na **karati 39,570.40** za madini mengine ya vito yenye thamani ya **shilingi triliuni 3.19** yaliuzwa kuitia masoko hayo na kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 222.07** ikiwa ni malipo ya mrabaha na ada ya ukaguzi.

37. Mheshimiwa Spika, vilevile uwepo wa masoko na vituo vya ununuza wa madini umechangia kuondoa changamoto ya ukosefu wa eneo la kufanya biashara ya madini hususan kwa wachimbaji wadogo na hivyo kuwahakikishia bei stahiki na mazingira salama ya kufanya biashara. Pia masoko yamezesha udhibiti wa utoroshaji wa madini na yameleta manufaa kwa wananchi ikiwemo kuzalisha fursa za ajira na kuongezeka kwa kipato cha wachimbaji wadogo.

(f) Kudhibiti Utoroshwaji na Biashara Haramu ya Madini Nchini

38. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari, 2021 Wizara ilifanya yafuatayo:

(i) imeendelea kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya ukaguzi wa kimkakati katika mikoa ya Manyara, Arusha, Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza, Geita, Kagera,

Shinyanga na Morogoro ili kuhakikisha kuwa madini yote yanafika na kuuzwa kwenye masoko rasmi.

(ii) kuendelea kuimarisha udhibiti wa usafirishaji wa madini katika maeneo ya mipaka ya nchi kama viwanja vya ndege, Bandari na mipakani kwa kufungua ofisi katika maeneo hayo; kuendelea kutumia vibali kama vibali vya kusafirisha madini nje ya nchi, *Kimberley Process Certification* (kutumika kwenye mauzo ya Almasi ghafi) na ICGLR Certification (hutumika kwenye 3T & G (Tin, Tungsten, Tantalum, and Gold)) ambavyo hukaguliwa mipakani kabla ya madini kwenda nje ya nchi; na kuweka mabango katika viwanja vyote vya ndege kuonesha taratibu mbalimbali zinazotakiwa kufuatwa kwa wanaotaka kusafiri na madini nje ya nchi; na

(iii) kufanya kaguzi za mara kwa mara katika mialo ya kuchenjulia madini na kwa wafanyabiashara ya madini ili kuhakiki kama takwimu zilizopo kwenye vitabu vyao vya kumbukumbu zinawiana na taarifa zilizopo kwenye masoko; **39. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti utoroshwaji wa madini katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wizara imeweza kukamata madini yenye jumla ya thamani ya **shilingi 2,797,916,259.83** na **Dola za Marekani 93,306.01**. Kati ya madini hayo, madini yenye thamani ya **shilingi 763,060,715.20** na **Dola za Marekani 33,617.48** yametaifswa na madini yenye thamani ya **shilingi 2,034,855,544.63** na **Dola za Marekani 59,688.53** bado kesi zake zinaendelea mahakamani.

(g) Kuendelea Kuweka Mikakati ya Kuimarisha Soko la Tanzanite na Madini Mengine ya Vito

40. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha soko la madini ya tanzanite na madini mengine ya vito Wizara imefanya yafuatayo:

(i) kuendelea kuimarisha miundombinu na vifaa vya ulinzi katika eneo tengefu la Mirerani kwa kuweka vifaa vya kusaidia ulinzi kama vile kamera, usimikaji wa kangavuke kwa ajili ya kuzalisha umeme wa dharura pindi umeme wa Grid ya Taifa inapopata hitlifu, pamoja na ujenzi wa barabara

ya ndani inayozunguka ukuta, kuongeza vyumba viwili vya upekuzi, njia za watembea kwa miguu na jengo la kupumzikia;



Picha Na. 12: Muonekano wa TV screen katika chumba cha kusimamia kamera zote Mirerani.

(ii) kusimamia shughuli zote za uchimbaji na biashara ya madini ya Tanzanite kwa kuhakikisha inafanyika ndani ya ukuta kupitia jengo la One-stop Centre. Aidha, madini yote yanayopelekwa soko la Arusha na masoko mengine yanaratibowi kwa kibali maalum kutoka kwa Afisa Madini Mkazi kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama; kuandaa na kutoa bei elekezi ya madini ikiwemo madini ya vito kwa kuwashirikisha TAMIDA na FEMATA na kusimamia bei hiyo katika masoko ya madini; na

(iii) kuongeza wataalam wa uthaminishaji madini, ambapo, Wizara ilipeleka masomoni watumishi 10 waliohitimu nchini India kwa lengo la kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa masoko ya madini.

(iv) kuondoa urasimu kwenye utoaji wa vibali vya usafirishaji madini ambapo kwa sasa kibali hutolewa ndani ya kipindi kisichozidi saa moja baada ya nyaraka za maombi kuwasilishwa

41. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa eneo tengefu la Mirerani linawekewa ulinzi thabiti na miundombinu imara kuhakikisha biashara ya madini ya Tanzanite inafanyika ndani ya ukuta. Lengo la uwekezaji huo wa Serikali ni kudhibiti utoroshwaji ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

(h) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

42. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini zinaimarika na kuongeza mchangano wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa, Wizara ilifanya yafuatayo:

- (i) kuendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito ambapo madini ghafi ya vito yenye uzito wa zaidi ya gramu 2 yanaongezewa thamani ndani ya nchi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi;
- (ii) kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya madini ya viwandani yanayotumika katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ambapo kwa sasa uzalishaji wa madini ya chokaa, jasi, udongo mwekundu wenyewe madini ya chuma (red soil) na *Bauxite* yanayotumika kutengeneza *clinker* ambayo inatumika kuzalisha saruji umeongezeka; na
- (iii) kuanza maandalizi ya awali ya mradi wa majaribio wa kuzalisha makaa ya mawe kwa matumizi ya nyumbani (Coal Briquettes) chini ya STAMICO. Kwa kuanzia Shirika litasimika mtambo wenyewe uwezo wa kuzalisha tani 2 kwa saa kufuatia kukamilika kwa majaribio ya awali ambayo yameonesha matokeo chanya. Mradi huo utakuwa katika eneo la TIRDO jijini Dar es Salaam na unatarajiwa kuanza robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021. Shirika limeainisha mtambo unaohitajika sambamba na kutenga fedha za mradi kiasi cha **Shilingi 450,000,000**.

43. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanda viwili (2) vya kusafisha madini (*refinery*) Mkoani Mwanza na Dodoma umekamilika. Kiwanda cha Eyes of Africa Ltd kilichopo Dodoma kina uwezo wa kusafisha kilo 35 za dhahabu kwa siku na kimeanza uzalishaji Machi, 2021. Aidha, kiwanda cha Mwanza Precious Metals Refinery kinachomilikiwa na ubia baina ya STAMICO, Kampuni ya Rozella General Trading ya Dubai na Kampuni ya ACME Consultant Engineers PTE Ltd ya nchini Singapore chenye uwezo wa kusafisha dhahabu kilo 480 kwa siku kwa kiwango cha kimataifa cha **asilimia**

99.9 (999.9 purity) ambacho tayari kimeanza uzalishaji Aprili, 2021. Vilevile, ujenzi wa kiwanda cha *Geita Gold Refinery* Mkoani Geita na Kiwanda cha kuyeyeyusha madini ya Bati cha Tanzaplus Company Limited umekamilika, hali kadhalika kiwanda cha African' Top Minerals Ltd kipo katika hatua ya kusimika mitambo ili ifanyiwe majaribio. Viwanda hivi vipo Wilaya ya Kyerwa, Mkoani Kagera.



Picha Na. 13: Waziri wa Madini akitembelea mtambo wa kusafisha dhahabu wa mjini Mwanza

44. Mheshimiwa Spika, Hatua hii ya ujenzi wa viwanda vya uyeyushaji na usafishaji itawezesha kuongeza thamani ya madini yetu na kuongeza fursa za ajira. Usafishaji wa dhahabu utasaidia kupata madini ambata yaliyopo kwenye mbale husika kama vile madini ya Fedha, Shaba na Palladium ambayo hutumika kama malighafi ya viwanda vingine ikiwemo usonara. Aidha, upatikaji wa dhahabu iliyosafishwa kwa viwango vya Kimataifa itaifanya nchi yetu iweze kununua dhahabu na kuhifadhi katika mfumo wa fedha ambayo itaiimarisha sarafu yetu na kuiongezea nchi uwezo wa kukopesheka. Hatua hii pia itaiwezesha Serikali kuanza kupokea mrabaha kwa dhahabu halisi theluthi moja ya mrabaha utakaotolewa.



Picha Na. 14: Muonekano wa jengo la kiwanda cha kusafisha dhahabu jjini Mwanza

(i) Kuimarisha Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

45. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuzimarisha taasisi zake ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kufanya masuala yafuatayo:

- (i) kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi za Tume ya Madini jjini Dodoma;
- (ii) ununuzi mashine tano (5) za XRF kwa ajili ya masoko na vituo vya ununuzi wa madini ambavyo vimeanzishwa na ambayo yalikuwepo ili kuhakikisha biashara ya madini inafanyika kwa ufanisi na Serikali inapata mapato stahiki;
- (iii) Kuzisimamia taasisi katika kuandaa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 ili kuhakikisha kuwa mipango na bajeti zao zinaakisi vipaumbele vya Wizara katika kufika malengo yanayotarajiwa;
- (iv) Kuzipatia Taasisi jumla ya watumishi 41 ambapo watumishi 27 walipelekwa Tume ya Madini, 13 STAMICO, saba (7) GST, na wanne (4) TGC; na
- (v) ununuzi wa magari sita (6) kwa GST kwa ajili ya shughuli za utafiti. Aidha, Wizara imeendelea kuijengea uwezo GST kwa

kuiwezesha kupata fedha zaidi za kununulia magari mengine manne (4) kwa ajili ya kuimarisha zaidi shughuli za kitafiti, ununuzi wa vifaa mbalimbali nya jiofizikia na maabara.

(j) Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

46. *Mheshimiwa Spika*, kwa kutambuaumuhimu wa rasilimaliwatu katika kuwezesha rasilimali nyingine kutumika kwa tija na kuleta mafanikio katika Sekta zote za uchumi ikiwemo Sekta ya Madini, hadi kufikia Machi, 2021 Wizara imeendelea kuongeza weledi na ufanisi wa utendaji kwa kuwezesha watumishi 13 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali ikiwemo Shahada katika fani za Uhasibu, Uhandisi Migodi, Jiolojia, Mazingira, Ununuzi na Ugavi, TEHAMA, Uchumi wa Madini na Utawala na Utumishi, Stashahada ya Uzamili, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu. Vilevile, Wizara imeweza Watumishi 19 kupata mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utunzaji Kumbukumbu, Usanifu Picha, Utawala na Utumishi, Mfumo wa Ununuzi, Jemolojia, Usafirishaji na Utendaji wa Makatibu Mahsusii.

47. *Mheshimiwa Spika*, aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa makundi mbalimbali kwa watumishi wake kuhusu uandaaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi kwa Taasisi, uandaaji wa bajeti, miongozo ya uandishi wa nyaraka mbalimbali za Serikali, na mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya (induction course).

48. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi Wizara imenunua magari matatu (3) kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali, kompyuta, printa, vichwa nya simu (intercom) kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano ya ndani, runinga, projekta, skana, viti, makabati ya kutunzia kabrasha, mfumo wa biometric kwa ajili ya mahudhurio ambaao hauweki kidole kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya UVIKO - 19, pamoja na vifaa nya afya kama mizani ya kupimia uzito, kifaa cha kupima sukari, vifaa nya kupimia shinikizo la damu, na shajala za ofisi.

IV. Utekelezaji katika Maeneo Mengine **(a) Ukaguzi wa Kimkakati**

49. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Vyombo vyaa Ulinzi na Usalama imeendelea kudhibiti utoroshaji wa madini nchini kwa kufanya operesheni maalum ili kuhakikisha kuwa madini yote yanafika na kuuzwa kwenye masoko rasmi. Hatua hiyo inatarajiwaa kuongeza maduhuli ya Serikali na hatimaye kuiwezesha Sekta ya Madini kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi Machi, 2021 Wizara ilifanya ukaguzi wa kimkakati mikoa ya Manyara, Arusha, Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga na Morogoro ambapo ilifanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya **shilingi 34,139,011,565.15** na **Dola za Marekani 29,509,821.84**. Wahusika wa Madini yaliyokamatwa walifikishwa Mahakamani na hukumu ya utaifishwaji kutolewa.

(b) Uendelezaji na Uboreshaji wa Eneo Tengefu la Mirerani

50. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea kuimarisha ulinzi ndani ya Eneo Tengefu la Mirerani, Wizara imekamilisha usimikaji wa jenereta nne (4) kwa ajili ya kuzalisha umeme wa dharura. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TARURA inaendelea na ujenzi wa barabara kuzunguka eneo lote ndani ya ukuta. Pia, Wizara kupitia Tume ya Madini inaendelea na upanuzi wa eneo la ukaguzi pamoja na eneo la kupumzikia wadau wa madini wakati wakisubiri ukaguzi. Ujenzi wa miundombinu hii unatarajia kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

(c) Ujenzi wa Kituo cha Pamoja katika Mpaka wa Manyovu (Manyovu One Stop Border Post)

51. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutoa ushirikiano katika ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mpaka wa Manyovu Mkoani Kigoma. Lengo la ujenzi wa kituo hicho ni kurahisisha shughuli za kuvuka mipaka ili kuvutia biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Rwanda ambapo Wizara itashiriki katika kudhibiti utoroshaji

wa madini kwa kuweka miundombinu ya ukaguzi wa madini. Miundombinu hiyo ni pamoja na ofisi mbalimbali, maabara na ghala la kuhifadhiya madini ghafi.

(d) Kusimamia Shughuli za Baruti na Utekelezaji wa Sheria ya Baruti.

52. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa baruti katika shughuli za uchimbaji wa madini, Wizara iliendelea kutoa vibali na leseni mbalimbali ikiwemo: leseni moja (1) ya mtambo wa kuzalisha baruti aina ya *emulsion* Mkao wa Mara; Leseni mbili (2) ya kufanya biashara ya baruti; leseni nane (8) za maghala ya kuhifadhiya baruti (explosives magazines); vibali 261 vya kuingiza baruti nchini na vibali sita (6) vya kusafirisha baruti nje ya nchi. Aidha, Wizara iliidhinisha vibali 23 vya kuitisha baruti nchini kwenda nchi nyingine (transit permit). Kutolewa kwa vibali hivyo kumeiwezesha Wizara kukusanya jumla ya **Dola za Marekani 148,700** na **shilingi 8,000,000**.

53. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha usalama wa matumizi na uhifadhi wa baruti kwa kuzingatia Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 na Kanuni zake, Wizara ilifanya ukaguzi wa maghala na stoo za kuhifadhiya baruti na kufuatilia shughuli za matumizi ya baruti katika mikoa ya Mara, Mbeya, Songwe, Tanga na Pwani. Aidha, ukaguzi huo ulihusisha ufuatiliaji wa matumizi haramu ya baruti kwenye shughuli za uvuvi katika mwambao wa Bahari ya Hindi kwenye mikoa ya Pwani na Tanga ambapo ilibainika kuwa kwa sasa matumizi haramu ya baruti katika shughuli za uvuvi yamedhibitiwa kwa kiasi kikubwa. Timu za kaguzi ziliwaelekeza wamiliki wa maghala ya baruti watumie na kutunza baruti kwa kufuata Sheria na Kanuni za baruti ikiwa ni pamoja na kutunza kumbukumbu za uingizaji, utoaji na matumizi ya baruti kwa usahihi na kusafisha mazingira yanayozunguka maghala.

54. Mheshimiwa Spika, ukaguzi pia ulifanyika katika Stoo tano (5) Mkao wa Dodoma, stoo tatu (3) mkoa wa Singida, maghala 15 mkoa wa Mbeya, maghala 15 mkoa wa Songwe

na maghala nane (8) mkoa wa Geita. Wamiliki wa Stoo 4 hizo ni: ESEH Investment Ltd, Mbogo Mining & General Supply Ltd, Umoja Polisi SACOSS and Lwamgasa Gold Mining SACOSS. Timu ya wakaguzi ilibaini kuwa baadhi ya wamiliki wa maghala ya kuhifadhia baruti kutozingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za Baruti kama vile; utunzaji wa baruti na vilipuzi katika ghala moja; kutokuwepo utaratibu wa kutunza kumbukumbu za uingizaji na utoaji wa baruti kwenye maghala; mifumo mibovu ya kutoa maji (drainage system) kutoka kwenye maghala; Uwepo wa nyasi nyingi kuzunguka maeneo ya maghala kwa baadhi ya wamiliki wa maghala ya kuhifadhia baruti.



Picha Na. 15: Moja ya ghala la kuhifadhia baruti

55. Mheshimiwa Spika, kufuatia mapungufu yaliyobainika, Timu ya ukaguzi ilitoa maelekezo yafuatayo: kampuni ya ESEH Investment Ltd kuhakikisha mfumo wa utoaji maji katika ghala la kuhifadhia baruti unajengwa ambapo tayari mfumo huo umeshajengwa; kampuni ya Mbogo Mining & General Supply walielekezwa kufanya usafi mara kwa mara kuzunguka maghala ya kuhifadhia baruti; Umoja Polisi SACCOS pia walielekezwa kufuata taratibu za Sheria ya Baruti juu ya matumizi salama ya baruti kwa kuhakikisha wanakuwa na vielelezo vyote vinavyohitajika katika biashara ya baruti; na kampuni ya Lwamgasa Gold Mining SACCOS ilielekezwa kutenganisha viwashio na baruti zilizokua zimehifadhiwa katika ghala moja na walielekezwa wanunue vilipuzi kulingana na matumizi ya wakati huo ili kuepuka utunzaji usio salama.

(e) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini na Uwajibikaji wa Wamiliki wa leseni za madini kwa jamii

56. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021 Wizara kupitia Tume ya Madini ilipokea na kuchambua jumla ya mipango 113 ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini kutoka kwa wamiliki wa leseni za madini na watoa huduma migodini, ambapo mipango 110 kati ya hiyo ilikidhi vigezo na kuidhinishwa. Aidha, mipango mitatu (3) haikukidhi vigezo na wahusika walielekezwa kufanya maboresho kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

57. Mheshimiwa Spika, Kati ya Kampuni 113 zilizowasilisha na kuidhinishiwa mipango ya Ushirikishwaji wa Watanzania kampuni nne (4) zinamiliki leseni ya uchimbaji mkubwa, nane (8) zinamiliki leseni za uchimbaji wa kati, mbili (2) zinamiliki leseni za uchimbaji mdogo, tano (5) zimeomba leseni za utafutaji wa madini, moja (1) ni ombi la leseni ya uchenjuaji na 93 ni Kampuni za watoa huduma migodini (Contractors and Sub-contractors).



Picha Na. 16: Naibu Waziri wa Madini Prof. Shukrani Manya akizungumza wakati wa Uzinduzi wa ujenzi wa Mgodi Mpya wa Kati wa Singida Gold Mining.

58. Mheshimiwa Spika, Wizara ilikagua na kufuatilia utekelezaji wa ushiriki na umiliki wa wazawa katika shughuli za uchimbaji madini (Local Content) na wajibu wa makampuni katika

kuchangia shughuli za kiuchumi na huduma kwa jamii (CSR). Ugaguzi huo ulihusisha wamiliki wa leseni kubwa na kati za madini za GGM, North Mara, Shanta – Songwe, na Tancoal, ambapo mambo mbali mbali yalikaguliwa kama vile bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na watanzania au kampuni za kitanzania (Supply of goods and services), Uwiano wa ajira kati ya watanzania na wageni, uwiano wa mishahara kati ya watanzania na wageni, Mafunzo na Uhuishaji wa teknolojia (Training and technology transfer) pamoja na uwajibikaji wa migodi kwa jamii inayozunguka Migodi (CSR). Aidha, katika kaguzi hizo ilibainika kuwa wamiliki wa leseni wamekuwa wakiwahusisha watanzania katika fursa mbalimbali za uchimbaji madini, ambapo karibia asilimia 90 ya ajira katika migodi hiyo ni watanzania: mathalani mgodi wa New Luika (Shanta) wa mkoani Songwe ni mgodi unaongoza kwa kuwa na wafanyakazi 761 sawa na asilimia 100 ya waajirliwa watanzania wanaofanya kazi katika mgodi huo. Vilevile katika Mgodi wa TANCOAL kwa asilimia 95 umekuwa ukitumia bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na watanzania au kampuni za kitanzania.

59. Mheshimiwa Spika, Wajibu wa Makampuni kwa Jamii zinazozunguka migodi (CSR) umekuwa wa tija ili kuwawezesha wananchi kiuchumi, ambapo makampuni yamekuwa yakitenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya jamii zinazowazunguka. Wizara ilibaini kuwa Mgodi wa GGM unaongoza kwa kuchangia jamii, ambapo kwa mwaka 2020/2021 GGM imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.1 kwa halmashauri ya mji wa Geita na imeshiriki katika ujenzi wa kituo cha uwekezaji cha EPZA na Soko la Katundu liliilo gharimu shilingi billioni moja, ambayo yamekuwa na tija kwa wananchi wa Geita. Aidha, barabara kutoka mgodi wa Bulyanhulu kwenda Geita iko kwenye mchakato wa kujengwa kwa kutumia fedha za CSR ambazo kampuni ya Barrick iliahidi kuzitoa kupitia makubaliano yake na Serikali (Framework Agreement).

60. Mheshimiwa Spika, Kufuatia ufuutiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya LC & CSR, ilibainika uwepo wa changamoto mbalimbali kama vile: kukosekana kwa watanzania wenye

weledi katika baadhi ya fani zinazohitajika migodini, ukosefu wa weledi wa kutosha kuendesha na kutumia fursa za biashara zilizopo migodini, ukosefu wa mitaji kuweza kutimia fursa za biashara zilizopo migodini, pamoja na uelewa mdogo wa watanzania juu ya fursa za biashara zilizoanishwa na Sheria ya Madini kwa lengo la kuwezesha watanzania kwenye Sekta ya Madini. Sambamba na hayo baadhi ya miradi ya CSR kutokuwa na ubora ukilinganisha na fedha zilizotumika na uwepo wa migongano katika usimamizi wa miradi.

61. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeshughulikia changamoto hizo kwa kuwataka wamiliki wa leseni kuandaa mpango wa mwaka wa urithishwaji (Succession Plan), ili kupata wazawa wenye weledi kwa baadhi ya fani zinazohitajika migodini. Sambamba na hilo Wizara imewakutanisha wazawa na taasisi za fedha zitakazowawezesha kupata mitaji, ili waweze kutumia fursa za biashara zilizopo migodini. Aidha Wizara imeendelea kutoa elimu kupitia makongamano, mikutano na warsha mbalimbali itakayowajengea uwezo wadau mbalimbali waweze kujua fursa za biashara zilizopo katika Sekta ya Madini. Kwa ujumla kaguzi za mara kwa mara zimekuwa zikitekelezwa na Wizara ili kujiridhisha juu ya utekelezaji wa mipango iliyokubaliwa na jamii zinazo zunguka migodi, pamoja na kutathmini juu ya thamani halisi ya miradi iliyofanyika.

(f) Kufuatilia Masuala ya Usalama Migodini na Utunzaji wa Mazingira

62. *Mheshimiwa Spika*, shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini huambatana na athari za usalama, afya na uharibifu wa mazingira. Ili kuhakikisha shughuli za madini zinakuwa na tija na athari zake zinadhibitiwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021 Wizara kupitia Tume ya Madini ilifanya yafuatayo: kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na utunzaji wa mazingira katika migodi mikubwa sita (6) ya Bulyanhulu, Buzwagi, WDL, Stamigold, Mantra na North Mara; migodi ya kati 12 ikiwemo: Tancoal Energy, Shanta Songwe, Cata Mining Co. Ltd, Ruvuma Coal, MMG, Mara Mine Development Ltd, ZEM (T) Co. Ltd, Busolwa

Mine - Nyarugusu na ZEM Development Ltd. Vilevile, migodi midogo 1,500 na mitambo miwili (2) ya uchenjuaji wa dhahabu ilikaguliwa na kufuatiliwa. Aidha, migodi mikubwa mitatu (3) ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara imekamilisha taratibu za kuweka hati fungani za mazingira na mgodi wa Geita Gold mine upo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu zinazohusika na uwekaji wa hati hiyo kama dhamana ya utunzaji wa mazingira.

63. *Mheshimiwa Spika*, pia Wizara kupitia Tume ya Madini imefanya kaguzi za kiufundi kuhusu usanifu wa ujenzi na matumizi ya mabwawa ya kuhifadhi topesumu kwenye migodi nane (8) ya Bulyanhulu, MMG, RZ Union mining, New Luika Gold Mine (Shanta), Canaco Mining, El Hilal Minerals, Busolwa Mine - Nyarugusu na Busolwa Mine – Ishokela. Aidha, kati ya vibali nane (8) vilivyoombwa vibali saba (7) vilitolewa kwa ajili ya ujenzi na matumizi ya mabwawa hayo isipokuwa kwa mgodi wa Shanta Songwe, ambapo wanaendelea kufanya tafiti za kisayansi kubaini njia bora na salama za kuongeza ukubwa wa bwawa hilo.

(g) Uboreshaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo katika Sekta ya Madini

64. *Mheshimiwa Spika*, ili kusimamia ushiriki wa nchi katika umiliki wa hisa za Serikali, Wizara imetunga Kanuni za Madini (Ushiriki wa Serikali), 2020 Tangazo la Serikali Na. 939 la tarehe 30 Oktoba, 2020 (The Mining (State Participation) Regulations, 2020 GN. 939 of 30 October, 2020). Kanuni hizi zinalenga kusimamia utekelezaji wa umiliki wa Hisa za Serikali zisizopungua asilimia 16 katika Kampuni za madini zinazomiliki Leseni za Uchimbaji wa Kati na Mkubwa wa Madini kama ambavyo umebainishwa katika Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini, Sura ya 123. Kanuni hizi zimeweka utaratibu wa kufuata utakaowezesha Serikali kumiliki hisa katika mitaji ya kampuni hizo kwa kuzingatia viwango vya uwekezaji, mamlaka ya kusimamia hisa za Serikali, utaratibu wa ulipaji wa faida inayotokana na hisa za Serikali, haki za Serikali kama mwanahisa na kwamba hisa za Serikali kwa kampuni zitakuwepo kwa kipindi chote cha uhai wa leseni.

65. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imefanya Marekebisho ya Kanuni za Madini (Haki Madini), 2018 Tangazo la Serikali Na. 1 la Mwaka 2018 (The Mining (Mineral Rights) Regulations, 2018 GN No. 1 of 2018) kwa kuainisha utaratibu na masharti ya Leseni za Uchimbaji wa Kati na Mkubwa wa Madini. Marekebisho hayo yamefanyika kwenye Kanuni za Madini (Haki Madini), 2020 Tangazo la Serikali Na. 937 la tarehe 23 Oktoba, 2020 (The Mining (Mineral Rights) (Amendments) Regulations, 2020 GN. No. 937 of 23 October, 2020) ili kuingiza maudhui ya Leseni za Uchimbaji wa Kati na Mkubwa katika Kanuni hizo.

(h) Kuelimisha Umma Kuhusu Sekta ya Madini

66. Mheshimiwa Spika, Viongozi wakuu wa Wizara na Taasisi walishiriki katika Vipindi na mahojiano mbalimbali na vyombo vya habari illi kuwezesha umma kuhabarishwa kuhusu masuala yanayohusu Sekta ya Madini. Elimu iliyotolewa ilihusisha masuala anuai ikiwemo fafanuzi mbalimbali kutolewa kwa Umma kuhusu Sekta ya Madini ikiwemo: Sheria ya Madini, Wajibu wa Kampuni za Madini kwa jamii (CSR), Ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content), Leseni za Madini, Masoko ya Madini, uwekezaji, na Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira.



Picha Na. 17: *Mheshimiwa Prof. Shukrani E. Manya, Naibu Waziri wa Madini, akiwa katika mahojiano na kituo cha runinga Channel Ten.*

(i)Masuala Mtambuka

67. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWIwaliojitokeza kwa kutoa fedha kwa ajili ya lishe bora, madawa na vifaa kinga ilikuimarisha afya zao. Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuhusu kudhibiti Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY)kwa watumishi na upimaji wa hiari umekua ukifanyika mara kwa mara. Aidha,mabonanza ya michezo mbalimbali yamekuwa yakifanyika kwa lengo la kuboresha afya za watumishi nakuimarisha ushirikiano mahali pa kazi. Vilevile, Wizara imeendelea kuelekeza watumishi kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam wa afya kuhusu jinsi ya kujikinga na maambukizi mapya ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO -19).

V. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

68. Mheshimiwa Spika, Wizara ilipangiwa kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara imepokea fedha za maendeleo jumla ya **shilingi 1,764,627,046.27** sawa na **asilimia 27.68** ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi cha miezi tisa (9) ambazo ni **shilingi 6,375,000,000**. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuzunguka ukuta ndani ya migodi ya Eneo Tengefu la Mirerani, ununuzi wa vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na ununuzi wa magari manne (4) kwa ajili ya shughuli za utafiti wa madini. Aidha, fedha hizo zilitumika kuendelea na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya umahiri vya Songea, Chunya na Mpanda.

VI. Kazi Nyingine Zilizotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

69. Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia taasisi tano (5) ambazo ni: Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Taasisi ya Uhamashajii Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) na Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC).

1) Tume ya Madini

70. Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelawa na Tume ya Madini kwa mwaka 2020/2021 ni pamoja na: kuimarisha Usimamizi wa Sekta ya Madini na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuimarisha ukaguzi wa usalama, afya, na utunzaji wa mazingira katika shughuli za madini; kufuatilia uzalishaji wa madini katika migodi Midogo, ya Kati na Mikubwa; kusimamia ushiriki wa watanzania katika Sekta ya Madini; kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi; na kuelimisha Umma na kuboresha mawasiliano kati ya Tume na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya Madini.

(i)Uzalishaji Madini na Ukusanyaji wa Maduhuli

71. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini imeendelea kuimarisha usimamizi wa uzalishaji wa madini katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa kipindi kinachoanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya **Kilogramu 42,084.76** za dhahabu zenyet thamani ya **shilingi 5,337,395,790,264.35** zilizalishwa na Migodi Mikubwa, Migodi ya Kati na Migodi Midogo. Aidha, **Kilogramu 12,650.24** sawa na **asilimia 30.05** za dhahabu zenyet thamani ya **shilingi 1,587,698,305,067.90** zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa madini nchini. Pia Jumla ya **kilogramu 38,561.21** za madini mengine ya metaliki yenye thamani ya **shilingi 28,194,495,600.97** na **Tani 7,612.06** za makinikiaya shaba yenye thamani ya **shilingi 149,791,154,705.97** zilizalishwa na kuuzwa.

72. Mheshimiwa Spika, katika kipindi rejewa Wachimbaji Wadogo wa madini ya Tanzanite walizalisha na kuuza **Kilogramu 5,964.82** za Tanzanite ghafi, **Karati 111,054.33** za Tanzanite iliyokatwa na kusanifiwana **Kilogramu 52,657.06** za Tanzanite yenye ubora wa chini (magonga). Aidha, katika kipindi hicho jumla ya **Karati 45,022.85** za madini ya almasi zilizalishwa na kuuzwa ambapo kiasi cha **Karati 30,448.97** zilizalishwa na Mgodi wa Almasi wa Mwadui (WDL) na **Karati 14,573.88** sawa na **asilimia 32.36** zilizalishwana Wachimbaji Wadogo. Pia, madini mengine ya vito kiasi cha **tani 15,587.53** kilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

73. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini ya viwandani hususan makaa ya mawe, jumla ya **tani 563,887.95** zilizalishwa kwenye Migodi mbalimbali ya madini hayo nchini na kuuzwa. Kati ya hizo, **tani 560,022.28** zilizalishwa katika Migodi ya Ruvuma Coal Ltd, Tancoal Ltd, Godmwanga Gems Ltd na wachimbaji wadogo mkoani Ruvuma; **tani 1,202.93** mkoani Songwe; **tani 762.83** katika migodi iliyopo Mkoani Rukwa; **tani 1,679.01** kutoka katika migodi iliyopo Mkoani Njombena **tani 220.90** kutoka Mkoani Tanga. Aidha, katika kipindi tajwa jumla ya **tani 17,971,504.00** za madini ya ujenzi na **tani 8,279,564.68** za madini mengine ya viwandani zilizalishwa ambapo thamani ya madini hayo ni **shilingi 610,964,652,907.55**

74. Mheshimiwa Spika, uzalishaji huo umechangia jumla ya makusanyo ya **shilingi bilioni 445.18** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 ambapo ni sawa na **asilimia 84.52** ya lengo la mwaka la **shilingi bilioni 526.72** ambayo yametokana namrabaha, ada ya ukaguzi, ada ya mwaka, ada za jiolojia; adhabu mbalimbali; na mapato mengineyo.

(ii) Usimamizi wa Masoko ya Madini Nchini

75. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi 2021, jumla ya **Kilogram 12,529.83** za dhahabu; **Karati 11,605.35** za madini ya almasi; **tani 221.56** za madini ghafi ya Tanzanite, **Karati 109,907.39** za Tanzanite zilizokatwa na kusanifiwa; **tani 67.48** za madini ya bati; **tani 1,207.22** za madini ghafi ya vito na **Karati 22,519.13** za madini ya vito yaliyokatwa na kusanifiwa yaliuzwa kupitia masoko hayo na kuipatia Serikali jumla ya **shilingi bilioni 109.22**.

(iii) Huduma za Maabara

76. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini pia ina jukumu la ukaguzi wa ubora na kiasi cha madini yaliyozalishwa pamoja na kuchunguza sampuli za madini yaliyozalishwa na wachimbaji Wakubwa, wa Kati na Wadogo. Majukumu hayo yanatekelezwa kwa kupitia maabara yake iliyoko jijini Dar es Salaam.

77. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Tume ya Madini imefanya uchunguzi wa sampuli 532 za mikuo ya dhahabu kutoka migodi mikubwa na kuripoti ubora na kiasi cha madini kilichomo. Zoezi hilo lilikwenda sambamba na uchunguzi wa sampuli 74 za makinikia ya shaba ambapo sampuli 55 ni kutoka Migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi na sampuli 19 kutoka Katavi Mining Ltd ya Katavi. Taarifa za uchunguzi huo zilitumika kukokotoa mapato ya Serikali.

78. Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tume ya Madini imeanzisha dawati maalum la kufanya ulinganisho wa mrabaha na ada ya ukaguzi ili kujiridhisha na kiasi cha mapato kinachostahili kulipwa na kilicholipwa. Ulinganisho huu unafanyika baada ya kupata matokeo ya uchunguzi wa sampuli na mapato ya mauzo ya mwisho yaliyofanyika ikilinganishwa na malipo ya awali. Kazi hiyo inafanyika kwa migodi mikubwa ya Bulyahulu, Buzwagi, North Mara, Geita na New Luika. Aidha, Tume ya Madini imeendelea kuimarisha maabara yake kwa kusimika mifumo kulingana na matakwa ya ISO/IEC 17025 ili kupata ithibati na kutambulika kimataifa.

(iv) Ukaguzi wa Fedha, Kodi na Ushirikishwaji wa Watanzania

79. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Tume ya Madini ilifanya ukaguzi wa masuala ya fedha, mapitio ya kodi na ushirikishwaji wa Watanzania kwenye kampuni 21 zinazojihusisha na uchimbaji wa madini. Madhumuni ya ukaguzi ni kuhakiki iwapo kampuni hizo zinalipa stahiki zote za Serikali na zinafuata Sheria katika masuala ya fedha, kodi na ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini.

80. Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo ulibaini yafuatayo: baadhi ya Kampuni kutolipa kiwango stahiki cha mrabaha, ada ya ukaguzi, ushuru wa huduma; kutolipa ada ya pango la leseni; na kutofuata matakwa ya Sheria na Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania pamoja na matakwa ya Sheria ya uwajibikaji wa makampuni kwa jamii. Aidha, kaguzi zilibaini kuwa jumla

ya kiasi cha **shilingi 6,513,645,762** kinatakiwa kulipwa na kampuni hizo.



Picha Na. 18: Wataalam wa Mifumo ya Fedha wakifanya Ukaguzi wa Fedha katika Migodi

(v)Utoaji wa leseni za Madini

81. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Tume ya Madini ilitoa jumla ya leseni 6,314 ikilinganishwa na leseni 5,935 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2019/2020 katika mchanganuo ufuatao: Leseni 10 za Uchimbaji wa Kati wa Madini (ML); 114 za Utafutaji wa Madini (PL); 3,540 za Uchimbaji Mdogo wa Madini (PML); moja (1) ya Uyeyushaji wa Madini (SL), 41 za Uchenjuaji wa Madini (PCL); Leseni Kubwa za Biashara ya Madini 643 (DL); na Leseni Ndogo za Biashara ya Madini 1,965 (BL). Pia, jumla ya maeneo nane (8) ya uchimbaji wa madini ya vito yaliyopo Mkoani Tanga yalifanyiwa ukaguzi na kutengwa kwa ajili ya kutolewa leseni kwa njia ya zabuni. Maeneo mawili (2) yamependekezwa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini ya vito.

82. Mheshimiwa Spika, kati ya leseni zote zilizotolewa, leseni 3,540 sawa na **asilimia 56** zilikuwa za uchimbaji mdogo. Hatua hii inaonesha kuwa pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji mkubwa kutoka nje, Serikali imeendelea kuwajali Watanzania kwa kuhakikisha kuwa wanahusishwa kikamilifu katika shughuli za kukuza uchumi wa Taifa.

(vi) Ukaguzi wa Viwanda vya Uyeyushaji (*Smelter Plant*)

83. Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachorejewa mtambo maalum wa uyeyushaji wa Madini ya shaba uliopo Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani ulifanyiwa ukaguzi. Lengo la ukaguzi huo ilikuwa ni kutathmini uwezo wa mtambo huo katika kuhakikisha Mradi unakidhi Sheria na taratibu za nchi. Ukaguzi huu ulibaini kwamba ujenzi wa mtambo umekamilika na una uwezo wa kuyeyusha **tani 20,000** za shaba kwa mwezi. Kwa sasa wamiliki wameshapewa leseni na wanaendelea na uyeyushaji ambapo hadi sasa tani 20 zenye thamani ya **shilingi 153,418,938** yalizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi na kuipatia Serikali mapato ya **shilingi 10,739,326.45** kutokana na mrabaha na ada ya ukaguzi.

(vii)Ukaguzi wa Migodi, Mazingira na Baruti

84. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini imefanya ukaguzi kwenye maghala ya kuhifadhi baruti katika mikoa ya Morogoro; Geita; Mbeya; Songwe; Ruvuma; Shinyanga; Mara; na Dodoma. Ukaguzi huo ulibaini mapungufu yafuatayo kwa baadhi ya wamiliki wa maghala: utunzaji usio salama wa baruti na vilipuzi katika ghalaj moja; kutotunza kumbukumbu sahihi za uingizaji na matumizi ya baruti na kutokuwa na watu wenye sifa na uelewa katika masuala ya utunzaji na usimamizi wa baruti. Wamiliki wa maghala na stoo yaliyobainika kuwa na mapungufu walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo. Aidha, hati za makosa zilitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 na Kanuni zake za mwaka 1964.

85. Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine, Tume pia ina jukumu la kuhakikisha mazingira yanabaki salama baada ya kukamilika kwa shughuli za uchimbaji. Katika kutekeleza hilo, Tume ya Madini ilichambua Mipango ya Ufungaji migodi kutoka kwenye migodi ya GGM, North Mara, Buzwagi, Bulyanhulu, Shanta, WDL, Twiga Portland Cement na Tanga Cement. Kati ya hiyo, mipango ya migodi ya GGM na Shanta illidhinishwa ambapo majadiliano ya kuweka Hati Fungani (*Rehabilitation Bond*) yanaendelea. Aidha, migodi ya Buzwagi Bulyamhulu, North Mara, Twiga Portland cement na Tanga Cement walielekezwa kurekebisha mipango yao.



Picha Na. 19: Makatibu Wakuu na wataalam walipotembelea mlgodi ya Mlerani

(viii)Kusogeza Huduma Karibu na Umma

86. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2021 Tume ya Madini imeanzisha jumla ya Ofisi 28 za Maafisa Madini Wakazi (RMOS) katika Mikoa yote nchini na Ofisi 13 za Maafisa Migodi Wakazi (MROS) ili kusogeza huduma karibu na Wananchi. Hivyo, nitoe wito kwa Wadau wa Sekta ya Madini nchini kuzitumia ipasavyo Ofisi hizo ili kuwa na uchimbaji salama unaozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu stahiki na kuепusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

2) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

87. Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) lilianzishwa kwa lengo la kuendeleza rasilimali madini kwa niaba ya Serikali. Majukumu makuu ya STAMICO ni pamoja na: kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati ya utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani madini; kutoa huduma za kibashara za uchorongaji wa miamba na utafutaji wa madini; ushauri wa kijiolojia, kihandisi na kimazingira pamoja na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wachimbaji.

88. Mheshimiwa Spika, nafurahi kukutaarifu kuwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Shirika limefanikiwa kukusanya kiasi cha **shilingi 11,235,837,822** sawa na **asilimia 77** ya lengo kwa kipindi husika ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 5,870,450,257.89** kwa kipindi kama hiki mwaka uliopita. Vilevile, utegemezi wa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake umepungua kutoka **asilimia 89** ya Mwaka 2018/2019 hadi **asilimia 16.6** kwa mwaka 2021/2022. Pamoja na mafanikio hayo, Wizara inaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa Shirika linaongeza ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi kutoka Serikalini.

89. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuimarika na kuungeza mchango wake Serikalini. Kutokana na Mapato yake katika shughuli za uwekezaji na utoaji huduma katika Sekta ya Madini Shirika liliweza kutoa mchango wa **shilingi billioni 1.1** Agosti 2020 Serikalini. Aidha, kwa 2019/20 Shirika lilitoa kiasi cha **shilingi billioni 1.0**



Picha Na.20 Mwenyekiti wa Bodl ya STAMICO Jen Mstaafu Michael Isamuhyo akimkabidhi aliekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati John Pombe Magufuli mfano wa Hundu ya Mchango wa Shirika

Utekelezaji wa Shughuli za Shirika

90. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Shirika limeendelea kutekeleza shughuli ambazo zinahusisha kuwekeza katika utafiti, uchimbaji, uongezaji thamani na uuzaaji wa madini kupitia miradi, kampuni tanzu na kampuni za Ubia. Aidha, Shirika limeendelea kutoa

huduma za kibiashara katika Sekta ya Madini zinazohusisha uchorongaji na kutoa huduma za kitaalamu na mafunzo kwa wachimbaji wadogo.

Miradi Inayomilikiwa na Shirika

a) Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo - Kiwira

91. *Mheshimiwa Spika*, uchimbaji wa Makaa ya mawe umeendelea katika leseni ya Shirika eneo la Kabulo -Kiwira mkoa wa Songwe. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, makaa ya mawe yaliyouzwa ni tani 11,346 zikijumuisha tani 6,369.2 za kiasi kilichochimbwa hadi Machi, 2021 na tani 4,978.8 ya kiasi cha bakaa ya mwaka wa fedha 2019/2020. Jumla ya thamani makaa yote ni **shilingi 979,385,448**. Kutokana na mauzo hayo Shirika liliweza kulipa jumla ya **shilingi 42,113,574** kama malipo ya mrabaha, ada ya ukaguzi na tozo ya huduma. Vilevile, Shirika linaendelea kutafuta wateja wapya wa makaa linayozalisha ili kuongeza mapato yatokanayo na mauzo ya makaa ya mawe.



Picha Na. 21. Uchimbaji na Upakiaji wa makaa ya mawe ukiendelea Kabulo

92. *Mheshimiwa Spika*, Shirika kwa kushirikiana na TANESCO limeandaa Rasimu ya Makubaliano ya Awali (MoU) ya kuendeleza mradi wa uzalishaji umeme wa Kiwira wa zaidi ya Megawatts200. Katika makubaliano hayo, Shirika litakuwa na jukumu la kuchimba makaa ya mawe na TANESCO itakuwa na jukumu la kujenga na kuendesha mtambo wa kuzalisha umeme.

b) Kampuni Tanzu na Miradi ya Ubia
(i) Mgodi wa Dhahabu wa STAMIGOLD

93. Mheshimiwa Spika, Mgodi wa STAMIGOLD umeendelea kufanya utafiti katika leseni yake na kuthibitisha uwepo wa tani **1,556,039** za mashapo ya dhahabu yenge **kiwango cha 1.23 g/t** ambazo ni sawa na **wakia 61,324** za dhahabu zinazotarajia kuchimbwa kwa miaka mitatu na nusu. Aidha, mgodi umeendelea na uzalishaji ambapo kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi February, 2021 mgodi umefanikiwa kuzalisha na kuuza jumla ya **wakia za dhahabu 8,683.34** na **wakia zamadini ya fedha 1,544.53** vyote vikiwa na thamani ya jumla **Shilingi 37,514,949,249.91** na kulipa Serikali jumla ya **Shilingi 2,738,591,294.77** kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma.



Picha Na. 22: Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Prof. Simon Msanjila alipotembelea mgodi wa STAMIGOLD.

94. Mheshimiwa Spika, mgodi wa STAMIGOLD unakabiliwa na changamoto ya gharama kubwa za uzalishaji zinazochangiwa na matumizi ya kangavuke katika kuzalisha umeme kutokana na kukosekana kwa umeme wa Gridi ya Taifa. Ili kutatua changamoto hiyo, Wizara kwa kushirikiana na TANESCO imeendelea na jitihada za kuunganisha umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa ambapo tayari kazi ya ujenzi wa njia ya umeme imekamilika. Ujenzi wa kituo cha kupokelea umeme (sub station) unaendele na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwaka wa fedha kuisha. Kupatikana kwa umeme

wa uhakika katika Mgodi huu kutapunguza gharama za uzalishaji kwa zaidi ya **shilingi milioni 700** kwa mwezi. Pamoja na changamoto zilizopo STAMIGOLD imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi na kuweza kupata hati safi ya ukaguzi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 kama ilivyokuwa kwa Kampuni mama ya STAMICO

(ii) Kiwanda cha Kusafisha dhahabu, Mwanza

95. Mheshimiwa Spika, STAMICO kwa kushirikina na Kampuni za Rozzela ya Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai) na ACME Consultant Engineers PTE ya Singapore, kwa pamoja zimeunda Kampuni ya ubia ya **Mwanza Precious Metal Refinery(MPMR)**. Kampuni hiyo ya ubia imekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kusafisha



Picha Na. 23: Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua kiwanda cha kusafisha madini ya dhahabu cha Mwanza Precious metals.

96. Mheshimiwa Spika, kujengwa kwa kiwanda hiki kitaiongezea Serikali mapato kupitia mrabaha na kodi mbalimbali pamoja na kutoa ajira mbalimbali kwa watanzania. Kupitia kiwanda hiki, dhahabu inayozalishwa Tanzania itatambulika kimataifa na kuwa na nembo yake maalum (**originality mark**). Aidha, Benki Kuu ya Tanzania itawenza kununua dhahabu kama Sheria ya nchi inavyoelekeza.

97. Mheshimiwa Spika, ili kukiwezesha kiwanda kupata malighafi ya kutosha, Shirika limeainisha maeneo ya

upatikanaji wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo nchini. Kadhalika, kiwanda kinatarajia kupokea dhahabu kutoka kwa wachimbaji wakubwa, wa kati na vyanzo vingine kutoka ndani na nje ya nchi.

(iii) Mradi wa Dhahabu wa Buhemba

98. Mheshimiwa Spika, Shirika kwa kushirikiana na Kampuni ya Ubia ya Goodfield DMC ya Dubai imeunda Kampuni ya ubia ya **Buhemba Gold Company** kwa ajili ya kuendeleza mradi wa uchimbaji dhahabu wa Buhemba uliopo Butiama mkoa wa Mara. Jumla ya **tanimilioni 5.12** za mashapo ya dhahabu yenye **kiwango cha 2.5g/t** sawa na **wakia 600,000** za dhahabu ambazo zinazotarajia kuchimbwa kwa miaka mitano (5). Mradi huu unatarajiwa kuanza Septemba, 2021.

99. Mheshimiwa Spika, shughuli zillzotekelawa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mgodi na TANESCO imeshaanza kuunganisha umeme katika eneo la mgodi. Uanzishwaji wa mgodi huu utakuwa na manufaa kwa Taifa letu kupitia malipo ya mrabaha, ada ya ukaguzi, ushuru wa huduma, kodi na tozo nyingine, fursa za biashara, ajira na kuboreshwa kwa huduma za jamii kupitia miradi ya CSR.

(iv) Mradi wa Buckreef

100. Mheshimiwa Spika, nafurahi kukutaarifu kuwa STAMICO na Mbia mwenza Kampuni ya TANZAM 2000 ambao kwa pamoja wanamiliki kampuni ya dhahabu ya Buckreef wamekubaliana kuendeleza mgodi wa Buckreef. Mradi huu una jumla ya **tani milioni 37.38** za mashapo ya dhahabu yenye **kiwango cha 1.35 g/t** sawa na **wakia 1,619,332.42** za dhahabu ambazo zinatarajia kuchimbwa kwa miaka 18. Aidha, katika kipindi husika mgodi umesimika mtambo wa majaribio ambao unaendelea na uzalishaji. Katika kipindi husika uchenjuaji wa tani 5 za mbale zenye jumla ya **wakia 885,523.20** za dhahabu zilipatikana zenye thamani ya **shilingi 3,996,662,374**. Kupitia mapato hayo, mgodi uliweza kulipa mrabaha, tozo ya huduma na ada ya ukaguzi zenye jumla ya **shilingi 291,756,353**.

101. Mheshimiwa Spika, lengo la mtambo huu ni kufanya majaribio ya uchenjuaji wa mashapo ya *Oxide* kwa kutumia *Carbon in Leach* (CIL) kabla ya ujenzi wa mtambo mkubwa wa kuchenjua tani 40 kwa saa. Maandalizi ya kununua mtambo huo yameshaanza baada ya kupatikana fedha za kuendesha mradi huo.

c) **Miradi Mingine Inayotekelawa na Shirika (i) M r a d i wa Makaa ya Kupikia - Coal Briquettes**

102. Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika Shirika limeanza maandalizi ya awali ya mradi wa kuzalisha makaa ya mawe kwa matumizi ya nyumbani (Coal Briquettes) kwa kuanza na mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani mbili (2) kwa saa kufuatia kukamilika kwa majaribio ya awali ambayo yameonesha matokeo chanya. Mradi huu wa majaribio utakuwa katika eneo la TIRDO jijini Dar es Salaam na unatarajiwu kuanza robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, Shirika limeainisha mahitaji ya mtambo unaohitajika sambamba na kutenga fedha za mradi kiasi cha **Shilingi milioni 450**.

(ii) **Mradi wa Kokoto Chigongwe**

103. Mheshimiwa Spika, Shirika limefanikiwa kukamilisha utafiti na kuanza maandalizi ya mradi wa kokoto katika eneo la Chigongwe mkoa wa Dodoma kwa kuanza ulipuaji wa jumla ya **tani 52** za mawe. Shirika limepanga kuanza na mradi wa majaribio utakaogharimu kiasi cha **Shilingi milioni 112** kwa kutumiamtambo wenye uwezo wa kusaga **tani 55** kwa saa unaotarajia kuanza katika robo ya nne ya mwaka wa Fedha 2020/2021. Aidha, mradi huu utakapoanza uzalishaji mkubwa utapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya upatikanaji wa kokoto kwa ajili ya ujenzi wa makazi na miundombinu mbalimbali katika Jiji la Dodoma na mikoa ya jirani.

d) **Huduma Zitolewazo na Shirika (i) Huduma ya Kibiashara ya Uchorongaji**

104. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea na Kandarasi ya uchorongaji katika maeneo mawili (2) kwa sasa ambayo ni

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mgodi wa GGM na eneo la kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi (Tanzania Geothermal Development Company - TGDC) mkoani Mbeya. Uchorongaji katika Mgodi wa GGM unahusisha kuchoronga jumla ya **mita 15,000** zenyetamani ya **shilingi bilioni nane (8)** na uchorongaji wa **mita 900** zenyetamani ya **shilingibilion 1.1** katika kampuni ya TGDC unahusisha utafutaji wa jotoardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme na tayari utekelezaji umeanza.



Picha Na. 24: Utiaji Saini wa mkataba wa Uchorongaji kati ya STAMICO na TGDC

105. Mheshimiwa Spika, ili kujimarisha katika biashara ya uchorongaji, Shirika limefanikiwa kununua mitambo mitatu (3) mipy ya kisasa yenye thamani ya **Shilingi bilioni 5.4**. Mitambo hiyo imenunuliwa kutokana na mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Shirika. Vilevile, Shirika limepanga kununua mitambo mingine miwili (2) mipy kutoka katika vyanzo vyake vya ndani katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 na tayari taratibu za ununuvi zimeanza.



Picha Na. 25: Prof. Simon S. Msanjila, Katibu Mkuu Wizara ya Madini (wa pili kulia) akiwa pamoja na Dkt. Venance Mwase, Kaimu Mtendaji Mkuu wa STAMICO (wa kwanza kulia) katika uzinduzi wa mitambo mitatu mipy ya uchorongaji

(ii) Kuwezesha na Kuhamasisha Shughuli za Uchimbaji Mdogo wa Madini Nchini

106. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuwezesha na kuhamasisha shughuli za uchimbaji mdogo kwa kutoa huduma za kitaalamu kwa wachimbaji wadogo katika nyanja za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini, biashara ya madini pamoja na utunzaji wa mazingira. Shirika limeendelea kutekeleza wajibu wake wa kulea wachimbaji wadogo ili kufikia uchimbaji madini wa kati.

107. Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa Vituo vya Mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi, jumla ya **wachimbaji wadogo 864** wameweza kupata mafunzo kwenye nyanja za uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini katika vituo hivyo. Aidha, jumla ya **tani 421.6** za mbale za dhahabu zilliweza kuchenjuliwa katika vituo hivyo na kuzalisha takribani **kilogramu 11.6** za dhahabu ambapo Serikali ilikusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 104,038,097.73**. Pia, Shirika limeweza kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo viziwi 52 waliopo Wilaya ya Geita katika nyanja ya uchimbaji na uchenjuaji salama wa madini.



Picha Na. 26: Matenki ya kuchenjulia Dhahabu katika kituo cha Katente

108. Mheshimiwa Spika, Shirika lilirejea tena kwenye biashara ya kununua madini ya bati kutoka kwa wachimbaji wadogo walioko Wilayani Kyerwa Mkoa wa Kagera. Katika

kipindi husika jumla ya **kilogramu 3,184.15** za madini ya bati zilinunuliwa na Shirika kwa **shilingi milioni 61.1**. Lengo la kurejea katika biashara hii ni kuwezesha kufungua soko la biashara ya madini hayo ambapo wachimbaji wadogo walikuwa wamekaa na madini ya bati kwa zaidi ya miezi sita bila kuuza madini yao. Hatua hii ya Shirika kurejea katika biashara, imefungua soko na sasa madini yananunuliwa kwa bei shindani.

e) Leseni za Shirika

109. Mheshimiwa Spika, Shirika limeweza kupata leseni tatu (3) za uchimbaji ambazo ni leseni ya madini ya dhahabu iliyopo Wilayani Bukombe mkoani Geita, leseni ya madini ya shaba iliyopo Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro na leseni ya Makaa ya Mawe iliyopo Ilima Wilaya ya Rungwe mkoa wa Mbeya. Hatua hii itaongeza ushiriki wa Serikali katika kuendeleza rasilimali zake za madini.

f) Kuendeleza Rasilimaliwateru

110. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Shirika limewawezesha watumishi 15 kupata mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali na watumishi wanne (4) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi shahada ya uzamili katika fani za Rasilimaliwateru, *Geology, Earth Science Engineering* na *Business Administrationin Marketing*.

3) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

111. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 GST ilitekeleza kazi zifuatazo: kuboresha kanzidata ya jiosayansi na rasilimali madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za jiosayansi; kuboresha na kuendelea kutoa huduma za maabara kwa wadau wa Sekta ya Madini; kufanya tafiti maalum za jiosayansi; kuratibu majanga ya asili ya jiolojia; kuchapisha na kusambaza habari na taarifa za jiosayansi na upatikanaji madini; na kuboresha vitendea kazi na kujenga uwezo kwa watumishi.

112. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2021 GST ilikuwa imekusanya jumla ya **shilingi 464,982,186.26** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 91.46** ya lengo la makusanyo la mwaka la **shilingi 508,386,000na asilimia 122** ya kipindi cha miezi tisa (9).

(i) Kuboresha Kanzidata ya Jiosayansi na Rasilimali Madini

113. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 GST imeendelea kuboresha Kanzidata ya Jiosayansi na rasilimali madini ili kuongeza uelewa wa Jiolojia ya nchi na kuchochaea uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kukamilisha ugani na utafiti wa jiolojia katika QDS 279 iliyoko Mpigamiti, Ndapata na kwenye hifadhi ya wanyamapori ya Selous na Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere Wilayani Lwale; *field checks* katika QDS 75 (Wilaya ya Kasulu), QDS 264 (Wilaya ya Malinyi) na QDS 316 (Wilaya ya Nanyumbu). Matokeo ya awali ya utafiti huo yameonesha uwepo wa madini ya agate katika kijiji cha Ndapata na ndani ya hifadhi; urani ndani ya hifadhi, dhahabu katika kijiji cha Lubanga Malinyi; chokaa huko Makere na hifadhi ya Moyowosi Game Controlled area; na dhahabu na *marble* katika maeneo ya Lukwika na Missuguru Wilayani Nanyumbu.

114. Mheshimiwa Spika, pia kampuni sita (6) zinazojihusisha na kazi za utafutaji na uchimbaji wa madini Tanzania ambazo ni Shanta Gold Mining Co. Ltd (Songwe), Sunshine Mining Ltd (Songwe), Mbeya Cement Company Ltd, Tancoal Energy Ltd, Ruvuma Coal na Marmo Granito zilitembelewa kwa ajili ya kukusanya taarifa, kukagua miamba choronge (cores) iliyopo pamoa na kuwakumbusha wajibu na utaratibu wa kisheria wa uwasilishaji wa taarifa na takwimu za kijiosayansi. Aidha, GST imekamilisha ukusanyaji na uchakataji wa taarifa na takwimu za uwepo wa madini ya aina mbalimbali katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Lindi, Simiyu na Tanga. Lengo ni kuboresha kanzidata ya madini yapatikanayo nchini na kuboresha **kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania**.

(ii) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za Jiosayansi

115. Mheshimiwa Spika, GST imefanya tafiti za Jiosayansi katika maeneo ya Nyamongo Mkoani Mara na Mkalama Mkoani Singida na kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo 250. Mafunzo hayo yalihusu namna ya kutambua ulalo wa miamba yenye mashapo na namna bora ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini kutoka kwenye mbale. Matokeo ya utafiti uliofanywa Mkalama – Singida yalionesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha madini ya chokaa na jasi yenye ubora mkubwa ambayo yanafaa kwa matumizi ya viwandani.



Picha Na. 27: A - Muonekano wa madini ya chokaa na B - Muonekano wa madini ya Jasi katika Wilaya ya Mkalama

116. Mheshimiwa Spika, GST pia imeandaa na kuchapisha Mwongozo wa namna bora ya uchenjuaji na uchukua ji wa sampuli kwa ajili ya uchunguzi katika maabara. Muongozo, ulitumika katika mafunzo yaliyofanyika Dodoma katika ofisi za GST ambapo jumla ya viongozi 40 wa FEMATA walishiriki mafunzo hayo. Mafunzo kwa wachimbaji wadogo yanatarajiwa kufanya kwenye maeneo yao ya uchimbaji mara baada ya kukamilika kwa maandalizi. Mwongozo huo utatumika kufundishia wachimbaji wadogo wa madini hapa nchini. **Nitoe rai kwa wachimbaji wadogo kuitumia Taasisi ya GST** katika kutambua tabia za mbale za eneo husika ili kuweza kutumia njia sahihi ya uchenjuaji kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji.

(iii) Kuboresha na Kuendelea Kutoa Huduma za Maabara kwa Wadau wa Sekta ya Madini

117. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa GST inaendelea kutoa huduma za maabara zinazokidhi viwango vya kimataifa, maboresho ya mifumo ya uendeshaji yalifanyika ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa sampuli tatu (3) za malinganisho (proficiency tests) kutoka kampuni ya Geostat ya Australia. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa GST ipo kwenye viwango vinavyo himilika vya utoaji majibu ya uchunguzi unaofanywa na maabara mbalimbali zenyе ithibati duniani. Aidha, ukaguzi katika utendaji kazi kwa mujibu wa taratibu za kimataifa (ISO Standards) ulifanyiywa na taasisi ya SADCAS inayosimamia ubora wa huduma za maabara katika Ukanda wa SADC na **GST iliweza kuendelea kukidhi vigezo vya kubaki na ITHIBATI** katika uchunguzi wa dhahabu kwa njia ya tanuru.

(iv) Tafiti Maalum za Jiosayansi

118. *Mheshimiwa Spika*, tafiti maalum ni zile ambazo zinafanywa kutatua changamoto za kijiolojia zilizojitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mfano kwenye maeneo mapya yaliyogundulika/kusadikika kuwa na madini na kuvamiwa na Wachimbaji (mineral rush); uhitaji wa taarifa zaidi za jiosayansi kwenye eneo maalum; maagizo au maelekezo kutoka kwa viongozi mbalimbali pamoja na maombi ya wananchi kwa ujumla. Katika kipindi husika, imekamilisha tafiti maalum mbili (2) za jiosayansi zilizolenga kubaini ubora wa madini ya jasi yaliyo katika maeneo ya Mpindiro, Mandwa, Mkomore na Hotel Tatu Mkoani Lindi; na uwepo wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Ngoheranga, Milima ya Furua, Milima ya Mbarika, Kwa Mpepo, Kwa Omari Nyama na Luwegu katika Wilaya ya Malinyi. Matokeo ya utafiti huo yamebaini uwepo wa dhahabu katika kiwango cha kuanzia 0.01g/t hadi 4g/t.

(v) Kuratibu Majanga ya Asili ya Jiolojia

119. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na majanga ya asili ya jiolojia na kutoa ushauri wa namna bora ya kupunguza madhara yanayoweza kutokana na majanga hayo, GST ilikusanya takwimu za matetemeko ya ardhi kutoka katika vituo vya kuratibu matetemeko ya ardhi vya Mtwara, Arusha, Mbeya, Geita na Dodoma. Katika kipindi husika, maeneo yaliyokumbwa na mitetemo yenye kiwango cha juu ni Dar es Salaam lenye ukubwa wa 5.9 katika kipimo cha Richter ambapo kitovu chake kilikuwa ndani ya Bahari ya Hindi; na Ziwa Nyasa lenye ukubwa wa 5.0 katika kipimo cha Richter na kitovu chake kilikuwa ndani ya Ziwa Nyasa. Taarifa za matukio hayo yote zilitolewa kwa Umma kuititia vyombo vya habari ili wananchi waweze kuwa na uelewa wa madhara yanayotokana na majanga ya asili ya jiolojia na kuweza kujikinga.

120. Mheshimiwa Spika, GST pia ilikamilisha utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kubaini kilichoripotiwa kuwa ni mlipuko wa volkano katika kijiji cha Lahoda Wilaya ya Chemba Mkoani Dodoma iliyotokea Septemba, 2020 na Kunduchi Wilayani Kinondoni katika Mkoa wa Dar es Salaam iliyotokea Novemba, 2020. Uchunguzi ulibaini kwamba kulikuwa na tabaka la tope lilidochanganyika na maji ambalo lilibubujika na kusukumwa kuja juu ya uso wa ardhi. Tukio hilo kitaalam huitwa *Liquefaction* na siyo volkano kama ilivyotolewa taarifa kabla ya utafiti.



Picha Na. 28: Eneo la Kunduchi liliilo bubujika tope (*liquefaction*)

(vi) Kuchapisha na Kusambaza Habari na Taarifa za Jiosayansi na Upatikanaji Madini

121. Mheshimiwa Spika, GST ilishiriki katika maonesho kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2021 uliofanyika jijini Dar es Salaam na Maonesho ya Tatu ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika katika Viwanja vya Bombambili mkoani Geita kwa lengo la kuendelea kuelimisha Umma juu ya huduma zinazotolewa na GST na kutangaza rasilimali madini zinazopatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi.

(vii) Kuboresha vitendea kazi na kujenga uwezo kwa watumishi

122. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi husika, GST imeboresha mazingira ya kufanya kazi na kuendeleza rasilimali watu kama ifuatavyo: Watumishi 15 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu. Kati ya watumishi hao, mtumishi mmoja amemalisha shahada ya uzamili, watumishi wawili (2) wanaendelea shahada ya uzamivu, watumishi kumi (10) waendelea na shahada ya uzamili na watumishi wawili (2) wanasona shahada ya kwanza. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, GST ilipata magari 6 kwa kazi za ugani na magari manne pamoja na vifaa mbalimba vya maabara, vifaa vya kuratibu majanga ya asili ya jiolojia na ugani vipo katika hatua mbalimbali za ununuzi.

4) Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

123. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha na kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia, TEITI inaendelea kukamilisha ripoti kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019 ya Malipo ya Kodi kutoka katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Mtaalamu Mshauri (M/S Mzumbe University) alisaini mkataba kwa ajili ya kuandaa ripoti hiyo. Ripoti hiyo ya ulinganishi wa mapato ya Serikali na malipo ya kampuni za Madini, itaweka wazi malipo ya kodi yaliyofanywa na kampuni za Madini,

Mafuta na Gesi Asilia kwa kipindi cha 2018/2019. Ripoti hii inatarajiwa kukamilika na kuwekwa wazi kwa Umma Juni, 2021.

124. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kifungu cha 16(1) (b) cha Sheria ya TEITA 2015 kuhusu uwekaji wazi wa majina ya wamiliki wa Hisa katika kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, TEITA ilikutana na uongozi wa BRELA kujadili namna bora ya uwekaji wazi wa majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Beneficial Ownership Disclosure). Kikao hiki kilipitia kifungu 16 cha Sheria ya TEITA, 2015 na Kanuni zake za mwaka 2019 pamoja na Marekebisho ya Sheria mbalimbali yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 na kukubaliana kuwa kampuni ziwasilishe taarifa hizo kulingana na Sheria ya TEITA ya mwaka 2015. Taarifa hizo zitawekwa wazi kupitia ripoti ya TEITI ya mwaka 2018/19 inayotarajiwa kukamilika Juni 2021.

125. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, TEITI iliandaa Mpango Kazi wa uwekaji wazi mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, Sheria mbalimbali zilipitiwa ili kubaini kama kuna marekebisho ya Kisheria yaliyofanyika juu ya uwekaji wazi wa mikataba; na kuainisha mikataba na leseni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia iliyoi hai ambayo ipo wazi na isyo wazi; na kutoa mapendeleko ya namna bora ya uwekaji wazi wa mikataba hiyo. TEITI kwa kushirikiana na Wizara ya Madini inafanya kazi mapendeleko hayo ili kutekeleza matakwa ya kimataifa ya EITI ambayo yanazitaka nchi wanachama wa EITI kuweka wazi mikataba hiyo kuanzia Januari, 2021.

Aidha, mawasiliano kati ya Wizara ya Madini na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu namna bora ya kutekeleza takwa hili yanaendelea.

126. Mheshimiwa Spika, TEITI iliendesha vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari ili kuhamasisha matumizi ya takwimu zinazotolewa na TEITI, kuitangaza TEITI na majukumu yake pamoja na kuibua mijadala kwa ajili ya kuboresha na kuhamasisha uwajibikaji katika usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

27. Mheshimiwa Spika, TEITI pia ilishiriki katika maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya 44 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba na Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji Katika Sekta ya Madini uliofanyika Februari, 2021 Dar es Salaam. Aidha, TEITI iliendesha warsha katika mikoa ya Mwanza na Geita kuhamasisha matumizi ya takwimu zilizopo katika ripoti za TEITI na kuwajengea uwezo madiwani, asasi za kiraia, Halmashauri za Tarime, Mwanza, Biharamuro, Geita, Kahama na Kishapu. TEITI ilitumia maonesho, warsha na mikutano hiyo kuelezea majukumu yake na kujitangaza.



Picha Na. 29: Mgeni rasmi- Mhe. Doto Biteko- Waziri wa Madini akiwa na Waheshimiwa Madiwani wa Geita walishiriki katika warsha ya kuhusu matumizi ya Takwimu zilizopo katika ripoti za TEITI Mkoani Geita.



Picha Na 30: Mjumbe wa Kamati ya TEITI-Bw. Donald Kasongi akitoa mada katika warsha kuhusu matumizi ya takwimu zilizopo katika ripoti za TEITI na kuwajengea uwezo Madiwani Mkoani Mwanza.

5) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

128. Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) ni pamoja na: Kutoa mafunzo kwa ngazi ya Cheti na Stashahada (Diploma) katika fani ya teknolojia ya madini na usonara (gem and jewellery technology); kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za *gemmology, gem identification, synthetic & treated gem identification, coloured gem grading & pricing, diamond grading & pricing, lapidary, gem & rock carving and jewellery design & manufacturing.*

129. Mheshimiwa Spika, Kituo pia kinatoa huduma za kusanifu madini ya vito na miamba; kutoa huduma za kimaabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara kwa kutoa vyeti vya uthibitisho (Certificate of Authenticity); utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo, ushauri elekezi; kufanya tafiti za kuyaongezea madini thamani; na Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Katika kipindi rejewa kituo kimetekeleza yafuatayo:

a) Kuendelea Kutoa Mafunzo kwa Ngazi ya Cheti Katika Fani za Teknolojia ya Madini na Usonara

130. Mheshimiwa Spika, katika kipindi rejewa, Kituo kimedahili wanafunzi 78 kwa Mafunzo ya Muda Mrefu katika ngazi ya Cheti (NTA Level 4, 5 na 6) katika fani ya Teknolojia ya Madini na Usonara. Aidha, wanafunzi 21 walidahiliwa kujunga na mafunzo ya muda mfupi (miezi mitatu na sita) katika fani za utambuzi wa madini ya vito, ukataji na ung'arishaji madini ya vito ambao kwati yao wanafunzi 10 walihitimu mafunzo hayo na wengine wanaendelea na masomo. Hivyo, kufanya jumla ya wahitimu 188 waliohitimu tangu kituo kianze kutoa Mafunzo hayo.



Picha Na. 31: Wanafunzi wakiwa darasani wakiendelea na mafunzo katika Kituo cha TGC

b) Kuzalisha Bidhaa za Urembo na Mapambo

131. Mheshimiwa Spika, Kituo kilizalisha bidhaa mbalimbali za urembo na mapambo kama vile vinyago, pete, hereni, vinyago vya mayai, *table trays*, *table mats*, vidani, bangili, Ramani ya Tanzania, tuzo na vito vilivyokatwa. Bidhaa hizi ziliuzwa kituoni na katika mikutano na makongamano mbalimbali.



Picha Na. 32: Baadhi ya Bidhaa za Urembo na Mapambo zinazozalishwa na Kituo cha TGC.

c) Kuendelea kutoa Huduma kwa Wadau

132. Mheshimiwa Spika, Kituo kinaendelea kutoa huduma mbalimbali za uongezaji thamani madini kwa wadau ikiwa ni pamoja na utambuzi na usanifu wa madini ya vito, uchongaji wa vinyago vya miamba pamoja na ung'arishaji. Aidha, wadau wa ndani ya nchi wameanza kuonesha mwitikio wa kutumia bidhaa zinazozalishwa kituoni ikiwa ni kielelezo cha uelewa wa thamani ya bidhaa zitokanazo na madini zinazozalishwa hapa nchini. *Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuendelea kutumia bidhaa zinazozalishwa na Kituo hiki kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani nchini na kukitangaza.*



ya vito vya thamani katika Kituo cha TGC

d) Kujitangaza na Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

133. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jemolojia kiliendelea kujitangaza na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini kwa kushiriki katika maonesho mbalimbali ikiwemo Maonesho ya Sabasaba na Mkutano wa Madini uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika kikanda Jijini Arusha na Maonesho ya Madini Mkoani Geita. Mikutano na maonesho hayo yalitoa fursa kwa Kituo kuonesha bidhaa mbalimbali za kisonara zinazozalishwa

na kutoa elimu kwa wananchi juu ya uongezaji thamani madini ya vito. Pia, Kituo kilitumia vyombo mbalimbali vya habari kujitangaza kama vile vituo vya runinga, redio na tovuti za kituo. Kupitia jitihada hizo maombi ya wanafunzi kuijunga na Kituo yameongezeka kutoka katika mikoa mbalimbali hapa nchini tofauti na hapo awali ambapo maombi yalikuwa yanatoka katika mkoa wa Arusha pekee.

D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022

134. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022, yamezingatia miongozo mbalimbali ya Kitaifa ikiwemo: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/2022; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Hotuba ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa uzinduzi wa Bunge la 12 Novemba, 2020 pamoja na hotuba ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipolihutubia Bunge tarehe 22 Aprili 2021, na maelekezo ya viongozi pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

135. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madinikwa mwaka 2021/2022 imepanga kutekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini; kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; kuhamasisha na kuvutia ufanyaji biashara ya madini na nchi nyingine za Afrika hasa za kanda za EAC, SADC na Maziwa Makuu ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya Madini kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza

majukumu yao kwa ufanisi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

I. Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa

136. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini ili uweze kufaidisha Taifa na wawekezaji kwa usawa; kutekeleza mikakati itakayowezesha kudhibiti vitendo nya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini; kuimarisha masoko ya madini nchini; kuanzisha na kuimarisha soko la dhahabu la Kalema; kufungua na kusimamia migodi ya uchimbaji mkubwa na kuweka msisitizo katika uchimbaji wa madini ya kinywe (graphite) na madini mengine; kuendeleza mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na vito vingine hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo na madini mengine ya vito; na kuhakikisha migodi yote mikubwa na ya kati inaa jiri, inanunua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha kwa kadiri ya upatikanaji wake na kutoa huduma za kijamii katika maeneo husika.

137. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia hiyo mikakati itakayotekelozwa, Wizara katika mwaka 2021/2022, inapanga kukusanya jumla ya **shilingi 696,441,872,667** ikililinganishwa na **shilingi 547,735,863,597** kwa mwaka 2020/2021. Kati f e d h a zitakazokusanya, **shilingi 650,010,002,000** sawa na **asilimia 93.33** zitakusanya na kuwasilishwa Hazina na **shilingi 46,431,870,667** sawa na **asilimia 6.67** zitakusanya na kutumika na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

II. Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na Kuwawezesha Wananchi Kushiriki katika Uchumi wa Madini

138. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: kubuni na kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea

maeneo au kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana taarifa za msingi za kijiolojia; kuwaunganisha na mabenki ili waweze kupata mikopo; kutoa huduma za utafiti kwa gharama nafuu, kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kuwa wa Kati na hatimaye Wakubwa, na kuwapa mafunzo yanayohitajika kuhusu uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini; kuzifuta leseni za baadhi ya watu ambao wamepewa leseni na hawajazifanyia kazi, na maeneo hayo kuyagawa kwa wachimbaji wengine, hususan wachimbaji wadogo; na kusimamia utekelezaji wa Sheria inayowataka wamiliki wa leseni za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji kutoa ajira kwa wazawa, kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuwasilisha mpango wa ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini.

III. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

139. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani, Wizara itafanya yafuatayo: kuhamasisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia teknolojia ya kisasa vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ikiwemo ujenzi wa viwanda vya uyeyushaji (*smelters*) na usafishaji (*refineries*); kuendelea kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini; na kuhamasisha biashara ya madini kwenye masoko kwa kuvutia nchi jirani kuyatumia masoko yetu kufanya biashara ili kuongeza wigo wa upatikanaji malighafi kwa ajili ya viwanda vya uongezaji thamani madini.

IV. Kuhamasisha Biashara na Uwekezaji katika Sekta ya Madini

140. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: kuweka mazingira yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini bila ya kuathiri ustawi na matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo; kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kufanya tafiti za madini ya kimkakati, viwandani na metali; kujenga imani kwa biashara

ya madini nchini kwenye nyanja za kimataifa kwa kutekeleza wajibu wa nchi yetu kama wanachama wa EITI; na kushiriki mikutano na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini.

V. Kuzijengea uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ili Ziweze Kutekeleza Majukumu yake kwa Ufanisi

141. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itatekeleza kipaumbele hiki kwa kufanya yafuatayo: kuendelea kuliimarisha Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) ili lishiriki kikamilifu na kuwekeza kwenye shughuli za madini kwa maslahi mapana ya nchi; kuwawezesha wachimbaji wadogo, ikiwa ni pamoja na kuwatengea maeneo ya uchimbaji, kuwapatia mafunzo, mikopo pamoja na vifaa; kuimarisha Tume ya Madini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na usimamizi wa Sekta ya Madini ili kuwawezesha maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii kutokana na uboreshaji wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa takwimu za madini; kuimarisha Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kufanya utafiti wa madini kwa lengo la kukusanya taarifa za jiosayansi zitakazosaidia kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuimarisha Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) ili kuweza kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini na kufanya shughuli za uongezaji thamani madini; na kuimarisha TEITI ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa Sekta ya Uziduaji.

VI. Kusimamia Mfumo wa Ukaguzi wa Shughuli za Migodi

142. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza kipaumbele hiki Wizara itaimarisha kaguzi katika masuala ya afya, usalama na utunzaji wa mazingira katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji wa madini na hesabu za uwekezaji (Capex and Opex) kwenye shughuli za madini ili kuhakikisha nchi inapata mapato stahiki.

VII. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

143. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: kuendelea kuajiri watumishi wa kutosha wenye sifa kwa kadri ya upatikanaji wa vibali; kuwapatia vitendea kazi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kuwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi; kuboresha maslahi na stahili za watumishi; kuendelea kutoa elimu na vifaa kinga kwa ajili ya kuzuia maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI na MSY pamoja na kuwashudumia wanaoishi na VVU na kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Wizara dhidi ya Rushwa wa Mwaka 2017/2022.

Kazi Zitakazoteklezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka 2021/22

i. Tume ya Madini

144. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2021/22, Tume ya Madini inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:- kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Madini na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuimarisha ufuatiliaji wa ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na uzalishaji wa madini kwa wamiliki wote wa leseni, kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini; kuelimisha Umma na kuboresha upatikanaji wa taarifa mbalimbali kwa wadau wa Sekta ya Madini; kuboresha ushirikiano kati ya Tume ya Madini na wadau mbalimbali kuhusu uendelezaji Sekta ya Madini; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Kuimarisha Usimamizi wa Sekta ya Madini na Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali Yatokanayo na Rasilimali Madini

145. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea kuboresha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na rasilimali madini nchini, Tume ya Madini itaendelea kuongeza kasi ya utoaji

wa leseni kwa kuimarisha Mfumo wa Utoaji na usimamizi wa Leseni; kuboresha usimamizi wa uzalishaji wa madini ujenzi kwa kuhakikisha Mfumo wa Ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini haya (MiMS) unatumika nchi nzima; kuendelea kuboresha huduma katika masoko ya Madini nchini ikiwa ni pamoja na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali pamoja na kusajili mialo ya Wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini.

Kuimarisha Ufutiliaji wa Ugaguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini kwa Wamiliki Wote wa Leseni,

146. Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uchimbaji madini salama na unaozingatia utunzaji bora wa mazingira, Tume ya Madini itaendelea kufanya ugaguzi ikiwa ni pamoja na ugaguzi wa miundombinu ya migodi kama vile Mabwawa ya kuhifadhia topesumu, mashimo ya uchimbaji, maeneo ya kutunzia miambata; maghala na stoo za kuhifadhia baruti, shughuli za ukarabati wa mazingira migodini, uchimbaji salama hususan kwa Wachimbaji Wadogo pamoja na ugaguzi wa mitambo ya uchenjuaji madini. Aidha, Tume itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mipango ya uendelezaji migodi na ufungaji migodi kwa wamiliki wa leseni kubwa na za kati; na kubuni miradi ya mfano ya uchimbaji madini salama na utunzaji wa mazingira kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo.

Kuendelea Kuboresha Mazingira ya Kuwawezesha Wananchi Kufaidika na Rasilimali Madini;

147. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchini, kusimamia ushirikishwaji wa wananchi kwenye shughuli za madini kwa mujibu wa Sheria, kuhakikisha Kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini zinatumia malighafi zinazosalishwa hapa nchini pamoja na huduma zinazotolewa na Watanzania, na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Kijamii (CSR). Aidha, Tume ya Madini itaendelea kuzishawishi Taasisi za kifedha kuendelea kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo.

Kuelimisha Umma na Kuboresha Upatikanaji wa Taarifa Mbalimbali kwa Wadau wa Sekta ya Madini

148. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonesho, makongamano pamoja na midahalo mbalimbali ndani nan je ya nchi ili kuhakikisha elimu juu ya uendeleazaji wa Sekta ya Madini unawafikia watanzania pamoja na wadau wengine wa Sekta ya Madini. Pia, itaendelea kuimarisha Kitengo cha Habari ikiwa ni pamoja na kuendelea kuboresha tovuti ya tume ya madini ili kuharakisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za Sekta ya Madini kwa wadau.

Kuboresha Ushirikiano Kati ya Tume ya Madini na Wadau Mbalimbali Kuhusu Uendelezaji Sekta ya Madini

149. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini itaendelea kushirikiana na Mamlaka zingine za Serikali zinazofungamana katika usimamizi wa Sekta ya Madini nchini kama vile Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Taasisi za Fedha, pamoja na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha changamoto mbalimbali kama vile changamoto za kisheria, mitaji, upatikanaji wa vibali na kodi ambazo zimekuwa zikiwakabili Wadau hao zinatatulliwa kwa wakati na kwa maridhiano.

Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanya Kazi

150. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha uwezo wa Tume ya Madini, Serikali itaendela kuboresha vitendea kazi na mazingira ya kazi; kuendeleza watumishi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na muda mrefu kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wao; kuboresha Muundo wa Tume ya Madini.

ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

151. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2021/2022, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo: kuboresha Kanzidata ya Jiosayansi ya Taifa ili kuongeza uelewa wa Jiolojia ya nchi na kuchochea

uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini;kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za jiosayansi katika utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji salama na uhifadhi wa mazingira;kuboresha Huduma za Maabara kwa Wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi;kuratibu Majanga ya Asili ya Jiolojia na kuelimisha wananchi namna bora ya kujikinga na majanga; nakuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma.

Kuboresha Kanzidata ya Jiosayansi ya Taifa ili Kuongeza Uelewa wa Jiolojia ya nchi na Kuchochea Uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini

152. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha kanzidata ya Jiosayansi nchini, GST inakusudia kufanya ugani wa jiolojia katika QDS 278 na 290 Lindi, Ruvuma na Morogoro na kuchora ramani zake katika skeli ya 1: 100,000. Aidha, GST itafanya ugani wa jiochema katika QDS 125 Dodoma na QDS 126 Manyara, tafiti maalum za jiosayansi angalau nne (4), tafiti za madini ya viwandani na kuboresha kitabu cha madini ya viwandani; kuchora ramani 55 na kunakili (*scanning*) machapisho 1,000 kutoka katika mfumo wa karatasi na kwenda katika mfumo wa kielektroniki. Vilevile, Taasisi itakusanya taarifa na takwimu mbalimbali za jiosayansi kutoka kwa watafiti na wachimbaji wa madini na kuzihifadhi katika kanzidata ya Taifa. Aidha, uhakiki wa madini yapatikanayo nchini utafanyika katika mikoa 10 ambayo ni Kilimanjaro, Manyara, Kigoma, Mtwara, Tabora, Rukwa, Dodoma, Arusha, Singida na Njombe; na kuboresha kitabu cha madini yapatikanayo nchini na vitabu vya madini katika mikoa kumi.

Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kwa Kufanya Tafiti za Jiosayansi

153. Mheshimiwa Spika, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: utafiti wa jiolojia, jiofizikia na jiochema kwa lengo la kutambua ulalo, muelekeo na tabia za mbale katika maeneo manne (4) ya wachimbaji wadogo yaliyotengwa; Utafiti wa jiosayansi katika maeneo mawili (2) yatakayotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Kuboresha Huduma za Maabara kwa Wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi

154. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za maabara, GST imepanga kufanya yafuatayo:- kufanya uchunguzi wa sampuli 15,000; kuzalisha vyungu vikubwa (crucibles) 40,000 na vidogo (cuples) 10,000; kuendeleza programu mbalimbali za kusimamia ubora wa huduma za maabara ikiwa ni pamoa na kupata **ITHIBATI** ya uchunguzi wa madini ya kinywe na makaa ya mawe pamoa na metali (chuma, shaba, kobalti na manganese); na kuboresha miundombinu, mitambo na vifaa vya maabara na kuwajengea uwezo watumishi wa maabara. Aidha, GST itaanisha vituo viwili vya kutoa ushauri wa jiosayansi na huduma za maabara katika Wilaya za Geita na Chunya ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata huduma hizo kwa karibu.

Kuratibu Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kuelimisha Wananchi namna Bora ya Kujikinga na Majanga

155. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na majanga ya asili ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi, maporomoko ya ardhi, na milipuko ya volkano, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: kukusanya takwimu na kuzichakata kutoka katika vituo vyote vitano (5) na kuhuisha ramani inayooonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini; kuunganisha vituo vitano (5) vya kupimia mitetemo katika mfumo mubashara (*real time*) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati mara tetemeko linapotokea; na kutoa elimu kwa Umma juu ya namna bora ya kujikinga au kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia kuititia machapisho, semina na vyombo vya habari.

Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika Kutoa Huduma

156. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato, GST inakusudia kufanya yafuatayo: kuboresha vitendea kazi na mazingira ya kazi; kuendeleza watumishi kwa kuwapatia mafunzo

mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wao; kuboresha muundo wa GST ili kuongeza ufanisi na kununua mtambo wa kutengeneza vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu na fedha.

iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

157. Mheshimiwa Spika, Shirika katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 limepanga kuongeza mapato kuititia shughuli za uwekezaji na kandarasi mbalimbali katika Sekta ya Madini na Uziduaji. Utekelezaji wa shughuli hizi unategemewa kuliwezesha Shirika kuongeza mchango kwa Serikali kutoka **shilingi bilioni 1.2** kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia **shilingi bilioni 3.5** mwaka 2021/2022

158. Mheshimiwa Spika, katika kufikia lengo hilo Shirika litatekeleza kazi zifuatazo:kuongeza uchimbaji wa makaa ya mawe; kuongeza usimamizi wa miradi; kuimarisha shughuli za uchorongaji; kutekeleza miradi mipy ya kimkakati; kuanzisha na kuendeleza mradi wa kuuza vilipuzi/baruti; kuanzisha na kuendeleza mradi wa kuuza kemikali za madini; na kuratibu shughuli za wachimbaji wadogo.

i. Kuongeza Uchimbaji wa Makaa ya Mawe

159. Mheshimiwa Spika, Shirika linatarajia kuanza utekelezaji wa majukumu yake kwa kuongeza uchimbaji wa makaa ya mawe katika leseni za Shirika za Ivogo na Kabulo mkoani Songwe. Kazi hiyo itahusisha ukarabati wa miundombinu ya mgodi wa Kiwira. Aidha, Shirika litakarabati barabara ya Kiwira hadi Kabulo na kuanza kuchimba katika leseni mpya ya Ilima. Utekelezaji wa shughuli hizi utaenda sambamba na kutangaza biashara ya makaa ya mawe ili kuweza kupata wateja wa ndani na nje ya nchi.

ii. Kuimarisha Usimamizi wa Miradi

160. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi na tija katika kukuza mapato yanayotokana na uwekezaji, Shirika linatarajia kuimarisha usimamizi katika miradi yake ikiwemo mradi wa dhahabu na Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD na

miradi ya ubia ya Buckreef, Buhemba na Kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza.

iii. Kuimarisha Shughuli za Uchorongaji

161. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza mapato Shirika limepanga kuongeza mitambo mingine minne (4) ya uchorongaji. Kwa mipango iliyopo, Shirika linatarajia kupata kandarasi tatu (3) zenye tija ili kuongeza mapato. Aidha, Shirika limepanga kuwajengea uwezo wataalamu wake katika kitengo cha uchorongaji ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi na ufanisi.

iv. Utekelezaji wa Miradi Mipyä a) Mradi wa Kuuza Vilipuzi na Baruti

162. *Mheshimiwa Spika*, Shirika linatarajia kuanza utekelezaji wa mradi mpya wa uuzaaji baruti na vilipuzi katika migodi ya wachimbaji wadogo nchini ili kuweza kuwapatia huduma bora na kwa bei shindani.

b) Mradi wa Kuuza Kemikali za Madini

163. *Mheshimiwa Spika*, Shirika linatarajia kuongeza uwekezaji wake katika Sekta ya Madini kwa kuanza mradi wa kuuza kemikali zinazohitajika katika shughuli za uchenjuaji madini.

v. Kuratibu Shughuli za Uchimbaji Mdogo

164. *Mheshimiwa Spika*, Shirika litaendelea kuboresha vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi kwa kuviongeza uwezo ili kuendelea kutoa huduma na elimu kwa vitendo ya uchimbaji na uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo nchini.

165. *Mheshimiwa Spika*, kwa kushirikiana na GST, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Benki za CRDB na NMB, Shirika limeandaa Mkakati wa Uendelezaji Wachimbaji Wadogo ili kuongeza uzalishaji. Mkakati huu utawawezesha wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi za kijolojia na kukopa mitaji

na vifaa vya kisasa kwa ajili ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Aidha, Shirika limepanga kununua mitambo mipyä mitano (5) ya uchorongaji maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

vi. Kuboresha Mazingira ya Kazi na Maslahi ya Wafanyakazi

166. *Mheshimiwa Spika*, Shirika litaendelea kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia vifaa vinavyohitajika sambamba na kuboresha maslahi yao. Aidha, Shirika limepanga kutoa mafunzo mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

iv. Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

167. *Mheshimiwa Spika*, kazi zitakazotekelezwa na TEITI katika Mwaka 2021/2022 ni kama ifuatavyo: ukamilishaji na utoaji kwa Umma ripoti kuhusu tozo, kodi na malipo mengine yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa Serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/2020; kuendelea kuelimisha umma juu ya matumizi ya takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI ili waweze kutumia takwimu hizo katika kuhoji uwajibikaji wa Serikali kwa njia ya warsha, matangazo, vipindi vya redio, televisheni na makala; na kuweka wazi majina na mikataba ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

168. *Mheshimiwa Spika*, kupitia Mradi wa *Extractive Global Programmatic Support (EGPS)* wa Benki ya Dunia, TEITI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: kutekeleza majukumu yatakayoiwezesha nchi yetu kukidhi viwango vya kimataifa vya EITI na kuwajengea uwezo wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya takwimu zinazopatikana katika ripoti za TEITI; kuimarisha ushirikano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuongeza manufaa yatokanayo na Sekta ya Uzidua hapa nchini; na kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na kampuni pamoja na Taasisi za Serikali kuripoti malipo yaliyofanywa na kampuni hizo kwa Serikali.

v.Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

169. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2021/2022, Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kutoa mafunzo na Uzalishaji wa Bidhaa

170. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza jukumu hili, Kituo kitaongeza udahili wa wanafunzi wa muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali za uongezaji thamani madini, kutoa ushauri kwa wadau wa madini; kufanya tafiti za kuongeza thamani madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini na kutengeneza bidhaa za mapambo na urembo (usonara). Aidha, Kituo pia kinakusudia kutoa mafunzo ya stadi za ufundi kwenye tasnia ya uongezaji thamani madini kwa vijana waliohitimu elimu ya msingi ili waweze kujiajiri kwenye Sekta ya Madini;

Kuimarisha Kituo cha TGC

171. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2021/2022, Kituo kupitia Wizara kinatarajia kusomesha watumishi wawili (2) nje ya nchi katika vyuo vilivyobobe a katika utoaji wa mafunzo ya uongezaji thamani madini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi tano (5) katika kada mbalimbali ambao watakuwa wakufunzi katika Kituo cha TGC.

E. SHUKRANI

172. *Mheshimiwa Spika*, nakiri kuwa juhudii kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano zimeifanya nchi yetu kufikia uchumi wa kati mwaka 2020 ikiwa ni mitano (5) kabla ya muda uliotarajiwa wa mwaka 2025. Ni imani yangu kuwa kutohana na kasi kubwa aliyanza nayo **Mhe.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, nchi yetu itaweza kufikia uchumi wa kati wa juu muda si mrefu.

173. *Mheshimiwa Spika*, ninamuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema amjalie Mheshimiwa Raisafya njema ili aweze kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa

Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitanowenye dhima kuu ya **Nchi ya Uchumi wa Kati na Maendeleo ya Watu** na ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020.

174. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru **Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yao wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kipekee nimshukuru **Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya(Mb.)**, Naibu Waziri wa Madini kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini.

175. Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Prof. Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Mha. David Robson Mulabwa Kamishna wa Madini, Prof. Idris Suleiman Kikula Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Justinian Rwezaula Ikingura Mwenyekiti wa Bodi ya GST, Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Wambura Isamuhyo Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO, Bw. Ludovic Utouh Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI; Dkt. George Mofuru Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na Makamishna wa Tume ya Madini na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini uendeshaji wa Sekta ya Madini.

176. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wizara ya Madini yanatimizwa ipasavyo na hivyo kuifanya Sekta ya Madini kuzidi kuimarika.

177. Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Benki ya Dunia kwa ushirikiano wake ambao kwa namna moja au nyingine umeiwezesha Wizara kufikia malengo yake.

178. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo watafutaji, wachimbaji, wenye mitambo ya uchenjuaji, na wafanyabiashara wa madini. Aidha, nizishukuru Taasisi za Fedha, vyombo vya ulinzi na usalama bila kusahau vyombo vyote vya habari kwa ushirikiano walio tupatia katika kuendeleza Sekta ya Madini.

179. Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee na za dhati pia naomba nizitoe tena kwawananchi wema wa Bukombe ambaao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunituma tena kuwakilisha maoni na matarajio yao yanayohusu maendeleo ya Jimbo na Taifa kwa ujumla. Pia nawashukuru kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Niendelee kuwaahidi na kuwahakikishia kuwa nitazidi kuwatumikia kwa kasi zaldl kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

180. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati kipenzi changu Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wangu Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Moses kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

F. HITIMISHO

181. Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu sasa liridhie na kupitisha makadirio ya Jumla ya **shilingi 66,816,467,000** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo:-

- (i) Bajeti ya Maendeleo ni **shilingi 15,000,000,000** ambazo zoteni fedha za ndani; na
- (ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 51,816,467,000** ambapo **shilingi 18,480,807,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 33,335,660,000** ni Matumizi Mengineyo.

182. Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Kwa rejea, hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.madini.go.tz. Vilevile, hotuba hii imeambatana na majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini.

183. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika,naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu ulio mbele yetu. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Seif Gulamali.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niweze kusoma Taarifa ya Kamati. Nianze na sehemu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118(1) na Kanuni ya 136(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini, Fungu – 100 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu; ikihusisha Taarifa ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Matokeo yake, Uchambuzi wa Taarifa ya Bajeti na Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia matakwa ya kikanuni kamati ilifanya kazi zifuatazo:-

(a) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020.

(b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2021/2022 ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020 na 2021 pamoja na matokeo na maoni ya ukaguzi wa miradi ni kama inavyoonekana katika taarifa hii katika ukurasa wa pili hadi hadi ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyokaguliwa na kamati yako katika mwaka wa fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa kituo cha pamoja cha Mererani (*One Stop Centre*);

(ii) Mradi wa kiwanda cha usafishaji dhahabu Mwanza (*Mwanza Refinery*);

(iii) Mradi wa soko kuu la madini Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili. Kamati ilifanya uchambuzi na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Madini, Fungu – 100 kwa mwaka wa fedha 2021 kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

(a) Makusanyo ya maduhuli ya mwaka wa fedha 2020 na 2021.

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

(c) Utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini kwa bajeti ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara na kubaini kuwa ongezeko la makusanyo ya Wizara limetokana na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya mrabaha kwa Serikali ambapo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2020 hadi Februari, 2021, malengo ya Wizara yalikuwa ni kukusanya Sh.274,914,010,000 hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Sh.320,419,409,107 sawa na ongezeko la asilimia 116.55 la makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilibaini kuwa ongezeko la makusanyo pia imetokana na ulipwaji wa ada za jiolojia na utafiti, ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Februari, 2021 lengo la Wizara ilikuwa ni kukusanya Sh.6,495,974,000. Aidha, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari, 2021, Wizara imekusanya kiasi cha Sh.5,293,255,417 sawa na asilimia 81.49 ya lengo la makusanyo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa makusanyo ya Wizara kutoptana na ulipwaji wa faini na malimbikizo ya ada mbalimbali yamepungua ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021 lengo la Wizara ilikuwa ni kukusanya Sh.3,799,284,000 hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Sh.1,540,645,095 sawa na asilimia 40.5 ya malengo ukillinganisha na takwimu za mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo kwa kipindi husika ukusanyaji wa fedha za faini na malimbikizo ulifikia asilimia 140.1 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa punguzo la ulipaji wa faini limetokana na wadau wengi katika sekta kutii sheria kanuni na miongozo ya kisekta katika mwaka

wa fedha 2020/2021. Kamati inatoa pongezi kwa wadau wote wa sekta ya madini kwa kuendelea kutii sheria bila shuruti na inatoa rai kwa wadau kuendelea kufuata taratibu na miongozo mbalimbali ili kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara ya Madini kwa kuvuka lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali madini, usimamizi wa makusanyo na utoroshwaji wa madini ili kuhakikisha malengo yanafikiwa kwa vipindi vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 62,781,586,000 katika Wizara ya Madini. Katika fedha hizo shilingi 8,500,000,000 sawa na asilimia 13.54 ya bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi 54,281,586,000 sawa na asilimia 86.46 ya bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2021 jumla ya Sh.46,280,275,324.21 ilipokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida, fedha hizi ni sawa na asilimia 85.25 ya lengo kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi cha fedha za matumizi mengineyo kilichopokelewa kilizidi lengo la kipindi hicho kwa shilingi 12,590,689,975. Fedha hizo zilitumika katika ununuza wa madini ya *Tanzanite* kutoka kwa mchimbaji wa madini Bwana Sanini Kuriana Laizer.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021, Wizara imepokea fedha za maendeleo jumla ya shilingi 1,220,924,131 kutoka Hazina sawa na asilimia 14.4 ya lengo la mwaka. Kamati ilibaini kuwa hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo uko chini ya malengo kwa asilimia 14.4. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa kiasi cha shilingi 7,279,075,868 kilichobaki kinatolewa

kwa kipindi kilichobaki ili Wizara iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato. Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 696,441,872,667 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti hii ya makadirio ya mapato na kubaini kuwa mwaka 2020/2021 makadirio ya mapato yalikuwa kiasi cha shilingi 547,735,863,597 hivyo kuwa na ongezeko la shilingi 148,706,970,000 sawa na asilimia 21.35.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya shilingi 66,816,467,000 ikilinganishwa na shilingi 62,781,586,000 zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2020/2021, hivyo makadirio haya ni sawa na ongezeko la shillingi 4,034,881,000 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 6 ya bajeti ukilinganisha na bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa nyongeza ya fedha hizi imetokana na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo pamoja na fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepungua kwa asilimia 12.18 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021, ambacho ilikuwa ni shilingi 21,045,927,000. Kamati ilielezwa sababu ya kupungua kwa bajeti ya mishahara ni kutokana na sababu kwamba wafanyakazi wa Chuo cha Madini Dodoma-MRI kwa sasa bajeti yao imehamishiwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imetengewa kiasi cha shilingi 15,000,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa mwaka wa fedha 2020/2021 fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni shilingi 8,500,000,000 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2021/2022

fedha za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa asilimia 76.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Madini kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya mwaka 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Madini na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ulinganisho huo ulilenga kubaini ni kiasi gani ongezeko la bajeti la Taifa kinaathiri mwenendo na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Madini katika mwaka ujao wa fedha. Katika uchambuzi huo, mambo yafuatayo yalibainika:-

(i) Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni shilingi 66,816,467,000 sawa na asilimia 0.18 ya bajeti yote ya Serikali ambapo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni shillingi trillioni 36.3

(ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 4 ikilinganishwa na mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 wakati bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 6 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021.

(iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.76 katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 36.68 ya bajeti ya Taifa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wakati bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Madini ambayo ni sawa na asilimia 1.8 ya bajeti ya Taifa imeongezeka kwa asilimia 76.4 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika Kanuni ya 117 (1) na (2) pamoja na Kanuni ya 136(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo ya asilimia moja inayotozwa na Wakala wa Meli nchini Tanzania (*TASAC*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kushughulikia tozo ambayo ilikuwa ni kero kwa wafanyabiashara wa madini kuititia Gazeti la Serikali Na.154 la Februari, 2021. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kuititia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi nyingine husika kutoa elimu ya kutosha kwa wachimbaji, wafanyabiashara na wadau wote wa sekta ya madini kuhusu aina na viwango vipyta vya tozo mbalimbali vya usafirishaji madini vinavyotumika sasa kama zilivyoainishwa katika Gazeti la Serikali Na.154 la Februari, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali iendelee kuchukua hatua stahiki kupunguza tozo zote ambazo ni kero katika biashara ya madini kwa ujumla na hasa zile zinazohusika na usafirishaji wa madini nje ya nchi. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Wizara husika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Katiba na Sheria hususan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kushirikiana na kuchukua jitihada za pamoja ili kuondoa kero hii, hasa kwa kutumia Sheria ya Fedha ya mwaka 2021/2022 ambayo itapitishwa na Bunge hili la Bajeti na kwa kufanya marekebisho ya sheria nyingine husika ili kuleta unaafuu na ufanisi wa wafanyabiashara ya madini wanaposafirisha madini nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwa wafanyabiashara wa madini katika masoko ya madini. Kwa kuwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Kanuni ya Madini ya mwaka 2019 kifungu cha 6(3) kinampa haki mchimbaji mdogo wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini asitozwe Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) wala Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*); na kwa kuwa Kanuni hii ipo kimya kwa *dealers* na *brokers* ambao nao wanauza na kununua madini katika soko hilo hilo, hivyo basi Kamati inaishauri *TRA* kuacha kutumia mwanya huu wa kisheria (*loophole*) vibaya kwa kuwataka wafanyabiashara hawa pindi wanapouziana madini kutozana Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Ni rai ya Kamati kuwa Wizara na

Tume ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine watamaliza changamoto hii kwa kushirikiana kuweka uwanja sawa wa ulipaji wa kodi na hatimaye kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji na utaratibu wa masoko ya madini. Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokabili masoko ya madini kwa wafanyabiashara wa madini katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Changamoto hizi zinajumuisha masoko kutokuwa kwenye maeneo stahiki ya kibiashara; baadhi ya majengo ya Serikali kuwatoza kodi kubwa wafanyabiashara; gharama kubwa za uendeshaji masoko hayo; mlolongo wa kodi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara na Tume ya Madini kushirikiana kwa karibu na mamlaka za Mikoa ili kuainisha maeneo stahiki yenye mwamko na hadhi za kibiashara ili kutumika kama masoko. Aidha, kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazomiliki majengo yanayotumika kama masoko ya madini kupunguza kodi ili kuwaondolea wafanyabiashara wa madini mzigo mkubwa wa gharama za uendeshaji. Sambamba na kupunguza changamoto za mlolongo wa kodi kwa wafanyabiashara kutachochea ufanisi wa dhana hii njema ya masoko ya madini na kuondoa kabisa changamoto ya utoroshaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika ajira na miundo ya miradi yote ya kimkakati chini ya Wizara. Kamati inatoa rai kwa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kuzingatia mlinganyo wa kijinsia katika ajira na fursa mbalimbali zinazopatikana katika sekta hii ili kujenga uwezo wa wanawake na kutoa fursa kwao kuchangia katika ukuaji wa sekta na vipato vyao binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti ya vyeti vya kitaaluma kwa waongeza thamani madini (*Craftsmen*). Kwa kuwa katika ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo zilizofanyika mwezi Machi, 2021, Kamati imebaini kuendelea

kuwepo na sharti la kuhitajika kwa vyeti vya kitaaluma kwa wachakata madini wanaoingia nchini kutoka nchi za nje zilizobobea kwenye sekta ya usonara; na kwa kuwa mfumo unaotumika kuwapata wataalamu kwenye nchi hizo ni ule wa kurithishana ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine badala ya taaluma ya darasani; hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuondoa sharti hili ili Watanzania wengi waweze kupata utaalamu huu na hivyo kuzidi kuchangia mapato ya nchi kutokana na shughuli za uongezaji thamani wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya teknolojia za kisasa za ulinzi na usalama katika maeneo yote ya migodi. Kwa kuwa suala la ulinzi na usalama ni muhimu sana katika kudhibiti biashara haramu na utoroshaji wa madini nchini; na kwa kuwa suala hili limehusisha ukaguzi wa hali ya juu wa watu wote wanaoingia na kutoka mgodini; hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara, taasisi zake na wadau wengine wa sekta hii kutumia teknolojia za kisasa za ulinzi na usalama migodini ili kudhibiti tatizo la utoroshaji madini nchini. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba teknolojia inayotumika haina madhara kwa mwanadamu na kwamba ukaguzi katika migodi ufanyike kwa staha na kwa kuzingatia miiko mingine ya kitamaduni na kijinsia bila kuwa na unyanyasaji wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) katika mradi wa kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza. Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine tena kuiangalia *STAMICO* kwa jicho la kipekee ili iweze kuwa chachu ya kuendeleza sekta ya madini hapa nchini kwa kuipatia mtaji utakaoiwezesha shirika kujikwamua katika uendelezaji wa migodi inayoismamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa makampuni ya uchimbaji kwa jamii zinazowazunguka. Kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa utekelezaji wa jukumu hili. Wigo huu sasa ushirikishwe na Makampuni nyingine zenyeye mikataba na Kampuni za uchimbaji za kutoa huduma mbalimbali ili kuongeza ufanisi wa kimatokeo kwa jamii husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa kiuchumi wa wachimbaji wadogo wa madini. Kamati inaishauri Serikali ichukue jitihada za kutosha kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo kwa kuwatengenezea mazingira wezeshi kwa kupata mikopo yenyе riba nafuu katika benki ili kuwekeza kwa ufanisi katika sekta ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa madeni kwa watoa huduma mbalimbali katika migodi ya Serikali. Ni ushauri wa Kamati kwamba madeni yote ya watoa huduma yalipwe kwa haraka na kwa wakati ili makampuni ya kizalendo yaendelee na utoaji huduma hizi kwa ufanisi na faida bila kuathiri utendaji wao kama kampuni halali za kizalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni mahsusи ya kisekta. Uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi. Kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais kuitaka Wizara ya Madini kuruhusu uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

- (i) Kufanya utafiti na kubaini maeneo yote yenyе madini katika maeneo ya hifadhi.
- (ii) Kufanya utafiti ili kujua kwa kina aina na kiasi cha madini yaliyopo katika maeneo ya hifadhi.
- (iii) Kufanya mapitio ya sheria na kanuni za maeneo ya hifadhi na maeneo mengine yanayohusu mazingira, wanyamapori na rasilimali nyngine ili kuweka mfumo sahihi wa sera, sheria na taratibu zitakazoruhusu uchimbaji wa madini katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa madini yenyе thamani kubwa. Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia (GST) ifanye utafiti wa kina ili kugundua maeneo yote nchini yenyе madini ya thamani kubwa ambayo ndio yanayohitajika ulimwenguni kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati Teule ya Bunge kuhusu madini ya Almas

na Tanzanite. Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati Teule za Bunge kuhusu madini ya Almasi na Tanzanite ili nchi iweze kunufaika na rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Naibu Spika, kwa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge na Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za kisekta za Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaombea afya njema na uzima katika kutekeleza majukumu waliyopewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu haya ya Kamati hususan wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara. Kwa heshima kubwa, naomba majina yao kama yalivyoorodhesha yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Waziri wa Madini; Mheshimiwa Profesa Shukrani E. Manya, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini pamoja na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Simon Samwel Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Michael Chikokoto; pamoja na Makatibu wa Kamati, Ndugu Felister Mgonja, Ndugu Dunford Mpelumbe na Ndugu Angelina Sanga kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (1) na Kanuni ya 136(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Naomba Taarifa yote hii iingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutupa tena uzima na uhai na kutuwezesha kukutana ili kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati katika bajeti ya kwanza ya Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe mwenyewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuaminiwa tena kuendelea kuliongoza Bunge letu tukufu. Kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tunawatakatia afya njema ili mzidi kutimiza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yanayotekelizwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yameelekezwa katika Fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kikanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatazo:

- a) Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 [*Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020*]; na
- b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 [*Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020*].

1.2. **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelizwa chini ya Wizara ya Madini katika Mikoa ya Manyara, Mwanza na Geita. Lengo la ziara lilikua ni kujionea Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake. Aidha,

Ziara hizi zilifanyika kuanzia tarehe 11 hadi tarehe 17 Machi, 2021.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo;

- (i) Mradi wa Kituo cha Pamoja Mirerani (One Stop Centre);
- (ii) Mradi wa Kiwanda cha Usafishaji Dhahabu Mwanza (Mwanza Refinery; na
- (iii) Mradi wa Soko Kuu la Madini – Geita

1.3. Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

1.3.1 Mradi wa Kituo cha Pamoja Mirerani (One Stop Centre) Pamoja na Ukaguzi wa Mgodi wa Franone Mining Co. Ltd uliopo Mirerani

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea eneo tengefu la Mirerani ambapo ilikagua Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Pamoja (One Stop Centre). Wizara ya Madini iliingia Mkataba tarehe 30 Novemba, 2018 wenyewe thamani ya **TSh. 1,354,946,210.00** (Pamoja na VAT) na Kampuni ya SUMA JKT kwa ajili ya kusanifu na kujenga jengo la “One Stop Centre”. Wizara ya Madini ilianza kukamilisha taratibu za ujenzi ikiwa ni pamoja na kukubaliana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuwa Meneja wa Mradi wa Ujenzi huu (MOD Consulting Unit). Makabidhiano ya eneo la ujenzi yalifanyika tarehe **12/12/2018** na kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe **19/12/2018** na ujenzi rasmi wa jengo lenyewe ulianza tarehe **30/01/2019**. Muda wa ujenzi kwa mujibu wa Mkataba ulikua wa miezi sita (6) ambapo ujenzi huo ulipaswa kukamilika tarehe **20/06/2019**. Hata hivyo, kulingana na sababu mbalimbali nyongeza ya muda wa Mkataba ilitolewa hadi kufikia tarehe **14/02/2020**.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu umehusisha ujenzi wa jengo lenye jumla ya mita za mraba 712. Jengo kuu la Ofisi (Main building) lina vyumba mbalimbali kama ifuatavyo;

- (i) Ofisi za Idara ya Uhamiaji;
- (ii) Ofisi za Usalama wa Taifa;
- (iii) Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);
- (iv) Ofisi ya Jeshi la Polisi;
- (v) Ukumbi wa Mikutano;
- (vi) Ofisi ya Madini;
- (vii) Vyumba vya Mahabusu;
- (viii) Chumba cha Uthaminishaji Madini;
- (ix) Vyumba vya Mabenki;
- (x) Chumba cha Usimamizi wa CCTV Camera;
- (xi) Chumba Maalumu cha kuhifadhia Madini (Strong Room);
- (xii) Chumba cha kuhifadhia Silaha (Weapon Store and Registration);
- (xiii) Server room;
- (xiv) Stoo ya Ofisi, jiko na vyoo vya Wanawake na Wanaume.

Jengo la Ofisi Kuu (Main building) tayari limeunganishwa na huduma za umeme, Maji Safi na Taka, Mfumo wa utambuzi wa moto na mitungi ya gesi za kuzima moto, Mfumo wa Mawasiliano ya Simu, Mfumo wa TEHAMA na mfumo wa kamera za ulinzi pamoja na miundo mbinu wezeshi kama vile:-

- (i) Ujenzi wa sehemu ya Maegesho ya Magari (Paved Area);
- (ii) Ujenzi wa barabara za ndani ya ukuta kwa ajili ya kuimarisha ulinzi; na
- (iii) Ujenzi wa Mfereji wa Maji ya Mvua (Rain Water Drainage Trench).

Mheshimiwa Spika, Jengo la Kituo cha pamoja kwa sasa linatumika kama clearance house pamoja na shughuli nyingine za Kimadini ikiwemo sehemu ya kutunzia Madini na uthaminishaji, na chumba cha kamera (Control room) kwa ajili ya usimamizi wa Mifumo ya kamera inayozunguka ukuta. Kukamilika kwa jengo hilo kumesaidia wadau wa madini kupata huduma kwa uharaka kwa kuwa Taasisi zote za Serikali zinazohusika zipo katika jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mirerani umeenda sambamba na ujenzi wa miradi mingine kama Mradi wa kusimika mfumo wa umeme na taa wenyе thamani ya **TZS 716,509,473.68/=** mradi wa kamera za Ulinzi (CCTV) wenyе thamani ya **TZS 1,383,555,252.50/=** pamoja na VAT, Mradi wa Usimikaji Jenereta lenye thamani ya **Tsh. 188,000,000/=**; Mradi wa Barabara ya ndani kuzunguka ukuta wenyе thamani ya **Tshs. 331,075,000/=** na mwisho kabisa Mradi wa Ujenzi wa Vyumba viwili vya upekuzi, eneo la kupumzikia Wadau wa Madini na Soko la Madini wenyе thamani ya **Tsh. 89,000,000/=** hadi kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu wa Kituo cha pamoja umekua na manufaa makubwa kwa wachimbaji, wafanyabiashara wa madini na Serikali kwa ujumla. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

- (i) Kuongezeka kwa mapato ya Serikali yanayotokana na tozo mbalimbali za madini. Mapato yameongezeka kutoka **Shilingi. Milioni 238 mwaka 2017** hadi **Shilingi Bilioni 1.417 kwa mwaka 2020** ambalo ni ongezeko la zaidi ya mara 5 ukiliganisha na mapato yaliyokuwepo mwaka 2017;
- (ii) Kupungua kwa matukio ya utoroshaji madini yaliyokua yakiisababishia Serikali hasara;
- (iii) Kuimarika kwa ulinzi wa watu wanaofanya shughuli mbalimbali ndani ya ukuta na mali zao;
- (iv) Imerahisisha shughuli za kiutawala na usimamizi wa rasilimali madini katika eneo tengefu la Mirerani.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huu Kamati ilibaini changamoto zifuatazo;

- (i) Kuendelea kuwepo na viashiria vya Tatizo la Utoroshaji Madini katika eneo Tengefu la Mirerani Pamoja na hatua Madhubuti za Ulinzi na Usalama zilizochukuliwa katika eneo hilo;

- (ii) Pamoja na kuwepo na njia mbadala ya kudhibiti hali ya ukatikaji umeme, Kamati ilibaini kuwepo kwa Upungufu wa umeme katika gridi ya Taifa ambao unasababisha umeme kukatika mara kwa mara;
- (iii) Ukaguzi unaofanyika katika eneo Tengefu la Mirerani hauzingatii Taratibu za kuheshimu Staha na Utu wa Binadamu (Respect for human dignity). Kamati imebaini kwamba kwa Utaratibu unaotumika sasa watu Zaidi ya Kumi (10) tena wa rika tofauti wanakaguliwa kwa pamoja na wakati mwingine lugha inayotumika katika Ukaguzi ni lugha isiyo na staha;
- (iv) Kukosekana kwa huduma toshelevu ya Maji katika eneo tengefu la Mirerani;
- (v) Kukosekana kwa vifaa sahihi na vyenye kutumia teknolojia sahihi kwa ajili ya kufanya ukaguzi;
- (vi) Idadi ndogo ya vyumba vyakula viliyopo kwa sasa ni viwili. Kwa wastani watu kati ya 8000 hadi 10000 hukaguliwa kwa siku.
- (vii) Kukosekana kwa soko la madini Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea Mgodi wa Franone Mining Co Ltd uliopo ndani ya Ukuta wa Mirerani. Huu ni Mgodi unaomilikiwa na Wawekezaji wadogo wa Kitanzania kwa 100%. Mgodi huu ulianza rasmi mwaka 2011 katika eneo lake la Uchimbaji (First site) na kwa sasa unaendelea na uchimbaji katika eneo lingine. Moja kati ya Malengo ya Mgodi huu ni kuwa wachimbaji wakubwa wa Madini na kuwa na uwezo wa kwenda nchi nyingine na kuwekeza katika Sekta ya uziduaji. Kamati ilipewa taarifa na Mmiliki na Mtendaji Mkuu wa Mgodi wa Franone Mining Co Ltd Ndg. Onesmo Mbise kwamba wamekua wakipata ushirikiano wa kutosha kutoka Wizara ya Madini na Tume katika kutekeleza shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati iligundua Changamoto zifuatazo wakati wa Ukaguzi wa Mgodi huu:-

- (i) Mtaji mdogo; hivyo kupunguza ufanisi katika utafutaji wa Madini na kuathiri uzalishaji kwa ujumla;
- (ii) Miundombinu hafifu iliyopo hasa katika mfumo wa upatikanaji na utoaji wa hewa; na
- (iii) Kukosekana kwa mifumo Madhubuti ya ulinzi na usalama katika Mgodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni yafuatayo ya Jumla kuhusu Miradi hii:-

- (a) Kamati inaipongeza Serikali kuptitia Wizara ya Madini kwa kazi nzuri ya ujenzi wa Uzio pamoja na kituo cha pamoja cha Tanzanite cha Magufuli. Aidha, inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha barabara zinazoendelea kutengenezwa kwa ajili ya kuimarisha ulinzi;
- (b) Serikali itazame fursa za matumizi ya Teknolojia za Kisasa kwa ajili ya kuboresha usalama;
- (c) Kutokana na uwezo wa kamera wa kuhifadhi picha kwa muda wa miezi nane tu baada ya hapo kuzifuta bila kubaki na kumbukumbu yoyote; Kamati inaishauri Serikali kuptitia Wizara kuona namna ya kuhakikisha kumbukumbu (data) hizo hazipotei kwa kuziunganisha katika Mfumo wa Taifa wa uhifadhi wa Kumbukumbu. Ushauri Mahsuswi wa Kamati katika eneo hili ni kuongeza bajeti kwa ajili ya kugharamia uunganishwaji katika Mfumo wa Taifa wa uhifadhi wa Kumbukumbu;
- (d) Uanzishwaji wa Soko la Madini Mirerani usiue mnyororo wa biashara ya madini bali uzingatie ushiriki wa watu wengine muhimu wanaoshiriki katika mnyororo wa biashara ya Madini hasa *Dealers* na *Brokers*;
- (e) Kamati haikubaliani na namna zoezi la ukaguzi linavyofanyika katika geti la kutokea kwenye machimbo ya Mirerani na hasa kwa kutokuwa na sura ya kibinadamu. Siyo jambo sahihi Watu kumi tena wa rika tofauti kukaguliwa kwa

pamoja na wakati mwingine kulazimika kukaguliwa kwa kuvua nguo zote. Kamati inatambua umuhimu wa kufanya ukaguzi kuwa ni kunusuru upoteaji wa pato la Taifa, hata hivyo inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kurekebisha suala hili kwa kutafuta mbinu zitakazotumika kufanya ukaguzi kwa staha bila kutweza utu wa binadamu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutumia Teknolojia za Kisasa zisizo na Madhara kwa binadamu;

(f) Serikali kupitia Tume ya Madini iangalie uwezekano wa kutengeneza na kuanza kutumia Vitambulisho vyake kwa watu wote wanaoingia na kutoka katika eneo Tengefu la Mirerani. Aidha, Vitambulisho hivyo vitolewe bure na kwa kadri itakavyowezekana utengenezwe mfumo wa Kieletroniki wa kuwatambua watu wanaoingia na kutoka katika eneo Tengefu la Mirerani kila siku;

(g) Kamati imefurahishwa na Mchimbaji Mdogo (Onesmo Mbise) katika Mgodi wa Franone Mining Co. Ltd kwa ari na kasi ya maendeleo inayoonekana katika mgodi huo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri ili kupata wawekezaji wengi zaidi kama huyu na ikiwezekana kuwasaidia ili waweze kuwa na uwezo wa kufanya uwekezaji mkubwa ndani na nje ya Tanzania kwani wameonyesha utayari wa kufanya hivyo;

(h) Kutokana na uhitaji wa kuwa na soko eneo la Mirerani kuchukua muda mrefu, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua na juhudzi za makusudi ili kuhakikisha kuwa jambo hili linafanyika kwa haraka. Hata hivyo Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuzingatia manufaa kwa makundi yote wakati wa ujenzi wa soko hilo;

(i) Serikali iongeze bajeti ya Mafunzo kwa Watumishi wa Tume ya Madini katika kada ya Uthaminishaji Madini ili kupata Wataalamu wa kutosha wa Kada hii na kuongeza Ufanisi katika Eneo Tengefu la Mirerani na Masoko ya Madini kwa ujumla. Kamati imebaini kwamba kwa sasa Wataalamu wa Kada hii wapo wachache sana na Mahitaji yao kwa nchi nzima ni Makubwa sana.

1.3.2 Mradi wa kiwanda cha Usafishaji wa Dhahabu Mwanza (Mwanza Refinery);

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza ni matokeo ya Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017 ambayo yalichangia kutungwa kwa Sheria ya **The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act** ya Mwaka 2017. Sheria hiyo iliweka msisitizo kuhusiana na Rasilimali za nchi na matakwa ya nchi kufaidika na Madini yanayochimbwa nchini kwa kuyaongezea thamani kabla hayajasafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni ubia katika STAMICO, Rozella General Trading LLC ya Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) Pamoja na Kampuni ya ACME Consultant Engineers PTE Ltd ya Singapore (RGTACE). Mradi unaendeshwa chini ya Kampuni ya ubia ya Mwanza Precious Metals Refinery Ltd. Katika ubia huu, STAMICO inamiliki **asilimia 25** na wabia kwa Pamoja wanamiliki **asilimia 75** ambapo hisa za STAMICO zitakua zinaongezeka kwa asilimia **5** kwa mwaka kwa kipindi cha miaka **15** na hivyo kufanya STAMICO kuwa na hisa asilimia **51** na wabia asilimia **49**. Vilevile STAMICO itakua inapata **asilimia 2.5** ya mauzo ghafi kama huduma za usimamizi (Management Fee) ya huduma zinazotolewa na Kampuni.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa mradi huu unasimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi na Kamati ya Usimamizi wa Pamoja (Joint Management Committee-JMC). Bodi ya Wakurugenzi ina Wajumbe wawili kutoka STAMICO na Wajumbe watatu kutoka kwa Wabia. Aidha mradi unasimamiwa kwa karibu na JMC ambayo ina Wajumbe wawili kutoka STAMICO na Wajumbe wawili kutoka kwa Wabia. JMC ina wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za mradi. Uenyekiti wa JMC unazunguka kila mwaka kwa kuanza na STAMICO na baadae Mbia.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wabia ni kujenga miundombinu ya Kiwanda, kutoa utaalamu wa kuendesha Kiwanda hicho na kutoa mtaji kwa ajili ya kuanzisha vituo

vya wachimbaji wadogo vya kuzalisha dhahabu nydingi ili kuweza kulisha mtambo wa kusafisha dhahabu. Kazi kuu ya STAMICO katika mradi huu ni kusimamia uendeshaji wa vituo vya wachimbaji wadogo vitakavyoanzishwa. Kiwanda kimejengwa chini ya mamlaka Maalumu ya uwekezaji nchini (EPZA).

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kiwanda hiki uliana rasmi **tarehe 15 Machi, 2020** na kukamilika **mwezi Disemba, 2020**. Kazi ya ujenzi wa mradi huu (Civil works) inafanywa na Kampuni ya Kitanzania ijulikanayo kama **AQE Associates Ltd** yenye Makuu Jijini Dar es Salaam. Mtambo wa kusafisha dhahabu (Plant) umetengenezwa na Kampuni ya Italimpianti Orafi ya Italia. Kampuni hii ndio Kampuni kubwa na maarufu kwa utengenezaji wa mitambo ya kusafisha dhahabu duniani. Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni kufanya majoribio ya mitambo na kukabidhi (Testing and commissioning). Mradi huu unatarajiwa kuanza uzalishaji hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Gharama za ujenzi, mitambo na vifaa vinginevyo ni Dola za **Marekani Milioni 4.1** Mradi huu kwa kuanzia utatumia Dola za Marekani **Milioni 58** ikiwa ni gharama za uwekezaji (CAPEX) Pamoja na gharama za uendeshaji na ununuaji dhahabu (Gold purchase) kwa siku 10 za awali.

Mheshimiwa Spika, Shirika kwa kushirikiana na Wabia wake limeweza kuainisha vyanzo mbalimbali vya upatikanaji wa dhahabu na litakua na uwezo wa kununua dhahabu yote itakayopatikana kwa siku. Vyanzo hivyo ni kama ifuatavyo;

- (i) Wachimbaji wadogo-kupitia Mradi wa kusaidia wachimbaji wadogo (ASM support project);
- (ii) Wachimbaji wakubwa wenye Migodi hapa nchini;
- (iii) Dhahabu kutoka nchi Jirani;
- (iv) Dhahabu kutoka kwa Madalali (*Dealers/brokers*).

Mheshimiwa Spika, Mtambo huu wa kusafisha dhahabu ni wa kwanza nchini kujengwa kwa umiliki wa pamoja na Serikali na utakua na faida zifuatazo;

- (i) Utaongeza mapato ya nchi kupitia mrahaba na ada za ukaguzi;
- (ii) Utaongeza mapato kwa STAMICO kupitia huduma za usimamizi na faida ya kila robo mwaka;
- (iii) Utaongeza mapato ya Halmashauri husika kupitia ushuru wa huduma (Service Levy);
- (iv) Utaongeza ajira kwa Taifa ambapo Watumishi Mia moja na Ishitini (**120**) wengi wao wakiwa Watanzania na wachache kutoka nje ya nchi wanategemewa kuajiriwa. Ajira hizi zitajumuisha wakandarasi, wazalishaji wa dhahabu, wazabuni, watoa huduma na wasarifishaji;
- (v) Utaongeza ubora wa dhahabu kutoka Tanzania katika soko la Kimataifa. Hii itafanya dhahabu kutoka Tanzania kununuliwa na Benki Kuu duniani na kuhifadhiwa. Hii inasababishwa na matumizi ya teknolojia ya Kisasa ya kusafisha dhahabu mpaka **999.9 purity** kwa kutumia mchakato wa kusafishia dhahabu ambao kitaalamu unaitwa '*Aqua Regia Gold Refining Processes and Electrolysis Technology*';
- (vi) Utapunguza tatizo la utoroshwaji wa dhahabu kwani kutakua na soko la uhakika la dhahabu ambayo haijasafishwa na ile iliyosafishwa;
- (vii) Utaifanya dhahabu inayozalishwa Tanzania kutambulika na kuwa na nembo yake maalumu (**Originality Mark**);
- (viii) Utawezesha kuwa na kituo cha kutunza tofari za dhahabu (**Vault**) kutoka kwa wazalishaji mbalimbali wa dhahabu ndani na nje ya nchi;

- (ix) Utawezesha kuwasafishia wateja dhahabu kwa kulipia gharama nafuu na kama wakipenda wanaweza pia kuuza dhahabu yao hapo kwa bei shindanishi;
- (x) Mtambo huu utakua **Bullion Vault** ambayo itakua na viwango vya Kimataifa ikiwa inasimamiwa na Kampuni za Kimataifa kama **Brinks Global**;
- (xi) Mtambo huu utashawishi nchi Jirani zinazozalisha dhahabu kwa wingi kuja kusafisha na kuuza dhahabu yao nchini kwetu na hivyo kuongeza mapato ya Serikali;
- (xii) Kupitia Mtambo huu kutakua na fursa ya kuliunganisha Taifa letu na Taasisi kubwa duniani zinazodhibiti biashara ya dhahabu kama **London Bullion Market Association (LBMA)**;
- (xiii) Utatoa fursa ya Madini Mengineyo (**By-products**) kuainishwa na kuthaminishwa hapa nchini;
- (xiv) Utawezesha benki kuanza kununua dhahabu kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu;
- (xv) Utatoa fursa kwa Serikali kuanza kukusanya mrahaba kwa kuchukua dhahabu badala ya Fedha (*1/3 royalty in kind*); na
- (xvi) Utatoa fursa za huduma kwa jamii (CSR) inayozunguka mradi.

Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati katika mradi huu;
a) Kutokana na Mradi huu kutumia kamera yenye uwezo wa kuhifadhi picha kwa muda wa miezi sita tu na baada ya hapo kuzifuta bila kubaki na kumbukumbu yoyote, Kwa unyeti wa eneo hili Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kuhakikisha inakuwa na teknolojia yenye kutunza kumbukumbuku (data storage) kwa muda wote.

b) Mikakati madhubuti iwekwe kwa ajili ya bima (Insurance) ya dhahabu itakayouzwa Kiwandani na uhakika wa mifumo ya ulinzi wa eneo la Kiwanda.

1.3.3 Mradi wa Soko la Madini Geita

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa masoko ya Madini nchini kumetokana na changamoto kubwa iliyokua inakabili Sekta ya Madini kwa kipindi kirefu, hasa ya utoroshaji na biashara haramu ya Madini. Changamoto hiyo imekua na athari kubwa kwa upande wa Serikali kwa kukosa malipo stahiki ya tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za Madini. Aidha, athari nyingine ni kwa upande wa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa Madini kuza madini yao kwa kificho na kupelekea kutokunufaika na bei halisi ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali kudhibiti utoroshaji wa madini ikiwemo Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017 ambayo yanaelekeza kuanzishwa kwa masoko ya Madini. Msingi wa uanzishajji wa Masoko ya Madini kwa mujibu wa Sheria tajwa ni kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini, kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika na kupata bei stahiki kwa bidhaa za Madini;

Matarajio ya uanzishwaji na uwepo wa Masoko ya Madini ni Pamoja na:-

- (i) Kusaidia Wachimbaji wadogo kupata huduma ya masoko;
- (ii) Upatikanaji wa bei stahiki za Madini yanayouzwa na wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini;
- (iii) Uwazi katika biashara ya Madini;
- (iv) Kuimarika kwa ufanisi katika ukusanyaji wa Maduhuli;
- (v) Kuwa kitovu cha biashara ya Madini Barani Afrika;
- (vi) Kuondoa Tatizo la utoroshaji na biashara haramu ya Madini na hivyo kusaidia upatikanaji wa mapato stahiki ya Serikali kupitia tozo za Mrabaha (6%) na ada ya ukaguzi (1%) za mauzo ya Madini kwenye masoko; na

(vii) Upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya Madini yanayozalishwa na kuuzwa na wachimbaji pamoja na wafanyabiashara wadogo wa Madini nchini kupitia masoko.

Mheshimiwa Spika, Soko la Dhahabu Geita lilianzishwa rasmi tarehe **17 Machi, 2019**. Soko hili lina jumla ya Wafanyabiashara wakubwa wa Madini (**Dealers**) 35, jumla ya Wafanyabiashara wadogo (**Brokers**) 67, na jumla ya Masoko Madogo (**Buying Stations**) nane (8) yaliyoanzishwa katika Nyakati tofauti tofauti kwenye Wilaya za Mbogwe (1), Bukombe (1), Chato (1), Nyang'wale (1) na Geita (4). Uanzishwaji wa Masoko ya Madini umekua na mchango mkubwa katika kurahisisha biashara ya Madini na ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Spika, Madini yanayozalishwa na kuuzwa Soko la Dhahabu la Geita yamekua yakiongeze ka toka soko lilipoanzishwa Mwezi Machi 2019 kutoka wastani wa Kilogramu 160 za Dhahabu hadi Kilogramu 450 za Dhahabu kwa mwezi. Kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa Masoko ambao kwa kiasi kikubwa umeimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, kiwango kikubwa cha uzalishaji kilikua Kilogramu 124.3 Mwezi Novemba na kiwango cha chini ikiwa Kilogramu 61.9 mwezi Oktoba huku baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa Masoko kiwango cha juu cha uzalishaji kimeripotiwa kuwa kilogramu 537.6 mwezi Oktoba 2019 na chini ikiwa Kilogramu 167.7 mwezi April,2020.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Madini umeongezeka kutokana na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa Madini kwa Wafanyabiashara wasio Waaminifu, kuongezeka kwa bei katika soko la dunia hivyo kuchochea uzalishaji, kusogea huduma ya biashara ya Madini karibu na maeneo ya uzalishaji hivyo kupunguza ulazima wa kusafiri umbali mrefu kwenda kuuza madini.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mwenendo wa mauzo unaonesha kuwa mwezi Juni hadi Oktoba imekua na uzalishaji wa juu kulinganisha na miezi mingine kutokana na kupungua

ama kutokuwepo kwa mvua kunakosaidia urahisi wa usafirishaji maeneo ya wachimbaji wadogo na maji kupungua kwenye mashapo kunakochochea kupungua kwa gharama za uzalishaji na urahisi wa kufikia miamba yenye madini. Miezi yenye mvua nydingi kuanzia Januari hadi Mei imekua na uzalishaji hafifu kutokana na ugumu wa usafirishaji na maji kujaa kwenye mashapo hivyo kufanya gharama za uzalishaji kuwa juu na hivyo kuwa kikwazo kikubwa kwa wachimbaji wadogo wenye mitaji midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iligundua changamoto zifuatazo katika mradi wa Soko Kuu la Dhahabu Mkoani Geita;

- (i) Upungufu wa Vitendea kazi katika soko na vituo vya ununuzi hivyo kupelekea kufanya kazi katika mazingira magumu. Vifaa hivyo ni fenicha (Viti, Meza na Kabati); Vifaa vya kupimia ubora wa Madini (**XRF Machines & Densimeter**); Mizani za kupima uzito na Kompyuta;
- (ii) Kukosekana kwa Miundombinu thabiti ya Kamera za Kiusalama (CCTV) kwenye majengo na Ofisi za Tume ya Madini zilizopo kwenye majengo hayo hivyo kupeleka ukosefu wa mrejesho wa Kamera pale panapotokea changamoto;
- (iii) Kuwepo kwa viashiria vya baadhi ya wafanyabishara kutokua waaminifu hivyo kutorosha madini nje ya nchi kinyemela hususani madini yanayozalishwa kwenye mialo.
- (iv) Wakala wa Meli nchini (TASAC) kuendelea kuwataka wafanyabishara kulipa tozo ya Usafirishaji Madini nje ya nchi Zaidi ya Tozo zinazotozwa katika Masoko ya Madini;
- (v) Kukosekana kwa Ufanisi kwa TASAC ukilinganisha na Makampuni ya Uwakala mengine ambayo yanaweza kufanya kazi ya Usafirishaji Madini Nje ya nchi kwa Masaa Ishirini na Nne (24);
- (vi) TRA kuendelea kuwataka Wafanyabiashara wa Madini Katika Masoko ya Madini; kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

1.3.4 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

- (i) Kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji na upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo ilio chini ya Wizara ya Madini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo;
- (ii) Kamati inashauri kwamba ajira katika Miradi yote iliyokaguliwa itoe kipaumbele kwa Watanzania na izingatie fursa sawa za Kijinsia ili kujenga uwezo na ustawi wa makundi maalumu katika jamii hasa Wanawake na Watu wenye ulemavu kwa kadri itakavyowezekana;
- (iii) Kwa mujibu wa Sheria ya Madini na Kanuni za Madini za Mwaka 2019 Kifungu cha 6 Kifungu kidogo cha tatu, mfanyakibashara wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini hatakiwi kutozwa. Kodi ya ongezeko la thamani, hata hivyo TRA bado wanataka pindi wafanyakibashara wanapofanya biashara ya kuuziana madini kati yao wenyewe ("Dealers", Sonara na "Brokers") kutozana VAT. Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara kuititia Tume ya Madini wanapaswa kumaliza changamoto hii kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine ili kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.
- (iv) Gharama ya uwekezaji ya Mradi wa Mwanza Refinery (**Bilionti 10**) hazikua na ulazima kwa STAMICO kuingia ubia na mwekezaji kutoka nje ya nchi. Ni vema STAMICO ikabuni uwekezaji wenye tija kwa manufaa mapana ya Taifa;
- (v) Serikali iendelee kusimamia mifumo ya ulinzi katika Maeneo ya Miradi hasa Eneo tengefu la Mirerani na Mradi wa Kusafisha dhahabu wa Mwanza ili kuongeza usalama katika maeneo hayo na kupunguza matukio ya utoroshaji wa Madini yanayoweza kupunguza mapato ya Serikali;
- (vi) Serikali ichukue jithada za kutosha kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo kwa kutengeneza mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo kupata mikopo yenyе riba nafuu

katika mabenki ili kuwekeza kwa ufanisi katika Sekta ya Madini.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021;

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Wizara ya Madini ni kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo thabiti ya utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka kazi zilizo tekelezwa na Wizara ya Madini katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Februari, 2021 ni pamoja na: -

- (i) Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini,
- (ii) Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa Madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika sekta ya Madini;
- (iii) Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija;
- (iv) Kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za Migodi, kukusanya takwimu za Madini na kufuatilia Maduhuli yatokanayo na Madini;
- (v) Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa Masoko ya Madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika Masoko hayo;
- (vi) Kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya Madini;
- (vii) Kuendelea kuweka Mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na Madini mengine ya vito;

- (viii) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini;
- (ix) Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara;
- (x) Kuimarisha shughuli za Kitafiti za Kijiosayansi; na
- (xi) Kuendeleza Rasilimali Watu na kuboresha Mazingira ya kufanyia kazi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa kuzingatia mambo Makuu matatu ambayo ni:-

- a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2020/2021;
- b) Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina na;
- c) Utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini kwa Bajeti ya mwaka 2020/2021.

2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 547,735,863,597.00** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 526,722,547,000.00** zilipangwa kukusanya na kuwasilishwa Hazina na **Shilingi 21,013,316,597** zilipangwa kukusanya na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2021 jumla ya **Shilingi 399,352,335,099.09** zimekusanya ambazo ni sawa na **asilimia 113.73** ya lengo la **Shilingi 351, 148, 364, 666. 67** la makusanyo katika kipindi husika. Hadi kufikia Februari, 2021 Taasisi zilikusanya **Shilingi 10,494,295,901** ambazo ni sawa na **asilimia 74.9** ya Lengo la Shilingi **14,008,877,731.33** katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara na kubaini kuwa ongezeko

la makusanyo ya Wizara limetokana na Ongezeko la Ukusanyaji wa Mapato ya Mrabaha kwa Serikali ambapo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2020 hadi Februari 2021 malengo ya Wizara yalikua ni kukusanya kiasi cha **Shilingi 274,914,010,000.00**, hadi kufikia mwezi Februari 2021 Wizara ilikua imekusanya kiasi cha **Shilingi 320,419,409,107** sawa na Ongezeko la **asilimia 116.55** la Makusanyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilibaini kuwa ongezeko la makusanyo pia limetokana na ulipwaji wa ada za kijiolojia na utafiti ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Februari 2021 Lengo la Wizara lilikua ni kukusanya **shilingi 6,495,974,000.00** Aidha, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Februari 2021 Wizara imekusanya kiasi cha **5,293,255,417.32** Sawa na Asilimia **81.49** ya Lengo la Makusanyo.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa Makusanyo ya Wizara kutokana na ulipaji faini na malimbikizo ya ada mbalimbali yamepungua ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Februari 2021 Lengo la Wizara lilikua ni kukusanya kiasi cha **shilingi 3,799,284,000.00**, hadi kufikia Mwezi Februari 2021 Wizara ilikua imekusanya kiasi cha **Shilingi 1,540,645,095.24** sawa na **asilimia 40.5** ya malengo ukilinganisha na Takwimu za Mwaka wa Fedha **2019/2020** ambapo kwa kipindi husika ukusanyaji wa Fedha za faini na malimbikizo ulifiki **asilimia 140.1** ya Lengo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa punguzo la ulipaji wa faini limetokana na Wadau wengi katika Sekta kutii Sheria, Kanuni na Miongozo ya Kisekta katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati inatoa Pongezi kwa wadau wote wa Sekta ya Madini kwa kuendelea kutii Sheria bila Shuruti na inatoa Rai kwa wadau kuendelea kufuata Taratibu na Miongozo mbalimbali ili kuongeza mchango wa Sekta katika Pato la Taifa na ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza sana Wizara ya Madini kwa kuvuka lengo la makusanyo kwa mwaka 2020/2021. Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali madini, usimamizi wa

makusanyo na utoroshwaji wa madini ili kuhakikisha malengo yanafikiwa kwa vipindi vyote.

2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Bajeti ya jumla ya **Shilingi 62,781,586,000** kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,500,000,000** sawa na **asilimia 13.54** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na **Shilingi 54,281,586,000** sawa na **asilimia 86.46** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zikijumuisha **Shilingi 33,235,659,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 21,045,927,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2021, Jumla ya **Shilingi 46,280,275,324.21** zilipokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni sawa na **asilimia 85.25** ya lengo la Mwaka kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 11,723,292,682.81** sawa na **asilimia 55.7** ni Fedha za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 34,556,982,641.40** sawa na **asilimia 103.97** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Fedha za Matumizi Mengineyo kilichopokelewa kilizidi lengo la kipindi hicho kwa **Shilingi 12,590,689,975**. Fedha hizo zilitumika katika ununuzi wa Madini ya Tanzanite kutoka kwa mchimbaji wa madini Bw. Sanini Kurian Laizer.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021, Wizara imepokea fedha za Maendeleo Jumla ya **Shilingi 1,220,924,131** kutoka Hazina, sawa na **asilimia 14.4** ya lengo la mwaka. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuzunguka ndani ya ukuta wa Migodi ya Mererani, ununuzi wa vifaa vya Mawasiliano kwa ajili ya vikundi vinavyotekelza jukumu la ulinzi eneo tengefu la Mererani na kuendelea na ujenzi wa vituo vitatu vya umahiri

vilivyopo Songea, Chunya na Mpanda. Wizara iliendelea kutekeleza majukumu ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kutumia Fedha za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali (SMMRP) .

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa hali ya Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo uko chini ya malengo (asilimia 14.4), hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa kiasi cha Shilingi Bilioni 7,279,075,868.27 kilichobaki kinatolewa katika kipindi kilichobaki, ili Wizara iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake.

2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 inayoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi ya maeneo machache yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Maoni ambayo Kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ni:-

(i) Tozo ya TASAC ya Asilimia 1 ya kusafirisha Madini nje ya Nchi; Pamoja na Serikali kupokea Ushauri wa Kamati wa kusimamisha na kufuta Tozo ya TASAC ya Asilimia 1 ya kusafirisha Madini Nje ya Nchi kuititia Gazeti la Serikali Na. 154 la Februari, 2021, bado kuna haja kubwa kwa Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wachimbaji, wafanyabiashara na wadau wote wa Sekta ya Madini kuhusu aina, viwango na tozo mbalimbali za Usafirishaji Madini zinazotozwa na TASAC kama zilivyoainishwa katika Gazeti la Serikali Na. 154 la Februari, 2021. Aidha, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba Tozo hii inafutwa, Kamati inaendelea kushauri Wizara zote zinazohusika na suala hili

zikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Fedha na Mipango kuwa na Mkakati wa pamoja kuondoa Tozo zote ambazo ni kero kwa Wadau wa Sekta hii ili kuleta unafuu kwa Wafanyabiashara wa Madini na hivyo kuongeza mchango wa Sekta katika Ukuaji wa Uchumi na katika Pato la Taifa.

(ii) Kuendelea kuwepo kwa Tozo ya Zuio kwa *Dealers* na *Brokers*-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini Sura 123 inampa uhuru Mfanyabiashara wa Madini anapouza Madini yake ndani ya Soko la Madini asitozwe kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Zuio (Withholding Tax). Kamati imebaini kuwa bado Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaendelea kutoza Tozo hizo kwa *Dealers*, Masonara na madalali (*Brokers*). Ni Rai ya Kamati kwamba Tozo hizi ziondolewe mara moja ili kuleta unafuu kwa Wadau wa Sekta na kuongeza ufanisi katika Shughuli zao. Ni Rai ya Kamati pia kwamba Wizara zote husika, yaani Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zikae pamoja na kushughulikia kwa uharaka suala hili ili Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021/2022 ijumuushe suala hili na kutoa utatuzi wa kuwepo kwa Tozo hizi katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kutekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Kamati yako na kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni haya kila inapotakiwa kufanya hivyo.

2.4 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

2.4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilibaini kuwa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

umezingatia azma ya Serikali ya kuhakikisha Sekta ya Madini inafikia lengo la mchango wa asilimia 10 katika Pato la Taifa ifikapo Mwaka 2025. Kwa msingi huu, Wizara ya Madini imeelekeza Fedha za Maendeleo Jumla ya **Shilingi 15,000,000,000/=** (Sawa na **Asilimia 22.45** ya Bajeti yote ya Serikali inayoombwaa katika mwaka wa Fedha 2021/2022) kutumika katika kutekeleza Miradi ya Kimkakati ya Kisekta kama ilivyoelekezwa na Serikali .

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 wa Wizara ya Madini umezingatia Miongozo mbalimbali ya Kitaifa kama vile;

- (i) Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/2022;
- (ii) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025,
- (iii) Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022-2025/2026;
- (iv) Sera ya Madini ya Mwaka 2009;
- (v) Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025;
- (vi) Maelekezo ya Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine wa Kitaifa waliyoyatoa kwa Nyakati Tofauti ; na
- (vii) Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa Nyakati Tofauti.

Aidha, Maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 katika Sekta ya Madini na kuzingatiwa katika Bajeti ni;

- (i) Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

- (ii) Kuwaendeleza Wachimbaji wadogo na kuwawezesha Wananchi kushiriki katika uchumi wa Madini;
- (iii) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji thamani Madini;
- (iv) Kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini;
- (v) Kusimamia Mfumo wa Ukaguzi wa Shughuli za Migodi;
- (vi) Kuzijengea uwezo Taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza Majukumu yake kwa Ufanisi zaidi; na
- (vii) Kuendeleza Rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na Malengo na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, hata hivyo Kamati inatambua kwamba, kuwa na Malengo ni jambo moja na kufanya juhud au kutekeleza Mikakati kufikia Malengo hayo ni jambo lingine. Hivyo Kamati inaanini kuwa Serikali itatekeleza Mikakati iliyo nayo kwa ufanisi ili kufikia Malengo iliyojiwekea kwa manufaa ya Taifa.

2.4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 696,441,872,667 kwa mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati ilifanya ulinganisho wa Bajeti hii ya Makadirio ya Mapato na kubaini kuwa mwaka 2020/2021 Makadirio ya Mapato yalikua kiasi cha **Shilingi 547,735,863,597** hivyo kuwa na ongezeko la **Shilingi 148,706,009,070.00** sawa na **asilimia 21.35.****

Jedwali Na. 1 na Na. 2 yanaonesha kiasi cha Maduhuli yatakayokusanya na Wizara pamaoja na Taasisi zake.

JEDWALI NA. 1 MADUHULI YATAKAYOKUSANYWA NA KUWASILISHWA HAZINA MADUHULI YATAKAYOKUSANYWA NA KUTUMIKA NA TAASISI

a.	Taasisi	Makadirio ya Maduhuli
	Idara na Vitengo vya Wizara	10,002,000.00
	Tume ya Madini	650,000,000,000.00
	JUMLA	650,010,002,000.00
MADUHULI YATAKAYOKUSANYWA NA KUTUMIKA NA TAASISI		
	Taasisi ya Jidoljia na Utafiti wa Madini Tanzania	889,035,100.00
	Shirika la Madini la Taifa	45,362,835,567.00
	Kituo cha Jemolojia Tanzania	180,000,000.00
	JUMLA	46,431,870,667.00

Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022

2.4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 66,816,467,000** ikilinganishwa na **Shilingi 62,781,586,000** zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hivyo Makadirio haya ni sawa na ongezeko la **Shilingi 4,034,881,000.00** ambayo ni sawa na ongezeko la **Asilimia 6** ya Bajeti ukilinganisha na Bajeti iliyotengwa katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Kati ya Fedha hizo **Shilingi 51,816,467,000** sawa na **Asilimia 77.55** ya Bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 15,000, 000,000.00** sawa na **Asilimia 22.45** ya Bajeti yote ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 51,816,467,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na **asilimia 77.6** ya bajeti ya Wizara. Kati ya fedha hizi **Shilingi 18,480,807,000** zitatumika kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 35.67** na **Shilingi 33,335, 660,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo(OC) sawa na **asilimia 64.33** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara na Taasisi zake. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa, Nyongeza ya Fedha hizo imetokana na kuongezeka kwa fedha za Miradi ya

Maendeleo pamoja na Fedha za Matumizi ya Kawaida. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba Fedha iliyotengwa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imepungua kwa **Asilimia 12.18** ukilinganisha na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambacho ilikuwa ni **Shilingi 21,045,927,000.00**. Kamati ilielezwa sababu ya kupungua kwa bajeti ya mishahara ni kutohana na sababu kwamba Wafanyakazi wa Chuo cha Madini Dodoma (MRI) kwa sasa bajeti yao imehamishiwa katika Chuo Kikuu Dar es Salaam kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imetengewa kiasi cha **Shilingi 15,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa, Kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **Shilingi 8,500,000,000** hivyo ukilinganisha na bajeti ya mwaka **2021/2022**, Fedha za Miradi ya Maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 96.76**.

JEDWALI NA. 2 MCHANGANUO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO


Kifungu	Maelezo ya Kifungu	Mchanganuo kwa kila Taasisi	Kiasi	Jumla ya Mradi
2001 - 1119	Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini	Wizara	6,400,000,000	15,000,000,000
		Tume ya Madini	2,180,000,000	
		GST	3,400,000,000	
		STAMICO	3,020,000,000	

Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022

MWENENDO WA BAJETI YA WIZARA YA MADINI KWA MIAKA MITATU KUANZIA MWAKA 2019/2020 HADII 2021/2022

Mwaka	2019/2020	2020/2021	2021/2022
O.C	25,953,263,000	33,235,659,000	33,335,660,000
P.E	16,473,825,000	21,045,927,000	18,480,807,000
Matumizi ya Kawaida	42,427,088,000	54,281,586,000	51,816,467,000
Maendeleo	7,039,810,200	8,500,000	15,000,000,000
JUMLA YA BAJETI	49,466,898,200	62,781,586,000	66,816,467,000

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Madini 2021/2022



2.4.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022;

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Madini na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Ulingenisho huo ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelizwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulingenishaji na utofautishaji na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

- (i) Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni **Shilingi Bilioni 66,816,467,000** ni sawa na asilimia. 0.18 ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni **Shilingi Trilioni 36.3 /=.**
- (ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 4 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; wakati Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 6 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021; na
- (iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.76 katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 36.68 ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022; wakati bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Madini ambayo ni sawa na asilimia 1.8 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa **asilimia 76.4** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021.

Jedwali Na.02: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Madini dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022

BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022			BAJETI YA Wizara ya Madini 2021/2022		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh, Milioni)	% ya Junla ya Bajeti Kuu	Mgawanyo	Bajeti ya Wizara (Tsh.Billion)	% ya Junla ya Bajeti ya Wizara
OC	3,944,164	10.98	OC	33.3	49.89
Malipo ya deni	10,663,278	29.6	-	-	-
Mshahara	8,150,509	22.68	Mshahara	18.4	27.65
Maendeleo	13,255,855	36.68	Maendeleo	15.0	22.45
Junla	36,258,806	100	Junla	66.8	100

Chanzo: Uchambuzi wa randama zilizowasilishwa kwenye Kamati

SEHEMU YA TATU

2.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 117(1) na (2) pamoja na Kanuni ya 136(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini;

2.1 Tozo ya 1% inayotozwa na Wakala wa Meli Nchini Tanzania (TASAC)

Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamisha Tozo ambayo ilikua ni Kero kwa Wafanyakijabu wa Madini kupitia Gazeti la Serikali Na. 154 la Februari,2021. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi,Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi nyingine husika kutoa Elimu ya kutosha kwa Wachimbaji, Wafanyakijabu na Wadau wote wa Sekta ya Madini kuhusu aina na viwango vipyta vya Tozo mbalimbali za Usafirishaji Madini vinavyotumika sasa kama zilivyoainishwa katika Gazeti la Serikali Na. 154 la Februari,2021.

Aidha, Serikali iendelee kuchukua hatua Stahiki kupunguza Tozo zote ambazo ni kero katika biashara ya Madini kwa ujumla na hasa zile zinazohusika na Usafirishaji wa Madini nje ya nchi. Aidha, Kamati inatoa Rai kwa Wizara husika (Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Katiba na Sheria hususani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali) kushirikiana na kuchukua jitihada za pamoja ili kuondoa Kero hii hasa kwa kutumia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 ambayo itapitishwa na Bunge hili la Bajeti na kwa kufanya Marekebisho ya Sheria nyingine husika ili kuleta unafuu na ufanisi kwa Wafanyabiashara wa Madini wanaposafirisha Madini nje ya nchi.

2.2 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara wa Madini Katika Masoko ya Madini;

Kwa kuwa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni za Madini za Mwaka 2019 Kifungu cha 6 Kifungu kidogo cha tatu kinampa haki Mchimbaji mdogo wa Madini anapouza madini yake ndani ya Soko la Madini asitozwe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wala Kodi ya Zui (Withholding Tax), na kwa kuwa Kanuni hii ipo kimya kwa "Dealers" na "Brokers" ambaao nao wanaauza na kununua madini katika soko hilohilo; Hivyo Basi Kamati inaishauri TRA kuacha kutumia mwanya huu wa Kisheria (Loophole) vibaya kwa kuwataka wafanyabiashara hawa pindi wanapo uziana madini kutozana Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara na Tume ya Madini kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine watamaliza changamoto hii kwa kushirikiana kuweka uwanja sawa wa ulipaji kodi na hatimaye kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.

2.3 Uendeshaji na Uratibu wa Masoko ya Madini

Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazo kabilii Masoko ya Madini kwa Wafanyabiashara wa Madini katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Changamoto hizi zinajumuisha, Masoko kutokuwa kwenye maeneo stahiki ya kibashara, baadhi ya majengo ikiwemo ya Serikali kuwatoza

kodi kubwa Wafanyabiashara, gharama kubwa za uendeshaji masoko hayo, mlolongo wa kodi n.k. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuititia Wizara na Tume ya Madini kushirikiana kwa karibu na Mamlaka za Mikoa ili kuainisha maeneo stahiki yenye mwamko na hadhi za kibiashara ili kutumika kama masoko. Aidha, kushirikiana na Mamlaka nyingine zinazo miliki majengo yanayo tumika kama masoko ya madini kupunguza kodi ili kuwaondolea wafanyabiashara wa madini mzigo mkubwa wa gharama za uendeshaji. Sambamba na hili kupunguza changamoto za mlolongo wa kodi kwa wafanyabiashara kutachochea ufanisi wa dhana hii njema ya masoko ya madini na kuondoa kabisa changamoto ya utoroshwaji wa madini.

2.4 Uzingatiaji wa Masuala ya Kijinsia katika Ajira na Miundo Mbinu ya Miradi yote ya Kimkakati Chini ya Wizara

Kwa kuwa Wanawake na Makundi Maalumu katika Jamii ni wadau muhimu katika Sekta ya Madini na wana mchango mkubwa katika ukuaji wa Sekta hii, na kwa kuwa ni Muhimu kuwashirikisha Wanawake katika Maeneo yote Muhimu ya Sekta hii; Kamati inatoa Rai kwa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kuzingatia mlinganyo wa Kijinsia katika Ajira na fursa Mbalimbali zinazopatikana katika Sekta hii ili kujenga uwezo wa Wanawake na kutoa fursa kwao kuchangia katika ukuaji wa Sekta na vipato vyao binafsi;

2.5 Masharti ya Vyeti Vya Kitaaluma kwa Waongeza Thamani Madini (Craftmen)

Kwa kuwa katika ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilizofanyika Mwezi Machi, 2021, Kamati imebaini kuendelea kuwepo na Sharti la kuhitajika kwa Vyeti vya Kitaaluma kwa Wachakata Madini (Craftsmen) wanaoingia nchini kutoka nchi za nje zilizobobea kwenye Sekta ya usonara, na kwa kuwa Mfumo unaotumika kuwapata Wataalamu kwenye nchi hizo ni ule wa kurithishana ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine badala ya Taaluma ya darasani; Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuondoa sharti hili ili Watanzania wengi waweze kupata Utaalamu huu na hivyo

kuzidi kuchangia mapato ya nchi kutokana na shughuli za uongezaji thamani wa Madini;

2.6 Matumizi ya Teknolojia za Kisasa za Ulinzi na Usalama katika Maeneo yote ya Migodi

Kwa kuwa suala la Ulinzi na Usalama ni muhimu sana katika kudhibiti biashara haramu na Utoroshaji wa Madini nchini, na Kwa kuwa suala hili linahusisha ukaguzi wa hali ya juu wa Watu wote wanaoingia na Kutoka Migodini, Hivyo basi Kamati inaishauri Wizara, Taasisi zake na Wadau wengine wa Sekta hii kutumia Teknolojia za Kisasa za Ulinzi na Usalama Migodini ili kudhibiti tatizo la Utoroshaji Madini nchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Teknolojia inayotumika haina Madhara kwa Mwanadamu na kwamba Ukaguzi katika Migodi ufanyike kwa Staha na kwa kuzingatia Miiko mingine ya Kitamaduni na Kijinsia bila kuwa na Unyanyasaji wowote.

2.7 Uwekezaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) katika Mradi wa Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu cha Mwanza

Kwa kuwa STAMICO ina dhamana kubwa ya kuanzisha na kusimamia uwekezaji wa Kimkakati katika Miradi yote ya Madini nchini kwa niaba ya Serikali; na Kwa kuwa STAMICO tayari ni Mbia kwa niaba ya Serikali katika Mradi wa Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu cha Mwanza Refinery; Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba STAMICO inaendelea kufanya uwekezaji wa Kimkakati na wenye tija kwa nchi kwa kuhakikisha kwamba Serikali inawekeza fedha za kutosha katika kila mradi ili kuwa na umiliki wa hisa nydingi katika Miradi husika na hivyo kuongeza mapato kwa Serikali na kutoa fursa za ajira kwa Watanzania wenye sifa na vigezo stahiki. Kwa msingi huu, **Kamati inaishauri Serikali kwa mara nydingine tena, Kuiangalia STAMICO kwa jicho la kipekee ili iweze kuwa chachu ya kuendeleza Sekta ya Madini hapa nchini kwa kuipatia mtaji utakaoliwezesha Shirika kujikwamua katika uendelezaji wa migodi inayoisimamia.**

2.8 Wajibu wa Makampuni ya Uchimbaji kwa Jamii zinazowazunguka

Kwa kuwa Serikali imeendelea kusimamia kwa umakini mkubwa kuhakikisha Makampuni mbalimbali ya Madini nchini yanatoa sehemu ya mapato yake kisheria kuhudumia maeneo ya jamii zinazo yazunguka; Na kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa kwa sehemu kubwa Kampuni za wazawa zimekuwa nyuma sana katika utekelezaji wa suala hili. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa utekelezaji wa jukumu hili. Wigo huu sasa ushirikishe na Kampuni nyingine zenye Mikataba na Kampuni za uchimbaji za kutoa huduma mbali mbali ili kuongeza ufanisi wa kimatokeo kwa Jamii husika.

2.9 Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Wachimbaji Wadogo wa Madini

Kwa kuwa Wachimbaji Wadogo wa Madini ni Wadau muhimu katika Sekta ya Madini na Wana mchango mkubwa katika ukuaji wa Sekta hii na Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa kuititia Kodi stahiki na Tozo nyingine; na kwa Kuwa Wachimbaji hawa wanakumbana na changamoto mbalimbali katika utafutaji, uzalishaji na uuzaji wa Madini, Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali ichukue jitihada za kutosha kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo kwa kutengeneza mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo kupata mikopo yenye riba nafuu katika mabenki ili kuwekeza kwa ufanisi katika Sekta ya Madini.

2.10 Ulipaji Madeni kwa Watoa Huduma Mbalimbali katika Migodi ya Serikali

Kwa kuwa uwekezaji katika Migodi ikiwemo Migodi ya Serikali kama STAMIGOLD unatumia gharama nyingi sana, na Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kutumia Watanzania na Makampuni ya Tanzania katika kutoa huduma Mbalimbali za Migodini kama vile Usambazaji wa Mafuta ya kuendeshea Mitambo Migodini; na kwa kuwa bado kuna Madeni ya Watoa Huduma katika Baadhi ya Migodi ya Serikali kama

STAMIGOLD iliyo chini ya STAMICO, ni Ushauri wa Kamati kwamba Madeni yote ya Watoa Huduma yalipwe kwa haraka na kwa wakati ili Makampuni haya ya Kizalendo yaendelee na utoaji huduma hizi kwa ufanisi na faida na bila kuathiri utendaji wao kama Kampuni halali za Kizalendo.

MAONI MAHSUSI YA KISEKTA

2.11 Uchimbaji wa Madini kwenye Maeneo ya Hifadhi

Kufuatia Agizo la Mheshimiwa Rais kuitaka Wizara ya Madini kuruhusu Uchimbaji wa Madini kwenye Maeneo ya Hifadhi; Kamati inaishauri Serikali yafuatayo;

- Kufanya Utafiti na kubaini maeneo yote yenye Madini katika maeneo ya Hifadhi;
- Kufanya Utafiti ili kujua kwa kina aina na kiasi cha Madini yaliyopo katika maeneo ya Hifadhi;
- Kufanya Mapitio ya Sheria na Kanuni za Maeneo ya Hifadhi na Maeneo Mengine yanayohusu Mazingira, Wanyamapori na Rasilimali ili kuweka Mfumo sahihi wa Sera, Sheria na Taratibu zitakoruhusu Uchimbaji wa Madini katika Maeneo ya Hifadhi .

2.12 Utafiti wa Madini yenye Thamani kubwa

Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) ifanye Utafiti wa Kina ili kugundua maeneo yote nchini yenye Madini ya Thamani kubwa ambayo ndio yanahitajika Ulimwenguni kwa sasa.

2.13 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati Teule za Bunge kuhusu Madini ya Almasi na Tanzanite

Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia Kazi Maoni na Ushauri wa Kamati Teule za Bunge kuhusu Madini ya Almasi na Tanzanite ili nchi iweze kunufaika na Rasilimali ya Madini.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika, Dr. Tulia Akson (Mb) Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Kisekta za Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaombea afya njema na uzima katika kuendelea kutekeleza majukumu waliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati hususani wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara. Kwa heshima kubwa naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);

	Mwenyekiti
1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb -	Mwenyekiti
2.Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb -	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb -	Mjumbe
4. Mhe. Amina Bakari Yussuf, Mb -	Mjumbe
5. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb -	Mjumbe
6. Mhe. Hamis Mwagao Tabasam, Mb -	Mjumbe
7. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb -	Mjumbe
8. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb -	Mjumbe
9. Mhe. Jesca Jonathan Msambatavangu, Mb - Mjumbe	Mjumbe
10. Mhe. John Marko Sallu,Mb -	Mjumbe
11. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb -	Mjumbe
12. Mhe. Katani Ahmad Katani , Mb -	Mjumbe
13. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb -	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb -	Mjumbe
15. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb -	Mjumbe
16. Mhe. Mussa Omari Salim, Mb -	Mjumbe
17. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb -	Mjumbe
18. Mhe. Nicodemus Henry Maganga, Mb -	Mjumbe
19. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb -	Mjumbe
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb -	Mjumbe
21. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb -	Mjumbe
22. Mhe. Stella Martin Manyanya, Mb -	Mjumbe
23. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb -	Mjumbe
24. Mhe. Ameir Abdallah Ameir , Mb -	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mhe. Doto Mashaka Biteko(Mb) – Waziri wa Madini, Mhe. Prof. Shukrani E. Manya (Mb) - Naibu Waziri wa Madini pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Samwel Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Felister Mgonja, Ndg. Dunford Mpelumbe na Ndg. Angelina Sanga kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na Naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

29 Aprili, 2021

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza uchangiaji, ninayo orodha hapa ya wageni. Kuna Wabunge wanaongea kama wako nje hivi.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni ambao hawakuweza kutajwa kwa sababu sikuwa na majina hapa,

sasa acha niwatambue, wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Madini Profesa Simon Msanjila, alikuwa ametajwa lakini ni muhimu watu wamfahamu. Huyu ni Katibu Mkuu, halafu yupo Mhandisi David Mulabwa ambaye ni Kamishna wa Madini. Karibu sana. (*Makofi*)

Yupo pia Profesa Justinian Ikingura, huyu ni Mwenyekiti wa Bodi ya *GST*, karibu sana. Yupo Prof. Idrisa Kikula ambaye ni Mwenyekiti wa *Tume* ya Madini. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Jenerali Mstaafu Michael Isamuhyo ambaye ni Mwenyekiti wa *STAMICO*, karibu sana. (*Makofi*)

Yupo Dkt. George Mofulu, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TGC*, karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunaye Ndugu Ludovick Utoo, Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITA*, karibu sana. (*Makofi*)

Sasa nimeona siku hizi watu wanaweka huku mwanzo sijui *CPA* ama inaitwaje, lakini karibu sana kiongozi wetu.

Tunaye pia John Bina ambaye ni Rais wa *FEMATA* karibu sana. Yupo Gily Mtinda Raja ambaye ni Mwenyekiti wa *TAWOMA*. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye Damian Valente ambaye ni *General Manager* wa Nyanzaga, karibu sana. Tunaye pia Ismail Diwani ambaye ni *Country Manager* wa *PR&G*, karibu sana. Tunaye pia Honest Mrema ambaye anatoka *Shanta Gold Mine*, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Gerald Mturi ambaye ni wa *Tanzania Chamber of Mines*, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Simon Shayo, huyu ni *Vice President* wa *Geita Gold Mine*, karibu sana. Tunaye pia Hilary Diara ambaye anatoka *Barrick* ama *Twiga Minerals*. Sijui amekaa upande gani huyu! Haya, tunaye Asha Sabrina Ayoub ambaye anatoka *Boman's Tanzania Ltd.*, karibu sana. Tunaye Benedicto Baragomwa ambaye sasa ndio anamwakilisha Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, karibu sana. (*Makofi*)

Mwingine ni huyu ambaye tulishamtangaza, lakini kwa sababu tunatangaza wote sasa, tunamtangaza pia; ni Ndugu Abdul Majid Mussa Nsekela ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya *CRDB*, ahsante sana. Namwona Dkt. Kimei hapa akipiga makofi kwa nguvu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Happiness Kizigira ambaye anamwakilisha Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NBC*, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Mtendaji Mkuu wa Azania Benki na huyu ni Charles Itembe *Azania Bank* sijui atakuwa amekaa upande gani? Pia tunaye Sammy Mollel ambaye anatoka *TAMIDA*, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni wa Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Madini. Anao wageni wengine, lakini walikuwa wameshatajwa kwa makundi yao.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa nipa ninayo orodha ya Wabunge walioomba kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, tutaanza na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, atafuatiwa na Catherine Valentine Magige, Mheshimwa Tumaini Bryson Magesa, ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma ambaye imempendeza kwamba tuendelee kuwa na uhai huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kazi kubwa iliyofanyika ya kuimarisha na kuboresha sekta ya madini nchini. Wote tunafahamu kwamba biashara ya madini sifa yake kubwa kwa kipindi kilichopita ilikuwa ni biashara ya kificho. Ilikuwa inaonekana ni biashara ya ujanja ujanja, biashara ya kupiga dili, biashara ambayo Watanzania walikuwa wanaisikia pemberi pemberi, lakini Serikali iliamua kuleta heshima

kwenye matumizi ya rasilimali madini katika nchi hii. Ikaweka mikakati ambayo leo hii Watanzania ni washiriki kwenye biashara hii muhimu. Imeipa heshima biashara hii, kwamba katika Afrika leo nchi za kiafrika zinaiangalia Tanzania jinsi ambavyo imeleta mageuzi ya umiliki wa rasilimali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali. Mkipitia hotuba ya bajeti na taarifa yetu, mtaona jinsi ambavyo mchango wa sekta hii umekuwa ukiongezeka kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Sekta hii inasimamiwa vizuri, hongereni sana Wizara, hongereni sana Serikali. Wakati tukitoa pongezi hizi, tusibweteke, tuongeze jitihada kwa sababu bado nafasi ya sekta hii kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi wetu bado ni kubwa sana. Tufanye zaidi ili sekta hii itusaidie Watanzania kuondokana na umasikini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitoe rai, Bunge liliopita liliunda tume ambapo jukumu lake lilikuwa ni kuishauri Serikali juu ya jinsi gani nzuri ya kuboresha sekta hii. Mheshimiwa Spika aliunda tume iliyoenda kuchunguza Mererani, vilevile aliunda timu iliyoenda kufuatilia mambo ya almasi. Bado utekelezaji wa mapendelekezo ya tume zile haujawkenda kikamilifu. Tuongeze *speed* Serikali kushughulikia mambo yale ili kuondoa sintofahamu zisizo na msingi ambazo bado ziko kwenye sekta hii. Rai yangu ya kwanza ni hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka kuipongeza Serikai kupitia Wizara kwa jinsi ambavyo imelisimamia Shirika letu la *STAMICO*. Shirika hili ilifika mahali tulikuwa tukizungumza humu ndani ya Bunge tunasema sasa lifutwe, lakini sasa kuna mabadiliko makubwa. Shirika hii linafanya kazi nzuri. Sasa kama tulikuwa na kigugumizi cha kulipa mtaji shirika hili kwa kisingizio kwamba halifanyi vizuri, kisingizio kile sasa kimeondoka. Twendeni tukalionezee mtaji Shirika hili ili liwe jicho letu na msimamizi wetu na ushiriki wetu kwenye sekta ya madini kiuwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza *STAMICO* kwa ubunifu ambao umetuwezesha kuwa na *refinery* yetu

kule Mwanza. Muda mrefu tumekuwa tukipiga kelele kwamba ifike mahali Benki Kuu inunue dhahabu, lakini kwa sababu huko nyuma tuliunguzwa vidole, wenzetu wa Benki Kuu wamekuwa na kigugumizi cha kununua dhahabu kuitia *STAMICO* na Wizara. Tumeondoa kigugumizi kile. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *refinery* ya kisasa inayotumia teknolojia ya kisasa ulimwenguni, dhahabu itakayosafishwa pale, *purity* yake ni 99.9, hatuna sababu ya kutonunua dhahabu sasa na kuiweka kwenye *reserve* zetu za Benki Kuu. Tukifanya hivyo, tunakwenda kuhakikisha sarafu yetu inaimarika. Sasa tusiwe na kigugumizi kwenye kufanya hilo. Tuna *refinery*ile, twendeni kwa haraka kuanza kununua dhahabu tuiweke kwenye *reserve* yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo *STAMICO* bado kuna changamoto. *STAMICO* na kampuni zake tanzu bado kuna madeni makubwa ya wazabuni waliokuwa wamefanya kazi na *STAMICO*. Tumefanya kazi ya kuitia, kutathmini madeni hayo kwa muda mrefu. Vyombo vyetu vya kiserikali vimefanya kazi hii, tuache kigugumizi cha kuwalipa wazabuni wale. Tena twende tukawalipe kwa haki, tusitumie ujanja ujanja wa kukwepa madeni yale, twendeni tukawalipe stahili zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tumelisema kwenye taarifa yetu, Mheshimiwa Rais alipokuja hapa, aliagiza kwamba sasa twende tukachimbe madini yetu kwenye maeneo ya hifadhi. Rai yetu, tunaomba Wizara ije kwa haraka kufanya mapitio ya sheria zote zinazogusa eneo hill; yale yanayoleta ukinzani wa kauli ile (agizo ile la Rais) kufanyika, tuzifute, tuje na sheria mpya zitakazowezesha jambo hilo; na jambo hili tulifanye kwa haraka ili madini yale yaweze kutusaidia ndani ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu Mererani. Tunafanya kazi kubwa lakini bado ina changamoto. Teknolojia tunayotumia au ile mitambo tunayotumia, bado kuna changamoto ambazo tumezisema ndani ya Kamati, twendeni tukatumie teknolojia za kisasa kuhakikisha pale

kwenye geti tunadhibiti ipasavyo; na kule kwenye kamera zetu tuhakikishe tunaunganisha mfumo ule na mfumo wa kutunza kumbukumbu wa Taifa ili taarifa zetu zisipotee. Hili tunalisema hata kule Mwanza kwenye *refinery*, zile kamera zetu zinatunza kwa miezi sita, twendeni tukaunganishe mfumo ule na taasisi yetu ya kumbukumbu ya Taifa ili tusipoteze kumbukumbu zozote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado uwezeshaji wa wachimbaji wadogo tulifkirie zaidi, tuje na maarifa mengine. Najua Wizara imefanya kazi kubwa ya kuzungumza na mabenki, lakini tufanye kazi zaidi ili upataji wa mitaji isiwe kigugumizi, iwe ni jambo rahisi kwa wachimbaji wetu kuweza kupata mitaji ya kuingia kwenye uchimbaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwasilishaji wa taarifa yetu amepongeza tozo ile ya asilimia moja ambayo imefutwa, nami naongeza sauti yangu hapa, tunaipongeza Serikali, lakini kuna kazi ya kufanya. Tulipokwenda *field* bado wachimbaji na wauzaji wa madini walikuwa hawana taarifa kwamba sheria ile imefutwa, bado kuna watendaji wetu walikuwa wanatumia kodi ya zamani ambayo ilikuwa imefutwa. Twendeni tukalirekebishe jambo hili, na pale ambapo watu walitozwa kodi ambayo tayari ilikuwa imeshafutwa, twendeni tukafanye utaratibu wa watu wale kurudishiwa fedha zao. Maana tulichokusanya ni haramu kwa sheria. Twendeni tukawarejeshee fedha zao lakini tufanye kazi kubwa ya kutoa elimu ili sekta hii iweze kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, vibali vya wale masonara kutoka nje bado kuna kigugumizi, twendeni tukaangalie utaratibu mzuri utakaotuwezesha kupata teknolojia ile kwa wepesi ili masonara wale wanapokuja kutoka nje, waweze kurithisha ujuzi ule kwa Watanzania. Baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini

Bryceson Magessa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ajiandae.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nijielekeze kwenye mchango wangu. Naipongeza Serikali kwa kutenga masoko ya madini karibu nchi nzima. Tumeshuhudia masoko ya madini katika mikoa mbalimbali. Serikali imeshirikiana na Makatibu Tawala wa Mikoa mbalimbali, wametenga masoko ya madini na tumeshuhudia masoko hayo zaidi ya 25 na vituo mbalimbali vya madini, hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kanuni za uendeshaji wa masoko haya, tunafahamu kuwa majengo mengi ambayo yana masoko haya ni ya Serikali. Mfano tu ni jengo la *National Housing* la Dar es Salaam PSSSF ya Arusha na AICC. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa wafanyabiashara wa madini ya vito ni kwamba wanalipa VAT asilimia 18 Serikalini. Wanatozo nyingi sana ambazo wanatozwa, lakini wanapokuja kulipa majengo yale ambayo ni ya Serikali, wanapokuja kulipia kodi za majengo, wanalipa 18% ya VAT na bado wanatozo nyingine nyingi ambazo zinaenda huku huku Serikalini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, mama yetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alisema, lazima tutengeneze mazingira rafiki ya biashara. Wafanyabiashara hawa wa madini kwa kweli mazingira haya ambayo wanapitia sasa hivi siyo rafiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kuhakikisha hii VAT ya asilimia 18 ambayo wanatozwa kwenye kodi ya majengo, iondolewe kabisa wabaki na kodi nyingine. Kwa sababu zote hizi zinaenda Serikalini. Kwa hiyo, inakuwa kama tunawatoza wafanyabiashara hawa kodi

mara nyingi hali ambayo inapeleka wanashindwa kabisa kufanya biashara zao; na inasababisha wafanyabiashara ambao sio waaminifu wanatorosha madini. Kwa hiyo, ukiangalia sisi wenyewe tunatengeneza hali ngumu ya wafanyabiashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni juu ya malipo ya *PAYEE* kwa wachimbaji wadogo wa Tanzanite. *TRA* imekuwa inawalazimisha wachimbaji kulipa *PAYEE* ya shilingi 200,000/= mpaka shilingi 400,000/= kwa wafanyakazi kila mwezi. Kibaya zaidi, hakuna uhalisia wa makadirio ya *PAYEE* ambayo wanalazimishwa kulipa kwa wafanyakazi kila mwezi. Kibaya zaidi na ni *double standard* ni wafanyabiashara wa *Tanzanite* Mererani tu ndio ambao wanalipishwa hii, lakini wafanyabiashara wa dhahabu, almasi hawalipishwi hii *PAYEE* kwa ajili ya wafanyakazi wao, ni wafanyabiashara wa Mererani tu, kwa hiyo, hii ni *double standard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, *TRA* watafute njia nzuri ya kutafuta kodi, siyo kuwaonea hawa wafanyabiashara. Wanaweza wakawalipisha hata asilimia moja ya madini yaliyothaminishwa, kuliko hivi ambavyo wanafanyiwa na ni wafanyabiashara walioko Mererani tu, yaani wafanyabiashara wa madini ya *Tanzanite*, lakini kwa akina rafiki yangu Mheshimiwa Musukuma hapa Geita na sehemu nyingine nyingi hawalipishwi. Kwa hiyo naiomba Serikali iangalie hiki kitu, inakuwaje na ni kwa sababu gani, wafanyabiashara wa *Tanzanite* wa Mererani ndiyo wanalipishwa peke yao? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mchango wangu nijielekeze kwenye malipo ya fidia ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*WCF*). *WCF*wamekuwa wakitaka wafanyakazi kukatwa, kuna malipo ambayo wanatakiwa walipe ambayo hayaeleweki. Hayaeleweki haya malipo ni ya namna gani, wanakatwa wanavyotaka wao. Sasa naomba Serikali ikae iangalie haya malipo ya *WCF* yanawekwaje wekwaje! kwa sababu, ili yaweze kuwa na uhalisia kamili na vile vile, ili tutende haki kwa hawa wafanyabiashara na tutende haki

kwa hii WCF. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba wakae waangalie haya malipo yako vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan alisema, kumekuwepo na madini kwenye hifadhi zetu. Hifadhi zetu zinafahamika na akasema madini yachimbwe. Ushauri wangu kwa Serikali, tuwatumie *GST* - Wakala wa Jiolojia na Utafiti, waende kule kwenye hifadhi zetu maana zote zinajulikana, waangalie sehemu zenye madini. Bila kutumia *GST* watu wataenda watafanya tu uchimbaji holela, maana hawajui wapi kuna madini wanaenda kwa kukisia, lakini *GST* wakifanya utafiti tutajua moja kwa moja wapi kuna madini na vile vile itatusaidia kuepukana na uharibifu wa mazingira kwenye mbuga zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *GST* kama hawana pesa Wizara, Serikali iwapatie *GST* pesa, wakafanye utafiti, tujue maeneo haya ya hifadhi, ni wapi kuna madini na wapi hakuna madini ili tuepuke uvamizi. Maana watu wanawea tu kwa kuwa wameambiwa hifadhi hii ina madini, wakaenda wakavamia bila kuwa na utafiti hasa eneo gani, matokeo yake tukasababisha uharibifu wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa kumpongeza mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassani, nimpongeze sana kwa kuwa Rais mwanamke wa kwanza, wanawake tunajivunia kuwa na Rais mwanamke. Vile vile, nimpongeze Mama Samia kesho anaenda kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Naomba nimpongeze sana maana najua tunampa kura zote za ndiyo tukiwemo na sisi wanawake, tuko mstari wa mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kumpongeza mama Samia na nimwambie hatutamwangusha, tunajua utendaji wake wa kazi na tupo naye. Nina imani na haya niliyoyaongea hapa, Wizara itayafanya kazi, Mheshimiwa Doto Biteko namwamini, najua

haya mtayachukua na mtayafanya kazi kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Salim Almasi ajiandae.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii, lakini nikushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwa mchangiaji wa tatu wa Wizara hii ya Madini. Nimpongeze sana Waziri na Naibu wake Profesa Manya kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea hapa. Bajeti ambayo inatuonyesha wazi kwamba, lengo lake ni kututoa katika mchango wa Taifa wa asilimia 5.2 kwenda kwenye asilimia 10 Mwaka 2025. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa malengo ni makubwa, ni karibu mara mbili, mchango wa Taifa unatakiwa kuwa karibu mara mbili, labda nirudi kwenye bajeti yenyewe sasa. Bajeti iliyopita, tuliweka bajeti ya shilingi bilioni 62 na katika matumizi ya kawaida tulibajeti bilioni 54, lakini bajeti ya maendeleo ilikuwa bilioni 8.5. Ukienda kwenye utekelezaji wake, utaona ile bajeti ya matumizi ya kawaida ni karibu inatekelezwa kwa asilimia mpaka mwezi Machi ilikuwa karibu asilimia 112, lakini bajeti ya maendeleo imechangiwa tu kwa shilingi bilioni 1.7. Hii inaonyesha kwamba imechangiwa kwa asilimia 22 tu kwa malengo tuliyokuwa nayo. Ikionyesha kwamba nia yetu ni njema kwenda huko tunakotaka kwenda, lakini mchango wa bajeti ya maendeleo wa Serikali kwenye Wizara hii ni mdogo, asilimia 22, lakini malengo yetu ni kwenda mara mbili. Kwa hiyo, kuna tatizo hapa wanatakiwa wawezeshwe sawasawa na malengo tuliojiwekea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda mwaka huu, tuna bilioni 66 kama bajeti; matumizi yetu yatakuwa bilioni 51.8,

bajeti ya maendeleo bilioni 15, imekuwa kama mara mbili hivi. Sasa ukijuliza kwenye *trend* kama mwaka jana tumetoa 1.7 bilioni, je mwaka huu tutatoa ngapi? Kwa hiyo, kwa ushauri wangu hapa kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunatoa pesa ya kutosha kwenye bajeti ya maendeleo. Bila hivyo tutaendelea kuona ukuaji mdogo kwa sababu ni lazima *input* iwe kubwa ili tuone matokeo makubwa. Pamoja na ukuaji huo ukiangalia mwaka 2017, pato la Taifa lilichangiwa kwa asilimia 4.8, lakini 2010 asilimia 5.2. Sasa tunatakiwa kuingiza pesa nyingi kwenye bajeti ya maendeleo ili tuweze kuona maendeleo ambayo tunayatarajia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye uchimbaji unaoendelea pamoja na ukuaji huu niliouona. Tunakusanya maduhuli; ukiangalia kwenye ukusanyaji wa maduhuli, tumekusanya maduhuli mengi maana yake ukiangalia kwenye bajeti hii, utaona kwamba rasilmali watu tulioingiza huko ni kubwa ndiyo sababu, bajeti ya kawaida ya matumizi ni kubwa sana kuliko bajeti ya maendeleo. Sasa je, kwa nini *tusiji-involve* kwenye teknolojia kupunguza hiyo bajeti ambayo ni ya matumizi ya kawaida iende kwenye bajeti ya maendeleo ili tuweze kukimbia kwa haraka zaidi? Kwa hiyo, kuna kazi kubwa ya kufanya hapo, kwa mfano, mwaka huu inaonekana imepungua kidogo kama bilioni tatu na tukaongeza kwenye bajeti ya maendeleo. Je. Kwa nini tusiendelee kuipunguza hii kwa *ku-employ* teknolojia, ili tuhakikishe kwamba sasa tunaweza kukimbia zaidi kuliko tunavyokwenda sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hawa wakusanyaji wa maduhuli, nitawaonyesha usoefu wa huko ninapotoka Jimboni Busanda. Asubuhi tunapoamka, samahani nitatumia neno zito inawezekana wengine wasilijue, kwenye *illusion*, mahali ambapo tunakwenda kuingiza *carbon* zetu kuchenjua dhahabu. Utakuta *illusion* ziko labda 10 au 15 lakini *group* la kudhibiti la kwenda kukusanya maduhuli ni moja. Kwa hiyo, utakuta *illusion* namba kumi itafikiwa saa tisa jioni kwa hiyo, ni hoja yangu kwamba ushauri wa Serikali waongezwe hii timu ya ukusanyaji wa maduhuli huenda tukakusanya kuliko tunavyokusanya sasa. Wasiendelee kuwa

wale wale kwa sababu, tumekusanya kidogo kwa sababu na wale tuliowaweka kwenye utaratibu huo ni wachache. Tuwaongeze hawa ili watu wetu wasiwe na shida ya kuwapata wakati wa ukusanyaji wa maduhuli haya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nishauri, tumesema kuna ujenzi wa hawa wachimbaji wadogo wadogo, tuwawezeshe wachimbaji wadogo, hili nimekuwa nalisema mara nyngi, ni wapi wanapowezezehwa hawa wachimbaji wadogo? Tulisema *STAMICO* wanafanya kazi hii, wachimbaji wetu wadogo kwa sababu ya teknolojia na utafiti mdogo tuliokwishaufanya ndani ya nchi kwenye madini, wamehamia sasa kuchukua nafasi ya wafugaji kuishi *nomadic life*. Wakisikia leo madini yanasemwya yako Singida, wanakimbia Singida; wakisema yako Songea, wanakwenda Songea. Je, sisi hatuna *map* yetu inayoonyesha kwamba dhahabu iko wapi, *helium* iko wapi, makaa ya mawe yako wapi, ili hawa watu wasihamehame kwa mtindo huo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka niseme, kuna mahali watu wetu wanachimba uchimbaji mdogo, lakini dhahabu inatakiwa ichimbwe labda kwa wachimbaji wakubwa, inapatikana labda kilometra moja. Tumefanya utafiti huu ili tuwaambie wasiendelee kuchimba hapo dhahabu iko mbali hawataweza kuchimba kama wachimbaji wadogo wakaipata?

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nafikiri niishauri Serikali, tutengeneze Mfuko wa Madini kwa ajili ya wachimbaji wadogo, ili vifaa vya uchimbaji vipatikane mahali fulani wanapoweza kuazimwa au wanapoweza kulipia, kwa sababu, sasa hivi hatuna mahali. Ukimwambia mtu aanze kuchimba leo dhahabu au aanze kuchimba makaa ya mawe, atahitaji *billions of money* kufikia hayo madini, ana hiyo mitambo? Hana. Hivyo, naomba tutengeneze Mfuko wa Wachimbaji Wadogo ambao *tutau-tax* kutoka kwenye mapato yetu tunayoyapata sasa hivi ili watu wajue kuna *center*ya kuweza kuwasaidia mahali fulani ndani ya nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, swalilangu, Wizara inayo mpango endelevu wa madini ndani ya nchi hii? Tuna *deposit* ya dhahabu, tuna *deposit* ya almasi, je tunajua tutakuwa nayo hii dhahabu na almasi kwa miaka mingapi? Tukiulizana leo, tusije tukaendelea kuchimba baada ya miaka 15 tukabaki tuna sifuri na mwisho wa siku hatujawa na mpango endelevu ambao unatuonyesha ni nini tunakifanya ndani ya nchi! Wizara iandae mpango endelevu unaoonyesha haya madini tuliyonayo yanaweza kwenda mpaka muda gani? Ili mashimo yaliyochimbwa kwenye maeneo yetu kwa kuwa wao ndiyo wanaosimamia mazingira ya maeneo yaliyochimbwa, yaanze kufukiwa kwa sababu yamekuwa mengi sana katika maeneo tuliyopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme....

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Almas na Mheshimiwa Aida Khenan, hapana.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ili kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Madini. Pia nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, ye ye pamoja na Naibu Waziri, lakini pia na timu yote nzima ya Wizara kwa

kazi kubwa wanayoifanya. Kwa kweli tuwapongeze Wizara hii kwa kuweza kuchangia pato la Taifa na mpaka kufikia mwezi Septemba, 2020 iliweza kukua kwa asilimia sita. Kwa hiyo, tunaipongeza kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niipongeze pia Wizara kwa namna ambavyo iliweza kusimamia uanzishwaji wa masoko. Masoko haya makubwa takribani masoko 39 yalianzishwa, masoko madogo zaidi ya 41 na mengine yanaendelea kuzalishwa, yanaendelea kujengwa. Pia vituo vya ununuvi vidogo vidogo vile katika vijiji, vinaendelea kujengwa katika vijiji vyetu na hili linaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana namna nzuri ambavyo tunaweza tukazuia utoroshaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hivi vituo kuna changamoto kidogo ambayo wananchi wetu wanaweza kuipata kule. Moja ya changamoto ambayo wanaipata ni masoko haya kutofanya kazi siku za Jumamosi na Jumapili, lakini pia siku za Sikukuu. Kwa sababu, wachimbaji wetu wadogo wengi uchimbaji wao na kipato chao kinategemea kwa siku, aende asubuhi achimbe na jioni aweze kuuza. Sasa mchimbaji huyo anachimba vizuri, lakini akienda muda wa kwenda kuuza anaambiwa kwamba, sasa leo weekend'soko limefungwa. Kwa hiyo tuone njia nzuri aidha haya masoko madogo kwa maana ya *brokers* na hizi *buying station* hizi ziweze kufunguliwa siku saba za wiki na hata siku ambazo ni za sikukuu pia, ziweze kuweza kufanya kazi ili wachimbaji wetu hawa wawe na uhakika wa kuuza dhahabu zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, tumeona hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna vipaumbele ambavyo ameviweka, kipaumbele kimojawapo ni kuweza kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Kweli juhudu kubwa zinafanywa, Wizara inafanya jambo kubwa kuwaendeleza wachimbaji wadogo na sisi sote tumekuwa mashahidi tunaona namna iliyokuwa bora ambavyo wachimbaji hao wanaweza kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbuke hapo nyuma kidogo wakati Wizara imetengeneza utaratibu wa kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo iliweza kutengeneza mfumo wa kuwapa ruzuku. Wachimbaji wadogo walikuwa wanapewa ruzuku. Nakumbuka miaka kadhaa walikuwa wanapenda ruzuku na mara ya mwisho nadhani kama 2017 au 2018 ndiyo ruzuku hii ilikoma. Sasa hivi tukitaka kuweza kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo, tuweke mazingira mazuri ya kuweza kurudisha tena ile ruzuku. Ile ruzuku inawasaidia sana wachimbaji hawa, inawasaidia kimitaji na wao wanaweza kukua. Waliokuwepo Wizarani watakumbuka, wachimbaji wengi waliopata ruzuku ile miaka ya nyuma, leo hii wamekuwa wachimbaji wa kat, wameweza kukua na wao wameweza kuajiri wachimbaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Wizara iweze tena kuweza kutoa ruzuku kwa wachimbaji hawa wadogo, ili na wao waweze kukua na wao wataweza kutoa ajira, lakini pia pato kwa Serikali kwa sababu wataweza kulipa kodi vizuri zaidi. Nizungumzie suala la *GST*, *GST* hii Taasisi inategemewa sana sana na wachimbaji kwa sababu inafanya kazi kubwa na sisi wachimbaji tunaiona kazi ambayo wanaifanya. Nikiangalia kwenye taarifa hapa aliyokuwa anasoma Mheshimiwa Waziri, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza utafiti kwenye hii taasisi ni takribani bilioni 3.4 tu. Kwa kweli fedha hizi ni kidogo mno, ukiangalia kazi kubwa ambayo taasisi hii inafanya na sisi wachimbaji tunategemea iendelee kufanya. Nashauri tuone namna iliyokuwa bora zaidi kuweza kuongeza fedha kwenye Taasisi ya *GST*, ili na wao sasa waweze kuwa na nguvu kubwa Zaidi, waweze kufanya kazi vizuri, waweze kuwafikia wachimbaji wetu huko na zile tafiti zao ziweze kuwasaidia wachimbaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hii *GST* tunafahamu kwamba wako hapa Dodoma, tunashauri waweze kupewa fedha ili washuke chini huku mikoani maeneo ambako uchimbaji huu unafanyika. Wakiweza kushuka huku itatupunguzia gharama kwa wachimbaji wetu, mchimbaji anatoka Chunya, anatoka Itumbi aweze kuja mpaka Dodoma kuja kuleta mawe yake ili yafanyiwe utafiti, gharama

inakuwa kubwa lakini pia inachukua muda, angalau ikitogezwa kwenye maeneo yetu ya mikoani kule itaweza kutusaidia sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *GST* hii vile vile, ikumbukwe kwenye mabadiliko ya sheria ya mwaka 2017, iliyataka makampuni yote yanayofanya utafiti yakimaliza tafiti zao, *copy* ya tafiti zile ziweze kupelekwa *GST*. Sasa nishauri pia *GST*, zile tafiti wanazopipata waweze kuzinyambua katika lugha ambayo ni rafiki kwa sisi wachimbaji wadogo, ili baadaye wachimbaji hawa wadogo wakihitaji zile tafiti waweze kupewa, ziweze kuwasaidia katika uchimbaji ambao wanafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji ambao wapo hapa wanafahamu namna ambavyo wachimbaji wadogo wanachimba kwa kubahatisha, ni kama vile wanapiga ramli tu. Sasa tuondoke kwenye uchimbaji wa kupiga ramli, sasa twende kwenye uchimbaji ambao umefanyiwa utafiti mzuri ili wachimbaji wetu wanapochimba wawe na uhakika na kitu kile ambacho wanakifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kodi, kuna wachimbaji wetu wa ndani lakini pia tuna wachimbaji wetu wa nje. Wachimbaji wetu wa ndani ambao wanachimba nje wakitoka na mali kule kuingia nazo ndani, bado *TRA* wanawakata kodi wanavyoingia na ule mzigo hapa ndani. Hata *carbon* wakitoka nazo nje, wakiingia nazo ndani bado *TRA* wanawakata kodi na bado wakija kuchenjua, baadaye wakipeleka mzigo sokoni bado wanaendelea kukatwa kodi kwa maana ya kwamba zile tozo ya mrabaha asilimia sita na *inspection fee* asilimia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sasa tuone namna iliyokuwa nzuri zaidi ya kwamba, kama mtu anatoa mzigo nje anatuletea ndani, tusiwe tena tunamkata hiyo kodi kule. Ibakie kodi ya ndani, hii itawasaidia wachimbaji wa kwetu ambao wako nje, waweze kutoa mali kule kuleta ndani na sisi tutapata kodi kubwa zaidi hapa ndani. Kwa hiyo, upande wa kodi niishauri pia namna iliyokuwa bora zaidi ya mchimbaji

huyu wakati anauza dhahabu zake tumkate kodi kwa asilimia, pale anapouza tumkate kodi kwa asilimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itaweza kuwasaidia sana kwanza itasaidia Serikali kuweza kupata mapato ya uhakika, maana yake kila anayeuzza dhahabu yake au madini yake atakatwa kodi pale pale. Pia itaweza kuwasaidia wachimbaji wetu, mchimbaji leo anachimba, anapata leo, lakini mwisho wa mwaka anakuja kulipa kodi. Kipindi ambacho anaambiwa aliye kodi fedha nayo hana, matokeo yake anakuwa na malimbikizo ya kodi na anashindwa kulipa hii kodi. Tukiweka utaratibu huo kwa asilimia utaweza kusaidia zaidi kwa wachimbaji hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna wale wachimbaji ambaao huwa wanachimba lakini hawana eneo, hawana *claim*, hawana *PML*, sasa huyu mchimbaji huyu kila anachokipata, maana yake kama amekipata shambani kwake, huyo hawezি kulipa kodi kabisa. Sasa tukiweka utaratibu huu, maana yake hata huyu ambaye amepata dhahabu yake kwenye shamba lake, ataweza kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upande wa *TASAC*. *TASAC...*

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Almasi atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

MHE. SALIM A. HASHAM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu japo ametumia jina langu Salimu Almas jina la biashara jina langu kamili naitwa Salimu Alaudin Hasham Mbunge wa Jimbo la Ulanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niniiponge Wizara kwa kazi kubwa waliofanya kwa kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya madini mpaka hii leo kuonekana sisi pia wachimbaji wadogo ni watu ambao tunachangia katika pato la Taifa. Lakini kuna vitu vichache ambavyo napenda kuvichangia kwenye Wizara ya Madini ili kuviveka sawa inawezekana ikachangia pato zaidi kwenye upande wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natokea kwenye upande wa madini ya vito na nimekulia kwenye madini ya vito cha kwanza kabisa naomba nichangie katika upande wa *value addition*. Kwenye upande wa *value addition*, Tanzania tuna madini ya aina nyingi sana na Tanzania inaachangia duniani kwa asilimia karibu 30 kwenye madini ambayo yanaingia kwenye soko la dunia.

Lakini niseme ukweli kabisa kwamba Serikali bado hatujajipanga vizuri kwenye upande wa *value addition* na hii nitatoa mifano michache kutokana na ufinyu wa muda mfano mkubwa kabisa tuna madini aina ya safaya ambazo zinachimbwa Tanga na ambayo yanachimbwa Tunduru kwenye Jimbo la ndugu yangu Hassani. (*Makofii*)

Mheshimimiwa Naibu Spika, madini yale yamewekwa kwenye utaratibu kwamba mwongozo unasema madini yale yasafirishwe kuanzia gramu mbili kushuka chini ndio yasafirishwe yakiwa ghafi. Kwa maana hiyo kwamba madini ya juu hayawezi kusafishwa lakini kinachotokea ni kwamba kwenye upande wa safaya madini ya safaya ili yawewe kuongeza thamani lazima yafanyiwe *treatment* kwa maana yachomwe na utaalamu ule bado haujaingia kwenye nchi yetu kabisa huko *Thailand* peke yake na hawajawahi kuugawa utaalamu ule kwenye nchi zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo Serikali itakuwa imeamua kuuwa biashara ya madini aina ya safaya, vinginevyo wangeruhusu yale madini mengine yaweze kusafirishwa madini ya vito yasafirishwe yakiwa ghafi ina maana labda kuna uwezekano ingesaidia utoroshaji wa madini katika sekta ya madini. Ninayo mifano mingi lakini kutokana na ufinyu wa muda kwa sababu nina vitu vingi vya kuchangia naomba niendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upande wa *ma-valuer* kiukweli Serikali ina *ma-valuer* wachache sana kwa upande wa Tanzania katika idadi ambayo tulionayo katika takwimu inaonyesha tuna *ma-valuer* 18 peke yake ambao hawatoshi lakini naamini kabisa Serikali inapambana kuongeza *ma-valuer* lakini pia *ma-valuer* wetu wengi awana uzoefu mkubwa wa kufanya *valuation* ya madini tuliyo nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naamini kipindi ambacho wanaendelea kufanya kazi watapata uzoefu ili kujihakikishia kazi ambayo wanaifanya. Lakini pia kuna maneno yanasemekana kwamba *ma-valuer* wetu ndiko mapato yanakopotelea jibu nasema sio kweli kabisa na inawezekana *ma-valuer* hawa wanawapatia faida zaidi Serikali kuliko wafanyabiashara kwasababu mara nydingi Serikali kuliko wafanya biashara kwasababu mara nydingi wakikosea wanakosea kwenye kuongeza thamani ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kodi utakayolipa itakuwa ni kubwa zaidi naomba Serikali ijikite zaidi kuangalia madini yanapotelea wapi lakini sio mapato yanakopotelea naamini kabisa madini yakifika kwa *ma-valuer* Serikali haina kinachopoteza. Kwa hiyo, ijikite kwenye kuangalia madini yanatoroshwa vipi lakini si yanapotea kutokana na wanaofanya *valuation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa lingine naomba nichangie na hii itakuwa ni *special case* Mheshimiwa Waziri unisaidie kidogo kwenye upande wa Jimbo langu kuna kampuni mbili ambazo zinataka kuja kufanya miradi mikubwa ya madini ya kinyo yaani *graphite*. Kampuni zile ni

Tanzagraphite na ingine inaitwa Mahenge - *resource*. Mwaka 2017 walifanya uthamini juu ya kuwalipa fidia wana Kijiji wa Ipango, lakini mpaka mwaka 2019 uthamini ule ulikuwa ume-expire kwa maana hiyo kampuni ya *Tanzagraphite* ilipaswa kuwalipa posho ya usumbufu wananchi wa Ipango kulingana na kucheleweshwa na kusitishwa shughuli zao za maendeleo na waliandikiwa barua walihimizwa kwamba wafungue akaunti ili waweze kulipwa posho hizo lakini mpaka leo hawakuweza kufanya kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, na bado watu wale wamesitishwa kabisa kufanya shughuli za maendeleo kwa hiyo nilikuwa naomba kupata muhafaka wa kampuni ile nini kinaendelea na nipate muafaka mzuri nione jinsi gani ya kuwajibu na katika sehemu ambayo nilipata changamoto kipindi nafanya kampeni zangu Mheshimiwa Waziri, nilifika niliwakuta wananchi wale wamekaa chini badala ya kunishangilia. Matokeo yake ikabidi nibadilishe mukutano kwa kikao kama cha familia ili waweze kunielewa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna kampuni nyingine ya Mahenge *resource* ambayo pia imeshafanya uthamini, tunaomba pia uhalali wa kampuni ile na uhakiki wa kampuni ile kwamba ipo tayari kuja kufanya kazi katika vijiji vyetu kwasababu Isije na wenyewe wakatokea ikawa kama yenye ni *Tanzagraphite* ambako wananchi wale pia wamesitishwa zaidi ya vijiji vinne havifanyi shughuli za maendeleo.

Mheshimia Naibu Spika, naomba nzungumzie kwenye *value of chain* kwenye upande wa madini kuna mchimbaji, kuna *broker* na kuna *dealer*, ukiweka hawa watu ukiwakusanya pamoja lazima mmoja wapo... *broker* ni mtu ambaye ana mtaji mdogo mwezangu na mimi au la hana mtaji kabisa. *Obvious* mchimbaji yule hawezি kufanya kazi na *broker* akachagua kufanya kazi na *dealer*, kwasababu *wanacash*, maana yake utakuwa umemuuwa yule *broker* hawezى kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wale tunawalazimisha wakate leseni watu wanakadiliwa kodi ya mapato mwisho wa mwaka wanapaswa kulipwa na ndio wengi zaidi ambao wanaunganisha biashara kati ya mchimbaji na *dealer*. Kwa hiyo, naomba pia Serikali iliangular hili kwa kina zaidi ione ni jinsi gani inaweza kufanya mabadiliko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia nirudi kwenye upande wa *GST*bado haijafanya vizuri sana kwenye upande wake, ningeomba Serikali iwawezeshe sana *GST* waende kufanya utafiti katika madini yenye thamani kubwa kama vile kama ya *aluminum, copper lithium maganize nickel graphite, silver* na mengine mengi lakini pia kuna *layer-ath-stone* kama *ruby spinel* na madini mengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *GST* iende ikafanye utafiti mkubwa ili kuongeza wawekezaji waje kwa wingi kufanya, lakini pia Serikali iwaangular sana wawekezaji wa ndani kwa sababu wawekezaji wa ndani sasa hivi wana uwezo mkubwa wa kufanya, na iwaangular kwa jicho la tatu ili waweze kuwasaidia na hasa kwenye upande wa mikopo ya wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo hatuamini kabisa mabenki pamoja wanashauriwa kwa ajili ya kutukopesha lakini mabenki bado hayatuamini kwa hiyo tungeifanya biashara yetu iwe biashara ambayo inatambulika duniani na watu waaamini kile ambacho tunakifanya naamini Serikali yetu ingeweza kuongeza pato zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jesca David Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa John Salu ajandae.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri lakini kwa namna ambavyo anaendelea kuonesha weledi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye maeneo mawili, eneo la kwanza ni la mikataba kuwekwa wazi, wote tunajua umuhimu wa mikataba kuwekwa wazi moja ya *advantage* kubwa ambayo tutaipata ni kutengeneza *trust* kati ya wananchi na Serikali, lakini *advantage* ya pili ambayo tutaipata kama tukiwa mikataba wazi ni *investarswatajenga trust* na Serikali na kuepusha migogoro baina yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *advantage* nyiningine ambayo ni muhimu sana taasisi mbalimbali kama haki rasilimali na nyiningine vyombo vya habari, watafiti watatoa mchango mkubwa sana kushauri Serikali namna bora ya kuingia mikataba hii kwasababu watakuwa wanauwezo wa kufanya ulinganifu wa mikataba mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo Serikali liweke akili ni rasilimali za nchi yetu ya Tanzania, ni rasilimali za wananchi wa Tanzania Serikali ni wasimamizi tu, ukiangalia kwenye Sheria ya *Extractive Industry Transparency and Accountability Act* ya Mwaka 2015 sheria inaeleza *very clearly* inataka mikataba iwekwe wazi. Nataka niihoji Serikali leo kupitia kiti chako pia ni kwa nini Serikali mpaka siku ya leo toka mwaka 2015 ukiangalia mwaka 2016, 2017, 2018 mpaka hivi ninavyozungumza hapa hakuna mkataba hata mmoja ambaao umekwisha kuwekwa wazi wa kwenye sekta ya uziduaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiogope kuweka mikataba wazi, nchi zimekwishafanya hivyo, Ghana wameweka mikataba wazi, Chad wameweka mikataba wazi, Mongolia wameweka wazi *Ukraine* wameweka mikataba wazi nchi nyingi nikisema nizitaje hapa nitamaliza muda wangu sisi tunafeli wapi? Kwa nini tunashindwa kuweka mikataba yetu wazi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie ni lini Taifa letu Nchi yetu itaanza rasmi kutekeleza sheria ambayo tuliiitunga wenyewe ya kuweka mikataba wazi, asipofanya hivyo na kama hataeleza na sitaridhishwa nitashika shilingi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekee kwenye *TEIT* bado tunaendelea kuziba mianya inaonyesha uwazi, tumekataa kuweka mikataba wazi tumejiondoa kwenye *OGP Open Government partnership* tulibakiza *TEIT* kama kiashiria pekee cha afadhali *at-least* kutuonyesha mwanga nini kinaendelea kwenye rasilimali zetu. Lakini nasikitika kukuambia kwamba, *TEIT* toka mwaka 2018 mwaka wa fedha 2018/2019 hawajapewa hata shilingi tano, mwaka wa fedha 1920 awajapewa hata shilingi tano mwaka 2021 awajapewa hata shilingi tano wanafanya kazi hawa? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pesa ambayo imetoka kutoka *world bank* bilioni 1.75, nafikiri ndio hii ambayo Wizara inatazama inakwenda *TEIT*, lakini wanatakiwa wajue kwamba fedha hii imetengwa na *world bank* purposely kwa ajili ya mradi wa *EGPS*, na hii ni *extra-resource* ni lazima Serikali itenye fedha kwa ajili ya *TEIT* ili *TEIT* iweze kujlendesha yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana *TEIT* inafanya kazi kubwa sana pamoja na kutokuwana fedha nimepitia ripoti za *TEIT* 10 toka mwaka 2009 mpaka mwaka 2019, kuna mambo yanositisha kwelikweli, *TEIT* wamelipoti wanasema hivi, kuna risiti za malipo kutoka makampuni ya madini kwenda Serikalini, hazionekani na wanasema zaidi ya fedha bilioni 90 za kitanzania hazina maelezo ziko wapi na vielelezo havipo hizi sio taarifa za Jesca Kishoa ni taarifa kutoka *TEIT*. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* alipewa kazi maalum ya kuchunguza ripoti ya saba na ya nane kuangalia fedha hizo zimekwenda wapi, nataka nikujulishe leo kwenye Bunge lako Tukufu ripoti hiyo toka *CAG* amefanyia kazi imefichwa makwapani hatujaiona na hatujui hiko wapi. Nina jedwali linaonesha fedha ambazo *TEIT* imeweuka wazi ambazo zinaonesha kuna *discrapperrza* hali ya juu sana kwenye ripoti ya kwanza ya *TEIT* wanaonyesha kuna fedha ambazo risiti zake zina maelezo yake hayaeleweki milioni 24 zaidi ya bilioni 24 ripoti ya pili inaonesha zaidi ya bilioni tano hazina maelezo na risiti zake haziko wazi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya tatu inaonyesha zaidi bilioni 10 ripoti ya nne zaidi ya bilioni 2 ripoti ya tano zaidi ya bilioni nane ripoti ya sita zaidi ya bilioni 2 ripoti ya saba zaidi ya bilioni 27 ripoti ya nane zaidi ya bilioni 30 ripoti ya tisa zaidi ya bilioni 1, ripoti ya kumi zaidi ya bilioni 3. Takribani zaidi ya bilioni 90 hazina maelezo yoyote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri Serikali kuna kila sababu ya kutunga sheria ya kumpa mamlaka *CAG* aweze kuwa na mamlaka ya kukagua pesa zinazotoka kwenye makampuni na pesa zinazolipwa Serikalini. Lakini pia ipo haja kupitia kitie chako kama itakupendeza uitake Serikali ripoti ambayo *CAG* aliipitisha ripoti ya saba na ya nane ambayo aliiagua akairudisha wizarani iletwe hapa Bungeni Wabunge tuihoji na tuipitie kwa pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naushauri wangu wa mwisho kwa Serikali kama itapendeza hebu ipeni mamlaka *STAMICO* ipeni nguvu kama ambavyo mmeipa nguvu *TPDC*, ili *STAMICO* kama itakuwa ina uwezo wakuwa na *shares* iweze kusajili *shares* zake kwenye soko la mitaji *automatically* hesabu zitakazokuwa zinaingia zitakuwa zinaonekana kwasababu ukishaingia kwenye soko la mitaji, ukishapeleka *shares* zako huko *automatically* wewe hesabu zako zinakuwa wazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa John Sallu, Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza niipongeze sana wizara lakini, nianze nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri kwa sisi tunaotoka kwenye maeneo ya madini ninaweza nikasema ni waziri wa kwanza umevunja rekodi hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia niwapongeze wasaidizi wako Katibu Mkuu pamoja na timu yake na hili ni fundisho kwamba ukiangalia hii wizara, ni mjumbe wa kamati. Tunama- *professor* wa kutosha na kweli wameutendea haki u-*professor* wao. Ukiangalia tulikotoka na tulipo mwenyewe na-appreciate mchango wa *ma-professor* wa madini, wa wizara ya madini hongereni sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini nianze kwa kusema tulipofilia sasa kwenye Wizara ya hii Madini tusirudi nyuma, tusikatishane tamaa, tuangalie wapi ambapo tuna mapungufu tubadilishe twende mbele. Na mfano mzuri unaweza ukaona leo wakati unatangaza wageni pale ni wizara ya kwanza ambayo mabenki yote yamehudhuria hapa kwasababu wanajua hii wizara ni pesa. Tusirudi nyuma turekebishe yale mapungufu ambayo yamejitokeza kwenye kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilitaka kushauri kwenye upande wa *Tanzanite*, ni mjambe wa kamati, Serikali lazima tuje na utaratibu mpya na ni lazima tuambizane ukweli na Mheshimiwa Rais ametuambia tuseme ukweli. Ni aibu kubwa sana kuwa na Taifa ambalo *lina-search* watu kwa kuvua nguo hii haiwezekani! Sisi tumeenda kama wajumbe mimi nimejionea mwenyewe mwanajeshi ambaye ni jeshi ambalo tunaloliamini anafanya kazi ya *ku-search* wamasai hii ni dharau ya hatari. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama kuna mtu alikamatwa nyie ambao hamjapita kwenye machimbo, mtu anaweza kukaa huko maduarani akakaa wiki nzima hajapata hata mia tano. Kwa hiyo, mtu ukimkamata anakagonga kashilingi 2000 inasababisha watu *wa-search-iwe* kuvuliwa nguo kweli una *benefit* nini nakajiwe kashilingi 2000. Na hata ukiangalia pale kesi nydingi anakamatwa mtu na vumbi kwenye koti linathamani ya Shilingi 700 halafu mnatumia difenda kutoa pale melelani kumpeleka kituo cha polisi hii ni kitu ambacho lazima tuone namna ya kubadilisha ule utaratibu wa pale *tu-deal* na *wezi tusi-deal* na watu wanaganga njaa. Lakini lingine...

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Kuna taarifa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka,

T A A R I F A

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge, sio tu kwamba wananchi na wachimbaji wa Mererani wanavuliwa nguo, wakati ule kabla ya kamati zote mbili za Mbunge kufika, bali hata baada ya maelekezo ya Waziri wa Madini na maelekezo ya Kamati ya Madini, na baada ya ziara ya Kamati inayoshughulikia masuala ya ulinzi, mpaka leo watu 20 wanawekwa chumba kimoja, wanavuliwa nguo, zote halafu mnaambiwa mchuchumae halafu ukaguliwe na mtoto wa miaka 23, ambaye amevaa kombati za jeshi ni ukiukwaji wa haki za binadamu nchi yetu inaheshimu na kuthamini misingi ya utu, usawa na haki za binadamu. Kitendo hiki ni cha aibu ni fedheha, na mimi baadaye nitataka kujua Waziri mwenye dhamana... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka tusije tukafanya mambo kinyume na kanuni zetu sisi wenyewe, naona hapa na yeye ana fursa yake ya kuchangia baadaye, na hicho alichokuwa anakisema kwasababu kama ninavyosema siku zote sina taarifa hapa maana hizo ni tuhuma mahususi. Kwa hiyo, ndio maana sitamuuliza Mheshimiwa Musukuma kwamba anapokea hiyo taarifa au hapana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Musukuma malizia mchango wako.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina dakika mbili nilizochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana ile timu ya Spika, Mheshimiwa Ndugai, alipounda timu kwenda kuchunguza Mererani, ilifanya kazi nzuri sana, ikiongozwa nadhani na Mheshimiwa Doto na Wajumbe wengine na Tume ndiyo ilimuondoa hata ndugu yangu, Mheshimiwa Simbachawene. Baada ya hapo Mheshimiwa Rais aliunde Tume iliyoongozwa na akina Profesa Mruma na Mheshimiwa Profesa Kabudi ya kuchunguza mgogoro wa Mererani. Baada ya kutoa taarifa ilionekana yule ni mwizi na akakubali kulipa. Sasa tunatafutiana ajali, kama mtu amehojiwa na timu ya maprofesa na ameshakiri kuachia mgodi, anaitwa Bungeni kuja kuhutubia Kamati yaani *criminals* tunaanza kuwaleta Bungeni, tunarudi kubaya. Niombe, tulipo ni kuzuri, tusikubali tena kurudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nizungumzie *CSR*. Mimi natoka Geita, tulipiga makofi mengi sana, *Alhamdulillah* tunapata *CSR* shilingi bilioni 10 kwenye halmashauri yetu. Hata hivyo, hii *CSR* haina mpangilio, ni kama likitu tu limetupwa, halina mwenyewe. Wizara ya Madini na TAMISEMI ni nini kiliwafanya mkatoa uhuru wa kumuachia Mkuu wa Mkoa anakuwa anatuamulia sisi? Mkuu wa Mkoa amepewa mamlaka ya kuamua hela za Halmashauri kajenge darasa, kajenge hoteli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vingine vinauma, najua nachokiongea na Mheshimiwa Waziri anakijua. Mimi ninazo nyaraka hapa, kwa mwaka mmoja Halmashauri za Geita na Geita Mjini, Mkoo wa Mkoa na timu yake wamejilipa posho zaidi ya shilingi milioni 600; hiki kitu hakiwezekani, ninao ushahidi hapa. Kwa nini hizi pesa za *CSR* zisitumike kwenye Halmashauri yetu, watu wa *GGM* wao waje kufanya kama ukaguzi na manunuzi yote yafanywe na *procurement* yetu ya Halmashauri. Tofauti na ilivyo sasa, mmempa mamlaka Mkoo wa Mkoa kuingia kama Waziri anasema sitaki hiki, nataka hiki, sasa sisi tuna kazi gani kama Halmashauri? Niombe sana Mheshimiwa Waziri akinyanyuka hapa aje na hayo majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wanafanya kazi kubwa sana na tunapolilia maeneo mkubali kuyaachia. Natoa mfano kule Geita, kuna eneo kule Busolwa linamilikiwa na *TLS*, miaka nenda rudi. Wachimbaji wanachimba kama mbayuwayu, halafu hapa tunajisifu tunakusanya kutoka kwa wachimbaji wadogo. Mheshimiwa Waziri, ni kwa nini asitamke leo kwamba lile eneo mnawaachia vijana wetu waweze kuhangaika kwa sababu hata muda wa leseni umeshamalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba Serikali mzungumze lugha moja. Mheshimiwa Spika jana amezungumza kitu kizuri sana kwamba Serikali ni moja, inakuwa na kauli tofauti, Wizara ya Madini inatoa leseni, ukipewa leseni ukiipeleka kule unakutana na *DC* naye ana maamuzi yake. Mimi sitaki kuwa muongo, Waziri nenda Bariadi leo, leseni zina karibu miezi sita *DC* amekataa.

Sasa nauliza Wizara na *DC*nani mkubwa? Zungumzeni lugha moja, kama mnataka leseni atoe Mkuu wa Wilaya tusihangaike kuja kutupa nauli zetu huku, tukae na Wakuu wa Wilaya wamalize. Mtu anakuja anakaa mwezi, anarudi kule tena anakutana na *DC* naye ana masharti yake anataka kufuta leseni, Tanzania gani hii? Ni vizuri sana tukazungumza lugha moja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba shemeji yangu, yeye ni Mjumbe mwenzetu...

MBUNGE FULANI: Nani?

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Anajijua, amezungumza kuhusu *TEITI*. Mimi nadhani ungeshauri waongozwe hela, sisi wote tunasoma, tunaletewa ripoti Pamoja, tunachoangalia hapa *OC* ya *TEITI* wanapewa asilimia 100; tunazo taarifa. Wamefanya utafiti kwa kum-consult Mzumbe, amelipwa shilingi milioni 250 mwaka jana na sasa wanaendelea. Tunaposema hawana hela, mimi nadhani...

TAARIFA

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza sasa hivi, ye ye anazungumzia fedha za *OC*, mimi nazungumzia fedha za maendeleo ambazo zimeweza kuwawezesha *TEITI* kuendelea kuboresha majukumu yao.

NAIBU SPIKA: Kwanza kabla sijakuuliza Mheshimiwa Musukuma, nilikuwa naijiliza, hapa nimemtambulisha Mwenyekiti wa Bodii ya *TEITI*, siyo? Ama mimi ndio nilikuwa nimesoma vibaya, si yupo?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

NAIBU SPIKA: Sasa kama anayosema Mheshimiwa Jesca Kishoa yako sawasawa, hii taasisi hapa ilikuwa inafanya nini? Kwa sababu si maana yake hawafanyi kazi yoyote kwa sababu hawana hela, ndiyo maana yake. Kama hawafanyi kazi sasa hapa wamekuja kufanya nini?

Mheshimiwa Waziri atatupa maelezo baadaye kwa sababu kama hawafanyi shughuli yoyote wanatumia hela zetu kwa ajili ya nini? Maana mchango unaonesha hakuna fedha isipokuwa za kula, si ndiyo *Other Charges*. Hakuna shughuli yaani, si ndiyo maana yake? Amesema hapa mwishoni ili wafanye kazi, maana yake hawafanyi kazi. Mheshimiwa Waziri, atatufafanulia jambo hilo.

Mheshimiwa Musukuma endelea na mchango wako.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, simuelewi Mheshimiwa Jesca, hii kazi inayofanywa na Mzumbe ni matumizi ama ndiyo kazi ya *TEITI*? Sasa sielewi,

lakini najua kinachomsumbu shemeji yangu, wala msiwe na wasiwasi, ni kukaa mbali na shemeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, hilo sidhani kama ndilo tatizo la Mheshimiwa Jesca, yeye ametoa mchango wake, ufanuzi utatolewa baadaye. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tuwe na utulivu. Mheshimiwa John Sallu, atafuatiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

MHE. JOHN M. SALLU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vilevile, naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri walifanya ya kuifikisha sekta yetu ya madini hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natajikita zaidi kwa wachimbaji wadogo. Wachimbaji hawa wana mchango mkubwa sana kwenye sekta ya madini na kwenye pato la Serikali kwa jumla. Kama ilivyoelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukiangalia upande wa madini ya dhahabu, wachimbaji wadogo wamechangia asilimia 30; kwa kweli nawapongeza sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nawapongeza sana wachimbaji wadogo kwani ndyo wagunduzi wakubwa wa madini ndani ya nchi yetu, pamoja na kwamba hawana vifaa. Migodi yote inayochimbwa karibuni wamegundua wao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji hawa wadogo tunatakiwa tuwashike mkono, Serikali pamoja na Wizara tutafute namna sahihi ya kupata mikopo yenye riba nafuu. Napenda kuyashauri mabenki yatafute namna ya kuzungumza na wachimbaji ili wajue hasa sekta inakwendaje, kwa sababu inaonekana hawaamini kuwakopesha wachimbaji wadogo, lakini nina imani wakikaa kwa pamoja

watakuja na namna sahihi ya wachimbaji hawa kuweza kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawakaribisha mabenki kwenye Jimbo langu la Handeni Vijijini, tuna vijihi zaidi ya kumi ambavyo vinachimba dhahabu; vijihi zaidi ya saba vinachimba *feldspars*; vijihi viwili vinachimba *dolomite*. Kwa hiyo, tuna vijihi zaidi ya 30 ambavyo vina madini mbalimbali, mabenki waje tukae nao tutafute namna sahihi ya kuweza kuwakopesha wachimbaji wadogowadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwa upande wa *GST*. *GST* inatakiwa itoe mchango mkubwa kwenye kuangalia wapi pana madini na kwa kiasi gani. Katika Jimbo langu la Handeni Vijijini, tuna madini ya chuma, *graphite* na dhahabu lakini wachimbaji wale hawawezi kujua chuma kile tulichokuwa nacho pale kiko kingi kiasi gani au *graphite* ile iko nydingi kiasi gani. Vilevile hii ni faida kwa Serikali kwani tukijua tuna *graphite* kiasi gani na tuna madini ya chuma kiasi gani, tunaweza kujipanga tuone tufanyeje kwa sababu kupanga ni kuchangua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uongezaji thamani madini. Jambo hili tukilitumia vizuri litatusaidia sana kwenye upande wa ajira za vijana wetu, kwani uongezaji thamani madini siyo lazima madini ya dhahabu au almasi peke yake, kuna madini ya viwandani ambayo yanaweza kutumika kutengeneza vitu mbalimbali. Kwa mfano, *insulators* za umeme na vito mbalimbali, nina maana vipuri vya akina mama vinaweza kutengenezwa kutokana na madini ya *feldspars*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa mfano nchi ya China, utakuta *insulators* zinatengenezwa na viwanda vidogo sana, ni kama *SIDO type*. Kwa hiyo, tukiweza kutafuta ujuzi tukawapa watu wetu ujuzi, kama vile ambavyo imefanya kwenye vikundi vya akina mama na vijana kupewa ujuzi wa kutengeneza sabuni na batiki, basi tukatengeneza namna vijana wakapata ujuzi wa kutumia

malighafi hii ya madini ya viwanda, itatusaidia sana kuongeza ajira kwa vijana wetu na kuongeza pato la madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala, naomba na mimi nichangie katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayoendelea kuifanya, lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba tunaona kabisa Wizara ya Madini inavyofanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba inachangia pato la uchumi wa nchi yetu katika kuimarisha mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Madini kwa kuanzisha masoko mbalimbali na hasa katika Jimbo langu la Msalala, tumeona Waziri wa Madini ameweza kutoa maelekezo na Serikali imeweza kuanzisha masoko ya madini katika Kata za Bulyanhulu na Segese. Niombe tu Mheshimiwa Waziri baada ya kikao hiki cha Bunge basi uweze kutembelea ili kusikiliza changamoto za wachimbaji wadogo katika maeneo hayo, hususan Kakola, Bulyanhulu na Kata ya Segese.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hotuba ya bajeti ilivyoelezea juu ya namna gani Wizara imejipanga katika kuhakikisha kwamba inakwenda kuwawezesha wachimbaji wadogowadogo. Niipongeze Wizara inafanya jitihada kubwa katika kuhakikisha kwamba inawawezesha wachimbaji wadogowadogo, lakini ni ukweli usiopingika kwamba bado

kuna changamoto ndogondogo ambazo kimsingi niombe Wizara iweze kuzishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii *STAMICO* wameonesha mkakati wao kwamba wanakwenda kujipanga katika kusimamia na kuwawezesha wachimbaji wadogo. Hata hivyo, katika maeneo yetu wachimbaji hawa wamekuwa wakinyanyasika sana kwa kukosa mitaji au mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali. Niombe Wizara iweze kufikiria sasa namna gani wanaweza kuanza kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo ambao ndiyo shokomzoba ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa mchango wa wachimbaji wadogowadogo katika kuchangia uthumi wa pato la Taifa. Ni ukweli usiopingika kuwa hawa watu wanafanya kazi ngumu sana. Naomba nishauri twende tukaweke mkakati kuhakikisha kwamba tunakabiliana na matapeli kwa sababu wamekuwa wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ametueleza hapa namna gani wamefanya jitihada kuwapatia wachimbaji wetu wadogo leseni, niipongeze Wizara katika baadhi ya maeneo yangu hususan Nyangarata na maeneo mengine katika Jimbo la Msalala, Wizara wamefanya hivyo lakini namna gani wanakwenda kutoa leseni hizi lazima tukueleze leo na tutoe ushauri, kwamba watu wanaokwenda kupata leseni katika maeneo haya ni watu ambao kimsingi sio *original* katika maeneo yale na wengi wao ukiwatafuta unakuta ni madalali. Leo hii unakuta mtu anamiliki shamba, lakini siyo shamba tu ameanzisha uchimbaji na akagundua madini katika maeneo yale, anatoka mtu anakotoka anakuja na leseni kujitambulisha pale na anasema yeye ndiyo mmiliki halali wa maeneo yale. Hii inamnyima haki mchimbaji wetu na tunampa kazi ngumu katika kuhakikisha kwamba anachangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Waziri wa Madini wakae kama Wizara waone namna gani wanaweza

wakauboresha huu mfumo wa kuomba kwa mtandao (*portal*). Watu wetu huko vijiji network hakuna Mheshimiwa Waziri inawanyima haki ya wao kumiliki leseni hizi. Niombi Wizara iweze kuona namna gani wanaweza wakaweka mfumo mzuri ili iweze kuwarahisishia wachimbaji wetu wadogo, hususan wakazi wa Bulyanhulu, Nyangarata, Segese na maeneo mengine katika Jimbo langu la Msalala kuwa na haki hii ya kuweza kupata leseni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali, imefanya kazi kubwa kuhakikisha wanaunda ubia kati ya Twiga na Serikali na nipongeze jitihada ambazo zimesemwa. Mimi nzungumzie suala hili katika maeneo mawili; katika *local content* na fedha za *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Musukuma amesema hapa katika Jimbo lake la Geita wanapewa fedha za *CSR* kiasi cha shilingi takribani bilioni 10, lakini inasikitisha kuona Jimbo langu la Msalala ambalo tunamiliki Mgodi wa Bulyanhulu, tunapokea fedha za *CSR* bilioni 2.5 tu na wakati migodi yote ipo Tanzania. Kwa nini Geita wapokee bilioni 10 na sisi tupokee bilioni mbili? Namwomba Mheshimiwa Waziri akimaliza hapa tufanye ziara tuone ni kwa nini kuna tofauti hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote tunayojadili hapa ni ukweli usiopingika kwamba watumishi wa kwenye Tume ya Madini ni wengi lakini bajeti yao ni ndogo. Ukiangalia watumishi katika Wizara ni wachache lakini bajeti kubwa inakwenda Wizarani na hii inasababisha Tume ya Madini isifanye kazi zake kiuhanika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni haya; *GGM* na makampuni mengine yote, hususan nzungumzie katika Jimbo langu la Msalala, Bulyanhulu pale, kumekuwa na uvunjaji mkubwa wa sheria ya *local content*. Leo hii tunazungumzia namna gani ya kuwakuza wachimbaji wadogo kutoka katika ngazi ya chini kwenda ngazi ya kati na tuwafanye wachimbaji hao wawe wakubwa lakini ni ukweli usiopingika tunaona kabisa migodi hii wanachangia kwa kiasi kikubwa kuvunja

Sheria ya *Local Content*. Tuna wafanyabiashara wana uwezo wa ku-*supply* katika migodi yetu hii hawana kazi, kumekuwa na matapeli katikati hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikiwa bado *M-NEC* nilimsikia Mheshimiwa Waziri akitoa maelekezo katika Mgodi wa *GGM* waweze kutekeleza sheria hiyo ya *local content* kuhakikisha kwamba wazawa wanapewa nafasi lakini watu hawa wana kiburi, hawajatekeleza yale aliyowaambia. Watu hawa wana dharau kubwa, nenda kawaeleze kwamba sisi kama wananchi tunaoishi katika maeneo yale ya mgodi tuna-*play part* kubwa ya kuhakikisha usalama wao na mali zao na ni lazima sasa wakazi tunaoishi katika maeneo yale hususan Bulyanhulu na meneo mengine kama ya Bugarama tunanufaika na migodi hiyo. Kama leo hii hawataweza kutekeleza sheria hii ya *local content*...

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kassim, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nampa taarifa mzungumzaji kwamba baada ya tamko la Mheshimiwa Naibu Waziri kule *GGM* kwamba *GGM* watekeleze *local content*, walitekeleza kwa kutoa zile kazi kama ku-*supply* nyanya na vitunguu, zile kazi zenye maslahi zote wanafanya Wazulu.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, napokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Musukuma kwa mikono miwili na sisi Wanamsalala tulishafikisha kilio chetu ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kassim, inabidi usubiri kwanza nikuite tena ndiyo uzungumze. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupokea taarifa hii kwa mikono miwili, lakini unisamehe kwa sababu ya unjuka, nitazoea. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana asilimia 100 na Mheshimiwa Musukuma. Leo hii makampuni haya ni ukweli usiopingika Mheshimiwa Waziri anafahamu, baada ya kuona Wizara imeweka mifumo ya kudhibiti utoroshaji wa madini sasa wameamua kuja na mfumo mpya kuhakikisha wanatupiga sisi Serikali lakini pia Halmashauri yangu ya Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nimeshalifikisha kwa Waziri na naomba alishughulikie haraka iwezekanavyo. Tumekuwa wavumilivu sana wananchi wa Bulyankulu na Msalala. Tunatamani mgodi huu uendelee kuwepo, leo hii tulikuwa tunazungumza kwamba kampuni hizi zimeanzisha kampuni ndogo pale Dar es Salaam, *TCL* Mheshimiwa Waziri, tumeshalizungumza hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mama anayelima nyanya katika Jimbo langu hawezi *ku-supply* nyanya kwenye mgodi mpaka aende Dar es Salaam. Hivyo mnatutoreshea mapato katika Halmashauri yetu. Naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri suala la barabara, fedha nendeni mkatekeleze haya barabara ianze kuititika. Mimi na wananchi wangu tumekubaliana ikifika mwezi wa Saba barabara haijatengenezwa, fedha hazijatoka, Mheshimiwa Waziri sisi tutaziba barabara, kwa sababu wananchi wangu wanahangaika mno. Tunanufaika vipi na madini haya kama wananchi wetu wanakula vumbi? Kwa hiyo, naomba Wizara ya itekeleze haya ili wananchi wetu waweweze kunufaika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja asilimia mia moja na mbili. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kassim Iddi. Nikutoe wasiwasi, humu ndani Wabunge wote ni wapya tu. Ninyi wenyewe mnampongeza kila siku hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ni Mbunge wa Kipindi cha Kwanza. Sasa ye ye ana tofauti gani na Wabunge ambao wamekaa sana humu na wengine hata hawasomi hiyo vitabu vinavyoletwa hapa? (*Makofii*)

Kwa hiyo, hakuna hoja ya Mbunge mgeni na mwininge mwenyeji. Wote kanuni zipo hapa na wakati mwininge wote tu mnakosea kanuni humu ndani. Kwa hiyo, wote tuna hadhi sawa. Hata mimi mwenyewe, naulizwa hata mimi? Hata mimi ni Mbunge mgeni. Ndiyo Mbunge wa Mbeya Mjini sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza na kama muda utaruhusu, tutamalizia na Mheshimiwa Deo Mwanyika.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nianze kuipongeza Wizara kwa bajeti yao nzuri, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri ambayo imeleta mapinduzi makubwa kwenye Wizara hii ya Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kusimamia vizuri suala la malipo ya mipasuko kwenye Jimbo langu la Geita. Tulikuwa na tatizo la mipasuko ambalo liliidumu kwa takribani miaka 20, lakini Mheshimiwa Waziri alikuja akaweka mguu chini na sasa *GGM* wamewalipa wale wananchi. Naomba kuwapongeza *GGM* na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelekezo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru sana juhud za Wizara. Pale Geita Mjini tumekamilisha *refinery* ya kisasa kabisa ambayo imejengwa na mwananchi Mtanzania na ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri atakuja na mpango mzuri ili kuhakikisha kwamba ile *refinery* yao ya Serikali isije ikawa inachukua mzigo wote Geita na kupeleka kule, kwa

sababu tunataka kuona ile *refinery* inaendelea kufanya kazi Geita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichosababisha mafanikio makubwa kwenye Wizara ya Madini ni baada ya Wizara hii kukaa na wadau na kuondoa utitiri wa kodi na kufanya watu kuwa walipa kodi wa hiari. Jambo hili limetufundisha kwamba kumbe siyo lazima kutumia nguvu nyingi, sheria nyingi, tozo nyingi ili tuweze kukusanya kodi. Sasa ni kwa mtazamo huo huo naiomba sana Serikali kuangalia maeneo yote ambayo wananchi wanalalamikia kuhusu tozo na kodi nyingi kuziondoa ili kufanya mazingira ya kufanya biashara kuwa mepesi Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hapa wakati wanachangia kwenye Mpango kwamba shida kubwa tullyonayo sasa kwenye wachimbaji wadogo wadogo ni *investment vis-a-vis production* inayofanyika kwenye madini, kwamba uwekezaji ambao wachimbaji wadogo wanaweka ni mkubwa sana kuliko faida ambayo wanaipata. Watu wengi wanaweza kuona mauzo yameongozeka, lakini katika wachimbaji wadogo 100 wanaoweka pesa zao, ni wachimbaji watano au 10 ndiyo wanaoweza kurudisha gharama, *the rest* wote wanakula hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini? Kwa sababu wanachimba kwa kubahatisha, wanachimba kwa kupiga ramli, wanachimba kwa kufuata mkumbo. Jambo hili limezungumzwa vizuri na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tuwape uwezesho *GST* wawe na *league* za kutosha. Hizi *league* nne ambazo wanazo, Tanzania ina madini kila mkoa na kila wilaya. Wawe na *league* za kutosha, tuajiri *manpower* za kutosha tuache kupeleka watu kwenda kupiga ramli na ndiyo maana msishangae kuona kwamba katika maeneo mengi ya machimbo ya madini Waganga wa Kienyeji wana soko sana kwa sababu wanapiga ramli sana na hii ni hatari sana katika nchi ambayo imepiga hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Geita pale mitaa yangu na Vijiji vya Magema, Nyamalembo, Katumaini, Mizingamo na Katoma imekuwa kwenye mgogoro mkubwa na mgodi wa *GGM* kwa takribani miaka 20. Eneo la *GGM* ni *Square kilometer* 192, eneo wanalochimba ni kama asilimia 10 ya eneo hilo. Eneo hili la vijiji hivi limewekewa ulinzi sasa wa Polisi. Wananchi wakienda shambani wanakutana na Polisi, wakienda kukata kuni wanakutana na Polisi, akichimba choo, anakutana na Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama Mheshimiwa Waziri, kule kwao Bulangwa wananchi wakiwa wanakutana na Polisi kila siku wanaweza kuishi kwa raha. Lile eneo wananchi wanasubiri fidia. Eneo lile ni kilometra zaidi ya 15 kutoka kwenye *pit* ya mgodi. Kama eneo lile ni *potential*/kwa mgodi hakuna sababu ya kulundika Polisi pale kulinda raia wanaoenda kulima na kukata kuni, wawalipe wale wananchi waondoke pale. Hakuna sababu ya watu kuishi kwa *tension* wakiamka asubuhi kwa *tension* kwa sababu tu lile eneo lipo ndani ya leseni. Leseni ya mgodi ni kubwa lakini hawaja tayari kulitumia eneo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wananchi hawa wanaendelea kuishi kama vile ni wakimbizi wapo kwenye nchi ya vita. Hatuhitaji sisi kuja kuona Polisi wanajaa kwenye mitaa yetu, waje wakamate kama kuna wahalifu, hatuvamii eneo linalochimbwa, hatuna shida na kule na tunaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme ukweli, kama kuna mtu anafaidika na uwepo wa wachimbaji wakubwa ni Geita. Nasi tunataka waendelee kuwepo, tunawaunga mkono, tunawaomba wananchi waache kuvamia maeneo yao, lakini kwenye makazi yao ambayo hawajalipwa fidia. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana wananchi wapewe uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, Mheshimiwa Musukuma amezungumza hapa kuhusu *CSR*. Nilizungumza

wakati nachangia Mpango kwamba tulitunga sheria nzuri sana, tukasema kwenye eneo la *Service Levy* 0.3 percent inalipwa Halmashauri. Haijulikani kwenye *CSR* ni percent ngapi? Shida kubwa nyingine tuliyonayo ni kwamba pesa hizi za *CSR*, sheria imebaki kimya kwenye manunuzi na kwenye matumizi. Sawa zinabaki kule *GGM*, tunashirikiana na *Local Council*, lakini matokeo yake zimekosa usimamizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwangu *supervision* peke yake nilikuwa nacheki, imegharimu zaidi ya shilingi milioni 250 ambazo zinalipwa kwa viongozi wanaokuja kuangalia kazi zilizofanywa na *CSR*. Sasa Mheshimiwa hii ni pesa ambayo inakuwa *declared* kwenye kodi, kwa sababu anapotoa hii pesa mwisho wa siku anasema kwenye kodi nimepeleka hizi pesa kwa wananchi. Huyu Mtumishi wa Umma anaenda kulipwa *supervision* shillingi milioni 250 akiwa ndani ya eneo lake? Anatumiaje zile pesa namna hiyo. Naomba hii sheria iwekwe vizuri, hizi pesa zibaki kwa wenye mgodi, lakini matumizi yake yafuate sheria za matumizi ya pesa za Umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema hapa Mheshimiwa Iddi, nilisema wakati ule *Local Content* wamekudanganya kwamba wamefuata sheria. Pale *logistic* wanazotoa, ni kazi ndogo ndogo, lakini sheria inasema zile bidhaa ambazo hazipatikani Tanzania, waingize ubia na Watanzania, lakini halifanyiki hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapigwa pesa kwa sababu kupitia *Local Content* kuna *transfer pricing*. Kama hakuna *Local Content*, akija mtu anayeuzza kutoka nje, kinachofanyika ni kufanya gharama ya manunuzi kuwa makubwa na matokeo yake pesa hizi zinarudi kule kule zilikotoka. (*Makofii*)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nusrat Hanje.

TAARIFA

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ni kweli tuna tazito kubwa sana la uelewa kuhusu *Local Content* kwa sababu hatuna sheria inayoitwa Sheria ya *Local Content* ambayo *ita-define* ni vitu gani na vitu gani sisi kama nchi *tunavi-regard* kama *local content*? Ndiyo maana kuna mwingiliano wa kila namna mtu *anavyo-define*. Kwa hiyo, nimpe taarifa hiyo, lakini pia tunahitaji kama inawezekana kupata sheria maalum kwa ajili ya *local content*. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, malizia mchango wako.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria ipo na imeeleza vizuri sana na sheria ile shida yake kubwa ni kwamba hakuna *compliance* kwa wale wanaolengwa na sheria yenye, lakini sheria yenye ipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo langu lina wachimbaji wengi. Wafanyakazi wengi wa mgodi ni wa muda (*contractual*). Tulitunga sheria hapa tukasema kwamba mafao ya maeneo haya yanarudi kwenye mfumo ambaao tulisema akishafutwa kazi anaanza kulipwa asilimia 80 sijui ya mshahara, lakini sehemu hii kubwa naiomba Serikali, wananchi wangu bado wanalilia sana Fao la Kujitoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni nyingi zinafanya kazi kwa miaka miwili zinafunga na zikishafunga, wananchi hawa wanapoteza kazi kwa miaka mitatu mpaka minne. Hii fedha ilikuwa inawasaidia kwenda kuanzisha biashara na wengine walikuwa wanaweza kusomesha watoto wao. Sasa hivi muda wa kufuatilia mafao haya ni mrefu sana na kwa kweli wanakula hasara kubwa. Nilikuwa naomba sana maeneo haya yaangaliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii fursa ya kuchangia Wizara ya Madini ambayo ni Wizara muhimu sana kwenye Uchumi wa Tanzania. Nianze kwanza kwa kumpongeza Waziri na timu yake, kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana na kazi imeonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata kwenye taarifa yake, pato letu mchango wa madini ulianzia 4%, 2014, lakini kwa sasa hivi unaelekeea kwenye 6% na nina imani kabisa kuwa katika hiyo *appetite* yao ya kufikia asilimia 10 itawezekana kabisa. Kwa hiyo, namshukuru sana tena sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi yako nzuri na Wizara kwa jinsi mnavyofanya kazi vizuri, *coordination* imekuwa ni nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madini kwa kiasi kikubwa duniani kote yanaweza kutumika kama rasilimali kwenye viwanda. Nasi Tanzania tumebahatiwa kupata madini mengi ambayo yanaweza kutumika viwandani. Kipindi hiki wakati uchumi wa dunia unayumba yumba sisi Tanzania tuna fursa ambazo zipo kuititia madini kama ilivyokuwa kwenye kilimo ambayo tunaweza kutumia madini yetu kupata hizo fursa za kuanzisha viwanda vingi kama hivi vilivyoanzishwa vya dhahabu ambavyo vimeanza kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa napendekeza na nimekuwa nikipendekeza mara nyingi, tuna madini ambayo ni adimu sana duniani na ni adimu sana Afrika. Tuna mgodi wa madini *Panda Hill Songwe Wilaya ya Mbeya*. Huu mgodi utazalisha *Niobium* na huu mgodi kuna fursa ya kuanzisha kiwanda ambacho kitakuwa ni cha kipekee cha kwanza Afrika nzima; na cha nne duniani. Kuna uwekezaji wa kutoka nje wa dola zisizo pungua milioni 200, vile vile kitazalisha kwa mwaka Dola zisizopungua milioni 200 na Serikali itapata mapato yasiyopungua Dola milioni 50 kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia kwa haraka haraka inawezekana hizi *projections* zikaonekana kama ni za ajabu, lakini hiyo ndiyo hali halisi. Kwa sababu kazi zote zimefanyika za namna gani waweze kuendesha huo mgodi na hicho kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali, hivi viwanda nya aina hii tungevipa kipaumbele hasa katika kipindi hiki ambacho tunahitaji sana pesa za kigeni hasa katika hiki kipindi ambacho tunahitaji ajira. Kwa sababu hiki kiwanda wakati wa ujenzi kitazalisha ajira zisizopungua 2,000, lakini mbele ya safari kitakuwa na ajira za kudumu siyo chini ya 600. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wakati mwingine tunakuwa tunalala na fursa tulizonazo na hili ndiyo tatizo ambalo tunakuwa nalo. Kwa sababu kama hiki kiwanda kikiwepo cha kwanza Afrika ina maana madini ya namna hiyo yanayozalishwa nchi nyingine duniani, siyo Afrika peke yake yataletwa Tanzania kama rasilimali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya madini ya *Niobium*, hiyo *productwatakayozalisha* inaitwa *ferroniobium*, ambayo ndiyo sasa hivi inatumika kutengeneza vyuma ambavyo vitasaidia kwenye ujenzi wa reli na madaraja kwa vile ndiyo vyuma nya kisasa ambavyo ni vyepesi na vinatumika hata kwenye madaraja ya kwenye maji na hata baharini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba labda kwa kipekee Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Uwekezaji na Viwanda wangejaribu kuliangalia kwa pamoja na nina imani Mheshimiwa Waziri yupo vizuri sana katika kusimamia sheria na mikakati yake ya kulinda rasilimali za Taifa Letu. Nina imani kwa kuzingatia hayo, tukiangalia vile vile katika *win win situation* tutaona namna gani nchi yetu inaongeza mapato kupitia haya madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe ni shuhuda, alishafika kwenye huo mgodi, aliutembelea na wawekezaji wamekuja mara nyingi

kuonana nao. Nafikiri katika hatua tuliyofikia leo, anaweza kuangalia ni namna gani nchi yetu inaweza kuongeza pato la Taifa na vile vile fedha za kigeni ili tuweze kuimarisha uchumi wetu na ili tufikie lengo letu la pato la Taifa ambalo linachangiwa na madini kufikia asilimia kumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautamtosha Mheshimiwa Deo Mwanyika. Kwa hiyo, tutaishia hapo kwa hiki kipindi chetu cha kwanza.

Niwataje baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao watachangia mchana tutakapokutana ama alasiri. Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mheshimiwa Nassor Hussein Amar, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutaja majina hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 alasiri leo.

(Saa 7.01 Mchana Bunge lilsitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Aah! Sina hakika kama Mheshimiwa Deo Mwanyika amekwishaingia, basi endelea Mheshimiwa Mwanyika. Ooh! Nakuona sasa.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Madini. Baada ya mageuzi makubwa

katika sekta hii ya madini, tumeshuhudia sasa mabadiliko makubwa. Mchango wa sekta umeongezeka, kukua kwa sekta kumeongezeka kwa kiasi kikubwa. Mchango wake sasa hivi ni asilimia 5.2 ya pato la Taifa na bado unaendelea kwenda, imekuwa *projected* kwamba, utaongezeka zaidi. Kwa hiyo, niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote ambao wameweza kutufikisha hapa na hasa kwa kuweza kutupa matokeo ya haraka kwenye maeneo mbalimbali ya sekta hii na hasa kwenye utoroshaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kama nitakavyooleza hapo baadaye tumeshuhudia sekta hii kukua lakini, hatujashuhudia sekta hii kuongeza uzalishaji kwa maana ya migodi mipya. Nianze kwa kusema Bajeti ya Wizara hii ni bilioni 66.8; kati ya hizo, bilioni 15.0 ni miradi ya mkakati na katika miradi ya mkakati tunaona kuna bilioni kama tatu zinakwenda *STAMICO* na bilioni 3.5 zinakwenda *GST*. Ni jambo jema kwa sababu, wengi wameongea hapa kwamba utafiti ni jambo la muhimu. Nipende kukazia maisha ya sekta ya madini yanategemea sana utafiti na utafiti wa uhakika. Wengi wamelia na kusema maneno mengi hapa hata kwa wachimbaji wadogo kuhusiana na suala la utafiti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nipende kusema kukua kwa sekta hii na kuongezeka kwa mchango wa sekta hii, kwa kiasi kikubwa bado naweza nikasema sio himilivu, inatakiwa tufanye kazi za ziada na sababu kubwa ni kwamba, bado sekta hii kwa kiasi kikubwa inategemea dhahabu kama zao ambalo ndio hasa linaifanya hii sekta ionekane na itoe mchango mkubwa. Kwa maana hiyo basi, kama nia ni kufanya *by 2025* tufikie asilimia 10 ya pato la Taifa, bado tuna kazi kubwa kwa sababu, napenda kuliambia Bunge lako kwamba, dhahabu ina tabia ya kupanda bei na kushuka bei.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba bei imekuwa ikipanda na nilishawahi kusema humu ndani kuna majira yanakuwa mabaya. Kwenye sekta ya

madini tunasema kuna *bust* na kuna *boom*, tupo kwenye *boomla* madini lakini *bust* na yenewe iko mahali fulani. Kwa hiyo, tujiandae na cha kufanya kama nilivyosema mara ya mwisho tuanze kuangalia madini mengine na madini haya, tunasema ni madini ya viwanda (*industrial minerals*). Tuna madini ya kila aina katika nchi hii, tuna utajiri mkubwa *cobalt*, *graphite*, *helium gas*, *rare earth*, mwenzetu mmoja ameongea kuhusu *niobium* hapa asubuhi, kwa hiyo, tuangalie haya.

Mheshimiwa Spika, vile vile, tujitendee haki kwa kuangalia ukuaji wa sekta hii, kwa kuangalia jambo la *exploration*. Ni ukweli usiopingika kwamba, sekta ya utafiti kwa maana ya pesa ambayo inaingia ndani ya nchi yetu kufanya utafiti imepungua sana kama haipo kabisa. Hata kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri sijaona akiongelea pesa ya utafiti na utafiti unaoendelea ndani ya nchi kwa pesa inayotoka nje kuja kufanya utafiti hapa ndani, ni ya muhimu. Lingekuwa ni jambo jema tukafanya utafiti kwa pesa zetu, tunalipenda lifanyike hilo, maana litatupa nguvu ya kuweza kujua nini kiko wapi kwa ukubwa gani na kwa miaka mingapi? Hiyo itatusaidia kuweza kuongea na watu wote ambao wanataka kuwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi tuliyonayo, inabidi tukubali kwamba uwezo huo hatuna. Tukitaka tufanye ili tujue kila kitu kiko wapi katika nchi hii, hiyo bajeti tunayoongelea ya bilioni 400 au 500 ya Wizara ya Madini itabidi tuzidishe mara tatu au mara tano tuizike yote kwenye *exploration*. Sidhani kama litakuwa ni jambo la busara wakati tuna mahitaji mengi makubwa. Hata hivyo, sekta binafsi inaweza kuifanya hilo, tena kwa vizuri kabisa. Tukubaliane kabisa kwamba, katika utafiti kuna utafiti wa aina mbili; kuna utafiti ambao unafanywa na migodi ambayo ipo tayari sisi tunaita, *brown exploration* na utafiti huu unaendelea bado kwa migodi ile kwa sababu, wanataka wao waendelee kuongeza mashapo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utafiti tunaouongelea ambao ni mkubwa wa kuongeza na kukuza hii sekta, ni utafiti

unakwenda kwenye maeneo mapya ambayo bado hayaajaonekana tunaita *green field exploration*. Tunahitaji kuwa na uwekezaji kwenye eneo la *green field exploration*, ni muhimu kwa uhimilivu wa sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, nNipende kusema vile vile pesa nydingi za uwekezaji katika sekta hii ya madini kwa upande wa *exploration*, mara nydingi ni pesa za watu mbalimbali wanakusanya na kuziweka na kuzifanya ziwe *available* kwa nchi au kwa wawekezaji. Nadhani baada ya miaka mitano ya kuwa na mafanikio mazuri baada ya mageuzi makubwa kwenye sekta hii, lazima tuanje kujiuliza maswali magumu. Hatuna budi kujiuliza ni kwa nini kwanza, hatupati hizi pesa kutoka nje za uwekezaji kwa maana ya *exploration*?

Mheshimiwa Spika, vile vile ni miaka 10 sasa, hatujaona migodi mipyä ikifunguliwa katika nchi yetu. Tunasikia michakato ya kutaka kufungua migodi, lakini ni wazi tunatakiwa kuwa makini sana ili tuweze kuhakikisha kwamba nchi yetu inanufaika, ni jambo jema. Pia ni wazi kwamba, bado tunaweza tukanufaika kwa kufanya *fine-tuning* tu katika sheria zetu. Hatuna sababu, tumefanya makubwa kwa kufanya mengi ya kubadilisha sheria, lakini kuna mambo madogo tunaweza tukayafanya ambayo yanaweza yakatupa faida zaidi...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika, dakika tano zimeisha.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, tuliambiwa dakika saba.

SPIKA: *No, ni tano! Ili orodha niliyonayo iweze kutimia, tunashukuru sana. (Makof)*

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, basi, naunga mkono hoja. *(Makof)*

SPIKA: Oooh! Pole sana, ahsante sana. Yaliybakia basi mwandikie Waziri.

Mheshimiwa Jumanne Sagini atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Maganga. Mheshimiwa Sagini dakika tano, tano jamani.

MHE. JUMANNE A. SAGINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Niungane na wasemaji waliopita, kuwapongeza viongozi wa Wizara hii, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mabadiliko yaliyo bora kwenye sekta hii ya madini. Tunachoomba ni kuboresha zaidi ili tuweze kunufaika kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya hawa *mineral explorers* wanachukua leseni, wanashikilia maeneo kwa muda mrefu sana wakionyesha kufanya utafiti, lakini wananchi hawa wachimbaji wadogo wadogo wanakuwa wanafahamu kwamba maeneo hayo kuna madini. Matokeo yake inaanza kuingia migogoro baina ya hao wenye leseni na wale wachimbaji wadogo wadogo. Ushauri wangu, haya nimeyaona kwenye Jimbo la Butiama yakijitokeza. Kwa mfano, ipo leseni ya muda mrefu eneo linaitwa Rwamkoma, wana zaidi ya miaka sita wana leseni ile ya utafutaji madini. Pia lipo eneo lingine Katario, huyu mwekezaji wa katiba ana leseni zaidi ya miaka nane lakini hajafanya chochote.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, Wizara ikubali wawekezaji wa namna hii, haya maeneo wayaaache kwa ajili ya wachimbaji wadogo waanze kuchimba madini, wafanye shughuli zao za kiuchumi badala ya kuendelea kuyaweka na wakati mwingine kukimbizana wakionekana ni vibaka wanaingia kwenye maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama hili litafanyika kwa mfano kwenye Wilaya ya Butiama, Vijiiji vya Nyakiswa, Kiawazaru, Katario, Kiabakari, Nyamisisi, Singu, Nyakiswa, watanufaika sana na wataweza kutoa *CSR* kwenye halmashauri na hivyo kuboresha huduma za wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine ambalo tunadhani Serikali itusaidie, nimewatembelea wananchi kabla ya kuja huku Bungeni, wanasesma, wamejifunza Mererani na Wizara ikawa-*encourage* kujenga *fence* kuzunguka kwenye mgodi wao unaitwa Irasanilo *Mine* kule Buhemba. Wamejenga ukuta ule zaidi ya milioni 200 wameshawekeza pale wale wachimbaji wadogo. Ushauri wetu kwamba Wizara isaidie kukamilisha *fence* ile ili wao waendelee kuwekeza kwenye uchimbaji, badala ya kuwaachia wananchi peke yao wale wachimbaji wadogo wakijenga *fence* kuzunguka eneo lote la mgodi. Hilo likifanyika litakuwa kwa kweli limewatendea haki sana watu wa Buhemba na Irasanilo *Gold Mine*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, nafahamu kwamba, Wizara imeipa nafasi *STAMICO* kuanza kuchimba madini na eneo hili la Buhemba ni eneo lilidochaguliwa na *STAMICO*. Sasa inavyoonekana kama Waziri ataiachia *STAMICO* ichimbe pale, wale wachimbaji wadogo wataathirika sana. Sasa, najua kuna maeneo mengi, lakini ikiwapendeza, Wizara ione uwezekano wa eneo la Kilamongo kuliacha kwa ajili ya wachimbaji wadogo badala ya eneo lote kuiachia *STAMICO*. Kwa sababu, *STAMICO* ni wachimbaji wa kiwango cha kat, itakuwa ngumu sana kwa wananchi hawa ambao walikuwa wanachimba pale itaonekana kama tumewatelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako malalamiko ya baadhi ya wawekezaji kwenye sekta hii hususan kwenye eneo la makinikia. Sasa, liko eneo ambalo lina dhahabu kule Butiama, eneo la Nyasirori, kuna wawekezaji wa Kichina pale, lakini tunamuuliza kwa nini hachangii maendeleo ya halmashauri, anasema zaidi ya miaka minne hajaweza kufanya chochote kwa sababu, *so far* nchini hapa hatuna teknolojia ya *ku-process* makinikia, bado yanatakiwa yasafirishwe nje, lakini anasema pana vibali ambavyo kwa muda wote huu havijaweza kutolewa na kwa hiyo, muwekezaji huyu yupo tu lakini hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wangu kama Serikali inatambua kwamba, hatujawa na *technologyya ku-deal*/na haya makinikia, basi hizo taratibu za kuwezesha hawa wawekezaji kusafirisha makinikia huko nje ziendelee. Bahati nzuri katika ripoti ya Mheshimiwa Osoro ilionekana wazi kwamba, wanawenza kufanya tathmini ya kujua kwenye makinikia kuna dhahabu kiasi gani. Sasa kama uwezo huo wanao, wafanye *assessment* kwa yale makinikia, huyu mwekezaji aruhusiwe kuyasafirisha, kodi za Serikali zilipwe ili halmashauri na wananchi wanufaikie.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba iwapo mgodi ule utaruhusiwa kuendelea, zaidi ya ajira 500 zitapatikana. Kwa hiyo, Serikali pia itapata kuitia *pay as you earn*. Kwa hiyo, nashauri haya yakifanyika yatakuwa yametusaidia sana kule Nyasirori ili Butiama nayo ianze kuchangamka kwenye sekta ya madini kama maeneo mengine yalivyochangamka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Sagini. Nilikutaja Mheshimiwa Nicodemas Maganga na utafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Bajeti ya Madini. Naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Madini kaka yangu Dotto Biteko, kutoka bilioni 168 mpaka bilioni 528 makusanyo hongera sana kaka. Pamoja na kumpongeza naomba niweke changamoto, lazima tufikirie kwamba ni kwa nini mwanzoni tulikuwa tunakusanya pesa kidogo na sasa hivi tunakusanya bilioni 528, ni jambo la kufikiria. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa watu wetu kuna malalamiko makubwa, hasa wachimbaji wadogo. Mimi natokea Jimbo la wachimbaji, Mbogwe. Juzi nimefanya mikutano mitatu kwenye Jimbo langu malalamiko ni makubwa sana. Naomba niishauri Serikali, Mama Samia, Rais wetu, najua maeneo yote

yenye uzalishaji wa madini, migogoro ni mahali pake na mimi kwangu nikiri wazi kabisa kuna mgogoro ambaao ni mkubwa sana ambaao unaninyima sana raha ni wa pale Mbogwe Nyakafuru. Kuna kikundi kinaitwa Isanjabadugu, nashukuru kaka yangu Mheshimiwa Dotto ameniahidi baada ya Mei Mosi tutaenda kutatua huo mgogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale wananchi wana haki, kama nilivyoeleza kwenye mkutano wa tarehe 27 Februari, kwa Mheshimiwa Rais, Marehemu Magufuli, wale wananchi mashamba yale ni ya kwao, lakini mzungu alilingia kwa kutafiti ikabidi sasa, baadhi ya watendaji wa Serikali wachache waingilie kati, zikafunguliwa kesi mahakamani. Uzuri wananchi wangu wameshinda zile kesi na wana nakala za hukumu, wanatakiwa wakabidhiwe mashamba yao ili waendelee kupokea ile asilimia 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Dotto anisaidie sana kwenye Jimbo langu la Mbogwe, maana wananchi wale machozi yao yatatufata siku tukifa, maana wanalia mpaka sasa hivi hawapati chochote wakati mashamba ni ya kwao.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwenye upande wa *TRA* aliishauri vizuri sana, lakini sekta nyiningine ambayo ni ngumu ni hii ya madini. Nilikuwa mfanyakibashara wa madini sasa hivi nimeacha kabisa. Nilichukua mkopo hapa milioni kama 500 na sheria za madini ni mbaya sana, yaani pesa yako ukiichukua tu ukununua makinikia, wanatoza tozo yaani bila kuangalia mtaji kwamba, umeingiza pesa kiasi gani, wao wanaangalia kulipa tu kodi, ndio maana makusanyo yamepanda namna hii. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tuangalia vizuri huku tukiangalia na wananchi wetu. Kwenye Hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema atawasaidia wachimbaji wadogo na naomba ufanuzi pale, atawasaidia kwa kuwapa pesa ama kuwapunguzia changamoto zilizoko vijiji? Maana kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama pale

unapochimba tu duara ukapata mifuko kwa mfano, kumi, ile Kamati ya Ulinzi na Usalama inachukua mifuko miwili halafu watu wanajiita sijui nani nani? Serikali ya Kijiji, mifuko miwili, ukiangalia mtu huyu anayepewa leseni naye anachukua mifuko mitano, kwa hiyo, mchimbaji anakutwa anabaki na mifuko 10, malalamiko ni makubwa sana kwa wachimbaji wadogo. Migodi ya Nyakafuru, Mwakitorio, Geita na Mabomba, ukikaa na wachimbaji wanailalamikia sana Serikali kwa hizi tuzo. Kwa hiyo, Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais wafanye juu chini kuhakikisha kwamba, wananchi hawa wanyonge, maana sera ya Chama cha Mapinduzi tulikuwa tukinadi majukwaani kwamba tutawajali sana wanyonge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanyonge hawana haki kwenye Taifa hili hawa wachimbaji wadogo. Sana sana labda, naona yanasaalidwa mashirika yale makubwa *STAMICO* pamoja na mashirika mengine yaliyoyoendelea na wazungu. Hata hivyo, hotuba ya Mheshimiwa Rais ilizungumza kwamba, hata sisi Wabunge tuwe mabilionea, kwa hiyo, hatuwezi kuwa mabilionea hata siku moja, kama umeingiza pesa milioni 100 hujapata hata faida, lakini ukikutana na Afisa Madini unaambiwa ulipe milioni saba hujapata hata faida. Mimi ni mfanyakishara na nina watumishi wazuri tu tunafanya hesabu wakati ule tunapoenda kulipa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiingia Wizara ya Madini hicho hakipo. Wanaangalia tu umeuza shilingi ngapi wanatoa *loyalty*, wanatoa *service levy*, pamoja na michakato mingine ambayo haieleweki, haina vichwa wala miguu. Kwa hiyo, tunaweza tukajisifu sana kwamba tumekusanya sana...

SPIKA: Sasa wewe mtani mbona sasa unaongea Kisukuma kwenye mchangano wako? (*Makofi/Kicheko*)

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante mimi si nilikuambia ni Msukuma. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Sasa hiyo *loyalty* ndio nini hiyo? (*Makofi/Kicheko*)

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, nini? *Iolaite?* (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Haya Mheshimiwa, endelea kuchangia. (*Kicheko*)

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, bado dakika tatu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba tunaiingizia Serikali pato kubwa na sisi tuangalie wale tunaotoka kwenye maeneo ya hii migodi inayoingiza. Maana hatuna barabara, hatuna afya, yaani wananchi wetu wana shida. Huwezi ukalinganisha na kwamba tumeingiza kwenye pato la Taifa bilioni 528, wakati hatuna chochote tunachopata katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Rais pamoja na watusika wote watuangalie kwa macho mawili, hii migodi inayotoa dhahabu kwa wingi Geita, hasa Mkao wa Geita na Shinyanga... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nicodemas Maganga. Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Nassoro Hussein Amar. (*Makofi*)

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Madini. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, sisi sote tukawepo hapa Bungeni tukijadili mambo muhimu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kutambua mchango wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, lakini nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mama Samia Suluhu kwa kazi kubwa, lakini pia kwa Hotuba yake nzuri iliyowafuta machozi Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri kijana Mheshimiwa Doto Biteko na Naibu wake, kwa kweli wameitendea haki wizara hii, wameituliza kiasi kikubwa wameweza kuongeza mapato kwenye wizara hii, kwa kweli mnafanya vizuri mheshimiwa Doto Biteko endelea na moyo huo Mwenyezi Mungu aendelee kukupigania. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni Mheshimiwa Doto Biteko amefanya vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sasa niingie kwenye hoja zangu za msingi kwasababu ya muda. Mkoa wetu wa Rukwa kuna utajiri mkubwa sana, utajiri wa *helium*. *Helium gas* inapatikana Rukwa, ipo kwa wingi sana, lakini Serikali haijawa *serious* sana kwenye jambo hili. Natoa ushauri, kwamba Serikali ihakikishe kwamba sasa inatafuta wawekezaji wakubwa ambao wanajiamini na wako *serious* kwenye jambo hili. Kwasababu utajiri tunao mkubwa sana wa hiyo *helium* ni utajiri kwa Taifa lakini utajiri kwa Mkoa wa Rukwa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata wawekezaji hao, tutaomba sisi kama wawakilishi wa Mkoa wa Rukwa tuweze kupata taarifa kwasababu sasa hivi tumesikia kuna wawekezaji ambao wamepatikana lakini hakuna taarifa ambazo tunazijua, tunazisikia sikia tu tunaomba Serikali sasa iwe inakuwa wazi. Kwanza kabisa iweze kuweka sheria ambayo itawabana wawekezaji wetu waweze kuwasaidia wananchi wa eneo husika. Wawekezaji wakipata fursa kama hizo wamekuwa wakisaidia vitu vidogo vidogo hasa utakuta amesaidia shule, amesaidia zahanati lakini utakuta mradi wenyewe ambao anaoupata pale ni mradi wa fedha nydingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iangalie hawa wawekezaji wawe wanasaidia wananchi wa eneo husika kwa kiasi kukubwa sana kulingana na mapato yao ya mradi husika. kwa mfano kama hao wawekezaji watakuoja kuwekeza kwenye *helium* tunaomba sana wawaangalie sana wale watu, wananchi wanaokaa kwenye maeneo husika kuwasaidia kwa kuwapa aidha, hizo shule lakini shule za maana, sio inajengwa shule tu ili mradi shule imejengwa lakini shule haina ubora wowote. Lakini pia Serikali iweze kuwapa elimu, elimu wananchi wa eneo husika faida za mradi lakini pia na hasara za mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye Mkoa wetu wa Rukwa, kwasababu kuna miradi mikubwa kama hiyo tunaomba basi Serikali ikumbuke kujengwa ule uwanja wa Ndege yaani miundombinu ikae vizuri. Lakini pia barabara, barabara ni changamoto kubwa sana kwenda kufika miradi kama hiyo kwa mfano; mradi huo uko kwenye Ziwa Rukwa. Kule upande wa Ziwa Rukwa barabara ni mbaya sana, sasa tulikuwa tunaomba Serikali iangalie sana miundombinu ya Mkoa wa Rukwa ikiwemo uwanja wa Ndege lakini pia ikiwemo barabara ambazo zinakwenda kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Spika, nihame kwenye eneo hilo sasa, niongelee sasa upande wa dhahabu. Kama nilivyompongeza waziri kwamba amefanya vizuri tunaomba sasa kama alivyotoa tamko mama yetu Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwamba yale maeneo ya hifadhi waachiwe wananchi waendelee kuchimba lakini kujipatia kipato kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika ni muhimu sana, Waziri Doto Biteko alifanyie kazi haraka iwezekanavyo suala hili ili sasa waraka utoke wananchi waweze kufaidika na maeneo hayo kwa kupata waraka maana toka alivyotoa tamko hilo mama, wananchi wamekuwa wakiingia kwenye maeneo hayo sasa watumishi wa wizara husika au watumishi wa idara husika wamekuwa wakiwapa adhabu kubwa sana wananchi wanaoingia kwenye hifadhi kujipatia kipato. Kwa hiyo,

nilikuwa naishauri sana Serikali ifanye haraka sana kutoa waraka kwenye haya maeneo ya hifadhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Lakini lingine ni hawa watu wa *TRA* wana wa-*harass* sana wachimbaji wadogo wadogo. Mchimbaji akioneckana tayari ana vitu vya kuchimbia basi wana mkadiria mapato kwa wingi bila kujali kwamba amepata dhahabu kiasi gani au bila kujali kwamba kiasi alichopeleka pale kwenda kupima kinafanana na hizo tozo ambazo wamamtoa.

Suala lingine ni ucheleweshaji wa leseni, leseni za wachimbaji zinachelewa sana utakuta mchimbaji ameomba sehemu ya kuchimba lakini kupata leseni imekuwa ni changamoto. Lakini hilo pia suala hilo Mheshimiwa Waziri aliangalie sana leseni ziwe zinawahi kutoka mchimbaji mdogo akiomba leseni basi apatiwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nilikuwa naomba wale wachimbaji wakubwa ambao wana maeneo makubwa

SPIKA: Malizia Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, ambao wana maeneo makubwa, kwa kumalizia. Yale maeneo ambayo hawayatumii wawagawie wachimbaji wadogo wadogo kwasababu mchimbaji mkubwa ana eneo kubwa halitumii. Lakini mchimbaji mdogo anahangaika pa kuchimba wakati maeneo yamekaa bure. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Wawe wanachukua wanawagawia wachimbaji wadogo wadogo. Ahsante sana, nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Ahsante Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata. Nishakutaja Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka atafuatia.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mada iliyopo mbele yetu. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema kufikia jioni hii ya leo. Lakini pia nianze kumpongeza Waziri wa Madini Mheshimiwa Doto Biteko pamoja na Katibu wake Prof. Shukrani Manya na watendaji wote wa wizara. Lakini pia naipongeza hotuba na naiunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kuipongeza wizara kwa hotuba yake nzuri kwa kuelezea wingi wa leseni ambazo zimeshatolewa kwa wachimbaji wadogo nchini; ikiwemo wachimbaji wadogo wa Jimbo langu la Nyang'hwale. Kwa kweli leseni zimeshatoka *PML* zaidi ya *PML* 50 kwa hiyo, wachimbaji wadogo wa Nyang'hwale wanaipongeza sana wizara, Waziri pamoja na Naibu Waziri. Lakini pia ukwelli usiopingika, madini yanaliingizia Taifa fedha nydingi, lakini pia tukumbuke madini kote yanakochimbwa kuna athari kubwa ya kimazingira. Nitatoa mfano kwenye jimbo langu la Nyang'hwale kulikuwa na msitu unaitwa lyenze, kwasababu msitu ule umezungukwa na wachimbaji msitu huo miti yote imekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaangalia namna gani tunavuna sasa hivi, lakini kizazi kijacho fedha hii ambayo tunaipata sasa hivi itarudi tena kwenda kuandaa mazingira. Nilikuwa nataka nitoe ushauri kwamba wizara iweke mpango mzuri wa kuweza kuwakopesha wachimbaji wetu wadogo ili waweze kupata zana za kisasa. Miti ile imekwisha kwenye ile misitu kwa ajili wanaitwa matimba; uchimbaji wowote wa dhahabu unahitaji matimba ni zile ngazi za kuingilia shimonii. Ukiangalia ule msitu wa lyenze umekwisha na kuna msitu ambaa ukitoka Geita unakwenda Katoro na wenyewe unakwenda kuisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu naomba sana wizara ijaribu kuangalia namna gani ya kuwasaidia wachimbaji hao wadogo waweze kupata zana hizi za matimba ama zana nydingine za uchimbaji ili kupunguza uhalibifu wa mazingira. Lakini ushauri wangu mwingine ni

kwamba Wizara ya Madini ishirikiane na Serikali za Vijiji. Nimezungumzia uharibifu wa mazingira leo unakuta maeneo ya wachimbaji ama kwenye vijiji ambako kuna wachimbaji unakuta kila mchimbaji anatengeneza kitu kinaitwa mwalo Kijiji kizima unakuta kuna miyalo miyalo, na ile miyalo inatumika Zebaki ambayo ni sumu, sumu hiyo itakuja kuleta madhara makubwa kwenye kizazi kijacho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali, naiomba sana wizara ishirikiane na Serikali za Vijiji kuangalia angalau maeneo maalum watakayofanya hizo kazi zao hao wachimbaji kama ni kuharibika eneo liharibike eneo fulani tu. Sio sasa hivi kila mchimbaji, ukikuta kijiji kina wachimba 200 kila mmoja unamkuta ana mwalo kwake anatumia sumu hii ni hatari sana kwa maisha ya wachimbaji wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa waziri nimekupongeza sana, ni mmoja wao wa uanzilishaji wa masoko ya dhahabu. Kama unakumbuka kulikuwa na Kamati ya Naibu Waziri Stanslaus Nyongo mimi nikiwa makamu, tulianzisha na leo kila anayesimama anasema wilayani kwangu kuna duka la dhahabu. Ninakupongeza tulianza vizuri na tunaenda vizuri, tuendelee vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya Mheshimiwa, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Sheikh Hussein Nassor Amar. Sasa anafuatia Mheshimiwa Christopher Ole-Sendecka kama nilivoyosema. Na Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya kwanza kukushukuru wewe mwenye kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye eneo linalonihusu la madini ya vito. Lakini kabla ya kufika huko niseme, waswahili wanasesma mnyonge mnyongeni lakini haki

yake mpeni, kwa muda mfupi niliokaa kwenye Bunge hili baada ya kurudi juzi Waziri Biteko amefika katika eneo la Mererani kama mara tatu hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na nilimnong'onezea juu ya kero zinazowakabili wachimbani wa madini ya vito aina ya *Tanzanite* pale Mererani. Kwa wale wasiofahamu wachimbaji wapatao kati ya 8,000 au 10,000 wanaingia na kutoka katika eneo la machimbo ya Mererani; 8000 – 10000 kwa siku. Nilimuomba Mheshimiwa Waziri asaidie kujenga *shade* ambayo ingeweza kusaidia wachimbaji wale kujikinga wakati wa mvua na wakati wa juu. Mheshimiwa Biteko alichukua uamuzi palepale na kutoa maelekezo na tatizo hilo sasa linakaribia kufika ukingtoni maana jengo hilo linajengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilimuomba Mheshimiwa Waziri aweke utaratibu rafiki unaoweza kuwasaidia wachimbaji wadogo na hasa wale wakipato cha chini kuweza kumudu kuendesha biashara katika eneo la uzio wa Mererani, nilipata majibu *positive* na alitoa maelekezo ambayo ni rafiki na wachimbaji walimpongeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilimuomba sana Mheshimiwa Waziri allondoshe janga lilitokuwa mbele yetu kitendo cha... natafuta lugha ya staha; kitendo cha fedheha cha ukaguzi usio na staha, wanaofanyiwa wachimbaji wa madini ya *Tanzanite* Mererani ambapo watu wapato 20 au 15 wa rika mbalimbali wanapotoka kwenye uchimbaji wakifika kwenye *gate* kuna vyumba viwili vya ukaguzi, kimoja cha wanawake na kimoja cha wanaume. Wanaume zaidi ya 20 au 15 kwa wakati mwagine; wanawekwa kwenye chumba hicho na kuvuliwa nguo zote, zote; na katika chumba cha wanawake vivyo hivyo, wanaingia kwenye chumba hicho bila kujali rika, bila kujali nini wanavuliwa nguo zao zote na wanaambiwa waruke kichura kidogo kitendo ambacho ni cha aibu. Haitarajiwi kwa Taifa kama letu ambalo linatambua na kuthamini misingi ya utu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Iakini cha kustaa jabisha zaidi, Mheshimiwa Waziri alitoa kauli mbele ya wachimbaji wadogo na mbele yangu kwamba jambo hili likome sasa na ukaguzi wa staha ufanyike. Alisema hivyo katika ziara yake ya kwanza, akarudia mbele ya Kamati ya Madini, baada yake siku iliyofuata ikaja Kamati inayoshughulika na masuala ya Ulinzi na Waziri wa Ulinzi ambaye ndiye anayeshughulikia mambo ya ulinzi wa madini pale getini.

Mheshimiwa Spika, ninapata mashaka, kwasababu Serikali haikuongea lugha moja, Wizara hizi mbili hazikuongea lugha moja na juzi tumefanya kikao cha pamoja kati ya Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati kwa pamoja kujadili masuala ya Mererani. Kinachoshangaza hata baada ya ombi langu mbele ya Kamati hizo mbili ya Nishati la Kamati ya Ulinzi; hata jana na leo asubuhi ukaguzi unaoendelea ni ule ule, walichotofautisha ni kwamba wamiliki wa migodi na mameneja wa migodi wamepewa mlango wao wa kutokea na kwamba hawavuliwi nguo hao. Lakini wale maelfu wengine wallobaki wanaendelea na kitendo hicho cha fedheha.

Mheshimiwa Spika, waislam wanasesma; “ukilliona jambo ovu liondoshe, kama huwezi kuliondosha lishtakie kwa mwenye uwezo kuliondosha na asipoliondosha endelea kulinyooshea kidole mpaka atakapopita mtu wa kuliondosha.” (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ovu, ni jambo ambaa halijarajiji litendeke hasa na Serikali ya chama changi Serikali ya CCM. Ninataka maelezo ya Mheshimiwa Waziri leo, kauli ya Serikali itolewe na kwasababu kuna kujikanganya kati ya Waziri wa Ulinzi na Waziri wa Madini. Waziri wa Madini yupo *clear* kwenye jambo hili, Waziri wa Ulinzi anapata kigugumizi, Waziri Mkuu atoe kauli juu ya jambo hili, kama Tanzania tumefika mahali ambapo Watanzania wanavuliwa nguo hadharani na kukaguliwa na watoto ambaa wanaweza kuwazaa...

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka nilitaka tu kukuhakikishia kwamba Waziri wa Ulinzi yupo.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana napokea maelekezo yako mkuu.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka ni kwamba atoe kauli ye ye vinginevyo ushauri wangu utakuwa ni vizuri kila mtu aonje fedheha hii. Tulikataa wakati wa Azimio la Arusha tukasema tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, tumeppuuzwa kiasi cha kutosha, unyonge wetu ndio uliotupelekea tuonewe, tunyanyaswe na tupuuzwe, sasa tunataka mapinduzi, mapinduzi yatakayotupelekea tusionewe tena, tusipuuzwe tena, tusinyonywe tena. Azimio la Arusha mwaka 1967 na tukaweka kwenye utangulizi wa Mwongozo wa *TANU* wa mwaka 1971. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tamko letu ni la mwaka 1967, kama mnadhani kitendo hiki ni kizuri na mnadhani watendewe watu wa Mererani onesheni *demo*, ninyi ambao mmepewa dhamana Mawaziri na Makatibu Wakuu tafuteni chumba cha wanaume peke yenu, bila kujali.... (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka, hiyo hairuhusiwa Bungeni kuwashauri Mawaziri waende wakaruke kichura. Aah dakika zako zimekwisha Mheshimiwa. Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Sendeka, dakika tano zimekwisha. (*Makofii/Kicheko*)

Nilikuahidi Mheshimiwa Salome W. Makamba. Mheshimiwa Soleme ni dakika tano. (*Makofii/Vicheko*)

SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru

SPIKA: Ni tano tu.

SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, sawa zinanitosha.

Mheshimiwa Spika, kwa dakika hizi tano ningependa kuongelea mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza ni ushiriki wa Watanzania kwenye ajira zinazohusiana na migodi na madini na jambo la pili, ukiacha ajira ni ushiriki wako katika manunuzi na uuzaaji wa bidhaa kwenye migodi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunao Watanzania wengi, tasnia ya madini imeanza kushamiri kuanzia miaka ya mwaka 1999/2000 wako Watanzania wengi wamehudumu kwenye sekta ya madini lakini hawatambuliki au hawajulikani wapo wapi. Ni mmoja wa wadau ambaao tumefanya kazi kwenye sekta ya madini, nilikuwa naiomba sana Serikali itengeneze Kanzidata inayoeleweka itawatambua watumishi waliofanyakazi kwenye Sekta ya Madini. Na hii itasaidia kupunguza idadi ya watu wanaojiita ma-expert au wazungu ambaao wanakuja kufanya kazi ambazo Watanzania wanaweza kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo hii tumeshudia Watanzania wachache wanapata nafasi za juu Serikalini / *I mean* sio Serikalini. Wanapata nafasi za juu kwenye migodi kwasababu Watanzania wale wamehudumu kwa muda mrefu. Tofauti na maeneo mengine ukihudumu kwa muda mrefu kwenye sekta za madini uwezo wako unakuwa ni mkubwa kiasi kwamba una uwezo wa kufanyakazi ndani ya Tanzania, ndani ya Afrika hata Duniani kwa ujumla. Kwasababu eneo hili utaalalm wake hauna tofauti kwenye maeneo mengine ambayo kuna migodi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe sana waziri na hili ni tatizo la muda mrefu tumekuwa tunalipigia kelele kwa zaidi ya miaka sita, miaka sana, miaka nane hakuna Kanzidata ya pamoja inayowatambua wataalam hawa waliofanya kazi muda mrefu. Lakini sio tu Kanzidata, iwafulilie haki zao watu ambaao wanasisa za kufanya kazi kwenye *managerial position* katika migodi kwasababu wakati mwingine wanaondolewa kwa hila.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano; migodi ina *system* inaitwa *blacklisting* ukifanya kosa kidogo wanakuweka

kwenye kitabu cheusi hutafanyakazi sehemu yoyote ile duniani. Vigezo vya *blacklisting* vinatokana na wale ambao wanakuja na hiyo migodi, mtu amekutwa na sigara kwenye mfuko wake wa suruali unakuwa *blacklisted*, umesomeshwa kwa gharama kubwa, wewe ni *geologist*, wewe ni *operator* huwezi kuajiriwa mahali popote. Tunataka Mheshimiwa Waziri uwalinde Watanzania; kwa kuhakikisha vigezo vya *blacklisting* vina-*qualify* na mazingira na utamaduni wa Kitanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Watanzania wanaoweza kutoa huduma na bidhaa kwenye migodi yetu hasa wawekezaji. Wapo Watanzania wengi wenye uwezo, wenye fedha tena hata zaidi ya wale ambao wana *supply* kwenye migodi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunazalisha bidhaa nyingi, tuki-*customize*, tukishusha chini viwango vya bidhaa zinazotakiwa kuwa *supplied* hasa vyakula, wakati mwininge *apples* zinapatikana Muheza Tanga lakini yule *supplier* anazitoa *South Africa*, hakuna sababu! Wamekuja Tanzania, *you are in Rome, act like Romans*. Wamekuja Tanzania watakuwa ma-*apple* ya Kitanzania na Watanzania wapo ambao wanaweza ku-*supply* kwenye migodi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri ili kulinda maslahi ya watu hawa ambao wanaweza ku-*supply*, *best practice* tulifanya wakati nahudumu kwenye Mgodi wa Buzwagi na hasa kwenye hili suala wanaloiliita *CSR* na mambo ya *local content*. Kule mkienda kuwatafuta katika *level* ya *ward* (kata), mkaingia kwenye *level* ya wilaya, mkapanda mkoa mpaka taifa, dhana ya *local content* itatekelezwa vizuri lakini tukisema tu-*generalize* useme leo mchicha uchukuliwe Tanzania nzima au ukachukuliwe Dar es Salaam ni lazima utawaacha wazawa wa Shinyanga kwa sababu uwezo wa kuzalisha hauwezi kuwa sawa na wa maeneo mengine. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kusimamia dhana hii ya *local content* tuwawezeshe na tuwape fursa Watanzania wanaoweza ku-*supply* kwenye migodi yetu.

TAARIFA

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anaendelea kuchangia kwamba siyo tu Watanzania wana uwezo wa kupeleka *apples* na vitu vingine, lakini wapo Watanzania wana uwezo wa *ku-supply chemicals* na vifaa vikubwa kwenye migodi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Mheshimiwa achukue taarifa hii kwamba Watanzania wapo wengi wenyе uwezo thabiti na wanakidhi mahitaji ya kuweza kufanya *supply* na kukidhi masharti yote kwenye migodi hii mikubwa. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Taarifa hiyo Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Saashisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeimaliza dhana ya *local content*, njie kwenye suala la *CSR*. Migodi mingi wawekezaji wakubwa wakitupa hizi pesa za *CSR* wanadhani ni hisani; wanazileta pesa hizi halafu wanatupangia namna ya kuzitumia. Tunazo Halmashauri zetu kuanzia *level* ya kijiji, kata mpaka manispaa, tunavyo vipaumbele ambavyo vimepangwa na wataalam na wananchi, kama wanatupa pesa za *CSR*, wapeleke kwenye Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Madiwani wanavyo vipaumbele, wala hawana haja ya kuchakata kwa sababu mwisho wa siku wasije wakatushauri tutengeneze bwawa la samaki Shinyanga Mwendakulima au Ibadakuli wakati pale asili yake ni *semi desert*. Kwa hiyo, walete kwenye *level* ya halmashauri, kule wana vipaumbele vyao, sisi tutatekeleza,

tukishakamilisha mradi wenyewe wafanye shughuli ya kufanya malipo na kusimamia viwango vya ubora. (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kumpa taarifa mjomba wangu Salome, nilikuwa nimeacha kumsalimia kwa sababu dishi liliyumba lakini leo mjomba wangu marahaba.

SPIKA: Lakini ninyi mnaopelekewa hizo hela za *CSR*, Mheshimiwa Musukuma wewe mweyewe umelalamika leo asubuhi zikija kule *supervision* peke yake wanakula milioni 600, mwininge amelalamika milioni 200, kwa hiyo maana yake zinakuwa *squandered*. Kwa hiyo, kupeleka huko halmashauri peke yake bado sio dawa.

Mheshimiwa Salome Makamba, dakika zako zilishaisha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nimalizie. Umeongea vizuri sana na hoja yangu nilikuwa nataka nii-cement kwa kusema wasipewe pesa, waende wakachukue miradi ya vipaumbele kwenye halmashauri. Ikishatekelezwa kama ni ujenzi wa barabara *certificate* itoke, mgodi upelekewe *certificate* ufanye malipo. Wasipewe pesa zikaingizwa mle kwa sababu kuna *risk* ya *re-allocation, misuse, corruption* na *risk* zingine. Wasipewe *cash money* isipokuwa watekeleze miradi ya vipaumbele kama ilivyofanyika kwenye *D and OD* kama ilivyotekerezwa kuanzia ngazo ya vijiji. Malipo yafanywe na mgodi siyo mgodi ndiyo unapanga halafu shule ya milioni 20 unajenga kwa milioni 50 wanakuja baadaye kusema wametekeleza *CSR*, *CSR* sio hisani ni haki ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Yaani Waheshimiwa mnaunga mkono hoja hiyo?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Aaaaaa. (*Kicheko*)

Yaani mnasema pesa ibaki kwa mzungu halafu huku wakifanya kazi *certificate* moja kwa mzungu, wakifanya *certificate* ya pili kwa Mzungu, pesa iende Serikali mahali.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

SPIKA: Kama siyo Halmashauri, hebu lifikirieni vizuri jambo hilo. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri kwa wasilisho zuri. (*Makofi*)

Vilevile nitumie nafasi hii kutoa pole sana kwa Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo la Ludewa kwa kuondokewa na Diwani Viti Maalum mama yetu mpendwa Grace Mapunda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nianze kwa kusema naamini kwamba rasilimali inafaa kuitwa rasilimali pale ambapo inatumika kikamilifu ili iweze kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa letu. Kama tuna rasilimali halafu tunaziangalia tu hapo inapaswa tutafute jina lingine, sio rasilimali tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, Jimboni kwangu Ludewa kuna madini mengi ambayo watu wa *GST*

wameweza kuyabaini na hivyo watafiti mbalimbali wamekuwa wakienda kule. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba anajitahidi kufanya vizuri sana, wale watafiti wa madini wanavyokwenda kwenye vijiji wanavamia mashamba ya wananchi bila kulipa fidia na mashamba mengine yanakuwa yako kwenye miliki za vijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.5 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Ibara ya 24 inazungumzia haki ya kila mwananchi kumiliki mali na mali yake ilindwe na Serikali na pale inavyotwaliwa anapaswa kulipwa fidia. Sasa watafiti wa madini wakienda kule wanavamia mashamba ya wananchi wanaanza kuchimba bila kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, zile fedha wangkuwa wanalipa kama ni kwenye vijiji au wananchi zingesaldia sana hasa kupunguza michango ambayo wananchi wanatozwa kila leo kwa ajili ya madawati, madarasa na vituo vyta afya. Kwa hiyo, kama vijiji vingekuwa vinalipwa ile fedha kama fidia ya ardhi yao ambayo wanaichimbachimba kufanya utafiti kwa sababu wanaochukua leseni za utafiti wengine wanachimba madini, wakilipa zile fidia zitasaidia vijiji vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nipongeze Bunge lako Tukufu hasa la Awamu ya Tano ambalo liliweza kuitisha sheria nyingi za kulinda rasilimali zetu. Naomba sasa elimu itolewe kwa wananchi na wapewe maandalizi hasa maeneo ambapo miradi mikubwa inakwenda kuhusu nini sheria hizi zinazungumzia kuhusiana na masuala haya. Kwa mfano, kule jimboni kwangu tunaenda sasa kutekeleza mradi wa Mchuchuma na Liganga lakini wananchi hawajaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, wale Waheshimiwa Madiwani pia wanaweza kupewa mafunzo kuhusiana na hii *CSR*, kwa sababu unakwenda kujadiliana na mtu ambaye ni tajiri, bepari, mwenye uwezo kwa hiyo nao wawe wamejengewa uwezo wazijue vizuri hizi sheria ili waweze kutetea haki zao. Kwa sababu hii *CSR* ukisoma Sheria ya Kodi ya mwaka 2004, kifungu cha 16 kinatumika katika kufanya *assessment* ya kodi

zingine. Wanaotoza kodi wanaangalia mchango wake alioutoa kwenye hizo *CSR* kwenye jamii. Kwa hiyo, sio hisani kama ambavyo tunadhani, wale wanasheria wa Halmashauri Waheshimiwa Madiwani na wakuu wa idara wajengewe uwezo ili waweze kujamini. (*Makof!*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba sana tumsikilize mchangiaji hata ninyi mkisikiliza kwa masikio yenu mtaona kuna haja ya kupunguza sauti.

Endelea Mheshimiwa Kamonga.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunilinda. Naomba hizi sheria nzuri ambazo zinalinda rasilimali zetu ziweze kutolewa elimu na wananchi wajengewe uwezo ili kuandaliwa na miradi mikubwa ambayo inakwenda kwenye maeneo yao waweze kujua haki na wajibu wao na waweze kutetea haki zao. Vinginevyo wananchi wataendelea kutembea kwenye ardhi tajiri lakini wao wataendelea kuwa maskini. Kwa hiyo, hivi ni vitu vya muhimu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nimuombe Mheshimiwa Waziri atoe tamko juu ya wachimbaji wadogo ambao waliomba vitalu vya makaa ya mawe pale Ludewa kwa sababu soko ni kubwa, rasilimali hizi zipo tumeendelea kuziangalia tu kwa miaka mingi. Ndiyo hayo sasa tunasema kama rasilimali hazitunufaishi hizo sio rasilimali tena. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wako tayari na masoko wanayo, kuna wachimbaji wengine wazalendo kama Kampuni ya Maganga Matitu na kuna vikundi kule niliwatembelea wengine nimeona wanachimba *copperkwa* kutumia nyundo na tindo. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kukuza mitaji yao, ikiwezekana kuwapa vifaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kamonga. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ngara ni mionganoni mwa majimbo yaliyojaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na madini ya aina mbalimbali. Tuna madini ya *manganese* ambayo *concentration* yake kwenye jiwe ni asilimia 30 hadi asilimia 55. Tuna madini ya *tin*, *concentration* yake kwenye sampuli ya jiwe ni asilimia 50 mpaka asilimia 68. Tuna madini ya *tungsten*, *concentration* yake ni asilimia 65 kwenye jiwe. Tuna madini ya chuma, *concentration* yake kwenye sampuli ya jiwe ni asilimia 75. Mbali na madini hayo, Ngara tumejaliwa kuwa madani ya *nickel*, *cobalt*, *palladium* na *platinum*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujaliwa huko kuna tatizo kubwa sana la ukosefu wa takwimu za wingi wa madini hasa madini ya *manganese*, *tin*, *tungsten* pamoja na chuma. Tunakosa takwimu ambazo zinaweza kuwafanya wawekezaji kuja kuwekeza kwenye jimbo la Ngara ili tuweze kuchimba madini hayo na wananchi walionichagua waweze kupata ajira kutokana na madini haya. Wananchi wa Jimbo la Ngara tumechoka kuendelea kukalia madini, kijiji kiko juu ya mwamba ambao umejaa madini. Wakati madini hayo yanaweza kuchimbwa yakatoa ajira na nchi ikakusanya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishauri Wizara ya Madini kuitia *Geological Survey of Tanzania* waweze kufika kwenye Jimbo la Ngara waje kufanya utafiti kwenye maeneo yote haya niliyotaja yenyenye madini haya; waweze kwenda Bugarama, Kihinga, Mgaza na Ntanga wakafanye utafiti na watuletee takwimu za wingi wa madini haya kwa maana ya mtandao mzima wa mwamba wenye madini haya. Tukiweza kupata takwimu hizo, tuweze kupata wawekezaji waje kuwekeza kwenye Jimbo

la Ngara na hatimaye wananchi waweze kupata ajira na madini hayo yaweze kutumika kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala *local content* pamoja na *CSR*. Kwa vile Jimbo la Ngara kuna mgodi mkubwa sana wa Kabanga Nickel ambao unakwenda kuanza hivi karibuni na kwa kuwa kwenye Jimbo letu la Ngara huu ni mgodi wetu wa kwanza mkubwa unaoenda kuanza, na kwa vile Halmashauri ya Wilaya ya Ngara haiungi mkono wale wanaosema fedha ibakie kwa Mzungu, sisi tunataka fedha tuletewe kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, miradi yetu ya maendeleo tusimamie wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwenye michango ya hapo leo asubuhi, nimesikia baadhi ya Waheshimiwa wanalamika kwamba kipindi kingine unaweza ukaambiwa na Mzungu unataka nini, unataja shule mbili, anakujengea shule mbili kwa shilingi millioni mia kwa shule moja wakati zingejengwa kwa shilingi milioni 50, matokeo yake unakuta kwamba mpaka chenji yenu imebakia kwa Mzungu. Kusema kwamba hizi fedha zibakie kwa hao wawekezaji ni kuendeleza mawazo ya kikoloni na kuonesha kwamba sisi kama Taifa hatuwezi...

SPIKA: Mheshimiwa Ndaisaba hebu rudia hiyo pointi yako, Waheshimiwa Wabunge muwe mnawasikiliza Wabunge wanachoongea, hebu irudie vizuri Mheshimiwa. (*Makofii/Kicheko*)

MHE NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nasema hivi, suala la kusema kwamba fedha ibakie kwa Mzungu ni kuendeleza mawazo ya kikoloni kuonesha kwamba sisi hatuna uwezo wa kusimamia rasilimalia zetu, mipango yetu na kwamba ili tuweze kufanya maendeleo inabidi watu wengine waweze kutufanya maendeleo jambo ambalo halikubaliki. Kwa minajili hiyo Mgodi wa Tembo Nickel utakapoanza kwenye Jimbo la Ngara naomba sana Wizara ya Madini ije itupatitie mafunzo Halmashuari ya Wilaya ya Ngara hasa Madiwani na

wananchi ili tuweze kusimamia fedha zetu sisi wenyewe.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama tunasema kwamba fedha ibakie kwa Mzungu, tunasema kwamba hata fedha tunayoletewa na Serikali Kuu kwenye halmashauri zetu hatuwezi kuzisimamia. Fedha inayotoka kwa Mzungu kama CSR na ile inayotoka Serikali Kuu haina utofauti, fedha ni fedha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmeona jinsi nilivyoshangaa, nani yuko *right* kati ya makofi yenu na maelezo haya? Mimi niko na Mheshimiwa Ndaisaba, malizia Mheshimiwa. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ngara tumejiandaa kunufaika na Mgodi wa *Kabanga Nickel*/almaarufu kama Tembo Nickel. Wananchi na makundi mbalimbali ya wafanyabiashara tumejiandaa kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwenye mgodi huu. Huduma hizo ni pamoja na usafiri, ulinzi, kuuza bidhaa mbalimbali hasa mbogamboga, matunda na vyakula vya aina mbalimbali ambavyo vinahitajika mgodini.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara ya Madini haiwezi kuja kuandaa wananchi ni ngumu sana kama mgodi unaanza mwaka huu kupanda parachichi likaota na tukaweza kuuza pale mgodini. Naomba Wizara ya Madini ije kwenye Jimbola Ngara iandae wananchi ili tuweze kunufaika na Mgodi huu wa *Kabanga Nickel* ambao unakwenda kuanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzoni, kwenye Jimbo la Ngara tuna madini mapya na mwenyewe nimeenda maabara kuhakikisha kwamba kweli haya mawe yana madini. Tuna madini ya *tin*, tungsten na manganese.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ije Ngara kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo tuanze kuchimba madini hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Kwa kweli Ngara ni Tajiri.

Tunaendelea na Mheshimiwa Tabasam tuko mwishoni mwishoni na wa mwisho kabisa ni Mheshimiwa Boniphace Butondo halafu Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, naomba kuchangia katika Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusiana na suala la wawekezaji. Tunao wawekezaji wengi ambao wamefanya kazi ya utafiti wa madini katika nchi hii. Wawekezaji hawa mpaka sasa hivi wako ambao wametoa taarifa zao na wako ambao taarifa zao bado hazijaenda katika Wizara kuonyesha kwamba wametafiti kitu gani na wamepata madini ya aina gani. Pamoja na hali hiyo, wako watafiti ambao tayari wameshamaliza utafiti wao na wako katika ngazi ya kupata leseni.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana mdogo wangu Mheshimiwa Doto Biteko, kafanya kazi kubwa sana. Kwa mfano, Sengerema tuna Mgodi mpya wa Nyazaga, ameshakuja Sengerema zaidi ya mara sita, tumefanya vikao pale. Vilevile tumeshakwenda na Waziri wa Uwekezaji wa wakati huo, Mheshimiwa Kitila Mkumbo tumepanda juu ya milima yote kule Nyazanga na wamemlalamikia kuhusiana na suala la kuchelewa kupata leseni. Wakati Waziri anakuja kufanya majumuisho ya bajeti yake, naomba anieleze lini leseni ya Mgodi wa Nyazaga itatoka? Kama hatatueleza leseni hiyo itatoka mwaka huu, leo ni mwaka wa nne, shilingi

ya mshahara wake japo ni mdogo wangu nitaing'ang'ania kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, haitawezekana, hatutakubali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo naishauri sana Wizara hii wajaribu kutengeneza sera maalum ya wachimbaji wadogo katika nchi hii. Leo hii sheria zilizopohaziendani na sera. Kwa hiyo, lazima tujue nchi hii imeandaa nini kuhusiana na hawa wachimbaji wadogo?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, leo tunazungumzia wachimbaji wadogo, wanagundua wao, wanafanya uvumbuzi wao wenyewe, wanaangalia eneo hili lina dhahabu, kesho kutwa anakuja mtu anakwenda pale na *GPS* anawahi kwenda kusajili. Waliogundua ni watu wengine wamekaa kule porini miaka sita au miaka mitatu, anakwenda mtu anapata leseni, anaanza kuwahangaisha hawa wananchi. Naomba sera yetu ya madini kuhusiana na wachimbaji wadogo na uwezeshwaji wao iwe bayana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, la tatu katika jambo hili la hawa wawekezaji, wakati wanakwenda kupewa leseni lazima wawekewe masharti maalum. Masharti haya ni kwamba watoe eneo la wachimbaji wadogo na liliopimwa. Siyo wanatoa eneo la wachimbaji wadogo hawaelezi kwamba mwamba uko wapi? Wanaendelea kuachwa pale, wanakaa wanahangaika kwa miaka mingi. Wale wanafanya roho mbaya, waeleze kwamba mwamba umeelekea Mashariki, watu wachimbe kuelekea eneo hilo na wapate dhahabu waendeshe maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la vifaa vyatia uchimbaji, tunaiomba Wizara kuitia *STAMICO*; kama *STAMICO* wameanza kutoa mafunzo, hawa *STAMICO* pia wanunue vifaa ambavyo vitakuja kuwasaidia wachimbaji. Kwa mfano, *pumpza* kutolea maji katika mashimo ya migodi, sasa hivi migodi mingi ina maji.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri, ye ye mwenyewe bahati nzuri anatoka katika lile eneo, anajua maji yanavyosumbua wachimbaji wetu. Umeme tunamshukuru Mwenyezi Mungu umeanza kupelekwa katika maeneo ya wachimbaji, lakini *pump* zilizopo ni za China ambazo zina muda mdogo sana wa kufanya kazi. Watafute *pump* kutoka Japan, kutoka Uingereza, zije zisaidie uchimbaji wa dhahabu mwone dhahabu itakayozalishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho tunaomba vifaa vya wachimbaji wadogo na vyenyewe vipewe ushuru. Kama mchimbaji mkubwa anapewa nafuu ya kodi, halipi kodi kwa miaka kadhaa, anaingiza vifaa vyake bila kodi, hawa wachimbaji wadogo ambao ndio wenyne nchi yao, hawapewi nafuu ya kodi katika vifaa vya kuchimbia. Jambo hili linahatarisha sana amani katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri, tunamwona anavyofanya kazi, anachakarika na maeneo mengi anakwenda, tafadhali sana wawahurumie wachimbaji wadogo katika nchi hii. Suala la vifaa vya uchimbaji kwa mfano gololi za kuchimba za kwenye makarasha, kuanda makarasha, hayo ni mambo ambayo mngeyapeleka *SIDO*, wakatengeneza makarasha ya gharama nafuu mkawapelekea wachimbaji wakakopeshwa haya makarasha, tungkuwa tunazalisha dhahabu nyingi sana ya kutosha. Leo karasha mtu anakwenda kununua kwa shilingi milioni saba, shilingi milioni kumi, ataiapata wapi mtu masikini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wasaidieni wananchi katika nchi yao. Naombeni sana katika jambo hili. Nakuomba sana katika jambo hili la hawa wachimbaji wadogo hata wewe Spika unaweza ukafanya ziara; ukipata nafuu ya pumziko, uje uwaangalie wachimbaji wadogo wanavyopata shida. Nawe utaomba kabisa kwamba sasa tutengeneze sera maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika nchi hii.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Tabasam. Mheshimiwa Boniphace Butondo ndio mchangiaji wa mwisho jioni hii ya leo.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza nami naomba nimshukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Biteko pamoja na Naibu Waziri wake kwa namna ambavyo wamekuwa wakisimamia vizuri sana sekta hii ya madini na Watanzania wote wanaona mafanikio na sote kwa ujumla tunanufaika kwa kuongeza pato la Taifa kwa asilimia zaidi ya tano kutokana na sekta hii ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza nataka nizungumzie kuhusiana na suala la Mgodi wa Mwadui. Mgodi wetu wa Mwadui sote tunafahamu kwamba, Serikali ina asilimia 25 na mwekezaji asilimia 75, lakini Mgodi huu tangu tarehe 8/4/2020 umesimamisha uzalishaji, lakini suala hili limetokana na kwanza kulikuwepo na kuporomoka sana kwa bei ya Soko la Dunia la Almasi na sote tunafahamu soko lile la almasi liko Ubelgiji peke yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya tatizo hilo, muda ule ule palitokea tatizo la *Covid 19* na tangu kipindi kile mgodi wa Mwadui hadi sasa tunavyozungumza; tangu tarehe 8 ya mwezi wa Nne, mpaka sasa mgodi huu haufanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukajua pale katika eneo lile kuna watumishi zaidi ya 1,200, sasa Serikali inaweza ikaona tu kwamba kuna watumishi wengi sasa ambao wanapata shida na mahangaiko makubwa. Tatizo kubwa hili la kuteremka kwa bei ya almasi, bado ni changamoto hadi sasa, lakini angalau kuna *improvement*; na juzi waliamua kuanzisha uzalishaji, tatizo linalosumbua pale ni mtaji kwa ajili ya kuhakikisha mgodi ule sasa unaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ziko taratibu ambazo wameanzanazo ili mradi waanze ku-run huo mgodi na waanze kuzalisha, lakini tatizo kubwa ni mtaji wa kuanzia kwa sababu, zinatakiwa dola milioni 25 ambazo unaweza ukaona ni karibu shilingi triliioni tatu. Fedha hizi ni fedha nyingi. Kuna wakati wamezungumza na CRDB na NMB. CRDB walionesha mwelekeo wa kutaka kusaidia Mgodi wa Mwadui ili mradi uanze kuzalisha, lakini baadaye walirudi nyuma. Wameanza mazungumzo na NMB, lakini NMB mpaka sasa hivi hawaja-respond sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni Serikali kuweka mkono wake ili mradi waone kwamba mgodi huu unaanza kuzalisha. Faida kubwa ya mgodi huu iko kote kote; kwenye Halmashauri kuna *Service Levy* ambayo Halmashauri Halmashauri ya Kishapu itaweza kupata, lakini kuna *CSR* ambayo inaweza ikasaldia mambo mengi sana kusukuma mbele shughuli za maendeleo, lakini na Serikali inapata mapato makubwa kutohana na mgodi huu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke jithada za karibu sana, pengine wazungumze na waweke mkono wao ili CRDB ama NMB waweze kutoa fedha na mgodi huu uanze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo lingine katika mgodi huo. Kulikuwepo na suala zima la almasi ambazo ziliweza kukamatwa zilizokuwa na matatizo, Serikali imeshughulika na baadhi ya watumishi wetu walihusika katika kuhujumu. Tatizo hilo nadhani lilienda Mahakamani likazungumzwa likafikia hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali iweze kutoa maamuzi, ikiwezekana kama sehemu hiyo ingefaa kurudishiwa sehemu ya zile mali Mgodi wa Mwadui waweze kurejeshewa, lakini hatua zile za kisheria kwa watumishi wetu ambao walikiuka ziweze kuchukuliwa, lakini mgodi uweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala yale ya VAT kabla ya sheria hajjaweza kubadilishwa, Serikali iweze kuangalia.

Kwa sababu, kuna VAT ambazo zilipaswa kurejeshwa katika mgodi huo, hizi nazo pamoja na mali zitakazorejeshwa zinaweza zikasaidia mgodi ukaweza kufanya kazi yake....
(Sauti ilikatika)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka kuzungumzia suala la migogoro ya mipaka kati ya Nyenze na Ng'wang'holo. Kuna mwekezaji aitwae El-hilal ambaye eneo lile la Mwan'gholo na Nyenze kabla ya miaka miwili huko nyuma wananchi walikuwa wanalitumia kwa kilimo, kuchunga na mambo mengine, lakini juzi wachimbaji wadogo wakaja kuibua madini ya almasi, lakini huyu mwekezaji aliibuka na kusema eneo lile ana hati.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha uchaguzi, aliyekuwa Rais wetu mpandwa Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alielekeza jambo hili kwamba anakwenda kulishughulikia kwa sababu alitambua kwamba wananchi ndio waliogundua kule, lakini akaona ukubwa wa eneo hilo na akasema kwamba ipo haja ya wachimbaji wadogo kukatiwa sehemu ya eneo hilo.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Boniphace!

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Serikali iweze kuchukua uamuzi na kuweza kufidia ili mradi...

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: ...wachimbaji wadogo waweze kupewa eneo hilo, lakini pia Wizara ya Ardhi waweze...

SPIKA: Mheshimiwa Butondo.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: ... katika eneo hilo...
(Sauti ilikatika) (Kicheko/Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Wachimbaji wadogo leo wana watetezi kweli kweli.

Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi dakika tano hivi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukrani zangu kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu. Nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Biteko na timu yake na Wizara ya Madini kwa ujumla kwa ushirikiano ambao wanatoa kwa Wizara tunapotekeleza majukumu yetu. Kwa hiyo, nawapongeza na kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, tumepewa jukumu la kulinda mgodi wetu wa *Tanzanite* kule Mererani, lakini labda niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, pia ni kwa mujibu wa Ibara ya Katiba ya...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeshawaomba tena na tena; eeh, taratibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, utanilinda dakika yangu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 105 ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatupa fursa ya kuendeleza kusimamia ulinzi na maeneo ambayo ni muhimu ya kimkakati. Kwa mgodi huu tunaoulinda pia kwa maelekezo ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama, tunalinda kule Mererani.

Mheshimiwa Spika, niseme, ukipewa kazi ya ulinzi, siyo jambo dogo na hasa lazima tuzingatia weledi ili tuweze kuvuka salama. Kwa hiyo, jeshi letu linafanya kazi nzuri, uniruhusu niwapongeze sana Askari walioko kwenye maeneo haya, wanafanya kazi kubwa kwa uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kuna changamoto nydingi, lakini vijana hawa ambao wako kwenye eneo la Mererani kwa ujumla, Mheshimiwa Mbunge alijaribu kukumbusha hapa kwamba tunakagua watu kati ya 8,000 na 10,000, lakini kwa hali halisi ukienda kwenye eneo tunakagua zaidi ya 10,000. Kuna siku ambazo tunakwenda mpaka kukagua watu 15,000 kwenda 20,000; na tulikuwa tuna sehemu mbili tu za kukagulia.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wizara ya Madini kwamba baada ya kuwa na maombi ya kuongeza maeneo ya ukaguzi, sasa kuna vyumba takribani 10 vinaongezwa ili tuendelee kuboresha ulinzi katika eneo hili. Kwa hiyo, vijana walioko pale wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, ukifanya kazi ya ukaguzi unalazimika wakati mwagine kufanya upekuzi na hii ni kawaida pale ambapo unakuwa na mashaka. Mashaka yanatoa uthibitisho kwamba, saa nydingine tutakapokuwa na mashaka tunakamata haya madini ingawaje Waheshimiwa Wabunge hapa umesikia wakizungumza kwamba, labda ni kidogo kidogo; lakini hiyo kidogo tunayokamata kwangu mimi naamini kwamba inazuia madini kuvushwa kwa wingi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba tutaendelea kufanya kazi hiyo, lakini tunavyofanya ulinzi, tunafanya doria, lakini tukiwa katika maeneo ya ulinzi tunashirikisha vyombo hivi vya ulinzi mbalimbali. Kwa hiyo, hatuko peke yetu. Mheshimiwa Mbunge Ole-Sendeka hapa rafiki yangu amezungumza hapa na kwa uchungu mkubwa, lakini niseme tu kwamba kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Sendeka atakumbuka kwamba tulivyotembelea tukiwa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Ole-Sendeka namshukuru, alikuja na tulikwenda kukagua sehemu ya ukaguzi tukiwa na Mheshimiwa Mbunge. Nawapongeza sana Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa sababu ya namna nzuri walivyofanya kumshirikisha Mheshimiwa Mbunge

na Mheshimiwa Mbunge alitoa hoja zake na rai yake kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, pia tarehe 12 mwezi wa Nne wakati tulikwenda kwenye Kamati kujibu maelekezo ya kamati baada ya ziara ile ya tarehe 16 mwezi wa Tatu, tulikuwa tumepata maagizo ambayo ninayo; yako maagizo 13 ya Kamati; na kati ya maagizo yaliyokuwepo, liko agizo la kufunga *scanner* katika maeneo ya ukaguzi ambalo wenzetu wa Utumishi na Utawala Bora wanalifanyia kazi. Tutakapopata *scanner* tutakwenda kutoka kwenye hii *tradition way* ya kukagua, tuanze kukagua kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Ole-Sendeka alipata nafasi wakati wa ziara na wakati wa Kamati. Haya maelekezo yaliyotoka kwenye Kamati ninaamini kabisa Mheshimiwa Ole-Sendeka yana mchango wake kwenye Kamati. Nami naamini hivyo kwamba tunaendelea kuyafanyia kazi. Niseme kati ya maagizo haya, yako maagizo sita ambayo tayari tulishayatekeleza kwa kushirikiana na Wizara ya Madini, vile vile yako mengine ambayo yako kwenye hatua, tunaendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi na wachimbaji waendelee kutoa ushirikiano kwa vyombo vyetu. Vyombo vyetu vinafanya kazi kwa weledi na kwa uzalendo wa hali ya juu na saa nyingine tutawasikitisha kuwaletea tuhuma au niseme kuwaletea maneno ambayo yatawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama nimepewa dhamana kwenye Wizara hii, nitaendelea kusimamia maelekezo ya Kamati, nitaendelea pia kusikiliza Waheshimiwa Wabunge na nimhakikishie tu Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba tuko pamoja kwenye jambo hili, pale ambapo tutapata *scanner* tutakwenda kufanya ukaguzi kwa staha na kwa uzalendo na kwa kushirikiana na wananchi. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Ooh, bahati mbaya ameshamaliza na muda wangu uko kushoto sana, niwie radhi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, jitahidi kama dakika saba hivi. Jitahidi kukimbia kimbia.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa mchango wao.

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba, wengi wa Waheshimiwa Wabunge wametoa mchango ya kujaribu kuboresha na kuendeleza sekta yetu ya madini, wakitambua kwamba ni moja ya sekta ambazo kama ikisimamiwa vizuri ni kweli kwamba itachangia pato la Taifa kwa kadiri ya malengo yaliyo katika sera. Pia ni sekta ambayo katika nyakati ambazo hazitabiriki inaweza ikawa ndiyo sekta mkombozi kwa ajili ya kuchangia uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na hoja ya Mgodi wa *WDL* ambao ni kweli kwamba umeacha uzalishaji kwa muda. Pia ni kweli kwamba kuacha uzalishaji kwa Mgodi huu wa *WDL* ambao Serikali ina hisa, inatokana na sababu ambazo ziko nje ya uwezo wetu. Kwa sababu, janga la *Covid 19* ndilo ambalo lisababisha kuanguka kwa soko la almasi kwa sababu walaji wengi wa madini haya ya almasi walikuwa wako katika *lock down* na kwa jinsi hiyo wakawa wameshindwa kununua almasi na soko la almasi likaanguka. Hata hivi tunavyoongea, ni kweli kwamba soko hili halijatengemaa sana na hivyo linakuwa ni sababu ambazo ziko nje ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kupokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Madini itakuwa

bega kwa bega na kusaidia kuwezesha *WDL* ili kuweza kupata fedha katika benki zetu.

Mheshimiwa Spika, tukupe tu taarifa kwamba katika siku za karibuni benki zetu za ndani zimepata mwamko mkubwa sana wa kuona kwamba, biashara ya madini ni biashara inayolipa nao wameanza kuwekeza fedha katika sekta ya madini. Hili jambo halikuwa huko nyuma na tukubali kwamba, maisha ni *dynamic*, maisha yanakwenda, hatimaye benki zetu zimeelewa kwamba wanaweza wakakopesha wachimbaji nao pia wakapata faida na Wizara ya Madini iko nyuma ya Mgodi wa *WDL* na tunaamini kwamba wataweza kufanikiwa. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuongea pia hoja ya *Geological Survey* ambayo imechangiwa na Wabunge wengi pia, kwamba *Geological Survey*ndiyo taasisi ya Serikali ambayo inaweza ikafanya utafiti na hatimaye kutoa takwimu na ramani za kuonesha wapi madini yalipo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema tu kwamba pia Serikali imeendelea kutambua umuhimu wa *GST*. Katika mwaka wa 2020/2021 *GST* ilipewa fedha maalum kiasi cha shilingi bilioni 3.3 na fedha hizi zilielekezwa katika kuboresha miundombinu ya maabara, vifaa vya ugani, ilipewa magari sita na pia vifaa vya kuratibu matetemeko ya ardhi na vifaa vya jiofizikia. Kwa mtindo huo basi, *GST*imeendelea kujizatiti kuona kwamba itaendelea kufanya utafiti na kutoa taarifa za awali na kutoa ramani ambazo kimsingi zinapatikana pale *GST*.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wakubwa wale ambao sasa wanaweza wakaja kuleta taarifa zinazotaka *feasibility study* wanaweza wakatumia taarifa hizo za awali na wana ramani na hatimaye kuwapa wawekezaji wakubwa ili tuendelee kupata madini mengine yaliyotafitiwa vizuri kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Ngara amesema kwa ajili ya *Tin, Tungsten, Iron* pamoja na madini mengine.

Mheshimiwa Spika, pia katika habari ya utafiti wa *GST* ni kweli kwamba utafiti katika hifadhi zetu umeshafanyika mahali mahali na hivi tunajua kabisa mahali ambapo kuna madini katika hifadhi za *Selous*, Rungwa, Moyowosi, Lukwati, Kigosi. Hivyo, Wizara itawasiliana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuweka utaratibu bora wa kuendelea kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais ili tuweze kufanya uchimbaji katika maeneo haya ya hifadhi huku tukizingatia usalama wa mazingira ya hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipende pia kusema kwamba tayari *GSTimeona* umuhimu wa changamoto za wachimbaji wadogo kwama sio wote wanaoweza kufika Dodoma na kuleta *sample* zao kwa ajili ya kufanya *analysis* katika maabara. Kutokana na hali hiyo, tayari *GST* imeanza kupeleka huduma za maabara na jiolojia katika maeneo ya Geita na Chunya kwa kuanzisha ofisi za muda, na zoezi hilli litakuwa endelevu ili kuendelea kupeleka huduma katika maeneo ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niongee hoja iliyioletwa na Mbunge inayohusu *helium gas*; ni kweli kwamba katika Ziwa Rukwa tunao wingi wa gesi ya *helium* na wakati mwingine tujue tu kwamba ipo katika hatua ya utafiti wa kina, maana utafiti hadi kufikia uzalishaji lazima upitie hatua. Kwa hiyo tunapoongelea geli ya *helium* ni kweli kwamba mwekezaji yupo, Kampuni ya *Helium One* ipo na walishafanya utafiti ule ya *preliminary* na sasa wapo katika *infill drilling*. *Infill drilling* ni kuonyesha kwamba baada ya kuona kwamba mashapo yapo, sasa wanakwenda katika hatua ya kuthibitisha. Sasa wakimaliza hapo ndipo wanapoweza wakaja na *feasibility study* ambayo sasa ndio itatuonesha jinsi uzalishaji utakavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kweli kwamba *helium gas* ipo, uzalishaji haujaanza na kabla ya uzalishaji kuanza ni kweli kwamba Wizara itatoa semina elekezi kwa watu wanaozunguka maeneo ya uzalishaji ili kwamba waweze kunufaika na gesi hii ya *helium*.

Mheshimiwa Spika, pia Wabunge wameongelea juu ya kwamba hatujaanzisha migodi mipyä siku za karibuni, ni kweli na kwamba pia tumekuwa na utegemezi sana juu ya madini ya dhahabu; naomba nitoe mfano kidogo ambao unaweza ukaleta *perspective* katika eneo hili. Tuna Madini ya aina nyingi, makaa ya mawe tani moja ni Dola 45, kilo moja ya dhahabu ni Sh.140,000,000, kwa vyovyyote vile wawekezaji watapeleka fedha zao katika madini yanayolipa. Kwa hiyo, kwa msingi huo ndio maana dhahabu imeendelea ku-*attract investment* kwa sababu ni madini yatakayolipa na kurudisha fedha haraka. Kutohana na hilo ndio maana yameendelea kuchangia kwa wingi katika pato letu linalotokana na madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuamini kwamba kwa kuingia ubia na Tembo *Nickel* tukaiingiza aina mpya ya madini katika uzalishaji wa nchi yetu, lakini pia napenda kuamini kwamba Serikali inafanya kazi utoaji wa leseni mpya mbili siku za karibuni, ambazo ni Mradi ya Nyanzaga uliopo Sengerema kwa Mheshimiwa Tabasam lakini pia na Mradi wa *Rare Earth* uliopo Songwe. Kwa kuingiza miradi hii pia tutaanza kuingiza maingizo mapya ya uchimbaji na uzalishaji katika nchi yetu...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Profesa.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Profesa Manya.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 76 na nikirejea lbara 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania inayolinda haki ya faragha ya kila raia wa nchi hii na Ibara ya 12 inayotambua na kuthamini utu wa mtu na kwa kauli aliyoitao Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ambapo anasema ukaguzi utaendelea mpaka zitakapopatikana mashine. Maana yake ni kwamba wachimbaji wa Mererani wataendelea kukaguliwa wakati hawana nguo kwa makundi ya watu 20, 20 kitendo ambacho kinavunja Katiba ya Nchi, kinaondoa faragha ya mtu na bado Waziri anasisitiza hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kama jambo hili linalovunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaweza kutamkwa na Waziri wa Serikali kwamba binadamu aendelee kudhalilishwa hivyo na Bunge likanyamaza kimya.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Naendelea kutafakari kuhusu mwongozo.

Mheshimiwa Waziri, hitimisha hoja yako lakini kwa sababu ya muda wetu ulivyo, nakuomba tujaribu kufanya hivyo kwa dakika 15.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Wizara imepokea michango mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa kwa matamshi na Wabunge wengine kwa kuandika. Pia tumepata ushauri na maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo ni muhimu kwetu katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ushauri na maoni pamoja na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kwetu sisi ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Madini.

Napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walioopata nafasi ya kuchangia hotuba yetu. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 22 wamechangia hotuba hii kwa kuzungumza na wajumbe wawili wamechangia kwa kuandika. Nichukue fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, hoja zote zilizowasilishwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara tunazichukua kwa uzito wa aina yake na kwamba itakuwa ni *tool* nyingine ya kufanya kazi katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliosema, hata walioandikia na hata wale tuliookutana nao tukazungumza nje ya Bunge. Tunaheshimu michango yao, na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba nijielekeze kutoa ufanuzi kwa hoja kidogo tu zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kutokana na muda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kueleza kwamba usimamizi wa Sekta ya Madini hautegemei mtu mmoja kwa maana ya Wizara ya Madini, unawategemea sana Waheshimiwa Wabunge ambao wao ndio wawakilishi wa watu mahali huko tunapofanya shughuli za uchimbaji madini. Tumefanya ziara maeneo mbalimbali, tumeona kiu ya Watanzania walio wengi ya kutaka kuwekeza kwenye Sekta ya Madini na tumewaona Waheshimiwa Wabunge wengi walivyo na kiu ya kuona madini yanawanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hiyo *spirit* peke yake kwangu mimi ni kiashiria tosha kwamba usimamizi wa Sekta ya Madini ni wetu sote. Kwa kweli naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hakuna hoja hata moja ambayo sisi tutaichukulia kama hoja *substandard*. Hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni *tool* yetu ya kufanya kazi na kuanzia leo nataka niwahakikishieni kwamba

hoja zote walizozitoa tutaziandikia majibu na tutaziwasilisha kwako ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzipata.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza nieleze kwa kifupi ni suala la *local content*. Suala hili limeongelewa kwa hisia kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge, *local content* huko ndiko uliko mzunguko wa fedha kwenye Sekta ya Madini. Ukipuhusu mzunguko ulioko kwenye *local content* uende kwa watu wa nje ukawaacha watu wa ndani, manufaa hayo hayaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, tulipotoka mbali, tumetoka kwenye mazingira ambayo mchele wa kulisha migodi ulikuwa unatoka nje ya nchi, nyanya zilikuwa zinatoka nje ya nchi, vitunguu vilikuwa vinatoka nje ya nchi, walinzi wanatoka nje ya nchi, Wahasibu wanatoka nje ya nchi, watu wa manunuzi wanatoka nje ya nchi, watu wa *Human Resource* wanatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia biashara zilizokuwa zinafanywa na migodi, *volume* kubwa ya fedha zile ilikuwa bado inarudi nje ya nchi na kwa gharama kubwa sana. Tumefanya mabadiliko hapa tukatoa mamlaka kwa Tume ya Madini ku-*approve* kila aina ya manunuzi, mgodi sasa hivi hata ukitaka kununua kikombe cha chai, ni lazima upate kibali cha Tume ya Madini. Kwa sababu hiyo nataka nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu, tulipofika tumepiga hatua kubwa. Leo wakati manunuzi ya Mgodi wa *GGM* yaliyofanyika kwa mwaka huu tulionao jumla ya Shilingi bilioni 849.9 ni fedha zilizofanyiwa biashara kwa *local content* kwa wazabuni wa ndani na Shilingi bilioni 182 peke yake ndizo zilizofanyiwa na watu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Buzwagi bilioni 105.8 ni zabuni zilizofanyiwa biashara na Watanzania wa hapa ndani na wakati huo huo bilioni 95 ni watu wa nje. Mgodi wa Shanta bilioni 106.5 ni bidhaa za ndani na huduma zimetolewa ndani, bilioni 30 peke yake ndizo bidhaa kutoka nje au huduma kutoka nje. Mgodi wa *WDL* bilioni 53.6 ni biashara iliyo fanyika

ndani na bilioni 5.4 peke yake ni biashara iliyotoka nje. Hatua hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata bidhaa kubwa ambazo walikuwa wanazungumza Waheshimiwa Wabunge mfano mafuta, vipuri, *consumables* na vitu vingine vyote kwa kiwango kikubwa ni biashara zinazofanyika hapa ndani. Biashara ya mafuta kwa mfano, kwa Geita, mtu anayefanya biashara ya kupeleka mafuta kwenye mgodi wa *GGM* ni Mtanzania yupo Geita kwa asilimia 30. Ukiangalia biashara ya kupeleka nguo, kupeleka vitu vyote unavyoviona zaidi ya asilimia 70 biashara hii inafanyika hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, *CSR*inayozungumziwa, tulipotoka tukiangalia Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Kanyasu watakuwa mashahidi; kabla hatujarekebisha sheria hapa *CSR* fedha zilizokuwa zinatumika zilikuwa nyingi na tena hazina uhalisia na wala ile miradi iliyokuwa inatumika hayakuwa mahitaji ya watu wanaozunguka migodi, matokeo yake yakawa ni nini? Matokeo yake ni kwamba fedha nyingi zinaonekana zipo *traded* kwenye migodi, lakini watu wanaozunguka ile migodi bado ni maskini wa kutupwa, bado watoto wao wanakaa chini hawana madarasa, bado watu wale hawana maji.

Mheshimiwa Spika, tukafanya mabadiliko kwenye sheria hiyo Mheshimiwa Musukuma atakumbuka shule moja pale Geita ilijengwa kwa bilioni tisa wakati shule ile haina ghorofa tulivyokwenda kufanya *valuation* tukakuta fedha hizo hata nusu yake isingeweza kutosha tumefanya marekebisho. Leo mpango wowote wa *CSR* unaotaka kufanya na mgodi mtu aliye na wajibu wa kuusimamia mpango huo ni halmashauri husika na halmashauri yenye we ina kazi mbili, baada ya kuwa imejiridhisha na mpango huo unaendana na mahitaji ya halmashauri kazi ya pili ni kuangalia *value for money*.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati fulani kuna miradi ilikuwa inatengenezwa, wanakwambia mfuko mmoja wa simenti unauzwa Sh.30,000 wakati ukienda kwenye soko

unakuta mfuko mmoja unauzwa Sh.15,000. Mambo hayo yote tumeyabadilisha sasa hivi *value for money* inaangaliwa na manufaa haya yanaonekana. Mheshimiwa Kanyasu hapa atakuwa shahidi Geita ilivyokuwa kabla ya kusimamia sheria hii na sasa hivi ni tofauti sana, imebadilika kwa sababu miradi mingi halmashauri wanasimamia.

Mheshimiwa Spika, yako matatizo tunayapokea ya usimamizi na nidhamu ya matumizi ya fedha; sisi kama Wizara Madini ambao tuna wajibu wa kusimamia *local content* pamoja na TAMISEMI, tutaendelea kusimamia matumizi ya fedha hizi ili yaweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa jambo moja la Mradi wa *Niobium*. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Njeza, hili jambo linaweza likaonekana Wizara tunachelewesha, nimwombe Mheshimiwa Oran Njeza awaambie wale wawekezaji tuliokuwa tunaendelea nao waje tupo tayari.

Mheshimiwa Spika, bado tumemaliza mambo mengi tunabishana mambo mawili tu; madini ya *niobium*, wao wanataka tuya-*treat* kama madini ya viwandani ambayo yanatozwa mrabaha wa asilimia tatu, sisi tuna ya-*group* yale madini kama madini ya *metal* na yenye yanatozwa asilimia sita. Sasa ubishani huo hatuwezi kuu-*resolve* kwa kuzungumza tu, ni lazima waje tuzungumze.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunalozungumza nao ni kwamba wanataka wachimbe kwenye Kilima cha Pandahill wakishachimba *processing* ya madini hayo wayaondoe kwenye Kilima waende wakafanye kwenye process ya EPZA. Sheria ya Madini inaeleza uchimbaji wa madini ni *chain* nzima, kuanzia uchimbaji na process. Sasa tunawaambia tukifanya tendo la kutenganisha huu mradi, uchimbaji ukafanyika kwenye mgodi na process ikafanyika mahali pengine, kwanza tutakuwa tumevunja Sheria ya Madini, lakini pili kwenye EPZA kuna misamaha mingi sana ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mapato ya asilimia 30 itakuwa na msamaha kwa muda wa miaka 10; kodi ya zui o na kodi nyingine pamoja na kodi ya pango, bado tunaendelea kujadiliana nao. Bahati mbaya baada ya kuwa tumewaaambia hoja hizi hawakurudi tena. Kwakuwa Mheshimiwa Mbunge anaweza kuwa sasa...

SPIKA: Waheshimiwa wote mnaokuja kukaa na kuongea Mheshimiwa Waziri Mkuu nilishatoa maelekezo, lakini basi nawaagizeni mtakaa kiti kile kama AG hayupo, mumlinde angalau afya yake na yeye. Haiwezekani watu 50 au 60 kila siku wanakutana naye hapa kwa hapa, hebu jaribuni sana kupunguza, hata kama ni Mawaziri kama hauna shida ya maana usiende pale, kwa sababu ana wajibu wa kuwasikiliza Wabunge na wale mnaokwenda basi kaeni kiti cha mbali pale kidogo ili kuweka ile *distance* ambayo ni salama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri, endelea.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo milango yetu ipo wazi Kampuni ya Panda Hill wakaribie wakati wowote tuzungumze, lakini watusaidie na wao ni lazima tulinde manufaa ya nchi yetu kwenye rasilimali madini, kwa sababu hizi rasilimali kuna siku zitakwisha.

Mheshimiwa Spika, kuja jambo lingine hapa limeelezewa la *TEIT*, kwamba *TEIT* hajapata fedha. Naomba kutoa taarifa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba *TEIT* walishapata fedha za maendeleo Sh.850,000,000 ambazo wamekwishapata kwenye bajeti yao. Hata hivyo, kuna mzozo mmoja unaozungumzwa hapa wa *reconciliation* ya bilioni 30 ambaao Mheshimiwa Jesca alikuwa akiueleza sana. Ni bahati njema kwamba Mheshimiwa Jesca amekuwa *consistent* na jambo hili Bunge lilipopita kwenye bajeti alieleza tulitoa majibu, lakini sijachoka tutatoa ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea, hakuna hata shilingi moja iliyobiwa wala kupotea, kilichotokea *TEIT* wanachofanya wanakwenda kwenye mgodi *X* wanaomba

malipo waliyolipa Serikalini, wanapewa iwe orodha ya malipo. Wanakwenda Serikalini wanaomba kile walichopokea, wanafanya *reconciliation*. Kilichotokea ni kwamba *reporting* ya Serikali na *reporting* ya migodi miaka yao ya fedha inatofautiana, ndio maana tulivyomtuma CAG Novemba, 2019 alituletea taarifa ya hoja hiyo, hizo fedha zote zilionekana hata kwenye *bank statement* zipo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa bado linaendelea kuzungumzwa, nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Jesca na Watanzania hakuna shilingi hata moja itakayoliwa kwenye migodi, inasimamiwa kwa uwazi na kwa ukweli na hata kwenye Semina tulioifanya uliyotupa kibali, Mheshimiwa Jesca nilimwambia, nadhani hapa leo aliamua kutuchangamsha kidogo kulirudia jambo hili, lakini majibu anayo.

Mheshimiwa Spika, limeongelewa jambo lingine la *blacklisting* ya wafanyakazi, ni kweli wapo wafanyakazi kwenye migodi wanakuwa *blacklisted* na nilishatoa maelekezo pamoja na wenzangu Wizarani kwamba, watu wanaoweza kuwa *blacklisted* ni wale waliotenda makosa makubwa sana. Mtu amechelewa kazini siku mbili unamfukuza kazi, halafu una m-*blacklisting* asiajiriwe kwenye migodi mingine, tulishatoa maelekezo ni marufuku na kuna Watanzania wawili waliokuja kwangu waliokuwa na kesi za namna hiyo niliwaambia wawaondoe kwenye orodha yao ya *blacklisting*.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii niwaombe Watanzania wale wote walioajija kwenye migodi, wajenge *image* ya nchi yetu, tunapambana kuhakikisha kwamba Watanzania wanachukua ajira zote kwenye migodi, hivyo ni lazima wawe waaminifu. Leo ninavyozungumza migodi mikubwa ya *GGM* asilimia 97 ya wafanyakazi wote ni Watanzania. Migodi ya *North Mara* asilimia 98 ni Watanzania hata *Country Manager* wa *Mgodi* wa *North Mara* kwa maana ya *group* nzima ya *BARICK* hapa Tanzania ni Mtanzania anaitwa Georgia na ni mwanamama yupo, amekuja hapa.

Yule mgeni aliyekuwepo hapa tumemaliza mkataba wake ameondoka Georgia sasa...

SPIKA: Meneja wa mgodi huo unaohusika hebu asimame. Makofi kwake waheshimiwa. Hongera sana dada yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, unaweza ukaendelea.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo...

SPIKA: Mheshimiwa Meneja hawajakuona kamera hizi hazijakuonesha. Hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaona, hata mavazi yake enhe! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Madini, endelea.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Labda wengine, lakini mimi niliwahi kwenda kwenye mgodi mmoja nitatoa mfano, nikazungumza maneno mengi na wenyе mgodi. Baadaye wakaniomba *side meeting*, wakaniambia tunaomba na wasaidizi wako tukae kule chumbani, jambo walilokuwa wanalamika ni uaminifu wa baadhi ya watu wetu, kwa kweli wanatuchafua wote, wanatuondolea heshima wote. Wale wanaopata nafasi ya kusimamia migodi hii wasimamie kwa haki na weweze...

SPIKA: Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa vile anaongelea neno la uaminifu. Nilizungumza hapa siku moja nimepigwa na mitandao yote, kwamba ninaongea kitu cha kufikirika. Leo Waziri anasisitiza. Endelea Mheshimiwa Waziri jambo hili, uaminifu unalipa. (*Makofi*)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, lingine wale Watanzania kama kina Georgia wanaopata nafasi za kuendesha migodi hii, wawasadie Watanzania wengine. Wanaowa-*blacklist* Watanzania hawa ambao wapo kwa kuwaonea wala sio Wazungu tusiwasngizie, ni sisi wenywewе. Nataka niwahakikishie jambo hili haliwezi kufanyika tena tumeshatoa maelekezo kwa watu wote wahakikishe wale

waliofanya makosa makubwa ndio wanakuwa *blacklisted*, lakini makosa madogo madogo ya kawaida mtu amechelewa kazini, hayo haya-*qualify* mtu kuwa *blacklisted*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii vile vile tumekuwa na changamoto ya utoaji wa fedha kutoka kwenye benki zetu. Huko tulipotoka makampuni makubwa yalikuwa yanasema benki za ndani ya Tanzania haziwezi *ku-finance* miradi ya uchimbaji madini. Nataka nitoe taarifa kwako na ndio maana tuliwaalika watu wa *CRDB* na *NMB*, hivi leo mradi uliokuwa umekwama kwa miaka mingi kotokana na *corona*, wawekezaji wamekwenda ku-*list* huko nje kutatufa *finance* wamekosa, wameamua kurudi kwenye benki za ndani na sisi tukawaita ili tuweze kuzungumza nao na Mheshimiwa Waziri Mkuu akaweka mkono wake wa kutusaidia kuzungumza na benki hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nafurahi kusema kwamba mradi mmoja wapo mkubwa wa uchimbaji wa *graphite* hapa nchini wa Ruangwa huko Lindi Jumbo tayari *CRDB* wametoa fedha zote za kuendesha huo mradi. *GGM* wana mkopo wanapewa na Benki ya *NMB* zaidi ya bilioni 250, uwezo huo uko ndani. Sisi tunachowaambia mabenki inawezekana huna fedha zote za *ku-finance* hii miradi, tufanye *synergy* ya benki mbili au tatu. Mbona kwenye miradi mingine wanatuletea, unakuta *Exim* ya China imeungana na *Barclays* ya London wamefanya *synergy* wana-*finance* mradi uko Tanzania na mabenki yetu yanaweza kufanya hivyo na hilo wametuelewa, sasa miradi mingi inatolewa fedha hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, hata wachimbaji wadogo wengi ningekuwa na muda ningekuletea orodha ya wachimbaji wadogo waliokopeshwa na mabenki ya ndani. Jambo hili mabenki wametupa heshima kubwa kwasababu wameona *trust* iko kwenye madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho najua kwasababu ya muda yako mambo mengine ni ya kiusimamizi mdogo wangu

Mheshimiwa Maganga la Nyakafuru Pamoja na *loyalty* kwamba ukiweka tu milioni 100 tunakata hapana sheria haiku hivyo. *Loyalty* utalipa baada ya kuwa umevuna lakini hatuwezi kukata kodi kwenye mtaji tukifanya hivyo tutakuwa tunamuibia Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, na hilo la Nyakafuru tutakwenda lina hadithi zake ndefu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa aliunda kamati, kamati imeshatoa majibu alilieleza wakati tuko kwenye ziara na nimemhakikishia kwamba hakuna mtanzania hata mmoja atadhulumiwa wala hakuna mtanzania hata mmoja ataonewa.

Mheshimiwa Spika, lakini la kweli tuchukue muda mwingi kuwaeleza watanzania ukweli kuna *drama* nyingine watu wanafanya ambazo ukweli ukienda kwenye *detail* unakuwa wao wanatudanganya viongozi na tunachukua maamuzi ya kuumiza wawekezaji bila sababu ya msingi. Wawekezaji wakubwa tunawahitaji jamani kwenye uchimbaji madini tunahitajiana wote wachimbaji wadogo tunawahitaji, wachimbaji wa katи tunawahitaji na wachimbaji wakubwa tunawahitaji akitokea mmoja katika *group* hizi akapata matatizo basi tunakuwa na *fallback position* tukiwaondoa wachimbaji wakubwa kwa kisingizio cha wachimbaji wadogo, mwisho wa siku hatuwezi kukuza hii sekta.

Mheshimiwa Spika, leo tunafurahi tunasema kwamba uchimbaji mdogo na wachimbaji wadogo wamechangia kwenye pato la Taifa kwenye ile *gross* asilimia 30. Tulikotoka wachimbaji wadogo hawakuwa na maana walikuwa wanachangia chini ya asilimia tano hatua hiyo tumeifikia kwasababu tumewapa heshima lakini heshima hiyo tunayowapa wachimbaji wadogo isigeuke kuwa fimbo ya kuwaumiza wachimbaji wakubwa na wa katи ambao nao wanaweka fedha zao tuheshimiane hatuwezi kutumia kigezo cha uchimbaji mdogo na uchimbaji mdogo

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri malizia

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie uchimbaji mdogo ni hadhi ya muda mfupi haiwezekani mchimbaji mdogo yeye ha-graduate mtoto anasoma darasa la kwanza yeye ni mdogo mdogo lakini ukienda kuangalia *finance* zake na vitabu vyake ana mtaji mkubwa lazima tuwafundishe Watoto kuona Fahari kuitwa wachimbaji wakubwa ili uchimbaji wa ndani uwe wa kwetu naomba nikushukuru sana. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa tafadhalii nisaidie suala la Nyanzaga likoje.

SPIKA: Ameshamaliza hapana hapana hamna taarifa vurugu hiyo hapana Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri huja toa hoja

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha naomba sasa Bunge lako likubali kujadili na kupidisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021 naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa hitimisho lako najua muda ulikuwa ni mdogo lakini kwa kweli umehitimisha vizuri sana kwa waliopata nafasi ya kusikiliza umehitimisha vizuri sana na umesitisita suala la uaminifu na mimi nalipigia mstari sana katika biashara za kimataifa *International Business* uaminifu ni muhimu sana.

Najua nikisema vijana waninishambulia mzee wao nyinyi pigeni, lakini ukweli unabaki palepale dunia ya leo usipokuwa mwanimifu wewe ni *short live* uaminifu ni muhimu sana katika biashara za aina zozote na hasa biashara ambazo zinahusisha na ukimataifa ndiyo kabisa uaminifu wetu unapaswa kuwa juu sana siyo unakuwa huna uaminifu mimi mtanzania utanzania ni kutokuwa mwaminifu? Hapana. Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

SPIKA: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Fungu Namba 100 Wizara ya Madini matumizi ya kawaida kitabu namba 2 ukurasa 503.

FUNGU 100 - WIZARA YA MADINI

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 4,953,181,167

MWENYEKITI: Hamida Mohamed.

MHE. HAMIDA A. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MWENYEKITI: Kifupi na kwa haraka.

MHE. HAMIDA A. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kwanza naishukuru Serikali kwa utoaji wa leseni kwa uwekezaji wa viwanda vyta usindikaji wa chumvi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunao wazalishaji wa chumvi wa ndani ya nchi katika Mkoa wa Lindi, Mtwara, Pwani, Dar es Salaam na Tanga. Lakini wawekezaji wa viwanda wa usindikaji wa chumvi wamekuwa wakiagiza chumvi nyingi kutoka nje ya nchi. Lakini wazalishaji wa chumvi wamekuwa wakikosa wateja na wazalishaji wa chumvi wa ndani wamekuwa masoko yao makubwa ni nchi za jirani pamoja na soko la ndani. Lakini cha kushangaza wawekezaji wa viwanda wa usindikaji wa chumvi wamekuwa chumvi yao

wanayoigiza toka nje badala ya kuingia kiwandani kwenda kusindika wamekuwa wakiiuza bila kusindika nchi za Jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba sasa kusikia kauli ya Serikali namna gani wanaweza kuwafanya wazalishaji wetu wa chumvi na kulinda masoko yao ya chumvi ndani ya nchi na nje ya nchi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante umeeleweka, ufanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Madini tafadhalii.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Hamida kwa hoja hiyo ni kweli kwamba changamoto kubwa ya wazalishaji wa chumvi ni Pamoja na ... kwanza na uzalishaji wenyewe uko chini sana na tulivyokutana na wadau wa sekta ndogo ya chumvi changamoto kubwa walliyolzungumza kwamba kwanini hawazalishi ilikuwa ni utitiri wa kodi na Serikali ilichukua hatua ya kufuta Zaidi ya kodi 11 kwa ajili ya kuwasaidia. Sasa hili jambo jingine la kuwatafutia masoko nadhani tuwe na mukutano tena na wadau wa chumvi tutakutana nao tuyaone kwa Pamoja halafu tuone wapi tunaweza ku-*unlock* ili sekta hiyo iweze kukua, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante Mariam Kisangi hayupo? Ni kosa kubwa kujianidikisha katika wakati kama huu halafu mtu anakuwa hayupo haipendezi hata kidogo kwasababu muda wetu mdogo sana *we are wasting our time*, Neema Lugangira.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nilitaka kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri wa Madini kuhusiana na suala zima la manunuzi kwenye maelezo yake amesema kwamba asilimia kubwa ya zabuni zinazotolewa, zinatolewa kwa kampuni za ndani lakini kwa uelewa wangu tafsiri ya kampuni za ndani ukienda BRELA ni kampuni yoyote iliyosajiliwa nchini. Wakati tukija kwa upande wa *Local content* tafsiri ya kampuni ya ndani inatakiwa iwe kampuni ambayo inamilikiwa na watanzania kwa Zaidi ya 51%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kufahamu kutoka kwake ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba tafsiri hizi zinakwenda sambamba na ile tafsiri halisi ya *local content*, lakini vilevile vigezo vinyavyowekwa kwenye hizi zabuni ziweze kumegwa ili zipatikane zabuni ndogo ndogo ili watanzania...

MWENYEKITI: Neema haina cha vile vile yaani katika wakati huu unazungumza jambo hili moja tu kwahiyo usichomeke vilevile ikawa kama la pili unataka ujibowi ni lipi?

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Ninalotaka kujibowi ni kuhusu zabuni yaani Mheshimiwa Waziri anajipanga vipi kuhakikisha kwamba zabuni hizi zinakwenda kwa Watanzania kwa maana ya umiliki wa kampuni za Watanzania ahsante.

MWENYEKITI: Nilifikiri amelijibu vizuri sana lakini hebu rudia tena Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza nieleze kwanza zabuni yoyote kwenye migodi kabla kabla ya kuitangaza mahali popote lazima uitangaze kwa watu wa ndani ukikosa watu wa ndani unaomba *approval*/Tume ya Madini ili uweze kutafuta watu wa nje. Lakini hata ukipata huyo mtu wa nje hawezi kuja kuchukua hiyo zabuni lazima aungane na watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria tunayoitumia sisi tunaitumia *regulation* ya *local content* ambayo ni zao la sheria ya madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake 2017 ambayo inasema *indigenous company* ni ile ambayo *at least* 21% awe mtanzania sasa tunaangalia kwa namna hiyo lakini kama kuna mtu ambaye anahitaji kufanya kazi atazingatia sheria ya *local content* ambayo tunaitumia Wizara ya Madini nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kasheku Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nilikuwa nataka kupata ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kwenye maelezo yake pia naye amekiri kwamba ile sheria ya CSR wao na TAMISEMI walikasimu mamlaka kwa Mkuu wa Mkoa na kama nilivyoeleza kwamba utendaji wake umekuwa ni mbovu kwasababu umempa mamlaka mpaka ya kuweka na yeye kifungu cha kukagua miradi kwenye halmashauri iliyoko mjini ya Zaidi ya shilingi milioni 600 kwa mwaka na imempa mpaka mamlaka ya kuajiri mtu wa kusimamia miradi anamlipa milioni 5 zaidi hata ya Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri kwa vile sisi tunatekeleza hii miradi nini kauli yako kama mnaona kweli mljichanganya na umekiri kwenye maelezo yako, kwanini sasa usitoe kauli ili utaratibu wakati mnaendelea sisi tuendelee kusimamiwa na TAMISEMI kwenye masuala ya fedha ya miradi halafu yeye abaki kama msimamizi wa miradi.

MWENYEKITI: Ufanuzi wa jambo hilo.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu Mheshimiwa Musukuma alichozungumza hapa sisi tunachosema ni kwamba fedha za CSR zinazotengwa ni lazima zitumike kwa nidhamu, kama kuna mahali ambako kuna matumizi yasiyokuwa ya kawaida nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba na sisi tutaenda kuchungulia pale tufanye ukaguzi kidogo tujiridhishe na hayo anayoyasema halafu hatua zitachukuliwa. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Lakini pia Serikali ni vizuri mjue jamani tuna-disparity kubwa sana katika nchi yetu hii kuna halmashauri zingine zimechoka zimechoka haizna chochote wenzetu wengine wanapata mabilioni lakini mwisho wa siku hatukatai ni vizuri wapate sababu ni waathirika wa mwanzo lakini kweli wengine sifuri kabisa? Kwanini wasingepata nusu, nusu hii ikaenda kwa wale wanyonge kabisa na wenyewe wakaambulia hivi vitu ni vya kuvitazama huko mbele ya safari hii kuachana achana kukubwa ambako wengine wanapata

mabilioni wengine hawapati kitu lazima tuwe na *rationalization policy* fulani katika rasilimali ambazo ni za kitaifa la sivyo tutaachana sana inazidi kugunduliwa wengine wanapata *helium* wengine nani Kongwa hamgundai chochote kila siku. (*Kicheko*)

Sasa sisi tutatoka lini? Hata utafiti hakuna ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Asia Halamga wa mwisho.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi naomba kupata ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri na nitashikilia shilingi kama sitapata majibu ya uhakika. Hapa Mheshimiwa Ole Sendeka ameelezea juu ya suala la ukaguzi unaoendelea kule *Tanzanite One-kwanza* kabisa tunaomba ifahamike wananchi hawapingani na ukaguzi kwasababu wote tunalinda rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachotokea wananchi wanawekwa kwenye chumba kimoja na bahati mbaya sana mfano ukichukulia kwa upande wa wanawake wanawekwa watu wenyewe umri wa miaka 18, umri wa miaka 50, umri wa miaka 30, wanawake wa jinsia wa miaka tofauti tofauti wanawekwa kwenye chumba kimoja lakini bahati mbaya sana wanapovua nguo zile wanakuwa wote kwenye hicho chumba kimoja kati ya watu 10 mpaka 15 lakini bahati mbaya katika umri huo huo bado askari anaowakagua hawakagui kwa wakati yaani anaendelea na mambo yake wakati wamama wale wako hawana nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini pia wakati mwingine wanawake hawa wanakuwa kwenye siku zao bado inakuwa ni changamoto tunachokiongea ni uhalisia. Lakini Pamoja na wanawake halikadhalika kwa wanaume sasa tuombe kwasababu Waziri amekiri kwamba vyumba ni vichache na ukizingatia thamani ya kinachotoka Tanzanite One na amesema kwamba tatizo na changamoto iliyopo ni kukamilisha vyumba 10 sasa Waziri atuambie kwa thamani inayotoka migodi ya Mererani tunashindwaje kujenga

vyumba 10 ili kuweza kulinda utu wa watanzania hapana! Nitaendelea kushika shilingi kama hatutapata ufanuzi wa hivi vyumba 10 na namna ya kuwakagua watanzania kwa namna ya staha ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja!

MWENYEKITI: Ngoja upate ufanuzi kwanza halafu ndio utsaona kama kuna haja ya kuendelea au hapana. Sasa sijui analijibu nani Waziri wa Ulinzi nadhani la Waziri wa Ulinzi hili.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kama ifuatavyo. Kwenye maelezo yangu niliyosema hapa naomba tu kuweka kumbukumbu kwamba ukaguzi unaofanyika siyo kwa watu wote kwa kuwavua nguo watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo na Mheshimiwa Ole Sendeka naomba ninukuu tu iko kwenye kumbukumbu ya Bunge wakati anachangia anasema kuna baadhi ya watu sasa ambao hawakaguliwi kwa mtindo ule na nimesema hivi pale ambapo wakaguzi wetu kwa uzoefu wao na kwa weledi wao wanamashaka ndio inaweza kwenda hatua hiyo. Kwa hiyo, ndio hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa idadi ya watu wanaoingia kwenye chumba tumeenda na kamati wakaguzi kwenye chumba cha wanaume wako wanne na tulivyoelizwa tukiwa na kamati watu wanne ndio wanaingia kwa maana ya mtu mmoja mkaguzi mmoja ndio hali ilivyo kuwa labda kama kuna vinginevyo na niahidi hapa Bunge lako nitafanya ufuatiliaji wa karibu sana ili kuona kama hali hii bado ipo na kama kuna namna fulani ya udhalilishaji Jeshi letu liko makini tutachukua hatua kama kuna jambo linafanyika ndivyo sivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ile hatua ya kujenga vibanda Mheshimiwa Waziri wa Madini yuko hapa vibanda

10 vinakamilishwa ili tuweze kufanya uboreshaji wa ukaguzi na hatua hizo kama nilivyosema inaendelea kukamilishwa ili tuweze kuongeza tija.

MWENYEKITI: Ahsante sana bado Mheshimiwa Ole-Sendeika jambo hili ni kubwa nadhani hatuna budi Mheshimiwa Waziri Mkuu kkusikia kidogo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia *concern* hii ya namna ya ukaguzi unavyoendelea pale Mererani na sikuliskia leo tu nishasikia hapa hata mwanzo na nilishapanga kutembelea Mererani kuona hali hiyo ili kutafuta ufumbuzi wa namna ya ukaguzi wa aina hiyo madini pale Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuahidi tu na Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea na Serikali tutalifanya kazi lazima tujielekeze kwenye teknolojia ambayo itawaondoa watu *physically*...Kwa kuwa Tanzanite inatuingizia fedha nyigi hatuwezi kushindwa kununua milioni, bilioni 1, 2 mtambo unaoweza kufanya ukaguzi wenyewe bila mtu tena kuanza kumuangalia angalia mtu unajua mwili wa mtu ni staha. Kwa hiyo, tutalifanya kazi niwaahidi Waheshimiwa Wabunge tutalifanya kazi ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunashukuru sana kwa kauli hiyo ya Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe nadhani Mheshimiwa Sendeka na wengine tutulie. Maana tulikuwa na walimu wetu enzi hizo wa kutoka Urusi wanatufundisha *Physics* na *Chemistry* wanasema *this is difficult to imagine* sasa tukawa tunafikiria sasa kama ni *difficult to imagine* *ume-imagine* vipi yaani sasa hata mambo ya Mererani kwa tusiokuwa huko unabaki una... *it is difficult to imagine* yaani inakuwaje! Mheshimiwa Jesca Kishoa

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nilikuwa nataka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ni kwanini mpaka leo mwaka wa sita sasa mikataba ya madini haiko wazi na sheria ipo ya

Extractive Industry Transparency and Accountability Act ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na asubuhi nimejaribu kuelezea faida nyingi ambazo zinaweza zikatokana na mikataba hii kuwekwa wazi. Sasa nilikuwa nataka ufanuzi wa kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwanini sheria hii haitekelezeki mpaka sasa na ninakusudia kushika shilingi kama maelezo yake hayatajitosheleza ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca hebu kwanza jifafanue vizuri kuwa wazi maana yake nini kwasababu uko utaratibu wa Mbunge kuweza ku-assess baadhi au yote mikataba ambayo Mbunge anahitaji kupitia Ofisi ya Bunge na akaupata. Unataka uwe wazi kwenye gazeti, kwenye *social media* unataka iwe wazi kivipi? Na je, uwazi huo unaosema na ndiyo *general practice* hapa duniani kwamba mikataba ya kimataifa inakuwa wazi kwenye mitandao au wapi maana lazima tunapokuwa Wabunge tushauri kitu ambacho ndiyo *practice* ambayo inaendelea fafanua.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianzie na hilo la mwisho la mifano iliyo po duniani, ni nchi nyingi sasa zinaweza mikataba wazi na asubuhi nililitaja ikiwepo nchi za Chad, Ghana, Ukraine, Mongolia, zipo nyingi sana.

MWENYEKITI: Yaani kule Chad ambako hata Serikali hakuna kweli? (*Kicheko*)

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Ahsante sana, umeeleweka, kwa sababu ya muda tuendelee maana hata wewe ukitazama...

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye sheria inavyo lezea namna ambavyo mikataba hii inatakiwa kuwekwa wazi.

MWENYEKITI: Subiri kidogo. Utasimama tena nitakuruhusu.

MHE. JESCA D. KISHOA: Sawa.

MWENYEKITI: Tunaye hapa Waziri wa Katiba na Sheria, ufanuzi kuhusu suala hilo.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikataba kuwa waziinategemea ni nani anataka iwe wazi. Kwa Mbunge kama ulivyoeleza Mheshimiwa Spika, utaratibu unaomruhusu Mbunge kupata nyaraka yoyote anayoihitaji upo. Kama atakuwa ameiarifu Ofisi ya Spika na Katibu wa Bunge impatie mkataba huo basi utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ifahamike hata hizo nchi za Ghana, Chad, kwa bahati mbaya sasa naweza kusema *is the failed state* na nchi nyininge, upo utaratibu wa kuionyesha mikataba hiyo, lakini lazima maeneo mengine yafanyiwe *sanitization* hasa yanayo-deal na *intellectual property rights* au baadhi ya siri. Kwa hiyo, hata mkataba ukiwekwa wazi kabla haujawekwa wazi yule aliyesaini mkataba na Serikali maeneo fulani lazima yafanyiwe *sanitization* ili kulinda ubunifu na maslahi maalumu ya yule mwekezaji.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inategemea aina ya mkataba. Mikataba mingine inategemea utaratibu uliowekwa na sheria jinsi ya kuwekwa hadharani. Nadhani kama ulivyoeleza Mheshimiwa Spika kwa upande wa Bunge tunao utaratibu wa sisi Wabunge kuweza kuipata mikataba hiyo na kuiona. Hata kwenye Fomu za Maadili ya Viongozi ambazo tunajaza pia uko utaratibu wa mtu kwenda kuona nani ana mali zipi kwa kulipa kiasi gani cha fedha, lakini haruhusiwi kutangaza kwa sababu kila kitu kina mipaka yake katika haki unayopewa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Anachosema ni kwamba mambo haya ya mikataba yanataka twende polepole kidogo, tuelewane maana hata zile Fomu za Maadili mnazojaza ni mkataba wa aina yake, sasa na wenyewe tuweke kwenye mtandao fomu za kila mmoja wetu hapa wengine si mtakimbia hapa? Natania kidogo, Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nasikitika sana kuona Mheshimiwa Waziri amejaribu kupotosha humu Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 16(1)(a), naomba nisome kinasema hivi: "*In order to ensure transparency and accountability in extractive industries ...*

MWENYEKITI: Unasoma kifungu kutoka kwenye sheria gani?

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria ya *Tanzania Transparency and Accountability Act, 2015*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema hivi: "*In order to ensure transparency and accountability in extractive industries, the Committee shall cause the Minister to publish in the website or through a media which is widely accessible all concessions, contracts and licenses relating to extractive industry companies. This means mikataba hii kulingana na sheria...*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Jesca.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba....

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Hebu msiletu fujo tulieni, sikilizeni majibu ya Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima jambo hilo liwekewe kanuni na ni kama nilivyosema, hauwezi kuu-*publish* huo mikataba kama ulivyo na iko hivyo duniani kote lazima upitiwe na baadhi ya *provision* lazima ziondolewe ambazo zinaweza zika-*compromise interest*. Nalisema hili kwa usoefu kwa sababu mimi ndiyo nili-*renegotiate* mikataba hii, nitawaambieni leo, mara baada ya Mahakama ya Ontario kutoamuru tulipe fedha ili ndege iachiwe walewale wenzetu walienda kwenye mahakama hiyo hiyo kuomba mikataba huo na hukumu hiyo isitolewe kwa sababu ilikuwa inalinda aina yao ya maslahi. Sheria siyo *self-operational* ni lazima itungiwe kanuni. Kwa hiyo, tutakwenda kwenye kanuni hizo ili zieleze inavyokuwa *published* itakuwa *published* kuweka nini na nini na kuondoa nini na nini. Katika mambo ya sheria sitaki kujifaragua, *I am holder of a First Class, Bachelor of Law Degree. (Makof/ Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Madini, nyongeza.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimsaidie tu Mheshimiwa Jesca, kwanza lazima afahamu kwamba ni kweli tuliingia mikataba wa kujunga na *TEITI* na kipengele kimojawapo ambacho ni masharti ilikuwa ni kuweka wazi mikataba. Hata hivyo, nchi wote wanachama mikataba mwaka 2019 tulikuwa Paris kwenye mukutano, moja ya jambo ambalo lazima lifahamike ni kwamba kila nchi ina sheria nyingine, kwa hiyo, hiki lazima uki-*customize* kwenye sheria zako kwa sababu kuna haya ya kulinda pia maslahi ya kibashara ya watu, ndiyo kinachozungumzwa; kuna teknolojia za watu ziko ndani ya mikataba lazima zilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema Waziri wa Katiba na Sheria kuna vitu tulishakubaliana *globally* kwamba hatuwezi ku-*disclose* kwa sababu ya ushindani wa kibashara duniani. Pia ili kuonyesha kwamba jambo hili tunalifanya kwenye *website* yetu ya *TEITI*/tayari tuna *dashboard* kwa ajili ya kuweka jambo hilo. Taratibu zinakamilika na tunashirikiana na watu wa *TEITI* *globally* kwa ajili ya kulifikisha mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zote wanachama wa *TEITI* wote tulikubaliana kwamba kila nchi iangalie sheria zake za ndani usije ukatekeleza kasheria kamoja ukaumiza sheria nyingine. Hicho ndicho alichozungumza hapa Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mkiangalia saa yetu tuko *over and above*, kwa hiyo ni *guillotine*, Katibu.

Kifungu 1001 – <i>Administartion & Human Resource Management</i>	Sh.4,953,181,167
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> ... Sh.1,018,831,861	
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Division</i> ... Sh.1,485,965,391	
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> Sh.518,364,594	
Kifungu 1005 – <i>Legal Services Unit</i>Sh.469,184,585	
Kifungu 1006 – <i>Government Communication Unit</i>Sh.1,014,304,854	
Kifungu 1007 – <i>Procurement Management</i> Sh.443,292,390	
Kifungu 1009 – <i>Management Information Systems Unit</i> Sh.587,332,000	
Kifungu 2001 – <i>Minerals Division</i>Sh.41,326,010,158	

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 100 – WIZARA YA MADINI

Kifungu 2001 - <i>Minerals Division</i> Sh.15,000,000,000 (<i>Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote</i>)	
---	--

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa tafadhali.

TAARIFA

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsanteni sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kama ilivyo ada, ili tukamilishe Kanuni inavyotaka napaswa kuwahoji kwamba Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa ijamuliwe)
(Hoja ilijamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 – Wizara ya Madini yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla

kwa kazi nzuri sana ambayo mnafanya. Mheshimiwa Waziri, Doto Biteko, Mheshimiwa Naibu Waziri Profesa Shukrani Manya, Katibu Mkuu na timu yako yote, Tume ya Madini chini ya Profesa, tunawapongeza sana na mnatujengea heshima. Tunazidi kuridhika na jinsi uwazi na utekelezaji wa shughuli za madini katika nchi yetu unavyokwenda. Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge walio wengi ni kuhusu wachimbaji wadogo, basi tujitahidi tuone namna gani tunazidi kufanya mazingira yao yawe bora zaidi na Zaidi. (*Makofi*)

Tunawashukuru wawakilishi wa mabenki na sifa hizi ambazo mmezipata na Watanzania wote ambao mmeajiriwa kwenye migodi basi mtubebe kwa uaminifu na kuchapa kazi kwa bidii. Tunaamini kabisa bajeti tuliyowapa siyo kubwa sana lakini mtajitahidi kuboresha masuala mbalimbali. Hili la Mererani tumepata ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaamini tutakapokutana hapa mwakani mazingira yatakuwa tofauti zaidi na tulivyosimuliwa.

Mwisho kabisa, lipo tangazo la Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, anasema kuna wageni sita wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Misenyi na Manispaa ya Bukoba, Mkoani Kagera wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Misenyi Dkt. Frank Muganyizi na Mwenyekiti wa CCM Manispaa ya Bukoba Ndugu Muganyizi Zachwa. Kama wapo wasimame, karibu sana akina Muganyizi (*Makofi*)

Pili, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ana mgeni wake ambaye ni Mwenyekiti wa Vijana wa CCM kutoka Mafia Ndugu Samaha Seif. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam; Dkt. Emily Woisso na Ndugu Winnie Lesheya. Karibuni sana akina Woisso. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, Waheshimiwa Wabunge kesho asubuhi tutapita hapa ile saa tatu kamili, tutakuwa na

maswali machache sana baada ya hapo mtaelekea kule. Ni muhimu kupita hapa kwa sababu za kiutaratibu. Nafikiri tunaelewana? Nimezingatia kanuni, usipopita hapa basi tusilaumiane. Kwa hiyo, nashauri mpite hapa ile nani yako nyingine weka kwenye begi acha katika gari huko halafu utajua namna ya kufaulisha mambo. (*Makofi/Kicheko*)

Baada ya shughuli za Bunge kwa kweli tumezikamilisha na kwa uvumilivu mkubwa tumefika hapa tulipofika, nawatakia kila kheri, tunaoendelea kufunga tuendelee kualikana futari. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa futari nzuri ya jana na ya uhakika. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, makofi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuandalia futari nzuri kabisa. Sasa nabanwa, naambiwa wewe je? Tutafanya utaratibu wiki ijayo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.17 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 30 Aprili, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*